Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

EQUIPPING CHURCH LEADERS
• EAST AFRICA •

# KANISA: ASILI YAKE, MISHENI, NA KUSUDI

**na**

**Jonathan M. Menn**

**B.A., University of Wisconsin-Madison, 1974**
**J.D., Cornell Law School, 1977**
**M.Div., Trinity Evangelical Divinity School, 2007**

**Equipping Church Leaders-East Africa**
**3701 N. Gillett St., Appleton, WI 54914**
**(920) 731-5523**
**jonathanmenn@yahoo.com**
**www.eclea.net**

**Kimetafsiriwa**
**na**
**Mchungaji Michael Danstan Nyangusi**

Mei 2017; kusahihishwa na kurekebishwa, Julai 2017

Kanisa ni shirika pekee ambalo Yesu alilianzisha. Ni Zaidi ya shirika la kawaida: kanisa ni "mwili wa Kristo"—udhihirisho wa Yesu unaoonekana duniani. Kwa hiyo, kanisa liko juu sana kwa umuhimu. Kitabu hiki kinajadili asili ya kanisa, tabia, muundo, uongozi, na utawala (maadili ya kanisa, ubatizo na Ushirika Mtakatifu). Pia kinaelezea makusudi manne ya msingi ya kitume ya kanisa: kuabudu; ufunzaji; utume; na umoja (wholeness). Katika kiambatisho kuna orodha ya zana za ufunzaji ufuasi na maelezo na kozi za bure zinazopatikana bure kwenye mtandao.

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

**YALIYOMO**

**I. Kanisa: Utangulizi……………………………………………………………………………………….......................3**
**A.** ***Kanisa ni la kiulimwengu na la mahali pamoja, lisiloonekana na linaloonekana……………………………........3***
**B.** ***Mifano ya Biblia ihusuyo kanisa, maelezo kuhusu kanisa…………………………………………………………..4***

**II. Kanisa: Sifa zake, Muundo wake, Uongozi, na Utawala……………………………………….............................5**
**A.** ***Sifa za kipekee za kanisa…………………………………………………………………………………….....…5***
**B.** ***Muundo na uongozi wa kanisa………………………………………………………………………...................6***
**C.** ***Uongozi wa kanisa……………………………………………………………………………………………….9***
**D.** ***Uadibishaji ndani ya kanisa……………………………………………………………………………………...10***
**E.** ***Ubatizo na Meza ya Bwana………………………………………………………………………….................12***

**III. Kanisa: Misheni na Kusudi lake—Utangulizi………………………………………………………………………17**
**A.** ***Kanisa lipo kwa neema ya Mungu kwa ajili ya utukufu wa Mungu…………………………………………………17***
**B.** ***Maisha ya mkristo—na hatimaye maisha ya kanisa—ni kamili………………………………….....................17***
**C.** ***Mungu anatukuzwa kwa imani yetu ambayo huonekana kwa matendo ya upendo kwa Mungu na kwa watu wengine………………………………………………………………………………….............18***
**D.** ***Misheni nne za msingi na makusudi ya kanisa…………………………………………………………………19***

**IV. KUABUDU……………………………………………………………………………………………………………19**
**A.** ***Kimsingi kuabudu ni hali ya ndani ya kiroho ambayo hugusa kila eneo la maisha yetu na sio tu matendo fulani ya nje ……………………………..……………………………………………………………………19***
**B.** ***Kuna dhana pana ya kuabudu (yaani, kuishi kwa ajili ya Mungu na kumtumikia katika nyanja zote za maisha yetu) na dhana finyu ya kuabudu (yaani, kukutanika pamoja kama kundi ili kumwabudu Bwana)...............20***

**V. KUFANYA WANAFUNZI…………………………………………………………………………………........21**
**A.** ***Msingi wa maandiko……………………………………………………………………………………………..21***
**B.** ***Msingi wa kufanya wanafunzi: injili………………………………………………………………………………22***
**C.** ***Nguvu ya kufanya wanafunzi…………………………………………………………………......................25***
**D.** ***Asili na tabia ya wanafunzi waliokomaa………………………………………………………….....................29***

**VI. Mambo Muhimu kuhusu Mafunzo Mazuri ya Kufanya Wanafunzi……………………………………………..33**
**A.** ***Vikundi vya kufanya wanafunzi………………………………………………………………………………….34***
**B.** ***Sifa za vikundi vizuri vya kufanya wanafunzi…………………………………………………………………...36***
**C.** ***Mchakato wa kufanya wanafunzi………………………………………………………………………………...39***
**D.** ***Mchakato wa kufanya wanafunzi unapaswa kuwa wa kujizidisha wenyewe…………………………………….41***
**E.** ***Kufanya wnafunzi: hitimisho………………………………………………………………………….............42***

**VII. Huduma Ndani Ya Kanisa………………………………………………………………………………..............43**
**A.** ***Kazi ya kanisa, na hasa ya viongozi wa kanisa, ni kuandaa na kuwawezesha watu ndani ya kanisa kufanya huduma zao…………………………………………………………………………………………………43***
**B.** ***Huduma inahusisha watu wote ndani ya kanisa, sio wachungaji tu……………………………………..................47***
**C.** ***Huduma ndani ya kanisa inahusisha huduma katika eneo la "kimwili" na pia katika eneo la "kiroho"……......47***

**VIII. MISHENI…………………………………………………………………………………………………..51**
**A.** ***Msingi wa Maandiko……………………………………………………………………………………………..51***
**B.** ***Kanisa limeitwa ili kufanya wanafunzi duniani kote……………………………..............................................52***
**C.** ***Kanisa limeitwa ili kuwa ushuhuda wa Kristo kwa kuwa mfano na kuwahudumia wengine kwa kutenda mema duniani……………………………………………………………………………………………...53***

**IX. Vipengele Bayana Vya Misheni Nzuri……………………………………………………………………………...55**
**A.** ***Ili kuwa la kimisheni zaidi, kanisa linahitaji kubadili mtazamo wake……………………………………….......55***
**B.** ***Ili kuwa la kimisheni zaidi, kanisa linahitaji kubadili mtazamo wake wa vigezo vya kile kinachofikiriwa kuwa kanisa "lililofanikiwa" …………………………………………………………………………………........59***
**C.** ***Ili kuwa la kimisheni zaidi, yabidi kanisa kupanga kwa upya mgawanyo wa matumizi ya rasilimali zake na kipaumbele kiwe umisheni ………………………………………………………………………..…...60***
**D.** ***Mifano ya kampeni za kimisheni…………………………………………………………………………………...62***

**X. UMOJA (UKAMILI)…..…………………………………………………………………………………….......64**
**A.** ***Umoja na ukamili wa kanisa hutiririka kutoka katika asili ya kanisa…………………………………………....64***
**B.** ***Umoja na ukamili wa kanisa hutiririka kutoka katika yale aliyofanya Kristo…….…………………………………..65***

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

**C.** ***Umoja na ukamili wa kanisa ni muhimu kwa ajili ya ushuhuda wa kanisa kwa dunia*****…..………………………..66**
**D.** ***Umoja na ukamili unapaswa kudhihirika kimatendo katika ngazi zote—ndani ya mtu mwenyewe; kimahusiano ndani ya kanisa la mahali pamoja; na kati ya makanisa na madhehebu tofauti*****…………..……...66**
**E.** ***Umoja na ukamili ndani ya kanisa hutendeka kwa njia tofauti*****……………………………………………………..67**
**F.** ***Kanisa linapofanya yale linayopaswa kufanya matokeo yake ni umoja na ukamili*****………………………………..67**

**XI. Kanisa: Hitimisho……..……………………………………………………………………………………….68**

**BIBLIOGRAFIA………………………………………………………………………………………….......68**

**MWANDISHI…………………………………………………………………………………………….....76**

**KIAMBATISHO 1—HISTORIA YA MAFUNDISHO: ECCESIOLOGI……………………………………………..76**

**KIAMBATISHO 2—KOZI YA KUFANYA WANAFUNZI NA NYENZO………..…………………………….80**

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

## I. Kanisa: Utangulizi

- "Kanisa sio jengo. Kanisa ni watu. . . . *Ekklesia,* neno la Kiyunani lililotafsiriwa 'kanisa' katika Agano Jipya, kamwe haikumaanisha jengo or muundo. *Ekklesia* ilimaanisha mkusanyiko wa watu. . . . Lakini ni Zaidi ya mkusanyiko wa watu wa kawaida; ni jamii mpya. . . . Tunapokuwa wafuasi wa Kristo, tunakuwa wanachama wa Kanisa lake—na kujitoa kwetu kwa kanisa hakutofautiani na kujitoa kwetu Kwake [ona **Math 16:15-18; 22:36-40; 25:31-46; Matendo 20:28; 1 Kor 12:12-27; Gal 6:10; 1 Yoh 3:14; 4:19-20**]." (Colson 1992: 64-65)
- "Injili ya Biblia ina mengi zaidi ya kule kubadilishwa kibinafsi na kupata nafasi ya kusajiliwa mbinguni. Ni kubadilika na kumfanya Yesu kuwa Bwana. . . . Injili hubadilisha mioyo yetu, fahamu na pesa, lakini pia hutubadilisha kuwa kitu kingine. Tunapobadilishwa, tunabadilishwa kuwa wa Kristo, wa kanisa, na kwa ajili ya misheni. . . . Kushindwa kubadilika na kuwa wa kanisa na misheni ni kushindwa kuelewa ujumbe wa injili." (Dodson 2012: 108, 116)
- "Ni kwa neema ya Mungu kwamba kundi la waumini linapata kibali cha kukusanyika kwa dhahiri hapa duniani kushirikishana Neno la Mungu na sakramenti. Si Wakristo wote hupokea Baraka hii. Wafungwa, wagonjwa, walio sehemu pweke za kujitenga, wahubiri wa Injili katika nchi zisizofikiwa na Ukristo husimama wenyewe. Wanajua kwamba ushirika ulio dhahiri ni baraka." (Bonhoeffer 1954: 18)

### A. *Kanisa ni la kiulimwengu na la mahali pamoja, lisiloonekana na linaloonekana*

Kanisa ni la kiulimwengu na la mahali pamoja. Ni "mwili wote wa wale wote ambao kupitia kifo cha Yesu wameokolewa na kupatanishwa na Mungu na wamepokea maisha mapya. Ni watu wote wa aina hiyo, kwamba wapo mbinguni ama duniani. Ingawaje ni la kiulimwengu kwa asili, hujidhihirisha katika makundi ya waaminio mahali mahali ambayo huonyesha tabia zinazofanana kama za mwili wa Kristo kwa ujumla." (Erickson 1998: 1044)

1. <u>Kanisa la kiulimwengu.</u> Vifungu mbalimbali vya Biblia huonyesha asili ya kanisa kiulimwengu. Katika **Math 16:18** Yesu alisema, *"Juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu, wala malango ya kuzimu haitalishinda."* Yesu analitaja kanisa kuwa "lake" katika umoja, sio wingi. Asili ya kanisa kiulimwengu husisitizwa katika vifungu kama **Efeso 1:22-23** (*"Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake,akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote"*); **Efeso 3:10** (*"Ili sasa kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho"*); **Efeso 3:21** (*"Naam, atukuzwe katika kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote vya milele na milele"*); **Efeso 4:4** (*"kuna Mwili mmoja"*); **Efeso 5:23** (*"Kristo . . . ni kichwa cha kanisa"*); **Efeso 5:25** (*"Kristo pia alilipenda kanisa na akajitoa kwa ajili yake"*); ona pia **Kol 1:18, 24; Ebr 12:22-23**.
2. <u>Kanisa ni la mahali.</u> Yesu huzungumza kuhusu kanisa la mahali pamoja kuhusiana na uadibishaji ndani ya kanisa. Mtu akitenda dhambi na hataki kupatana na aliyemkosea na hata shahidi, hapo aliyekosewa *"aliambie kanisa."* Biblia pia huzungumzia kanisa katika dhana ya kundi la mahali, kwa mfano, kanisa katika eneo fulani la kijografia, mijini, au hata majumbani. **Matendo 9:31** inazungumzia *"kanisa katika Uyahudi wote na Galatia na Samaria."* **Ufu 1:4** inazungumzia *"makanisa saba yaliyoko Asia"* (ona pia **1 Kor 16:19**). **Gal 1:2** inazungumzia *"makanisa ya Galatia."* **1 Kor 1:2** inazungumzia *"kanisa la Mungu lililoko Korintho."* **1 Thes 1:1** inazungumzia *"kanisa la Wathesalonike."* **Rum 16:5; 1 Kor 16:19; Kol 4:15;** na **Filemoni 2** yote huzungumzia makanisa yakutanayo nyumbani.
3. <u>Kanisa halionekani na linaonekana.</u> Kanisa la kiulimwengu halionekani. Hii ni kwa sababu washirika wa kanisa la kiulimwengu *"wameandikishwa mbinguni"* (**Ebr 12:23**), na *"Bwana awajua walio Wake"* (**2 Tim 2:19**; ona pia **Math 7:21-23; Luka 13:25-27**). Wayne Grudem hulielezea namna hii: "Kanisa lisiloonekana ni kanisa kama Mungu anavyoliona [na] kanisa linaloonekana ni kanisa kama Wakristo duniani wanavyoliona" (Grudem 1994: 855, 856).

   Hii inamaanisha ya kuwa *yapasa* uwepo mlandano mkubwa kadri iwezekanavyo kati ya haya mawili: waaminio wa kweli wanapaswa wawe wanachama wa kanisa linaloonekana, na wanachama wote wa kanisa linaloonekana wanapaswa kuwa waongofu wa kweli. Chakusikitisha, maandiko na hata uzoefu hutuonyesha kuwa mlandano huu ulio bora hauko halisi katika mazingira yote. Ndio maana, Yesu alionya kuhusu *"manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, walakini ndani ni mbwa mwitu wakali"* (**Math 7:15**; ona pia **Matendo 20:29-30** [*"Najua mimi (Paulo) baada ya kuondoka kwangu mbwa mwitu wakali wataingia kwenu, wasilihurumie kundi; tena katika ninyi wenyewe watainuka watu wakisema mopotovu, wawavute hao wanafunzi wawaandamie wao"*]). Yesu pia alizungumza kuhusu mfano wa ngano na magugu (**Math 13:24-30, 36-43**) kwa namna ya kwamba ni katika hukumu ya mwisho tu kanisa litasafishwa, kwa sababu ni Bwana peke yake ajuae mioyo ya

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

watu (ona **1 Kor 1:10-13; 3:1-4; 5:1-7; 11:17-22; 1 Tim 1:3, 19-20; 4:1-3; 6:20-21; 2 Tim 2:16-18; Yuda 12-13; Ufu 2:14-15, 20-21; 3:3-4, 15-17** ambayo huelezea matengano, ugonvi, uovu, na mafundisho potofu ndani ya makanisa mbali mbali). Kwa sababu ya hali hii, viongozi wa makanisa wanapaswa kujua "tunda" la maisha yao na ya maisha ya watu ndani ya kanisa (ona **Math 7:16-20; 21:43; Luka 6:43-44; Yoh 15:4-5; Gal 5:22-23; 1 Tim 4:15-16**); vifungu vya Biblia "vinavyoonya" inabidi vihubiriwe (mfano, **Math 7:21-23; Marko 4:1-29; 1 Kor 6:9-10; Gal 5:16-21; Efeso 5:5; Ebr 2:1-14; 13:4; Yak 4:4; Ufu 21:8**); na washirika wote wa kanisa yabidi waadibishwe vema katika ijnili kuhusiana na namna tunavyopaswa kuisha sawasawa na injili. Kanisa yabidi lifanye kila liwezavyo kuwasogeza waaminio katika kumfanania Kristo zaidi.

**B.** ***Mifano ya Biblia ihusuyo kanisa, maelezo kuhusu kanisa***

Katika AJ kuna mifano kadhaa inayolielezea kanisa:

- Mifano inayohusiana na Kilimo: Shamba la Mungu (**1 Kor 3:9**); Mzaituni (**Rum 11:17-24**); Mzabibu wa Mungu (**Yoh 15:1-5**); Mavuno ya Mungu (**Math 13:1-30; Yoh 4:35; 1 Kor 3:6-8**).
- Mifano ya Mifugo: Kundi la Mungu (**Luka 12:32; Yoh 10:15-16; 1 Pet 5:2-3**).
- Mifano ya Kisiasa: Ukuhani wa Mifalme, ufalme, au taifa takatifu (**1 Pet 2:5, 9; Ufu 1:6; 5:10**); jamii ya Israeli (**Efeso 2:12, 19**); Israeli wa Mungu (**Gal 6:16**).[1]
- Mifano ya Kimajengo: Nyumba ya Mungu, jengo, hekalu, au hema (**1 Kor 3:9, 16, 17; 2 Kor 5:1; 6:16; Efeso 2:21-22; 2 Thes 2:4; Ebr 3:3-6; 1 Pet 2:5; Ufu 3:12; 7:15; 11:1, 19; 13:6**); nguzo na msingi wa kweli (**1 Tim 3:15**).
- Mifano ya Kimahusiano na Kifamilia: Mke au bibi arusi wa Kristo (**2 Kor 11:2; Efeso 5:22-32; Ufu 21:2, 9**); Wana au watoto wa Mungu (**Rum 8:14, 16; 9:26; Gal 3:26; 1 Yoh 3:1-2**); Watu wa Mungu (**Rum 9:25; Tito 2:14; 1 Pet 2:9-10**); Nyumba au familia ya Mungu (**Math 12:49-50; 2 Kor 6:18; Efeso 2:19; 1 Tim 3:15; 5:1-2**).[2]
- Mifano ya Mwili: Mwili wa Kristo (**Rum 12:4-5; 1 Kor 10:17; 12:12-27; Efeso 1:22-23; 2:16; 3:6; 4:4, 12, 15-16; 5:23, 30; Kol 1:18, 24; 2:19; 3:15**).

Mifano ya kanisa ambayo imedhihirika Zaidi ni ile inayohusu majengo, ya kimahusiano na familia, na mifano ya mwili. Kila mfano kati ya hii imedhihirika kimsingi kwa sababu za kimahusiano. Kama vile Kristo asivyogawanyika (**1 Kor 1:13),** vivyo hovyo mwili umeunganika na kichwa, viungo vya mwili vimeunganika pamoja, mume huunganika na mkewe, na "mawe yaliyo hai" yote yamejengwa sawasawa kuwa hekalu takatifu. Hukazia upendo wetu mkuu na kujitoa kwetu kwa na umoja wetu wa karibu na Mungu pamoja na Kristo (**Kum 6:5; Math 22:37-38; Marko 12:29-30; Luka 10:27-28**) na kati ya sisi kw sisi (**Law 19:18; Math 19:19; 22:39; Marko 12:31; Luka 10:27-28; Gal 5:14**). Matokeo ya mkazo huu wa kimahusiano ni kwamba ili tuwe kama Kristo (**Rum 8:29**) and *"Iweni watakatifu, kwa kuwa mimi [Mungu] ni mtakatifu"* (**Law 11:44-45; 19:2; 20:7, 26; 1 Pet 1:15-16**). Sababu ya hili ni kwamba moyo wa agano la Mungu kwa watu wake wakati wote umekuwa *"nami nitakuwa Mungu wenu, nanyi mtakuwa watu wangu"* (**Mwz 17:8; Kut 6:7; 29:45; Law 26:12; Yer 7:23; 11:4; 24:7; 30:22; 31:1, 33; 32:38; Ezek 11:19-20; 14:10-11; 36:28; 37:23, 27; Hos 2:23; Zek 8:8; 13:9; 2 Kor 6:16; Ebr 8:10; Ufu 21:3**).

Mifano yote na maelezo kuhusu kanisa ina maana za kimatendo: "Yapasa ukweli kwamba kanisa ni kama familia utuongezee upendo wetu na ushirika kati ya sisi kwa sisi. Wazo kwamba kanisa ni kama bibi arusi wa Kristo lituchochee tutafute usafi wa moyo na utakatifu zaidi, na pia upendo mkuu kwa Kristo na kumnyenyekea yeye. Sura ya kanisa kama matawi ndani ya mzabibu itufanye kumtegemea kikamilifu zaidi. Wazo la zao la kilimo litutie moyo kuendelea kukua katika maisha ya Kikristo na kujipatia virutubisho sahihi vya kutukuza sisi na wengine. Picha ya kanisa kama hekalu jipya la Mungu ituongezee uelewa wetu wa uwepo wa Mungu unaojidhihirisha tunapokutanika. Dhana ya kanisa kama ukuhani itusaidie kuona kwa uwazi zaidi furaha aliyonayo Mungu katika dhabihu za sifa na matendo mema tunayoyatenda kwake (ona Ebr. 13:15-16). Mfano wa kanisa kama mwili wa Kristo uongeze hali ya kutegemeana sisi kwa sisi na kuthamini kwetu vipawa

---

[1] Kanisa kudhihirika kwa njia nyingi kama Israeli mpya ya kiroho na ya kweli. Kwa mfano, AJ huchukua mawazo, makubaliano, ishara za manabii za Agano la Kale ambazo zilihusiana na Israeli na kuzihusisha na kanisa. Kanisa kama Israeli mpya, ya kirorho imezungumziwa kwa kirefu katika Menn 2016: 49-59.

[2] Dhati Lewis anaonyesha, "Katika mifano na maelezo yenye ya picha kuhusu kanisa, mfano mmoja unabaki kuwa juu zaidi ya yote: familia. Kwa kweli, ni kielelezo hasa cha kanisa kiasi kwamba huwezi kusema ni mfano kisawasawa. Mifano huelezea kanisa ni nini au linafanana na nini—nuru, kundi la kondoo, shamba, jengo—lakini familia si mfano hasa; ni maana halisi ya kile tunachokijua kama kanisa." (Lewis 2015: n.p.; tunaweza kusema vivyo hivyo kuhusiana na maana ya kanisa kama wana wa Mungu au watu wa Mungu)

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

mbalimbali ndani ya mwili." (Grudem 1994: 859)

## II. Kanisa: Sifa, Muundo, Uongozi, na Utawala

### A. *Sifa za kipekee za kanisa*

Aya ya mwisho ya Kanuni za Imani za Nicene-Constantinople (AD 325/381) inasema, "Naliamini Kanisa moja takatifu la duniani kote na kitume"[3] Hii inaonyesha sifa nne za kipekee za kanisa la kweli liwe la mahali pamoja au kiulimwengu. Kanisa ni: (1) moja; (2) takatifu; (3) la duniani kote (ina maana, la kiulimwengu); na (4) la kitume.[4]

- Umoja. Umoja huonyesha asili ya kanisa katika hali ya kiulimwengu na kutoonekana (ona hapo juu). Hata hivyo, hali hii ya kiumoja inaonekana pia katika kanisa la mahali pamoja kama inavyoonyeshwa katika **Efeso 4:4-6**: *[4] Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu; [5]Bwana mmoja, Imani moja, ubatizo mmoja. [6]Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote.* Kuna mambo ya kiimani ambayo huunganisha wakristo wote na makanisa yote ya kweli. Kinachosikitisha ni kwamba, katika kanisa la mahali pamoja, umoja umedhoofishwa na matengano kati ya makundi makubwa ya makanisa (Farakano Kuu ["Great Schism"] la 1054 kati ya Waothodoksi wa Mashariki na Makanisa ya Kikatoliki na Matengenezo ya miaka ya 1500 katika ya Waprotestanti na Makanisa ya Kikatoliki) na migawanyiko kati ya madhehebu na hata katika makanisa ya mahali pamoja.
- Utakatifu. Utakatifu hutokana na ukweli kwamba Wakristo wamepatanishwa na Mungu kwa kufutiwa dhambi kwa kifo cha Yesu, na Roho Mtakatifu sasa anakaa ndani ya waaminio. Twapaswa *"kuwa watakatifu, kwa sababu mimi [Mungu] ni mtakatifu"* (**Law 11:44-45; 19:2; 20:7, 26; 1 Pet 1:15-16**). Katika maisha haya, hata hivyo, hakuna aliye takaswa kwa ukamilifu, na kuna magugu katikati ya ngano na mbwa mwitu kati ya kondoo katika kanisa linaloonekana.
- La duniani kote (la kiulimwengu). Katika Agano Jipya, utambulisho wa watu wa Mungu si wa taifa moja tena (Israeli) bali sasa ni *"watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha"* (**Ufu 5:9;** ona pia **Ufu 7:9**). Kuna makanisa sasa kila mahali duniani.
- Lakitume. **Efeso 2:20** husema kwamba kanisa limekuwa *"Limejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Yesu Kristo mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni."* **Ufu 21:14** vivyo hivyo inasema *"Na ukuta wa mji [Yerusalem Mpya] ulikuwa na misingi kumi na miwili ya wale mitume kumi na wawili wa Mwana Kondoo."* Makanisa mengine (hasa Kanisa Katoliki, Waothodoksi wa Mashariki, na Makanisa ya Kianglikana) yanakazia *kurithi utume*, inamaanisha, Petro na wale mitume wengine waliteua wale watakaokuwa warithi wa utume wao, mfumo ambao wameufuata hadi hivi lelo.[5] Sehemu kubwa ya makanisa mengine (Waprotestanti na Wapentekoste) wafuata uongozi wa Lutha na Kalvin katika kuweka mkazo kwenye *kweli ya kitume* kama alama inayotofautisha kanisa la kweli, hasa, Neno la Mungu kufundishwa na sakramenti kutolewa kwa usahihi. Hivyo, Tamko la Augsburg la mwaka 1530 (tamko la kiimani la Lutheran) hulitaja kanisa kuwa ni "lakitume" mahali ambapo "Injili hufundishwa kwa usahihi na sakramenti kutolewa kwa usahihi" (Augsburg 1530: Art. 7). John Calvin katika *Institutes of the Christian Religion* vilevile alisema, "Popote tunapoona Neno la Mungu likihubiriwa na kusikika kama lilivyo, na sakramenti zikitolewa kama alivyoagiza Kristo, hapo haihitajiki kutia shaka kwamba kanisa la Mungu lipo" (Calvin 1960: 4.1.9).

  Alama hizi mbili za kanisa—Neno la Mungu kufundishwa na sakaramenti kutolewa kwa usahihi—ni wazi ni muhimu: "Hakika ikiwa Neno la Mungu halihubiriwi, badala yake Mafundisho potofu au mafundisho ya watu, hapo hakuna kanisa la kweli. Katika mazingira fulani inaweza kuwa vigumu kuamua ni upotofu wa mafundisho wa kiwango gani unaoweza kuvumiliwa kabla ya kulikataa kanisa ya kuwa ni la kweli, lakini yapo mazingira mengi ambayo tunaweza kusema kwamba kanisa la kweli halipo. . . . Alama ya

---

[3] Neno "katoliki" humaanisha "ya kiulimwengu," na lazima litofautishwe na Kanisa Katoliki la sasa. "Katoliki" ni neno ambalo lilitumika kwa miaka kama 1000 ya kwanza ya historia kanisa kuelezea imani sahihi ya Kikristo, hasa kama ilivyoelezewa na matamko ya mamlaka zilizokuwa zikitambulika kidunia na kuendelezwa katika mabaraza ya kidini.

[4] Timothy George anachambua mambo mnne ya kanisa katika jarida la *Christianity Today* Makala yenye kichwa "Kile ambacho ningetaka kumwambia Papa kuhusu kanisa," inapatikana kwenye mtandao (George 1998).

[5] Michael Holmes anaonyesha, "Madai kwamba hawa maaskofu na waliowatangulia ni mnyororo wa kimamlaka unaounganika kurudi nyuma hadi kwa mitume wenyewe ni wazi huonyesha baadae juhudi za kuhalalisha muendelezo wa sasa wa mfumo wa kurithishana madaraka ya kiaskofu. . . . Inafurahisha kwamba Ignatius [Askofu wa Antiokia; aliyekufa mwaka 110] alionyesha misingi sahihi ya mamlaka na nafasi ya askofu na hakuwekea utaratibu, kama alivyokuwa mfuasi wake Clement wa of Roma [Askofu wa Roma; alikufa mwaka 99] alifanya, kwa kufuata dhana ya kupokezana ya kitume." (Holmes 1989: 9, 81)

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

pili ya kanisa, utoaji sahihi wa sakramenti (ubatizo na Ushirika Mtakatifu) ilitamkwa kwa kupinga mtazamo wa funzo la kikatoliki ambalo husema kwamba neema ya kuokoa imekuja kupitia sakramenti na hivyo sakramenti zimefanywa kwa 'matendo' ambayo kupitia hayo tumepata haki ya wokovu. Kwa hiyo, Kanisa Katoliki lilikazia juu ya kulipia badala ya kufundisha Imani kama njia ya kupata wokovu. Lakini kuna sababu nyingi ya kuijumuisha sakramenti katika alama za kanisa. Ushirika unapofanya huduma ya kubatiza na kushirikisha Meza ya Bwana, hiyo ni kazi endelevu na *inakusudia kutenda kazi kama kanisa* [kinyume na, kwa mfano, huduma ya kanisa]. . . . Ubatizo na Meza ya Bwana hutumika kama 'vidhibiti uanachama' kwa ajili ya kanisa. Ubatizo ni njia ya kuwaingiza watu ndani ya kanisa, na Meza ya Bwana ni njia ya kuwaruhusu watu kuonyesha ishara ya kuendelea kama washiriki ndani ya kanisa." (Grudem 1994: 865-66)

Baadhi ya Wana Matengenezo wameongeza alama ya tatu ya kanisa la kweli kwamba lazima Neno lifundishwe kwa usahihi na sakramenti itolewe kwa usahihi, ikimaanisha, uadibishaji ndani ya kanisa ufanyike ipasavyo. Hili lilidhihirika katika Ukiriwa Scots ["Scots Confession"] (1560) na Ukiri wa Belgic ["Belgic Confession"] (1561): "Kwanza, kuhubiri Neno la Mungu kwa kweli, ambako Mungu amejidhihirisha kwetu, kama maandiko ya manabii na mitume yanenavyo; pili, utoaji sahihi wa sakramenti ya Kristo Yesu, ambavyo lazima vuhusianishwa na Neno na ahadi ya Mungu kuweka muhuri yake na kuthibitisha katika mioyo yetu; na mwisho, nidhamu ya kiutumishi kudumishwa kisawasawa, kama Mungu anavyoagiza, ambapo maovu hukemewa na matendo mema huinuliwa." (Scots 1560: Art. 18) "Viashiria, vya kulitambua kanisa la kweli, ni hivi: endopo fundisho halisi la injili linahubiriwa hapo; endapo utoaji halisi wa sakramenti unafanyika kama Kristo alivyoagiza; endapo uadibishaji dhidi ya dhambi unafanyika: kwa kifupi, endapo mambo yote yanatendeka kwa kufuata Neno la Mungu lisiloghoshiwa, kila yaliyo kinyume yakiwa yamerekebishwa, na Yesu Kristo pekee akitambulika kama Kichwa cha Kanisa." (Belgic 1561: Art. 29)

**B.** ***Muundo na uongozi wa kanisa***

Biblia ilipokuwa ikiandikwa, kanisa lilikuwa katika hali ya uchanga.[6] Mitume wa kwanza (wale kumi na mbili) walikuwa hai bado. Zaidi ya hayo, nyaraka za AJ ndizo ambazo zajulikana sasa kama barua zilizoandikwa "kwa vipindi fulani", ikimaanisha ziliandikwa kwa makanisa halisi au watu kama matokeo ya tatizo fulani au tukio lililotukia kwa wakati ule. Ingawaje baadhi ya vifungu hugusia swala la muundo na uongozi ndani ya kanisa, Biblia haielezi kwa ufasaha kuhusu muundo na mfumo wa uongozi kwa ajili ya kanisa. Zaidi ya hayo, mazingiza ya makanisa katika dola yote ya Rumi yalitofautiana: katika maeneo Fulani kulikuwa na mateso, katika maeneo mengine hayakuwepo; makanisa mengine yalikutana nyumbani, mengine yalikuwa makubwa; mengine yalikuwa mijini, mengine vijijini; kanisa la kwanza pale Yerusalem lilikuwa la Wayahudi zaidi, makanisa mengineyo mengi katika dola yote yalikuwa ya watu wa Mataifa. Kwa hiyo, katika vipindi vyote vya historia ya kanisa kumekuwako mifumo mbali mbali tofauti ya kiuongozi na utawala katika kanisa, na hata ndani ya mapokeo tofauti ya kanisa mfumo wa uongozi wa kanisa umekuwa ukibadilika kadiri muda unavyoendelea kusonga mbele.

Kimsingi Biblia huzungumzia ofisi mbili au ngazi za uongozi katika kanisa la AJ. Maneno ya kiyunani kwa ajili ya nafasi za juu za uongozi wa kanisa ni *episkopos* ambayo humaanisha "mwonazi" au "askofu" na *presbuteros* ambayo humaanisha "mzee." Maneno hayo mawili yanaonekana kuwa na maana sawa na moja laweza kutumika mahali pa hilo jingine (ona **Matendo 20:17, 28; Tito 1:5, 7**). Kwa ujumla hawa ndio watu ambao waliweka dira na kuhusika zaidi na huduma ya Neno (kuhubiri, kufundisha, kushauri, kuadibisha, nk.).

"Kuna muundo ambao unaonekana wakati wote wa *wazwee zaidi ya mmoja* kama chombo kikuu cha utawala katika makanisa ya Agano Jipya" (Grudem 1994: 912). Mahali popote pale ambapo kanisa limetajwa katika kitabu cha Matendo, na kila wakati Paulo alipoanzisha makanisa mapya, wakati wote waliweka wazee zaidi ya mmoja (ona **Matendo 11:30; 14:23; 15:2-6, 22-23; 16:4; 20:17-18; 21:18; Tito 1:5**). Katika **1 Tim 5:17** na **Yak 5:14** "wazee" ni wingi. Vivyo hivyo, katika **1 Tim 4:14** wakati Timotheo anasimikwa "baraza la wazee" walimwekea mikono. Huo ndio muundo wa kibiblia wa uongozi wa kanisa: wazee zaidi ya mmoja, si utawala wa mtu mmoja. Uongozi wa wazee zaidi ya mmoja huudhihirisha ukweli kwamba wakristo wote mbele ya macho ya Mungu wana nafasi ya "ukuhani" (**1 Pet 2:5, 9; Ufu 1:6**). Pia huidhihirisha ile hekima ya kibiblia kwamba *"kwa wingi wa washauri huja wokovu [au, hekima]"* (**Mith 11:14; 26:4**) na kama *"chuma hunoa chuma; Ndivyo mtu aunoavyo uso wa rafiki yake"* (**Mith 27:17**).

Kuwa na wazee zaidi ya mmoja ni muhimu. Kila mmoja ana vipawa na uwezo tofauti—lakini pia

[6] Wakati wanazuoni wengi huamini kwamba AJ lilikamilishwa mwaka kati ya 95-96 (ikimaanisha miaka 65 au zaidi kidigo baada ya kifo cha Yesu), John A. T. Robinson amefanya utafiti wenye hoja ya nguvu kwamba AJ lote lilikamilishwa kabla ya kuharibiwa kwa hekalu mwaka 70, hii itakuwa imemaanisha kwamba AJ lilikamilishwa miaka 40 au pungufu baada ya kifo cha Yesu (ona Robinson 1976).

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

tofauti ya madhaifu na maeneo ya kutoweza. Kwa hiyo, hakuna mtu mmoja anayeweza kuongoza kanisa la mahali pamoja yeye mwenyewe kwa utoshelevu. Wazee zaidi ya mmoja huwajibishana wao kwa wao kimaadili, kiroho, na katika maswala ya fedha. Zaidi ya hapo, endapo uongozi wa kanisa utakuwa juu ya mtu mmoja, atakapopatikana na tukio baya kanisa laweza anguka. Yatupasa kukumbuka kwamba kanisa halituhusu sisi, ni kuhusu Kristo. Kanisa ni mwili wake, si wetu. Yatupasa tuhakikishe kuwa kanisa linaongozwa sawasawa na watu wanaume na wanawake wenye sifa za kuongoza (**1 Tim 3:1-13**). Kwa njia hiyo, tukio lolote likimpata mchungaji au kiongozi mmojawapo, kanisa linaweza kuendelea vema, kwa sababu limejengwa kwenye msingi imara wa uongozi.

Neno "mchungaji" linaonekana mara moja tu katika AJ. Ni tafsiri ya Kiyunani *poimēn* katika **Efeso 4:11** ambayo inasema, *"Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilist na wengine kuwa wachungaji na walimu."* Grudem anatoa maoni kwamba "mstari huu ungetafsiriwa vizuri zaidi kama 'mchungaji-walimu' (kundi moja) badala ya 'wachungaji na walimu' (ikiashiria makundi mawili) ni kwa sababu ya muundo wa maneno wa Kiyunani" (Ibid.: 913). Hasa kwa vile, kila kundi lililotajwa katika huu mstari limetangulia neno "wengine kuwa," lakini hakuna "wengine kuwa" ikitangulia "walimu"; badala yake, wachungaji na walimu wako kundi moja. Zaidi ya hapo, "wachungaji na walimu" ni nomino ambazo mwandishi huziona kana kwamba zimeungana kwa namna fulani kama ambavyo inaonekana katika muundo wa maneno katika lugha ya Kiyunani" (Ibid.: 913n.13). Grudem anahitimisha, "Kuhusiana na kufundisha inaashiria kwamba hawa wachungaji walikuwa baadhi (au pengine wote) miongoni mwa wazee walifundisha, kwa maana moja ya sifa ya mzee ni 'ajue kufundisha' (1 Tim. 3:2)" (Ibid.). Kwa kuongezea, nomino *poimēn* kwa kawaida kutafsiriwa kama "mchungaji," na muundo wa matamshi wa *poimēn* (*poimainō*) unatumika kwa wazee katika **Matendo 20:28** (*"lichungeni kanisa la Mungu"*) na **1 Pet 5:2** (*"lichungeni kundi la Mungu"*). Haya yote yamaanisha, katika AJ, "mchungaji" ni sawa na "mzee."

Ngazi ya pili ya uongozi iliyotajwa katika AJ ni mashemasi. Ofisi ya mashemasi ilianza katika **Matendo 6:1-7.** Wajibu wa mashemasi ni mmoja wa masaidiano, huduma, na kuhudumia mambo yahusuyo mahitaji ya mwili ya kusanyiko. Neno "shemasi" latokana na neno la Kiyunani *diakonos* ambalo humaanisha wale wanaotumikia wengine; wasaidizi, wapambe (ona Danker 2000: 230-31).

Kadiri muda ulivyokwenda, mfumo a uongozi ndani ya kanisa umekuwa ukiendelea kubadilika. Kufikia mwaka wa 55-65 "miundo mbali mbali ya uongozi wa ndani (uongozi wa kundi, uongozi wa wazee, na uongozi wa maaskofu) ilikuwa ikijaribiwa" (Holmes 1989: 5). Wakati wa kipindi cha miaka ya 60-80 ulikuwepo mwelekeo "kuelekea kuwa na miundo ya kanisa mikuu na iliyosanifiwa. Vyanzo vilivyopo havina uhakika kuhusiana na kiwango halisi cha ukubwa wa badiliko, lakini hatua za kwanza katika uelekeo huo ziko Dhahiri katika kipindi hiki, hasa katika nyaraka za Ignatius [Askofu wa Antiokia, alikufa mwaka 110]. Wakati ambapo idadi kubwa ya makanisa ambayo Paulo aliyaanzisha yalisimamiwa na mfumo wa uongozi ambao ulikuwa na wazee/waonazi (maaskofu) na mashemasi, tunaona katika mfumo wa uongozi wa kanisa wa Ignatian ulikuwa na muundo wa ngazi tatu ambazo ni askofu mmoja na chini yake walitumika wazee na mashemasi." (Ibid.: 9) Miundo mitatu mikuu ya uongozi wa kanisa ambayo imekuwa ikiendelea kujengeka na kutambulika kama mifumo ya uongozi wa kanisa ni: (1) uongozi wa maaskofu; (2) uongozi wa wazee; na (3) uongozi wa kundi:

1. <u>Uongozi wa maaskofu.</u> Neno hili linatokana na lugha ya Kiyunani *episkopos* ("mwonazi" au "askofu"). Huu ndio mfumo unaotambulika zaidi wa ngazi za kiuongozi ndani ya Kanisa. Mfumo huu wa uongozi kwa kawaida una ngazi tatu za uongozi: maaskofu, wazee (ni pamoja na wachungaji na makuhani), na mashemasi. Muundo wa uongozi wa jinsi hii hutilia mkazo fundisho la mitume na umoja na huwa na hali ya kuzuia migawanyiko ambayo huweza kutokea katika uongozi wa makundi. Mfumo huu wa uongozi wa kanisa ilitokea mapema katika historia ya kanisa; kwa mfano, Ignatius alikuwa askofu wa Antiokia katika nusu ya mwisho ya karne ya kwanza. Asili ya hili inapatikana katika Baraza la Yerusalem katika **Matendo 15**; Yakobo akiliongoza baraza na, baada ya kusikia ushuhuda, alijibu na kuseme "uamuzi wangu mimi" (**Matendo 15:19**). Hiyo inaonyesha wadhifa wa juu zaidi ya ule wa mzee wa kanisa la mahali pamoja. Kanisa Katoliki limechukuwa mfumo huu kwa upeo uliokwenda zaidi ya inavyopasa, Papa akiwa mamlaka iliyo kuu juu ya Kanisa Katoliki lote, akifuatiwa na Makadinali, Maaskofu na Mapadre[7]

2. <u>Uongozi wa wazee.</u> Jina hili linatokana na lugha ya Kiyunani *presbuteros* ("mzee"). Muundo huu wa uongozi una ngazi mbili hasa za uongozi: wazee na mashemasi. Wazee wanaweza kutajwa kuwa ni ama "wazee vongozi" au "wazee wanaofundisha" (wachungaji) (ona **1 Tim 5:17**). Kwa kawaida, atakuwepo

[7] Mfumo huu wa utawala uliendelezwa baadaye. Barua ya kwanza ijulikanayo kama *1 Clement*, ambayo iliandikwa mnamo mwaka 95 au 96 kutoka kwa viongozi wa kanisa la Roma kwa kanisa la Korintho, huonyesha kwamba "uongozi, ilionyesha ulikuwa umewekwa juu ya kundi la waonazi au maaskofu (haya mawili yanaonekana kukubaliana katika *1 Clement*; ona 44.1-6)" (Holmes 1989: 24).

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

mwonazi wa kanda au jimbo, ikimaanisha mwakilisha wa makanisa ya mahali pamoja mbalimbali tofauti, ambaye atakuwa na mamlaka fulani juu ya makanisa ya mahali pamoja katika jimbo au kanda hiyo. Aina hii ya uongozi inafuata mfumo wa AJ (ambo umezungumziwa hapo juu) wa wazee zaidi ya mmoja wakiongoza kanisa huku wakisaidiwa na mashemasi kadhaa. Msingi wa waonazi wa jimbo kuwa na mamlaka juu ya makanisa ya mahali pamoja tunaupata katika maamuzi ya baraza la Yerusalem (**Matendo 15**) ambapo kanisa la Antiokia lilituma wajumbe (Paulo, Barnaba, na wengine) Yerusalemu (**Matendo 14:26-15:3**), na Baraza likatoa maamuzi yaliyopaswa kufuatwa, sio maoni yenye kuweka uhiari. Wapresbiteri wanamchukulia Yakobo kama "wa kwanza miongoni mwa walio sawa" katika Baraza, inamaanisha aliongoza mikutano na kutangaza maamuzi, lakini ule uamuzi ulifanywa na washiriki wote wa Baraza (ona **Matendo 15:22, 25, 27, 28; 16:4**).

3. <u>Uongozi wa kundi.</u> Washirika wa kanisa la mahali huchagua viongozi wao, kwa kawaida mzee mmoja (mchungaji) na mashemasi, au mchungaji (sawa na "mzee anayefundisha" katika muundo wa uongozi wa wazee), wazee zaidi ya mmoja (sawa na "wazee viongozi" katika muundo wa uongozi wa wazee), na mashemasi. Katika muundo huu wa uongozi wa kanisa, kanisa la mahali, sio askofu wa jimbo (au mkoa) au mwonazi, ndiye mamlaka ya juu. Mamlaka ya juu inabaki kwa kusanyiko, ingawaje katika baadhi ya makanisa yanayotumia mfumo huu wa uongozi, mamlaka ya juu imewekwa juu ya mchungaji au wazee. Muundo huu wa uongozi kimsingi umejengwa katika dhana ya kwamba katika AJ kanisa la mahali halihitaji kukata rufaa kwa mamlaka yoyote juu yake hata katika maswala makubwa ya kinidhamu (**Math 18:15-17; 1 Kor 5:4-5; 2 Kor 2:6**). Zaidi ya hapo, katika **Matendo 6** kanisa lilichagua viongozi wake (mashemasi; mitume waliridhia, lakini uchaguzi ulifanywa na kanisa. Pia, inaonekana kwamba uongozi wa kundi unakwenda sambamba na kanuni ya "ukuhani wa waamini wote" (ona **1 Pet 2:5, 9; Ufu 1:6**).

4. <u>Unaweza kuona tofauti ya kanisa lile la kwanza pale Yerusalemu (ambalo lilikuwa na washirika ambao walikuwa Wayahudi kwa idadi kubwa) na makanisa ya kwanza ya Wamataifa:</u>

a. *Kanisa la Yerusalem.*

(1) <u>Mitume (wale kumi na mbili).</u> Mitume walijitoa kwa huduma ya kuomba na kufundisha Neno (**Matendo 1:14; 6:4**); walichagua mitume kuziba nafasi (**Matendo 1:21-26**); walifundisha na kuhubiri (**Matendo 2:42; 4:31, 33; 5:19-21; 6:4; 8:25; 10:42**); walifanya ishara, miujiza na kuponya (**Matendo 2:43; 3:7; 5:15-16**); waliitisha na kusimamia mikutano ya kusanyiko (**Matendo 6:2**); waliwasimika mashemasi (**Matendo 6:6**); waliwatuma mitume na wapanda makanisa kwenye umisheni (**Matendo 8:14; 11:22**); waliweka mikono juu ya waumini wapya na kuwaombea, wakapokea Roho Mtakatifu (**Matendo 8:15-17**); walilijulisha kanisa maono waliyoona katika nafasi yao ya mamlaka (**Matendo 11:1-18**).

(2) <u>Wazee.</u> Wazee walichunguza na kujadili tofauti za kitheolojia pamoja na mitume (**Matendo 15:6**); waliipokea (na Yakobo) ripoti ya huduma ya Paulo aliyoifanya kwa Wamataifa (**Matendo 21:18-19**); waliandika maamuzi ya kitheolojia pamoja na mitume (**Matendo 15:20; 21:25**).

(3) <u>Mashemasi.</u> Mashamasi walisimamia swala la kuwalisha wote kwa usawa (**Matendo 6:1, 3**); walihubiri injili (**Matendo 8:5, 40**); walitenda ishara, walitoa pepo, na kuponya (**Matendo 8:6-7**).

(4) <u>Mapato.</u> Watu waliuza mali zao na kuwapa waliokuwa wahitaji (**Matendo 2:44-45; 4:32-37; 5:1-4**); mapato ya mauzo yaliingizwa katika mfuko wa pamoja ambao ulisimamiwa na mitume (**Matendo 4:34-35**).

(5) <u>Maisha ndani ya kanisa.</u> Kila mmoja aliingiwa na hofu (**Matendo 2:43**); walikuwa na umoja (**Matendo 2:46; 4:32**); walikuwa na furaha na mioyo safi (**Matendo 2:46**); walikusanyika hekaluni kila siku (**Matendo 2:44**) na pia walikutanika nyumba kwa nyumba kuomba (**Matendo 12:12**).

b. *Makanisa ya Wamataifa.*

(1) <u>Mitume (wale kumi na mbili).</u> Mitume waliandika nyaraka kwa makanisa (**Mathayo, Yohana, 1-2 Petro, 1-3 Yohana, Ufunuo**); walituma wapanda makanisa kwenye maeneo ambayo walitaka kuyafikia kiumisheni (**Matendo 11:22**); walikuwa ndio mamlaka ya juu kuhusiana na mijadala yote ya kitheolojia (**Matendo 15:1-29; 16:4**).

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

(2) Wamishonari (akiwemo na Paulo).[8] Wamishonari walihubiri injili (**Matendo 11:26; 13:4-5, 14, 21, 42-44; 16:13; 17:17, 19; 18:4**); waliponya wagonjwa (**Matendo 14:9-10**); walifundisha, walitia moyo na kuimarisha makanisa (**Matendo 14:22; 18:11, 23-28; 20:2**); waliweka wazee katika makanisa waliyoanzisha (**Matendo 14:23**); walipeleka nyaraka zilizotumwa na mitume kwa makanisa (**Matendo 15:30; 16:4**); walijitegemeza wao wenyewe katika mahitaji yaliyohitaji pesa (**Matendo 18:3**); waliita wazee kukusanyika walipotembelea (**Matendo 20:17**); waliandika nyaraka kwa makanisa (**Warumi-Filemoni**).

(3) Wazee. Walichagua na kutuma wamishonari (**Matendo 13:1-3**); waliwajibika kutunza kanisa lao (**1 Tim 3:5**); waliweka wahubiri (**1 Tim 4:14**).

(4) Mashemasi. Mashemasi walitumika ndani ya kanisa na walijaribiwa (**1 Tim 3:10**).

(5) Mapato. Watu wote walikuwa na mali zao (**Matendo 11:29; 20:33-35; 2 Kor 8:1-15; Efeso 4:28**); walitoa kwa kanisa kila wiki kutokana na mahitaji ya kanisa yaliyojitokeza (**Matendo 11:29; 1 Kor 16:1-2; 2 Kor 8:1-9:15**); mara nyingine waliwatunza wamishonari ambao kwa kawaida hujitegemeza wenyewe (**Matendo 20:33-35**).

(6) Maisha ndani ya kanisa. Watu waliishi katika nyumba zao wenyewe lakini walikusanyika kila siku ya Jumapili (**Matendo 20:7**); watu walilipoke Neno kwa furaha na makanisa yalikuwa (**Matendo 11:21-26; 13:48-49; 14:21; 16:5; 17:10-12**); hawakuwa na umoja wakati wote, kuna ambao walikosa maadili, na wengine walianza kupoa (**Matendo 15:36-40; 1 Kor 1:11-13; 3:3-4; 5:1-5; 11:17-21; Gal 2:12-13; Ufu 2:14, 20; 3:15-16**).

### C. *Uongozi wa kanisa*

Kanisa ni mwili mmoja, sio tu mkusanyiko wa mtu mmoja mmoja. Shirika lolote litakuwa zuri, lenye nguvu na lililofanikiwa sawa sawa na kiwango cha viongozi wake. Kuanzia mwanzo wa mjadala wake wa sifa za kuwa kiongozi wa kanisa, Paulo anasema, *"Mtu akitaka kazi ya askofu, atamani kazi njema [au kazi adilifu] atamani kufanya"* (**1 Tim 3:1**). Kwa hiyo, "Paulo anatafsiri kuwa mwonazi kwa kuhusianisha na majukumu yake ('kazi adilifu'), si ya cheo au madaraka. Hawatii moyo watu kutafuta vyeo bali wajibu." (Liefeld 1999: 116) In **1 Tim 3:2-7**, Baada ya hapo Paulo anaorodhesha sifa 15 muhimu kwa kiongozi wa kanisa, awe ni mchungaji, askofu, waanagalizi au wazee. Sifa hizo hizo hutumika kwa wale wanaoongoza makanisa mbali mabli. Sifa hizo ni: kuwa mtu asiyelaumika; mume wa mke mmoja (inamaanisha, "mwanamume wa mwanamke mmoja"); mwenye kiasi; mwenye busara; mwenye heshima; mkarimu; ajuae kufundisha; asiyezoelea kileo; asiwe mgonzi; muungwana; mpenda amani; asiwe mpenda fedha; ajuaye kutumza nyumba yake vema; asiwe mwongofu mchanga; mwenye kuheshimiwa hata na wale walio nje ya kanisa. Sifa za kuwa mzee au shemasi ni kama zinafanana (linganisha **1 Tim 3:2-7** kuhusiana na wazee [ona pia **Tito 1:5-9**] na **1 Tim 3:8-13** kuhusiana na mashemasi [ona pia **Matendo 6:1-3**]), ukiondoa sifa ya kuweza kufundisha (ingawaje mashemasi wa kwanza walikuwa na uwezo wa kufundisha (ona **Matendo 7:1-53** [Stephano]; **Matendo 8:4-13, 26-38** [Philipo]).

Mambo mawili yapasa kuzingatiwa. Kwanza, Paulo anaposema katika **1 Tim 3:2** kwamba mwonazi *"awe mtu . . ."* hamaanishi kwamba ili mtu awe kiongozi ni lazima awe na sifa moja, au tano, au hata sifa nyingi kati ya zile alizoziorodhesha. Badala yake anasema ili uwe kiongozi kanisani ni lazima uwe na sifa zile zote. Pili, kinachoshangaza kuhusu hizo sifa ni kwamba (ukiondoa ule uwezo wa kufundisha na kutokuwa mwimini mchanga) hizo zote ni sifa ambazo *kila mkristo* anapaswa kuwa nazo—ndio maana uanafunzi kwa kila mwamini ni muhimu sana. Hakuna sifa maalum kuhusiana na kabila la mtu, kiwango cha elimu, utajiri alionao, au sifa nyinginezo za "nje". Badala yake, sifa zote zinahusiana na *tabia* ya mtu. Sifa zote 15 za uongozi zahusisha tabia, moja kwa moja au kwa namna isiyo dhahiri. Chakufurahisha, katika **1 Tim 1:9-10** Paulo aliorodhosha mifano 15 ya watu wasio haki ambao kwa ajili yao sheria ilitengenezwa. Anachosema Paulo hapa ni kwamba tabia yetu kama viongozi inatakiwa iwe *tofauti kabisa* na aina ya watu wale ambao wako chini ya sheria, kwa sababu *hatuko tena chini ya* sheria ya zamani. Badala yake, twapaswa kuwa na tabia ya Kristo, kwa sababu tuko chini ya "sheria ya Kristo." Matendo yetu hutiririka kutoka katika tabia yetu. Kama jinsi ambavyo tabia yetu inapaswa kuwa tofauti kabisa cha waovu, kadhalika matendo yetu yanapaswa kuwa kinyume kabisa cha matendo ambayo yameorodheshwa katika **1 Tim 1:9-10**. Watu ambao wako katika nafasi za uongozi ndani ya kanisa ndio

[8] Ingawaje Paulo alikuwa mtume (**Rum 1:1; 1 Kor 1:1; 9:1**), AJ (na Paulo mwenyewe) hutambua utofauti kati ya utume wa Paulo na "wale kumi na wawili" (ona **Matendo 6:2; 1 Kor 15:5, 8**). Hili linaweza kuhusiana na ukweli kwamba huduma ya Paulo ilikuwa kwa watu wa Mataifa (**Matendo 9:15; 13:46; 18:6; Rum 11:13; Gal 1:16; 2:7**), wakati ambapo Petro, kiongozi Dhahiri na mnenaji wa wale kumi na wawili walikuwa mitume kwa Wayahudi (ona **Gal 2:7-8**).

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

wawakilishi wa Kristo ambao wanaonekana kwa uwazi zaidi katika kusanyiko la waumini na kwa wasioamini katika jamii. Kwa hiyo, ni lazima wawe na tabia ya Kristo na kuwa kielelezo cha kweli kwa namna wanavyoishi.

Kwa sababu msingi wa uongozi ndani ya kanisa ni tabia na unahusiana na majukumu, sio cheo, **1 Tim 5:22** inasema, *"Usimwekee mtu mikono kwa haraka, wala usizishiriki dhambi za watu wengine."* Kifungu hiki "kinakataza kusimika viongozi haraka [ambacho] kinakubaliana vizuri na mjadala mkuu wa sura hii. Na kuwekewa mikono kwa watu mara kwa mara katika nyaraka hizi kunaonekana kuhusiana kwa sehemu kubwa na kusimika viongozi (cf. 4:14; 2 Tim 1:7)." (Earle 1978: 381) Kule *"kushiriki dhambi za wengine"* kunaonekana kuhusiana na ukweli kwamba, kwa kumsimika mtu, unachukua dhamana ya tabia yake na sifa zake na hapo unawajibika kwa dhambi yoyote ambayo anaweza kuitenda.[9] Ikiwa makanisa yanatumia vigezo hivi kwa dhati kabisa wakati wa kuchagua viongozi badala ya kuona sifa za kidunia, bila shaka makanisa yangekuwa tofauti tukiyalinganisha na vile yalivyo sasa. Yangekuwa pia na ufanisi mkubwa sana kuliko yalivyo leo kuhusiana na swala la kuwaleta watu kwa Kristo na kuwafanya waamini wawe na maisha yaliyobadilika kumfanania Kristo, kwa sababu yangekuwa ni aina ya makanisa ambayo Mungu anataka kuyaona.

**D.** ***Uadibishaji ndani ya kanisa***

Kama tulivyotaja hapo nyuma, baadhi ya Wanamatengenezo waliongezea sifa ya tatu ya kanisa la kweli zaidi ya Neno kufundishwa sawa sawa na kutolewa kwa sakramenti kwa usahihi, nayo ni uadibidhaji ndani ya kanisa kufanyika inavyopasa. Kusudi kuu la aina yoyote ya uadibishaji ndani ya kanisa ni toba na matengenezo ya yule mwenye kukwaza na upatanisho wa mwenye kuleta makwazo na waamini wote na Mungu. Makusudi haya yasipowekwa maanani, uadibishaji ndani ya kanisa waweza kutumiwa vibaya.

Ifuatayo ni mifano ya Kibiblia ya uadibishaji kanisani:

1. Mifano ya Kibiblia kuhusu mambo yanayohitaji nidhamu ya kanisa. AJ hutoa mifano kadha wa kadha ya mambo ambayo yalihitaji kanisa kuwaadibisha wale waliohusika katika mambo ya jinsi hiyo: magonvi na matengano (**Rum 16:17; Tito 3:10**); zinaa kati ya ndugu (**1 Kor 5:1-5**); wale waishio maisha yasiyo na utaratibu au yenye vurugu na wanaokataa kufanya kazi (**2 Thes 3:6-12**); wasiotii alichoandika Paulo (**2 Thes 3:14-15**); wenye makufuru (**1 Tim 1:19-20**); wanaofundisha mafundisho potofu (**2 Yoh 10-11**). Wayne Grudem anasema kanuni iliyosimamia mifano hii ya dhambi ambazo zilihitaji uadibishaji wa kanisa: "Kanuni ambayo ilikuwa ya hakika ilionekana ikitenda kazi: dhambi zote ambazo kanisa la Agano Jipya lilizichukulia hatua za kinidhamu zilifahamika wazi wazi au zilitendwa kwa dhahiri kwa nje na nyingi ya hizo ziliendelea kwa kipindi fulani cha muda. Ukweli kwamba zilifahamika waziwazi ulimaanisha aibu ilikuwa ya kanisa, Kristo aliaibishwa, na ulikuwepo uwezekano wengine wangehamasika kufuata tabia zile mbaya ambazo zilivumiliwa waziwazi." (Grudem 1994: 896-97)

2. Viwango vya Jinsi ya Kuadibisha Kanisani: *uwiano.* In **Math 18:15-17**, Yesu aliainisha kanuni ya uwiano ya kuadibisha kanisani: [15] *"Na ndugu yako akikukosa, enenda ukamwonye, wewe na yeye peke yenu; akikusikia umempata nduguyo.* [16] *La, kama hasikii, chukua pamoja nawe mtu mmoja au wawili, ili KWA VINYWA VYA MASHAHIDI WAWILI AU WATATU KILA NENO LITHIBITIKE.* [17] *Na asipowasikiliza wao, liambie kanisa; na asipolisikiliza kanisa na awe kwako kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru."* Kanuni hii, kuwa adhabu iliyotolewa iwiane na kiwango na aina ya kosa la mkosaji ilijulikana kama "uadibishaji endelevu." Inarudi nyuma kwa **Kut 21:24-25** (*"jicho kwa jicho, jino kwa jino, mkono kwa mkono, mguu kwa mguu, kuteketeza kwa kuteketeza, jeraha kwa jeraha, chubuko kwa ajili ya chubuko"*). Uwiano ndiyo alama ya haki katika mahakama na kwa hakika yapasa iwe ikifuatwa hivyo ndani ya kanisa.

Vigezo ambavyo viongozi wa kanisa wanapaswa kuviona kuhusiana na kuwango cha adhabu watakacho toa ni pamoja na: ni kwa kiwango gani kosa limefanyika na kwa muda gani limerudiwa, endapo kosa linatambulika ndani ya jamii au la; toba ya mkosaji; endapo malipizi yamefanyika (ambayo ni ishara mojawapo ya toba ya kweli); athari zilizosababishwa na kosa kwa kanisa na kwa walio nje ya kanisa; na vigezo vinginevyo (ona mfano, **1 Kor 5:6** [*"chachu kidogo huchachusha donge zima"*]; **Gal 2:11-14** [Paulo anamkemea Petro ili wengine wasifuate mfano wake mbaya]; **1 Tim 5:20** [*"Wale wadumuo kutenda dhambi uwakemee mbele ya wote, ili na wengine waogope"*]). Viongozi wa kanisa wanapaswa pia kutambua kwamba kuna mambo yahusuyo tabia ambayo Wakristo tunatofautiana

---

[9] Kitabu cha ECLEA kiitwacho *1 Timotheo: Dondoo/Mwongozo Mfuypi; Uchambuzi; Kijarida chaMafunzo ya Kiutendaji* (http://www.eclea.net/courses.html#timothy) huchambua kwa kina sifa za mtu anayefaa kuwa kiongozi wa kanisa. Ni chanzo kizuri cha mafunzo kwa kanisa kutumia katika kuwaandaa washirika katika eneo hili.

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

misimamo yetu. Hivyo Paulo anahimiza kuwepo na kiwango kikubwa cha uvumilivu (ona **Rum 14:1-23**).

3. <u>Kutoa adhabu sawia.</u> Katika **Math 18:15-17**, ambayo ilihusisha dhamba kati ya waumini wawili ambao walikuwa washirika wa kanisa, Yesu alizungumza kwanza kuhusu kutatua tatizo lao wao wenyewe peke yao (**Math 18:15**); endapo itashindikana, aliyekosewa ajaribu tena, mara hii achukue mashahidi wawili au watatu (**Math 18:16**); ikiwa hatua hiyo haikufanikiwa, swala hili sasa lifikishwe kanisani, hapa ikimaanisha kwenye uongozi wa kanisa (**Math 18:17**). Katika mazingira fulani makaripio na maonyo yanaweza kutosha kutatua tatizo hilo (ona **2 Tim 4:2; Tito 1:13; 2:15; 3:10; Yak 5:19-20**).

Adhabu ya juu zaidi ya kanisa ni kumtenga mtu, inamaanisha kumnyima ushirika mtu aliyeshindwa kuwa na toba ya kweli na kumtoa kanisani. Ikumbukwe kwamba kutenga ni adhabu ya mwisho ambayo yaweza kutumika baada ya adhabu nyingine zote kutumika bila mafanikio, dhambi inapokuwa imekithiri, inatambulika na hata walio nje ya kanisa, na huenda kadiri inavyoendelea inaweza kuwafanya wengine kupotea au kusababisha matengano kanisani isiposhughulikiwa, na mkosaji hatubu. Ukweli kwamba kutenga ndio adhabu ya mwisho kwa kanisa na hutekelezwa endapo tu kuna mazingira ya dhambi yaliyokithiri inaonekana katika ukweli kwamba kutenga katika AJ ni utekelezaji wa kanuni ya AK la sheria: "Walawi 20:11 iliwataka Israeli kumuua mtu ambaye amejamiiana na mke wa baba yake. Mtume Paulo, akikabiliana na tatizo la jinsi hiyo katika 1 Wakorintho 5:1-13, analiagiza kanisa kutekeleza adhabu ya kanisa ya kutenga, na sio kuua." (Johnson 2007: 281) Katika **1 Tim 1:20** Paulo anaiita adhabu hii "kumkabidhi mkosaji kwa shetani." Kifungu kingine ambacho kinazungumza kuhusu *"kumkabidhi [au kumtoa'] kwa shetani"* mkosaji ni **1 Kor 5:5**, ambapo mwanamume alikuwa akilala na mke wa baba yake (inamaanisha, kama yale mazingira katika **Law 20:11**). Maandiko yote haya mawili **1 Tim 1:20** na **1 Kor 5:5** yanahusisha tatizo kubwa sana ndani ya kanisa: fundisho potofu lenye asili iliyo dhahiri, inamaanisha, "kufuru" (ona **1 Tim 1:3-4, 20; 4:1-7a; 6:3-5; 2 Tim 2:16-18**); na kashfa ya ngono iliyokuwa wazi hadharani (**1 Kor 5:1**).

4. <u>Kusudi la msingi la adhabu yoyote kanisani</u> Katika kuadibisha kanisani, viongozi wa kanisa wanahitaji kuzuia dhambi isienee kwa wengine. Hivyo, "hatua za kuadibisha ndani ya kanisa ambazo zilibainishwa na Yesu (Math. 18:15-20) na mitume wake (1 Kor. 5:1-13; 1 Tim. 5:20-25; nk.) ni njia ambayo kwayo Mungu anawaita watu wake wa agano jipya kuulinda utakatifu wake" (Johnson 2007: 282). Hata hivyo, kusudi la msingi la kiwango chochote cha adhabu kanisani, hata kutenga, ni kumfanya mkosaji afike kwenye toba na kurejea. Katika **1 Tim 1:20**, Paulo anasema ya kwamba lengo la "kumtoa kwa shetani" ni ili wakosaji *"ili wafundishwe wasimtukane Mungu."* Katika **1 Kor 5:5**, kumtolea shetani *"ili mwili uadhibiwe, ili na roho iokolewe katika siku ya Bwana."* Ikiwa mkosaji *anatubu kiukweli na kubadilika,* Paulo anasema kwamba kanisa linapaswa *"kumsamehe na kumfariji, mtu kama huyo asije akamezwa katika huzuni yake ipitayo kiasi. Kwa hiyo nawasihi kumthibitishia upendo wenu"* (**2 Kor 2:7-8**). Paulo anakazia msingi huu wa kuadibisha kanisani katika **Gal 6:1** anaposema, *"Ndugu zangu mtu akighafilika katika kosa lolote, ninyi mlio wa Roho mrejezeni mtu kama huyo kwa roho ya upole, ukijiona nafsi yako usije ukajaribiwa wewe mwenyewe."* Ni wajibu wa kanisa kupima kama toba ni ya kweli au la (ona **2 Kor 7:10**). Kwa hiyo, hata itakapotokea kwamba mtu fulani "ametolewa kwa shetani," viongozi wa kanisa wanapaswa kuendeleza mawasiliano na mtu huyo, kuendelea kumshauri, na kujaribu kumrudisha kwa Bwana (ona **Gal 6:1**).

5. <u>Nidhamu kwa viongozi wa kanisa.</u> **1 Tim 5:19-21** inahusu swala la kuadibisha wazee wa kanisa. Kile anachosema Paulo kinahusu kila aliye katika nafasi ya uongozi rasmi wa kanisa, awe ni askofu, mzee, mchungaji, shemasi, au nafasi nyingine ya uongozi. Paulo anapozungumzia swala la nidhamu ya viongozi wa kanisa swala hili linaweza kutokana na ukweli kwamba mfumo wa biblia wa kuongoza kanisa si wa mtu mmoja bali ni wa wazee zaidi ya mmoja: uongozi wa wazee zaidi ya mmoja unapaswa kusababisha mfumo wa uwajibikaji wa kila kiongozi badala ya utawala wa mtu mmoja.

Swala la kuadibisha viongozi wa kanisa mara kwa mara limepelekea kwenye pande mbili zinazotofautiana za maamuzi yenye mwelekeo wa matumizi mabaya ya utoaji wa hukumu: upendeleo kwa watu fulani au chuki dhidi ya wengine. "Utumiaji mbaya wa kuadibisha umesababisha roho ya ukali na isiyo na subira, lakini matokeo ya kutokuadibisha yamesababisha hatari ambayo yaweza kuwa kubwa zaidi. Unapokabiliwa na mazingira ambapo wazee ndio watenda dhambi hali ya kukosa msimamo ni ya kuilaani." (Guthrie 1990: 118-19) Wafadhili wakubwa wa kanisa, watu wa kabila moja na mchungaji, wana familia wa familia ya mchungaji, na marafiki wa karibu mara nyingi husimikwa kuwa wazee, hata kama hawana sifa kama zilizoandikwa katika **1 Tim 3:1-7**. Zaidi ya hapo, dhambi za hao wazee hazitiliwi maanani kwa sababu ni wafadhili wakubwa, wana familia, au marafiki, ingawaje

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

dhambi hizo hizo zikifanywa na wale washirika wasio wafadhili wakubwa, wana familia, au marafiki hazingekubalika. Hivyo, "tabaka mbili za Wakristo" zinatengenezwa—wanaopendelewa na wasiopendelewa—na matokeo ambayo huleta madhara kwa kanisa. Paulo anatukumbusha kwamba, tukiwa viongozi wa kanisa, uadilifu wetu na mwenendo ni lazima uhusishe kila uamuzi tunaoufanya. Tutatoa hesabu kwa Kristo kwa kila tufanyacho kwa jina lake kama viongozi wa kanisa lake. Kwa hiyo, ni bora *"uyatende hayo pasipo kuhukumu kwa haraka; usifanye neno lolote kwa upendeleo"* (**1 Tim 5:21**) ili kwamba tuwe na *"dhamira njema"* (**1 Tim 1:5**) na *"dhamira safi"* (**1 Tim 3:9**) tunaposimama mbele zake (kama tutakavyofanya siku ya hukumu, na kama tunavyofanya wakati wote sasa kwa hakika).

6. Hitaji la Ushahidi. Katika mjadala wake wa nidhamu ya viongozi wa kanisa katika **1 Tim 5:19-21**, Paulo anasema, "*Usikubali mashitaka juu ya mzee, ila kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu*" (**1 Tim 5:19**). Hii ni kanuni inayotumika katika kesi zote zinazohusu kuadibisha kanisani. Ni kanuni kwamba ushahidi wa kosa ukiambatana na mashtaka vinahitajika kuwasiliswa kabla adhabu haijatolewa. Kanuni hii ambayo Paulo anaitaja inatokea tangu wakati wa **Kum 19:15** (ona pia **Kum 17:6**). Kanuni kwamba shitaka inabidi liambatane na shahidi mwingine ilikusudiwa kuzuia mashtaka yasiyo haki. Hata hivyo, ikiwa tamko kuhusu *"mashahidi wawili au watatu"* litatumika katika mtindo tu wa jinsi ilivyoandikwa, na tunazingatia tu *sura* ya tamko na sio *kiini* au kanuni inayoeleza kwa ufasaha, basi hapo kutotenda haki kwaweza kutokea kwa namna iliyo kinyume. Katika mazingira ya kihistoria na kiutamaduni ya **Kum 19:15**, Israeli ilikuwa jamii ambayo haijaendelea inayojishughulisha na kilimo. Ndivyi ilivyokuwa katika kipindi cha Paulo. Vitu kama upigaji picha, simu za mkononi, vifaa vya kurekodi na vinginevyo vinavyohusu teknolojia havikuwepo. Sasa hivi vitu hivyo vyote tunavyo katika tamaduni zote. Zaidi ya hayo, dhambi nyingi (kama vile za zinaa) hutendwa kwa kawaida katika mazingira ambapo hakuna ushahidi wa mwanadamu. Kwa hivyo, mtu akishtakiwa kwa dhambi ya kuzini, inaweza isiwepo mantiki, na kusababisha kutotendeka kwa haki, kwa wale viongozi wengine kukataa kupokea shitaka kwa sababu hakuna ushahidi wa watu wawili au watatu kwenye hilo tukio la zinaa. Mashtaka ya aina hiyo yanaweza husianishwa na ushahidi wa jumbe za simu ambazo zimebaki katika simu, picha, mashahidi waliomwona mzee akiwa mahali na huyo aliyezini naye au katika saa ambazo hawakupaswa kuwepo mahali kama hapo muda ule, nk. Mazingira yote ya aina hiyo yanakubalika katika mahakama hivyo ni vema yazingatiwe endapo shitaka limetolewa dhidi ya mzee wa kanisa. Hata Paulo aliitaja kanuni ya **Kum 19:15** katika hali ya "kutoshinda" katika **2 Kor 13:1**. Pale alihusika zaidi na dhambi na matatizo yaliyokuwa ndani ya kanisa la Korintho. Alinukuu kanuni ya AK kwa kuona ukweli kwamba *"Hii ndio mara ya tatu ya kuja kwenu."* Alimaanisha safari zake za awali na nyaraka kwa kanisa vilikuwa ni *"mashahidi wawili au watatu"* na vingetosha kushughulikia wakosaji ndani ya kanisa. Yesu alifanya vivyo hivyo katika **Yoh 8:17-18** aliposema, *"Tena katika torati yenu imeandikwa kwamba, ushuhuda wa watu wawili ni kweli. Mimi ndimi ninayejishuhudia mwenyewe, naye Baba aliyenipeleka anishuhudia."* Kanuni hii ya ushahidi na kuthibitisha ni matokea ya *"kuzitenda kanuni hizi bila kuhukumu kwa haraka, na bila kufanya lolote kwa upendeleo"* (**1 Tim 5:21**). Ili kanisa libaki kuwa takatifu na safi, basi si tu kwamba watu wake wanapaswa kuwa watakatifu na safi katika mwenendo wao, lakini pia viongozi lazima wawe watakatifu na safi katika namna *wanavyotekeleza* uadibishaji kanisani: bila kubagua au kupendelea; wakitekeleza majukumu yao kwa mwenendo wa "unyenyekevu na uungwana" na kutambua kiukweli madhaifu yao wenyewe na kuogopa kwamba wao wenyewe waweza kuanguka katika dhambi za jinsi hiyo hiyo" (Grudem 1994: 899-900; ona **Math 7:3-5; Luka 6:42**); wakifanya maamuzi yao kutokana na ushahidi uliopo tu; wakiwa na malengo ya kutunza jina zuri la kanisa, kuzuia kuenea kwa dhambi, na kuleta toba na urejesho wa maisha ya mkosaji.

### E. *Ubatizo na Meza ya Bwana*

- "Kristo aliasisi kaida mbili kwa ajili ya wafuasi wake kufuata: ubatizo, kaida ambayo hufanyika mara moja tu (Math. 28:19; Gal. 3:27), na Meza ya Bwana, kaida ambayo hufanyika mara kwa mara ya ukumbusho (1 Kor. 11:23-26). Hizi zinaitwa 'sakramenti' katika kanisa la Magharibi, 'mafumbo ya kidini' katika kanisa la Kiothodoksi la mashariki, au 'mapokeo ya kidini.' Maandiko hayana jina halisi kwa ajili ya kaida hizo mbili au mila nyingine kama hizo katika Agano la Kale, kama, tohara kwa wanaume (Mwz. 17:9-14, 23-27) na Pasaka ya kila mwaka kama kaida ya ukumbusho (Kut. 12:1-27). Hata hivyo, mafundisho yanaruhusu kuziweka pamoja kama alama na muhuri za uhusiano wa kiagano na Mungu.

  'Sakramenti' ni neno la Kilatini ambalo humaanisha takatifu. Utafiti wa kaida za Kikristo zenyewe hukupeleka katika kuzielezea sakramenti kama mila zilizowekwa na Kristo ambazo ndani yake ishara zinazopatikana katika fahamu hutupa neema ya Mungu ndani ya Kristo na Baraka za agano lake.

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

Huwataarifu na kuzithibitisha Baraka hizi kwa waamini, ambao kwa kuzipokea sakramenti huielekea neema ya Mungu na kuitangaza imani yao na wajibu wao kwake. . . . Kanisa la kipindi cha miaka ya 1100 -1500 lilikosea kwa kuongeza sacrament nyingine tano (komunio, kitubio, ndoa, kuweka wakfu, mpako mtakatifu). Hizi tano hazimo katika muhuri ya uhusiano watu wa kiagano na Mungu. Hazikuwekwa na Kristo, na hazina 'alama yoyote inayoonekana kwa macho au vitendo maalum vilivyoagizwa na Mungu' (*Thirty-Nine Articles,* XXV).

Sakramenti ni njia ya neema, kwa maana Mungu anazitumia kujenga uthabiti wa imani katika ahadi zake na kuhimiza matendo ya kiimani ili kuzipokea karama njema zilizotajwa. Uletaji wa matokeo wa sakramenti hautokani na imani au uzuri wa mtumishi, lakini hutokana na uaminifu wa Mungu, ambaye, akiwa ni yeye aliyetupa hizo alama, anapendezwa kuzitumia. . . . Kama vile kuhubiriwa kwa Neno kunavyofanya injili isikike, hivyo sakramenti hufanya ionekane." ("Sacraments" 2005: 1411)

- "Sakramenti sio tu kitu cha asili ambacho kimeumbwa ili kiwe alama ya neema (upinde wa mvua, kwa mfano). Sakramenti ni alama ya *ushiriki* katika neema *iokoayo*. Si tu kwamba inaweka wazi uwepo wa Mungu na ile kazi yake, lakini pia namna anavyowapatia wenye dhambi wokovu wake. . . . Ishara hizi za nje huonyesha ushirika kwa dhahiri; hulijenga kanisa la Kristo kama jamii yenye wanachama. Ubatizo unahitaji uamuzi kuhusiana na kujiunga katika jamii hii. Meza ya Bwana, ni ishara ya kuendelea katika ushirika, inaweka wazi wale ambao wamejitenga na Bwana." (Clowney 1995: 271, 272)

1. Ubatizo. Ubatizo ni kaida ya mwanzoni ya kanisa. Ni ishara katika ngazi mbali mbali:
    - Ubatizo unaonyesha utambulisho wa mtu na kuungana kwake na Kristo (**Rum 6:3-5; Gal 3:27**);
    - Ubatizo ni hafla ya kutaja majina mahali ambapo mtu anayebatizwa anabatizwa kwa jina la Mungu wa utatu (**Math 28:19**), inamaanisha, "jina walilonalo kama yale ya watoto wa Mungu (Is. 43:6b-7)" (Clowney 1995: 278);
    - Ubatizo ni ishara ya toba na kusamehewa dhambi, matumizi ya maji humaanisha utakaso na kufanywa upya (**Ezek 36:25; Matendo 22:16; Kol 2:11-13; 1 Pet 3:21**);[10]
    - Ubatizo ni ishara ya ubatizo katika Roho Mtakatifu, ujazo wake na kazi yake ya kutufanya wapya (**Math 3:11; Yoh 1:33; Matendo 2:3, 38; 10:47; 11:16-18; 1 Kor 12:13; Tito 3:5**);
    - Ubatizo huonyesha utambulisho wa mtu kwa kanisa, humfanya mtu kuwa wa kanisa na ni ishara ya umoja wa waamini wao kwa wao (**Matendo 2:41-42; 1 Kor 12:13**);
    - Ubatizo pia huonyesha kitu fulani kuhusu asili ya kanisa: "Kwa muktadha huu ubatizo huonekana kama 'kaida ya kuingilia' ambayo huonyesha tabia ya kanisa—ya kwamba ni jamii ambayo ubaguzi wa rangi, kiuchumi, na kijinsia haupo (1 Kor. 12:12-13; Gal. 3:27-29)" (Leithart 2012: n.p.).

Ingawaje Wakristo wengi na makanisa wanakubaliana na hayo yaliyotangulia hapo kuhusiana na kile ubatizo unachoashiria, kihistoria na leo kumekuwa na mabishano kuhusiana na endapo ni sawa kuwabatiza watoto wadogo na watu ambao hawajajayatoa maisha yao kwa Yesu kikamilifu. Pia ni njia ipi ya kubatiza itumike (kunyunyiza, kumimitia, au kuzamisha).

---

[10] **Rum 10:9** inasema, *"Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka."* **1 Pet 3:21** inasema, *"Ubatizo sasa unawaokoa ninyi—siyo kuwekea mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu."* John Piper huuelezea wokovu kama uhusiano wa ukiri wa imani na ubatizo katika mistari hii kwa njia hii: "Mwendo wa midomo hewani [**Rum 10:9**] na mwendo wa mwili majini [**1 Pet 3:21**] huokoa tu kwa kumaanisha kwamba hutoa kielelezo cha tendo moja linalisababisha kuhesabiwa haki, ambalo ni, imani (Rom. 3:28). Ubatizo ni wito wa nje wa imani kwa Mungu aliye moyoni." (Piper 2013: 158)

Inafaa ifahamike kwamba mtazamo wa kiutamaduni wa Wakatoliki ni kwamba ubatizo wenyewe ni *njia ya kuingiza* neema iokoayo ("kubadilishwa kunakotokana na ubatizo"). Biblia iko wazi, hata hivyo, ya kwamba tunaokolewa kwa neema ya Mungu kwa njia ya imani peke yake, si kwa kufanya matendo ya mwili kama ubatizo (mfano, **Rum 3:28; 4:1-5; Efeso 2:8-9; Tito 3:5-7**). Hili linathibitishwa na tamko la Yesu kwa yule mwizi pale msalabani, *"Amin, nakuambia, leohvi utakuwa pamoja nami peponi"* [**Luka 23:43**]; yule mwizi aliokolewa ingawaje alikuwa hajabatizwa). Andreas Kostenberger anaeleza kwa muhtasari, "Kwa misingi ya Kithiolojia, *ubatizo wa maji unasisitiza upya wa kiroho* kama kazi ya kwanza na ya msingi ya Mungu ndani na kwa njia ya nafsi ya Roho Mtakatifu. Hili lilifuatiwa na tangazo la Wabaptisti kwamba Masihi atawabatiza watu katia Roho. Hivyo kutubu dhambi na imani katika Kristo, ikiambatana na kufanywa upya, kimantiki hutangulia kabla ya mtu kubatizwa katika maji. Hili, kwa upande wake, huweka ubatizo wa maji katika mtazamo sahihi. Hakuna dhana ya kufanywa upya kwa njia ya ubatizo katika Injili." (Kostenberger 2006-2015: n.p.; ona pia Hunt 1995, White 2005-2006, na Johnson 2016 kwa mjadala zaidi kuhusu kufanywa upya kwa njia ya ubatizo) Ubatizo ni muhimu kwa sababu ni tendo linalofanyika nje wazi wazi kuonyesha kwamba Mungu ameshafanya kazi ya kumbadilisha mtu tayari na kutuokoa; si tendo la mwili tunalolifanya ili tubadilishwe na kuokokoka au linalohitajika ili kumfanya Mungu kutubadilisha na kutuokoa.

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

a. *Ubatizo wa watoto dhidi ya ule wa waamini.*

- Ubatizo wa watoto wadogo. Wale wanaoamini katika ubatizo wa watoto kimsingi hoja yao iko katika kulinganisha na muendelezo wa Agano la Kale la kutahiri na Agano Jipya la ubatizo (**Kol 2:11-12**) na "ubatizo wa wana familia wote" ambao, wanaona, iliwahusisha na watoto (**Matendo 10:46-48; 16:15, 33; 1 Kor 1:16**) (ona Clowney 1995: 280-84; Strawbridge 1998; Strawbridge, ed. 2003; "Ubatizo wa watoto" 2013 [vyanzo mbali mbali kuhusu ubatizo wa watoto]).
- Ubatizo wa waaminio. Wale wanaoamini kwamba ni waaminio tu ndio wabatizwe wanasisitiza kuwa kila mahali katika Agano Jipya ni walioamini tu walibatizwa (hata ubatizo uliofanyika katika familia hausemi kwamba watoto wachanga walibatizwa), kile kinachoonekana wakati wote katika ubatizo wa Agano jipya (ikiwa pamoja na "ule wa kwenye familia") ni toba na kuamini, sio kutarajia kwamba mtoto atatubu atakapokuwa mkubwa (mfano, **Marko 16:16; Matendo 2:38; 10:47; 16:14-15; 16:31-33; Kol 2:12**). Wanaonyesha wazi alama ya maana ya kutokuendelea kati ya watu wa Mungu wa Agano la Kale (ambalo lilikuwa kwa *uzao wa mwili* na liliwahusu wa Isiraeli tu) na watu wa Agano Jipya (ambalo ni kwa *imani* na linawahusu watu wa kila kabila, lugha, taifa (**Rum 4:16; 9:7-8; Gal 3:7, 9, 25-29; Ufu 5:9; 7:9**) (ona Piper 2013: 154-62; Welty 1996; Schreiner na Wright 2006; "ubatizo" n.d. [Makala mbali mbali zihusuzo ubatizo baada ya kuamini]).

b. *Namna za Kubatiza.* Mapokeo tofauti tofauti ya kanisa wametumia namna tofauti za kubatiza, kunyunyiza, kumiminia, au kuzamisha. Kila jadi husimamia kifungu au mstari fulani wa Maandiko ili kutetea jadi hiyo.

- Kuzamisha. Wale wanaokubaliana na kuzamisha kwanza wanaona uchambuzi wa lugha ya Kiyunani katika AJ kwa neno "batiza" (*baptizō*): "*Namna* Yohana na Yesu walivyobatiza bila shaka ilikuwa ni kwa *kuzamisha*. Na hii hutokana na mzizi wa neno lenyewe *baptō*, 'kuzamisha' (mfano, Yosh 3:15 LXX; Ruthu 2:14 LXX baptizō, 'kubatiza,' ni ya kiwango cha juu au mara kwa mara. Pia imeonyeshwa kwa LXX matumizi ya *baptizō* ikimaanisha kuzamisha (ona 2 Wafalme 5:14)." (Kostenberger 2006-2015: n.p.) Pili, kuzamisha (mwili uliozamishwa majini kisha ukaibuka kutoka humo) hiyo ni ishara iliyobora ya kufananishwa na kubatizwa pamoja na mauti, kuzikwa na kufufuka na Kristo (**Rum 6:3-5; Kol 2:12**). Tatu, vifungu mbali mbali vya Agano Jipya husema ni kuzamisha (**Math 3:16** [*"Naye alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini"*]; **Yoh 3:23** [*"Yohana naye alikuwa akibatiza huko Ainoni, karibu na Salimu, kwa sababu kulikuwa na maji tele"*]; **Matendo 8:36-39** [Ili aweze kubatizwa towashi wa Kushi *"alitelemka majini"* baada ya kubatizwa *"alipanda kutoka majini"*]). Maandishi pekee ya kanisa, *Waraka wa Barnaba* (c. 70-131) na *Mchungaji wa Hermas* (c. 95-154) vile vile huzungumzia ubatizo kama "tunashuka majini" na "tuna panda juu" (*Waraka wa Barnaba* 1989: 11.11) na "tunashuka majini" (*Mchungaji wa Hermas* 1989: 31).
- Kunyunyiza au kumiminia. Wale wanaokubaliana na kunyunyiza au kumiminia maji wanahoji kwamba "ingawaje *baptizō* na asili yake humaanisha kuzamisha au kuchovywa majini, maneno hayo pia yametumika kumaanisha kuosha au kutakasa. Hivyo, yanapotumika maneno kama hayo basi hakuna mtindo wowote wa ubatizo unaoweza kukidhi kisawasawa." (Pipa 2003: 115) Wanaendelea kuhoji kwamba moja ya njia za msingi ambazo huzungumzia kuongoka ni kama kutakasa au kuosha kwa maji (ona **Ezek 36:25; Yoh 3:5; Tito 3:5-6**): "Waebrania 9:13, 19 inafundisha kwamba kuosha ilikuwa ni kwa njia ya kunyunyiza [ona pia **1 Pet 1:2** (*"kunyunyiziwa damu yake"*)]. . . . Hapo nyuma katika mstari wa 10, mwandishi huzungumzia maneno haya yahususo jadi ya utakaso ikitafsiriwa kuwa ni 'kuosha.' Neno hilo lina matumizi katika nomino *baptismos*. Uhusiano kati ya 'ubatizo' wa mstari wa kumi na jadi ya kunyunyiza katika mstari 13 na 19 unaonyesha uko wazi." (Ibid.: 124) Zaidi ya hapo, **Tito 3:5-6** anazungumzia kwamba uongofu wetu umewezeshwa na Roho Mtakatifu ambaye *"amemiminwa juu yetu"* Kwa kuwa ubatizo humaanisha kupigwa muhuri wa umoja wetu na Kristo, kupitia kazi ya Roho Mtakatifu, "mtindo [wa ubatizo] lazima uwe na dhana ile ya jadi ya utakaso (kunyunyiza) au angalau dhana ya kazi kuongoa ya Roho Mtakatifu (kumimina)" (Ibid.: 126). Ushahidi mwingine wa jambo hili, angalau kuhusiana na mahali ambapo kuzamisha haiwezekani, tunaupata katika miongozo ya *Didache* kwa kanisa (c. 70-110), ambayo inasema ubatizzo ufanywe katika "maji yanayotiririka. Lakini kama hakuna maji yanayotiririka basi batiza

katika maji mengine; na kama huwezi kubatiza katika maji baridi, basi fanya hivyo katika maji vugu vugu. Lakini kama huna hata hayo, basi mimina maji kichwani mara tatu." (*Didache* 1989: 7.1-3)

c. *Wazo la kuhitimisha kuhusu ubatizo.* Makanisa mengi huwa na tabia ya kumbatiza mtu kishapo husahau kuhusu jambo hilo. Lakini katika **Warumi 6** Paulo anawasihi Warumi kuachana na dhambi na kuishi maisha ya haki *kwa misingi ya ubatizo wao.* Kama ilivyotajwa hapo mwanzo, ubatizo ni ishara ya juu sana inayohusiana na maisha ya Kikristo. Kristo ndiye aliye amuru ukiwa ni moja ya kaida mbili alizozianzisha (**Math 28:19**). Hivyo, viongozi wa kanisa wanapaswa kuwaita watu wao katika nyakati tofauti, ili kuwakumbusha ubatizo wao ni vile unavyomaanisha, ya kuwa wametangaza wazi wazi kwamba wao ni wa Kristo na kanisa lake na hilo linamaanisha nini katika maisha yao. Makanisa mengine hufanya ibada maalum mara moja kwa mwaka ambapo washirika huzikiri tena ahadi zao za ubatizo, au wakati mtu anapobatizwa, washirika wengine wanakiri tena ahadi za ubatizo na kuahidi kumwombea yule anayebatizwa. Matendo ya namna hiyo husaidia kuliunganisha kanisa na kusaidia washirika kutafakari kuhusu maisha yao ndani ya Kristo

2. <u>Meza ya Bwana.</u> Meza ya Bwana (kama inavyotajwa katika Eucharist katika makanisa mengine[11]) ni kaida ya kanisa ambayo huendelea na hurudiwarudiwa. Kama ilivyo kwa ubatizo, Meza ya Bwana huonyesha kuwa mtu ni wa Kristo na pia inasema kitu fulani kuhusu asili ya Kanisa: "Wakati sote tunaposhiriki mkate mmoja, kanisa linatangaza wazi wazi na kijadi kwamba tu mwili mmoja na Kristo, washirika wake wote wakitenda kazi pamoja kwa ajili ya kujengwa kwa mwili wote. Jadi hii inafanyika kipimo ambacho kwacho tunapima ubora wa maisha yetu pamoja." (Leithart 2012: n.p.)

a. *Meza ya Bwana na kifo cha Yesu.* Yesu alianzisha Meza ya Bwana wakati wa "Chakula Cha Mwisho" (chakula cha Pasaka) (**Math 26:26-29; Marko 14:22-25; Luka 22:14-20; 1 Kor 11:23-26**). Katika chakula kile, Yesu aliufananisha mkate na mwili wake ambao ulikuwa karibu kuvunjwa, kikombe (mvinyo) kama damu yake ambayo ilikuwa imiminwe, na akasema tufanye hivyo *"kwa ukumbusho wangu"* (**Luka 22:19; 1 Kor 11:24-25**). Katika **1 Kor 11:26** Paulo anasema, *"Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo."* Haya ni maneno ya Yesu ambayo yaliianzisha Meza ya Bwana na uhusiano wake na Pasaka (ambayo ilikuwa ukumbusho wa malaika wa mauti "apiteye juu" ya Israeli na ilihusisha dhabihu ya mwana kondoo; ona **1 Kor 5:7**, *"Kwa maana Pasaka wetu amekwisha kutolewa kuwa sadaka, yaani, Kristo"*) inatuonyesha yafuatayo kuhusu kifo cha Yesu:

- <u>Umuhimu wa kifo.</u> John Stott anasema, "Mkate haukuwakilisha mwili wake uliokuwa hai, kama alivyokuwa pamoja nao mezani, lakini mwili wake kama ambavyo 'ungetolewa' kufa kwa ajili yao muda si mrefu. Vivyo hivyo, mvinyo haikuwa badala ya damu yake ambayo ilitiririka katika mishipa yake wakati akisema nao, lakini damu yake kama itakavyo mwagika muda mfupi ujao kwa ajili yao katika kifo. . . . Ilikuwa ni mauti yake ndiyo alitaka ikumbukwe kuliko kitu kingine chochote. Hapo sasa, ni salama kusema, hakuna Ukristo bila ya msalaba. Msalaba usipokuwa shina letu katika dini yetu, dini yetu si ya Yesu Kristo." (Stott 1986: 68)
- <u>Kusudi la Kifo chake.</u> Kutokana na **Math 26:28; Luka 22:20;** na **1 Kor 11:25** kikombe kiliwakilisha damu ya Yesu lakini katika Agano Jipya. Agano Jipya ndilo agano pekee ambalo Mungu ameahidi kutusamehe dhambi. (**Yer 31:34; Math 26:28**). Kifo cha Yesu kilikuwa "dhabihu ambayo iliahidiwa na Mungu ambayo kwayo agano jipya lenye ahadi ya kusamehe dhambi ingitekelezwa. Alikuwa anakwenda kufa ili awalete watu wake katika mahusiano ya kiagano na Mungu." (Stott 1986: 70)
- <u>Hitaji la kupokea kifo chake kibinafsi.</u> Kuula mkate na kukinywea kikombe ni kumchukua Yesu Kristo ndani yetu (ona **Yoh 6:53-58**). "Kama ambavyo haikutosha kwa mkate kumegwa na divai kumiminwa, bali iliwapasa kula na kunywa, vivyo hivyo haikutosha yeye kufa bali ilipasa kila mmoja binafsi afaidike na kifo chake. Kula na kunywa vilikuwa, na mpaka sasa ni, mfano uliowazi kabisa wa kumpokea Yesu kama

[11] Neno Ekaristi maana yake ni "shukrani." Holmes anasema, "Neno *eucharistia*, ambalo katika Agano jipya linatumika kwa maana ya kiujumla ya 'kushukuru' au 'shukrani' (mfano, Matendo 24:3; Fil. 4:6; 1 Thes 3:9), lilifanyika kuwa neno halisi la msingi la 'kutoa shukrani,' kwa jina Meza ya Bwana (cf. Ign. *Smyrn.* 6.2; Justin Martyr, *1 Apology* 65)" (Holmes 1989: 153-54n.29).

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

mwokozi wetu aliyesulubiwa na wa namna tunavyolishwa mioyoni mwetu na yeye kwa imani." (Stott 1986: 70)

b. *Maoni mbali mbali ya uhusiano wa Kristo na misingi ya Meza ya Bwana.* Kama ilivyo katika ubatizo, makanisa tofauti kwa kadiri ya itikadi zao yana uelewa tofauti wa uwepo wa Yesu kwa kuhusiana na elementi za (mkate na kikombe).[12] Kuna mitazamo mine hasa:

- Itikadi kwamba mkate na mvinyo hubadilika kuwa mwili na damu ya Yesu. Msimamo wa Kanisa Katoliki ni kwamba Yesu aliposema, *"Huu ndio mwili wangu"* (**Math 26:26; Marko 14:22; Luka 22:19; 1 Kor 11:24**), kile alichokuwa amekishika mkononi mwake "bado kilikuwa na *muonekano* wa mkate: 'spishi' hazikubadilika. Hata hivyo . . . *kiuhalisia* (vipande) vya mkate vilibadilika na kuwa vya mwili wake. Kwa maneno mengine, ilikuwa *hasa ni* mwili wake, ingawaje kwa kuonakwa macho na kwa ufahamu kiuhalisia dhahiri kila kitu kilikuwa bado kama kilivyokuwa mwanzoni, yaani mkate." ("Kubadilika kwa mkate na divai kuwa mwili na damu ya Yesu halisi" 2017: Kanisa Katoliki la Roma) Vile vile hata leo, kasisi anaposhirikisha Meza ya Bwana, vipande vya mkate na mvinyo inasemekana hubadilika na kuwa mwili na damu ya Yesu halisi, ingawaje "spishi" (muonekano wa nje) hubakia kama ulivyo.
- Muunganiko wa kisakramenti (imani kuwa damu na mwili wa Yesu Kristo upo pamoja na divai na mkate). "Walutheri huamini kuwa Mwili na Damu ya Yesu 'kwa hakika vipo kati yao, pamoja na ndani ya elementi za mkate na divai ambavyo vimewekwa wakfu, kiasi kwamba wanaoshiriki walapo na kunywa zile elementi papo hapo hula na kunywa mwili na damu ya Kristo mwenyewe katika Ekaristi ya Sakramenti uwe umemwamini Yesu au la. Fundisho la Walutheri la Uwepo Halisi hujulikana pia kama muunganiko wa kisakramenti [imani kuwa damu na mwili wa Yesu Kristo upo pamoja na divai na mkate]." ("Eucharist in Lutheranism" 2017: Beliefs)
- Uwepo wa kiroho. Makanisa ya uamsho (Wapresbiteri na wengine wenye mizizi kutoka kwa John Calvin) wanafundisha kuwa "mwili na damu ya Kristo viko pale kwenye sakramenti, lakini uwepo huu huwasilishwa kwa njia ya kiroho badala ya kwamba mwili wake kuwa tunaula kiuhalisia. Anakuwepo kwa Roho wake wakati mtu anapokula na kunywa kwa imani, Hivyo, katika Meza ya Bwana waamini huhisi, hufurahia na kushuhudia kwamba Kristo yuko nao na yu hai; hivyo, ni hakika ni "ushirika" na yeye. Fundisho hili la wana uamsho la uwepo halisi wakati mwengine huitwa uwepo uliofichika au uwepo wa kiroho halisi." ("Lord's Supper in Reformed theology" 2017: Introduction) Hii hasa ndiyo namna ambavyo makanisa ya Anglikana na Wamethodisti pia wanaamini.
- Mtazamo wa kumbu kumbu. "Mtazamo mwingine ambao unashikiliwa na madhehebu ya kiprotestanti ni kwamba elementi za mkate na divai (au juisi) katika ekaristi (ambayo mara nyingi ikimaanisha Meza ya Bwana) huwa ni ishara tu zinazosimama badala ya mwili na damu ya Yesu, chakula kikiwa kimekusudiwa kuwa kwa ajili tu ya ukumbusho. Neno hilo hutoka katika Luka 22:19: 'fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu' na tafsiri ya mhudumu kwamba kusudi kubwa la Meza ya Bwana ni kumsaidia mshiriki *kumkumbuka*

---

[12] Maombi ya Ekaristi ya zamani zaidi yameandikwa katika *Didache* (c. 70-110) kama ifuatavyo:

"9. Sasa kuhusiana na Ekaristi, shukuru kama ifuatavyo: Kwanza, kuhusiana na kikombe: Tunakushukuru, Baba yetu, kwa ajili ya mzabibu mtakatifu wa Daudi mtumishi wako, ambao umetujulisha kupitia kwa Yesu, mtumishi wako; utukufu una wewe milele.

Na kuhusiana na mkate uliomegwa: Tunakushukuru, Baba yetu, kwa ajili ya uzima na ujuzi uliotupa kupitia Yesu, mtumishi wako; utukufu ni wako milele. Kama vile huu mkate uliomegwa ulivyotawanyika juu ya milima na kisha ukakusanywa na kuwa mmoja, vivyo hivyo na kanisa lako likusanywe kutoka miisho yote ya dunia katika ufalme wako: kwa kuwa utukufu ni wako na nguvu kupitia Yesu kristo milele.

Lakini asiwepo atakayekula au kunywa Ekaristi yako ispokuwa wale waliobatizwa kwa jina la Bwana, kwa kuwa Bwana amesema pia kuhusu jambo hili: Usiwape mbwa kilicho kitakatifu.'

10. Mtakapokuwa mmetosheka, shukuruni kama ifuatavyo: Tunakushukuru, Baba Mtakatifu, kwa ajili ya jina lako takatifu ambalo umelisababisha liingie ndani ya mioyo yetu, na kwa ajili ya ujuzi na imani na hali ya kutokufa ambayo umetujulisha kupitia Yesu mtumishi wako; utukufu ni wako milele.

Wewe, Bwana mwenye nguvu zote, muumbaji wa vitu vyote kwa ajili ya jina lako, na umewapa watu vinywaji na chakula wavifurahie, ili wakushukuru; lakini kwetu sisi kwa neema umetupa chakula na kinywaji cha kiroho, na uzima wa milele kwa kupitia mtumishi wako. . . ." (*Didache* 1989: 9.1-10.3) Kwa uchache, hii inaonyesha fundisho la Kanisa Katoliki kwamba 'mkate na divai hubadilika kuwa mwili na damu ya Yesu halisi' lilikuja baadae.

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

Yesu na dhabihu yake msalabani." ("Memorialism" 2016: n.p.) Maneno ya Kristo wakati alipokuwa akianzisha kaida hii hakuwa akisema kwamba mwili wake ulikuwepo Dhahiri katika mkate na divai au kwamba mkate na divai vilibadilishwa kuwa mwili wake, kwa kuwa alikuwa katika mwili wake bado mbele ya wanafunzi, na kabla ya kupaa kwake na kumiminwa kwa Roho Mtakatifu siku ya Pentekoste haukuweza kuwepo kila mahali kwa wakati mmoja, badala yake maneno yake yalikuwa yanatambua kutokuwepo kwake na kuwataka wanafunzi wake wakumbuke mauti yake na kusubiri ujio wake tena (tumaini). Huu ndio msimamo wa Wabaptisti, Makanisa ya Kiinjili na Wapentekoste.

c. *Fikra hitimisho kuhusu Meza ya Bwana.* Kushiriki kwetu katika Meza ya Bwana humaanisha: (1) *Tunakumbuka* kifo cha Kristo (**Luka 22:19; 1 Kor 11:24-25**); (2) *Tunatangaza* mauti ya Kristo (**1 Kor 11:26**); (3) *Tunamsherehekea* Kristo, ushirika wetu na yeye, na uwepo wake na sisi; (4) *Tunatarajia* kurudi kwa Kristo na hatimaye kula karamu katika uwepo wake (**Math 26:29; Marko 14:25; Luka 22:16, 18; 1 Kor 11:26;** ona **Ufu 19:7-9**); and (5) *Tunasherehekea na kuonyesha* ushirika wetu na waamini wengine (**Luka 22:17; 1 Kor 10:16-17**).

Makanisa hutofautiana katika namna wanavyosherehekea Meza ya Bwana kuhusiana na mara ngapi tukio hilo hufanyika (wengine kila wiki, wengine kila mwezi, na wengine kwa vipindi tofauti). Bila kujali ni mara ngapi Meza ya Bwana husherehekewa, kwa sababu ya umuhimu wake, Paulo anatuambia kwamba tunahitaji "kujihoji wenyewe" ili tushiriki kwa namna "ya kustahili" na si "kula na kunywa hukumu" yako (**1 Kor 11:27-29**). Kujihoji huko kuhusishe: (1) Je mimi ni mwamini? (2) Je kuna dhambi ambayo haijatubiwa maishani mwangu? (3) Ja nina mahusiano mazuri na washirika wote katika mwili wa Kristo na watu wengine kwa ujumla? Tukiichukulia Meza ya Bwana kwa kumaanisha, inaweza kuwa kama namna ya neema ya Mungu ituletayo karibu na yeye.[13]

## III. Kanisa: Misheni na Kusudi lake—Utangulizi

### A. *Kanisa lipo kwa neema ya Mungu kwa ajili ya utukufu wa Mungu*

1. Mungu ametuokoa kupitia Kristo na kuanzisha kanisa kwa neema peke yake (**Math 16:18; Yoh 1:14-17; Rum 3:21-24; 5:14-21; 8:29-30; 11:5-6, 36; 1 Kor 15:10; Efeso 1:5-6, 18-23; 2:8-10; 3:1-7; Kol 1:13-23; 2 Thes 2:16-17; 1 Tim 1:12-15; 2 Tim 1:8-11; Tito 2:11; 3:5-7; Ebr 2:9**).
2. Hatima kuu ya kanisa ni kumtukuza Mungu (**Isa 43:7; 44:23; 46:13; Math 5:16; Yoh 5:44; 12:27-28; 14:13; 17:22-24; Rum 11:36; 15:7-9; 16:27; 1 Kor 6:19-20; 10:31; Efeso 1:3-14; 3:21; Fil 1:9-11; 4:20; 1 Tim 1:17; 2 Tim 4:18; 1 Pet 2:12; 4:11; 2 Pet 3:18; Yuda 25; Ufu 1:6**).

### B. *Maisha ya mkristo—na hatimaye maisha ya kanisa—ni kamili*

Yesu alisema, *"Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu, mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele."* (**Yoh 10:10**). Yesu anatuambia kuwa "kuna njia moja tu ya kupata uzima wa milele . . . chanzo kimoja tu cha maarifa ya Mungu, chemchemi moja tu ya kurutubisha kiroho, msingi mmoja wa usalama wa kiroho—Yesu peke yake" (Carson 1991: 385). Uzima wa milele ambao Yesu anatoa "si muda wa ziada kuishi na kujaza (yaani tu 'maisha ya milele'), lakini maisha ambayo haiwezekani kuyafikiria kwa jinsi yalivyo bora, maisha yafaayo kuishi". Kwa maneno mengine, uzima wa milele huanza sasa. Uzima wa milele si tu maisha yale ambayo huendelea milele bali ni maisha ya *aina* tofauti. Ni maisha kama ya Yesu. Maisha ya Yesu hayaishii pale tu ambapo watu hufikiria kuwa ni mambo ya "kiroho" tu kama (maombi, kusoma Biblia, nk.). Bali, Yesu alidhihirisha kuwa maisha yaliyo kweli, maisha ya utele anayotupa, ni kamili na yanahitajika katika kila eneo la maisha. Kama mwandishi mmoja anavyosema, "Yesu alitembea huko na huko akiishi maisha ya utele mbele ya kila mtu. Katika maisha yake aliachana na hali ya kujitwalia madaraka na hali ya kujiona kwa kuona mahitaji ya wengine. Yesu alithibitisha kwa mtazamo wa maisha kama huu hutengeneza njia ya kuyafikia maisha ya utele." (McNeal 2009: 31) Baada ya kuwaosha wanafunzi wake miguu, Yesu alisema, *"Nimewapa kielelezo ambacho mnapaswa kukifuata"* (**Yoh 10:15**). Mfano wa Yesu wa maisha tele unapaswa kutenda kazi katika maisha ya kila mmoja anayemfuata.

Kwa kuwa kanisa lote ni 'mwili wa Kristo' (**Rum 12:5; 1 Kor 12:12-27; Efeso 3:6; 5:23; Kol 1:18, 24**), Mfano wa Yesu wa maisha tele unahusu kanisa lote kama kitu kizima. Jonathan Dodson anasema, "Tunapoongoka kuwa wa *Yesu*, tunaongoka *kuwa wa kanisa lake*. . . . Tunapoifikiria injili, kimsingi tunafikiria

[13]Muhtasari wa maoni ya kihistoria ya asili ya kanisa na sakramenti vimeambatanishwa kama **KIAMBATISHO 1—HISTORIA YA MAFUNDISHO: ECCESIOLOGI**.

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

kuhusu kuongoka kwa mtu mmoja. Kinyume chake, Biblia huonyesha kuongoka kama tukio la watu kijumuia au kijamii. . . . Tunapompokea Kristo kama Bwana na Kichwa (Kol. 2:6), mara hiyo hiyo tunashikamanishwa na mwili wake (Kol. 1:18; 2:2). . . . Jamii ambayo kiini chake ni Yesu ni jamii inayovutia—jamii inayotia moyo, inayosamehe, inayohudumia, yenye upendo na inakaribisha wasio Wakristo kujiunga na jamii hii. Injili hupatanisha watu na Mungu na wao kwa wao, na kuunda jamii mpya ya kipekee ambayo ina tamaduni na lugha mbali mbali na kuunda jamii moja (Kol. 2:15). . . . Tunapoisha kama kanisa sisi kwa sisi, tunaudhihirisha utawala wa Yesu wenye neema na unaokomboa duniani. Utawala wa Yesu unaokomboa unapopata nafasi katika dunia hii, kanisa linakua kufikia kimo cha Kristo." (Dodson 2012: 109-110, mkazo kwenye nakala ya asili)

**C.** ***Mungu anatukuzwa kwa imani yetu ambayo huonekana kwa matendo ya upendo kwa Mungu na kwa watu wengine***

1. <u>Imani ni mwenendo ambao kwa kiwango kikubwa humtukuza Mungu kwa sababu, kwa tafsiri, imani hukufanya usijitazame wewe bali umtazame Mungu.</u> *"Pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu"* (**Ebr 11:6**). *"Na kila tendo lisilotoka katika imani ni dhambi*" (**Rom 14:23**). Imani ni hali ya kumtegemea Mungu kikamilifu bila shaka katika nyanja zote za maisha yetu (**Waebrania 11**). Imani na kumtegemea Mungu huleta maana maishani mwetu, kusudi, na utoshelevu ndani yake, na si katika vitu vya dunia hii (ona **Fil 4:10-13; Ebr 13:5-14**). Kama anavyosema John Piper, "Mungu hatukuzwi ndani yetu tunapokuwa katika kiwango cha juu cha kuwa tumeridhika ndani yake" (Piper 2003: 288).

2. <u>Imani sahihi siku zote hudhihirika kwa njia ya utii kwa Mungu (**Math 7:13-27; Yoh 14:21-24; 15:1-11; Yak 1:22-2:26**), na imani sahihi na utii wa kweli kwa Mungu utajidhihirisha kwa njia ya upendo kwa Mungu na watu wengine.</u> Kinachofanya hili liwe kweli ni kwa sababu upendo unatoka kwa Mungu kwa sababu Mungu ni upendo (**1 Yoh 4:7-8, 16**) na sisi tunapaswa kuwa kama yeye (**Rum 8:29; 1 Kor 15:49; 2 Kor 3:18**). Kwa hakika, *"Sisi twapenda kwa maana alitupenda sisi kwanza"* (**1 Yoh 4:19**; see also **Efeso 5:2**). "Ikiwa yeyote atauliza, 'Ni kwa namna gani upendo wa Mungu unasababisha wewe kuwapenda wengine?' jibu ni: Kuzaliwa upya ndiko kunaleta huo muunganiko. Kuzaliwa upya ni tendo la Roho Mtakatifu la kuunganisha mioyo yetu iliyokufa, na ya ubinafsi na Mungu aliye hai, mwenye upendo ili kwamba maisha yake yawe maisha yetu na upendo wake uwe upendo wetu." (Piper 2009: 157) Kwa hiyo, upendo huu ndio kipimo cha msingi au ishara kama ni kweli mtu ameokoka au hapana. Jinsi upendo ulivyo kiini katika mahusiano ya Kikristo, kwa kanisa na kwa Ukristo wenyewe inaonekana katika namna zifuatazo:

- Yesu alisema amri mbili, *"Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote,"* na *"Mpende jirani yako kama nafsi yako,"* ndio msingi wa Biblia yote (**Math 22:36-40; Marko 12:28-34; Luka 10:25-28**).
- Mtume Yohana alisema *"Yeye asiyependa, hakumjua Mungu"* (**1 Yoh 4:8**), and *"Mtu akisema, nampenda Mungu, naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo; kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona, hawezi kumpenda Mungu ambaye hakumwona"* (**1 Yoh 4:20**). Kwa hivyo, tunafanyaje "amri ya pili" (inamaanisha, namna tunavyowapenda watu) ni ushahidi na kipimo cha kama kweli tunatekeleza "amri ya kwanza" (yaani, kumpenda Mungu).
- Upendo umeunganishwa na msamaha wa dhambi zetu (**Luka 7:36-50; 1 Pet 4:8**).
- "Lengo" la fundisho la Kikristo ni *"upendo utokao katika moyo safi na dhamiri njema, na Imani isiyo na unafiki"* (**1 Tim 1:5**).
- Sheria yote imetimizwa katika tamko, *"mpende jirani yako kama nafsi yako"* (**Rum 13:8-10; Gal 5:14**).
- Usiku ule kabla hajafa, "amri mpya" ambayo Yesu aliwapa wanafunzi wake ilikuwa *"Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo."* (**Yoh 13:34; 15:17**).
- *"Upendo wa mmoja kwa mwingine"* ni ishara pekee ambayo Yesu aliitoa ambayo kwayo *"watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu"* (**Yoh 13:35**).
- Upendo ni *"njia iliyo bora"* (**1 Kor 12:31**). Ni mkuu kuliko Imani na tumaini (**1 Kor 13:13**). Endapo mtu hana upendo, yeye "si kitu" hata aseme kwa lugha za wanadamu na malaika, awe na karama ya unabii, awe na maarifa yote, na awe na Imani kiasi cha kuhamisha milima (**1 Kor 13:1-2**). Kama hana upendo, "hapati kitu" hata akitoa vitu vyake vyote kuwasaidia masikini na hata autoe mwili wake wote uchomwe moto (**1 Kor 13:3**).
- *"Kupendana kwa juhudi nyingi"* kuonekane *"zaidi ya yote"* (**1 Pet 4:8**).
- Upendo ni wa kwanza katika "tunda la Roho" lililoorodheshwa katika **Gal 5:22-23** na kulielezea "tunda la Roho" kwa ufupi (kimsingi, "tunda la Roho" ni umoja, sio wingi).
- Upendo ni *"kifungo cha ukamilifu"* ambao yapasa udhihirike juu ya vingine vyote (**Kol 3:14**).

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

- Maandiko huuita upendo *"sheria ya kifalme"* (**Yak 2:8**).
- Kilele cha upendo ni kujitoa dhabihu: *"Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake"* (**Yoh 15:13**).
- Sheria ya upendo ni ya kimatendo: *"Basi yoyote mtakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo; maana hiyo ndiyo torati na manabii"* (**Math 7:12; Luka 6:31**).
- Mtume hakuacha kuhimiza waaminio kuhusiana na umuhimu wa upendo na kuhimiza kwamba wapendane wao kwa wao zaidi na zaidi (**1 Kor 8:1; 16:14; 2 Kor 2:8; 8:24; Gal 5:6, 13; Efeso 3:17-19; 4:2, 15; 5:2, 25, 28; Fil 2:1-2; Kol 2:2; 3:14; 1 Thes 3:12; 4:9; Fil 9; Ebr 10:24; 1 Pet 2:17; 4:8; 2 Pet 1:7; 1 Yoh 4:7-11; 2 Yoh 5**).

Tunapofikiria kuhusu misheni na kusudi la kanisa katika muktadha wa upendo tunatakiwa: (1) tulifikirie kanisa katika muktadha wa *kimahusiano*; na (2) kuzingatia si tu *kile ambacho* kanisa linatakiwa kufanya lakini *kwa namna gani* kanisa lifanye.

### D. *Misheni nne za msingi na makusudi ya kanisa*

Zifuatazo ni misheni nne za msingi na makusudi ya kanisa ambavyo vimekusudiwa viwe na mahusiano na vyote ni kwa kusudi la kuionyesha imani yetu na kumwinua na kumtukuza Mungu:

1. Kumwabudu Mungu. Kuabudu *huakisi* neema na upendo wa Mungu kwake Mungu. Kuabudu kimsingi si matendo fulani lakini ni mwenendo wa maisha unaohusisha yote tufanyayo maishani.
2. Kufunza waaminio kuwa wanafunzi. Kufunza waaminio wawe wanafunzi *hutumia* neema na upendo wa Mungu kwa mwili wa Kristo. Kufunza waaminio kuwa wanafunzi huhusisha maendeleo na asili ya mwamini katika nyanja zote za maisha ya mwamini, "kiroho" na vinginevyo.
3. Misheni kwa wasioamini. Misheni (huduma, kuwaendea wasioamini) *hupeleka* neema na upendo wa Mungu kwa wale ambao bado hawajaamini.
4. Umoja (ukamili). Umoja na u-kamili *hutambulisha* kanisa kama chombo ambacho kina afya ya kuweza kupokea neema na upendo wa Mungu na kuupeleka kule unakotakiwa kwenda. Kuonyesha upendo na u-kamili ni ishara muhimu kwamba kanisa kweli linamwabudu Mungu, huku likiadibisha watu wake, na ya kuwa kweli liko katika misheni ya Mungu duniani.

## IV. KUABUDU

Wito na kusudi la kanisa hupatikana katika kumwabudu Mungu. **Zab 29:2** inatuita kuabudu: *"Mpeni Bwana utukufu wa jina lake; Mwabuduni Bwana kwa uzuri wa utakatifu"* (ona pia **Zab 96:7-9**).

### A. *Kimsingi kuabudu ni hali ya ndani ya kiroho ambayo hugusa kila eneo la maisha yetu na sio tu matendo fulani ya nje*

"Kilicho lazima, muhimu, kisichoweza kuwa badala ya kingine, kinachotafsiri moyo wa kuabudu ni ile hali ya *kutoshelezwa na Mungu ndani ya Kristo*. Kiwango hiki cha uzoefu hukuza thamani yake kwetu, na hali hiyo ya ukuzwaji ndiyo kuabudu. . . . Kuabudu si tendo alifanyalo mtu kwa nje kwanza; ni hali ya ndani ya kiroho inayothamanisha uungu na njia za Mungu ndani ya Kristo. Ni kumfurahia Kristo, ni kutoshelezwa na vile vyote alivyo Mungu kwa ajili yetu ndani ya Kristo. Vitu hivi vinapokosekana, hakuna kuabudu, hata kama kuwe na mitindo mbalimbali mingineyo inayojionyesha kwa nje." (Piper 2010: 250-51, mkazo kwenye nakala ya asili)

1. Kiini cha Kuabudu ni Mungu na Kristo. Kuabudu ni *mwitikio* wetu wa Mungu ni nani kwetu, amefanya nini, anafanya nini, na atafanya nini. Asili ya kuabudu ni kutoshelezwa na Mungu ndani ya Kristo (ona **Zab 32:11; 37:4; 42:1; 100:2; Fil 1:20-21; 4:4, 10-13; Kol 3:4**).
   a. *Kiini cha ibada kwa Mungu kule mbinguni ni:* Mungu ni nani (utukufu wake; asili yake ya kushangaza), na kile alichofanya Mungu kupitia Kristo, anafanya, atafanya (uumbaji; wokovu; utawala wake; hukumu yake ijayo)—ona **Isa 6:1-8; Ufu 4-5; 7:9-17; 11:15-19; 15; 19:1-6**.
   b. *Mambo yale yale*—Asili ya Mungu na matendo yake—ndio kiini cha kuabudu katika zaburi kuu za kuabudu (ona **Zaburi 8; 19; 24; 29; 33; 46-48; 63; 65-68; 76; 84; 87; 92; 93; 96-100; 103; 104; 111; 113; 115; 117; 135; 145-150).**
   c. Kuabudu kutadumu milele kwa sababu Mungu adumu milele.
2. Kuabudu humtukuza Mungu na hutusaidia sisi kubadilishwa kuwa katika sura ya Kristo.
   a. *Mungu ndiye mwenye viwango vya juu na vilivyo bora zaidi vya sifa njema*—utakatifu, wema, upendo, kweli, hekima, haki, huruma, neema, uaminifu, nk.
   b. *Watu huthamini kile wanachokisifu.* "Tukimsifu Mungu kwa haki yake, tunaizawadia haki. Tukimsifu kwa ajili ya rehema zake, tunatunza rehema. Tunapomsifu Mungu kwa ajili ya ubora huu, tunathamanisha ubora wake na sisi wenyewe tunavutwa na ubora huo." (Doriani 2001: 92)

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

**B.** ***Kuna dhana pana ya kuabudu (yaani, kuishi kwa ajili ya Mungu na kumtumikia katika nyanja zote za maisha yetu) na maana finyu ya kuabudu (yaani, kukutanika pamoja kama kundi ili kumwabudu Bwana)***

Hizi maana mbili zinahusiana—*kumwabudu kwetu Bwana kwa maana iliyo finyu kutakuwa ni bure endapo hakutaunganika na kuabudu kule kwa maana iliyo pana* (ona **1 Sam 15:22-23; Zab 51:14-17; Isa 1:11-17; 29:13-16; Yer 6:16-20; 7:21-26; Ezek 16:48-50; Hos 6:6; Mika 6:6-8; Math 12:1-8; 15:5-9; 23:23; Marko 12:28-33; Luka 6:6-10; Rum 12:1; Kol 3:23-24; Yak 1:27**).

1. <u>Kuabudu kwahusisha maeneo yote ya maisha yetu na utu wetu.</u>

a. *Kuabudu kwa kweli huhusisha maisha yetu yote, na sio tu tukio la siku ya Jumapili.* Mwenendo wa kuabudu kwetu wapaswa uathiri mtazamo wetu kuhusu watu na maeneo mengineyo ya maisha yetu (ona **Yoh 4:21-24; Rum 1:9-10; 12:1; Fil 3:3**). Rick Warren anasema, "Mara kwa mara twapata changamoto ya kufanya *'vitu vikubwa'* Kwa ajili ya Mungu. Kwa kweli, Mungu hupendezwa Zaidi tunapofanya mambo madogo kwa ajili yake kwa utii utokanao na upendo wetu kwake. Inawezekana wengine wasione, lakini Mungu anaona na kuyatambua hayo kama matendo ya ibada. Fursa kubwa zaweza kuja mara moja katika mhula wa maisha yetu, lakini fursa ndogo hutuzunguka kila siku ya maisha yetu. Hata kwa matendo madogo kama kusema kweli, kuwa mwema, na kuwatia moyo wengine, twaupa uso wa Mungu tabasamu. Mungu anathamini matendo ya kawaida ya utii kuliko maombi yetu, sifa na sadaka. Biblia yatuambia, *'Ni nini kinachompendeza Mungu zaidi: sadaka za kuteketeza na dhabihu au kuiutii sauti yake? Kutii ni bora kuliko kutoa dhabihu'* [**1 Sam 15:22**]." (Warren 2002: 96, mkazo kwenye nakala ya asili) Tabia hii inaelezewa vizuri katika **1 Kor 10:31** ambayo inasema, *"Basi, mlapo, aumnywapo, au mtendapo neno lolote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu"* (ona pia **Efeso 5:18-20; 6:7; Kol 3:17, 23**). John Piper anafupisha, "Agano Jipya hutumia sentensi zile zilizo kuu kati ya sentensi za kuabudu [**1 Kor 10:31; Kol 3:17**] bila hata ya kutaja ibada za kuabudu. Huyaelezea maisha. . . . Kwa kweli, maneno ya msingi ni 'kila wakati' na 'na kwa mambo yote''—'kushukuru *wakati wote* na *kwa mambo yote*' [**Efeso 5:20**]. Hivi ndivyo kwa kweli tungepaswa kufanya katika ibada, lakini huu si mzigo wa Paulo kutuambia hayo. Mzigo wake ni kuinua ari kubwa, hali halisi ya kutoka ndani ya kuabudu na ambayo inatuzunguka na kutuzingira katika kila eneo la maisha." (Piper 2010: 245)

b. *Kuabudu halisi kunahusisha kila Nyanja ya kuishi kwetu (kichwa na moyo; ufahamu, hisia, na utashi).* Ibada ya kweli kwa Mungu ni *"katika roho na kweli"* (**Yoh 4:21-24**).

(1) <u>"Roho"</u> inaonyesha kwamba ibada inapaswa kuhusisha mioyo yetu, hisia, na roho tunapowezeshwa na kuja kuabudu na Roho Mtakatifu (ona **Math 15:8-9; 1 Kor 14:25**).

(2) <u>"Kweli"</u> inaonyesha kwamba kiini cha kuabudu kinapaswa kuwa ni injili na Neno (Biblia), kwa sababu Mungu analiinua Neno lake na amejifunua kwetu kupitia Neno aliyefanyika mwili (Yesu) na katika Neno lake lililoandikwa (Biblia), ambalo ndilo kweli (**Zab 119; 138:2; Yoh 1:1-14; 14:6; 17:17; Efeso 1:13; 1 Tim 2:15; 3:16-17; Ebr 1:1-2; Yak 1:18**).

2. <u>Kuabudu humuonyesha Mungu kujitoa kwetu kwake katika njia zote alizoziamuru.</u> Hivyo, tunamwabudu Mungu kwa:

a. *Kuimba* (**Zab 47:67; 95:1-7; 96:1-10; 98:1-6; Marko 14:26; 1 Kor 14:26; Efeso 5:18-19; Kol 3:16; Ufu 5:8-10**).

b. *Kumsifu* (**Zab 111:1-10; 112:1; 135:1-4; 144:1-150:6; Luka 24:52-53; Matendo 2: 46-47; Rum 15:7-13; Ebr 2:11-12; 13:15; 1 Pet 4:11; Ufu 4:8-11; 5:11-14; 7:9-14; 19:4-6**).

c. *Kuungama na kutubu dhambi.* Kumuinua Mungu kutuongoze kwenye ufahamu uliosahihi kuhusiana hali yetu ya dhambi. Hali hiyo itupeleke katika toba ya kweli na kisha uhakika wa msamaha (ona **34:18; Zab 51:16-17; Isa 6:3-7; Luka 5:8; 2 Kor 7:9-11; Yak 5:16; 1 Yoh 1:5-9; Ufu 5:2-5**).

d. *Meza ya Bwana* (**1 Kor 10:16-17; 11:23-26**).

e. *Kusoma, kuhubiri, na kufundisha neno lake* (**Matendo 2:42; 5:42; 1 Kor 14:19; 2 Kor 4:5; 1 Tim 4:6, 11, 13, 16; 6:2b; 2 Tim 2:2; 3:16-17; 4:1-4; Tito 2:1**).

f. *Maombi* (**Matendo 1:14; 2:42; 1 Timotheo 2**).

g. *Kutoa* (**1 Kor 16:1-2; 2 Wakorintho 8-9**).

h. *Mwitikio wa maisha ya kujidhabihu* (**Yoh 10:27; 15:8; Rum 12:1; Efeso 2:8-10; 4:11-5:21; Kol 1:9-10; 2:6-7; 3:23-24**).

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

## V. KUFANYA WANAFUNZI

- Neno la Kiyunani "mwanafunzi" ni *mathētēs.* "*Mathētēs* yamaanisha zaidi katika AJ kuliko tu mwanafunzi au ajifunzae. Ni ufuasi wa uaminifu unaokubali maagizo yaliyotolewa kwako na kuyafanya mfumo wa maisha yako." (Zodhiates 1993: *mathētēs,* 936)
- "Maana ya Yesu ya mwanafunzi inahusisha mambo matatu ambayo ni busara, uhusiano na utume. Mambo haya hudhihirishwa kupitia kuhubiriwa kwa injili ya kweli (busara) ndani ya mahusiano ya kila siku ya upendo (uhusiano) kwa agenda ya neema ya kuwabatiza watu kwa jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu (utume). *Kwa hiyo, mwanafunzi wa Yesu ni mtu anayejifunza injili, anayejihusisha na injili, na kuwashirikisha wengine injili.* Kwa kifupi, kiini cha maisha ya wanafunzi ni injili." (Dodson 2012: 37-38, emph. in orig.)
- "Mwanafunzi ni yule: Anayemfuata Kristo (kichwa). Mwanafunzi amemkubali Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa maisha yake. . . . Anaendelea kubadilishwa na Yesu (moyo). Yesu alisema tutautambua mti kwa matunda yake (ona Mathayo 7:17-20). Hakumaanisha matunda yaliyokamilika; Alimaanisha matunda yanayokua. Tunapoendelea kumfuata Yesu, anatubadilisha utu wa ndani—Anabadilisha hadhi yetu. Tumejitoa katika wito wa Yesu kuokoa watu kutoka katika dhambi yao (mikono). Yesu alituokoa kwa kusudi maalum. . . . Sasa wito wa Mungu ni wito wetu, na tunatambua kwamba tunahusika katika kipindi chetu cha historia. Mikono yetu ipo kwa ajili ya utumishi wake. . . . Ni kazi na heshima ya kila Mkristo kuwa mwanafunzi wa Yesu, na ni wajibu wa kila kanisa kuwafanya watu kuwa wanafunzi." (Putnam 2010: 32-33, 35)
- "Kufanya watu kuwa wanafunzi ni uhusiano wa makusudi ambao tunaufanya kwa kwenda sambamba na wanafunzi wengine ili kuwatia moyo, kuwajenga na kupeana changamoto kila mmoja kwa mwenziwe katika upendo ili kukua na kukomaa katika Kristo. Hii ni pamoja na kuwafunza wanafunzi ili na wao wawafunze wengine." (Ogden 2007: 4n.5)
- "Unapowafanya watu kuwa wanafunzi, hatimaye utakuwa na kanisa. Lakini unapotengeneza kanisa, si rahisi kupata wanafunzi. . . . Yapasa tuelewe kuwa kanisa ni *matokeo* ya uanafunzi na sio linalosababisha uanafunzi. Ikiwa umeamua kujenga kanisa, hakuna uhakika kama utakuwa na wanafunzi. Ni Dhahiri kwamba utatengeneza watu tegemezi ambao hutegemea, kupata huduma za kiroho ambazo hutolewa na watu wa kidini wenye taaluma hiyo." (Breen 2011: 11)
- "Ubora wa kanisa lako ni wanafunzi wake. Mziki mzito, mahubiri ya kusisimua, hali ya kuvutia ya majengo na mpangilio mzuri wa vipindi kamwe havifanyi kanisa kuwa la kustahili kusifika endapo wanafunzi wake ni wapokeaji tu na hawajihusishi na kazi kubwa ya kuwafanya wengine kuwa wanafunzi. Lakini ikiwa wanafunzi kanisani mwako wamewezeshwa na wanajihusisha na umisheni, hapo kanisa lako lina nguvu na lenye afya. . . . Mambo yamefanyika kinyume kwa muda mrefu sasa. Lazima tugeuze huo utaratibu. Tunafikiri ili tuwe na wanafunzi wazuri ni kuwa na makanisa yenye mifumo mizuri zaidi, wakati kwa kweli namna ya kuwa na makanisa mazuri zaidi ni kuwa na wanafunzi bora." (Cole 2011: n.p.)
- "Ndani ya kundi la kanisa lenye afya, kuabudu hupeleka watu kwenye uinjilisti, kisha kwenye kufunza wanafunzi. . . . Uinjilisti sharti ufanywe kwa namna ambayo itawaingiza waongofu kanisani, mahali ambapo kazi ya kuwafunza yaweza kufanyika. . . . Uinjilisti usipofanyika kwa kuhakikisha waongofu wapya wanajiunga na kanisa la mahali, utakuwa sawa na kumsaidia mtu kuzaa mtoto na baadae kukiacha kichanga peke yake kwenye baridi bila uonazi. . . . Maneno muhimu: Kusudi halisi la uinjilisti katika muktadha wa Agizo Kuu, kufanya watu kuwa wanafunzi." (Colson 1992: 343-45, mkazo kwenye nakala ya asili)

### A. *Msingi wa maandiko*

Wito na kusudi la kanisa huonekana katika kuwaandaa watakatifu kwa ajili ya kazi ya huduma—kwa maana nyingine, watu kufanywa kuwa wanafunzi. Kifungu cha msingi kinachoelezea kipaumbele hiki kikuu cha kanisa ni **Efeso 4:11-16:** ***11****Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na walimu;* ***12****kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe;* ***13****hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufikia kwenye cheo cha kimo cha Kristo;* ***14****ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku na kila upope wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja,tukizifuata njia za udanganyifu.* ***15****lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo.* ***16****katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo* (ona pia **Rum 8:29; Kol 1:28-29; 1 Thes 3:11-13; 2 Tim 2:2; 1 Yoh 2:3-6**).

Katika vifungu mbali mbali, Yesu aliwaita watu wamfuate kama wanafunzi wake na akaeleza maana ya wao kuwa wanafunzi (ona **Math 4:18-22; 5:3-16; 10:24-25; 12:46-50; Marko 3:31-35; Luka 6:40; 8:19-21;**

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

**9:23-24, 57-62; 14:25-33; Yoh 8:31-32; 13:34-35; 15:1-8, 18-20**).

**B.** ***Msingi wa kufanya wanafunzi: injili***

Mungu ni mtakatifu, atendaye haki, mwenye haki, na mwema (**Mwz 18:25; Kut 34:6-7; Law 11:44; Ayubu 34:10-12; Zab 5:4; 136:1; 145:17; Hab 1:13; Rum 1:18; Yak 1:13**). Ingawaje wanadamu wa kwanza (Adamu na Hawa) waliumbwa bila ya dhambi, walichagua kumfuata shetani na kumwasi Mungu na hivyo wakawa wenye dhambi (**Mwz 3:1-19**). Matokeo yake, kila mwanadamu tangu Adamu na Hawa amezaliwa katika hali ya upotovu ijulikanayo kama dhambi ya asili; hii dhambi ya asili ni "sheria" au nguvu ambayo inafanyakazi ndani ya kila mtu (**Rum 7:5, 8-11, 14-24; Gal 5:17; Ebr 3:12-13**). Matokeo yake ni dhambi ambazo zimekubalika duniani kote kadiri maisha yanavyoendelea (**Mwz 8:21; Zab 51:5; 143:1-2; Yer 17:9; Marko 7:20-23; Rum 3:9-18, 23; 5:12-14; 7:14-24**). Biblia inasema waziwazi matokeo ya hili: *"mshahara wa dhambi ni mauti"* (**Rum 6:23;** ona pia **Mwz 2:17; Ezek 18:4, 20; Rum 5:12**). Kwa sababu Mungu ni mtakatifu, hawezi kuvumilia dhambi (**Hab 1:13; Rum 1:18**). Vile vile Mungu ni mtenda haki: "Kutokana na hali yake ya utakatifu na ukamilifu Mungu hawezi kujifanya haoni uovu wa mwanadamu kana kwamba hauna tatizo. . . . Ikiwa Mungu yabidi awe mkweli katika asili yake ya haki, kila uovu lazima uadhibiwe." (Alexander 2008: 130, 131)

Ikiwa wanadamu yabidi wawe wenye haki mbele za Mungu na wafurahie maisha ya milele, inabidi dhambi yao iondolewe. Hili ni tatizo kubwa. Kwa sababu Mungu mwenyewe ni mtakatifu na mkamilifu, na ndivyo anavyotutaka tuwe (**Math 5:48**). Tatizo lililopo kwa wanadamu ni kwamba hatuwezi kamwe kuwa na kiwango cha utakatifu na ukamilifu wa Mungu kwa kutumia nguvu zetu wenyewe. Kwanza, "mara mtu atendapo dhambi, haiwezekani tena awe mkamilifu" (Sproul 2002: 94). Pili, hata matendo yetu mazuri yana madoa ya dhambi. Kwa hakika kama tunatenda matendo mazuri ili tukwepe hukumu ya Mungu na Jehanamu, hilo pekee hufanya matendo yetu mema kuwa *si* "mema" kwa sababu ikiwa lengo letu ni kukwepa jehanamu kwa kutenda "matendo mema," basi hayo matendo, kwa tafsiri, ni ubinafsi na umimi, ambayo hiyo pia ni dhambi. Tatu, hakuna kiwango cha matendo mema kinachoweza kutosheleza hata kuibadilisha asili ya dhambi na mwelekeo wa dhambi ulio moyoni. Hivyo, matendo mema hayawabadili watu waovu, wenye dhambi kuwa wenye haki, wasio na dhambi; mioyoni mwao, watabaki kuwa wenye dhambi. Hata hivyo, Mungu ni wa upendo na hapendi hata mmoja apotee (**Ezek 18:23; 33:11; 2 Pet 3:9; 1 Yoh 4:8**).

Kwa hiyo injili ni nini? Neno "injili" ni neno la Kiyunani (*euaggelion*) ambalo humaanisha "habari njema" (Danker 2000: *euaggelion,* 402; Green and McKnight 1992: 282). "Msamiati wa Kiyunani 'injili' (uinjilisti) ulitofautisha ujumbe wa Kikristo na jumbe zile za dini nyingine. Hii ilikuwa ni habari ya tukio la kihistoria, kama vile ushindi katika vita au kuinuka kwa mfalme mpya, ambayo ilibadilisha hali ya wasikilizaji na ilitaka mwitikio kutoka kwa msikilizaji. Kwa hiyo injili ni habari za kile alichofanya Mungu kutufikia sisi. Si ushauri kuhusu kile tunachopaswa kufanya ili tumfikie Mungu." (Keller n.d.: 1) Injili ni habari njema ya kuwa Mungu amefanya kwa ajili yetu kile ambacho tusingeweza kamwe kufanya kwa nguvu zetu. Mungu alifanyika mtu ambaye alikuwa ni Yesu Kristo. Yesu aliishi maisha ambayo tungeliishi sisi *kama mwanadamu*; alimtii Mungu Baba katika kila jambo kwa ukamilifu; alijaribiwa *"alijaribiwa sawa sawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi"* (**Ebr 4:15**). Hiyo ilimfanya astahili kuwa badala yetu, achukewe dhambi zetu juu yake na kulipa kwa adhabu ambayo tungepaswa sisi kulipa ingawaje kamwe tusingeweza (**Rum 8:1-4; 2 Kor 5:21; Gal 3:13; Kol 2:13-14; 1 Tim 2:5-6; 1 Pet 2:24**). Wakati huo huo, Yesu Kristo alikuwa Mungu. "Mungu hakumwadhibu mwingine, badala yake pale msalabani aliyachukuwa maumivu, kipigo, na uovu wa dunia yote juu yake mwenyewe. . . . Huyu ni Mungu ambaye anafanyika mwanadamu na kuutoa uhai wake kwa upendo na rehema zake ili haki itendeke ili aharibu uovu wote bila ya kutuharibu sisi. . . . Ni kwa nini *ilibidi* Yesu afe ili sisi tusamehewe? Lilikuwepo deni la kulipa—Mungu mwenyewe alililipa. Ilikuwepo adhabu ya kubeba—Mungu mwenyewe aliibeba. . . . Msalabani haki na rehema havikupotea—vyote vilitimizwa kwa wakati mmoja. Kifo cha Yesu kilikuwa lazima ili haki itendeke kama ambavyo ingestahili ili Mungu aendelee kutupenda." (Keller 2008: 192-93, 197)

Kufufuka kwa Yesu na kupaa kwa Baba kumedhihirisha Yesu ni nani na kuonyesha kwamba Baba aliikubali dhabihu ya Kristo yeye mwenyewe msalabani kwa ajili yetu. Hivyo, Yesu ni nani na amefanya nini ndicho kiini cha inijli. Hili limetamkwa mara nyingi katika AJ yote, mfano, **1 Kor 15:1-5:** *"Basi, ndugu zangu, nawaarifu ile injili niliyoihubiri; ambayo ndiyo mliyoipokea, na katika hiyo mnasimama, na kwa hiyo mnaokolewa; ikiwa mnayashika sana maneno niliyowahubiri isipokuwa mliamini bure. Kwa maana niliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe, ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko; na ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo maandiko; na ya kuwa alimtokea Kefa; tena na wale Thenashara;"* (ona pia **Yoh 20:30-31; Matendo 10:36-43; 16:30-31; Rum 1:1-4, 16-17; 3:23-28; 10:8-13; 1 Kor 2:2; 1 Pet 3:18**). Wokovu *unatolewa* na Mungu kwa watu kama *zawadi*

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

ya *neema* yake*; Unapokewa* na watu kwa *imani* ndani ya Kristo. Kama **Efeso 2:8-9** inavyosema, *"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu."* Kuokoka maana yake ni kutubu dhambi zetu, kukubali kile alichofanya Yesu kwa ajili yetu kwa imani, na kumgeukia Yesu kama Bwana wa maisha yetu (**Math 11:28; Marko 1:14-15; Yoh 1:12; 3:16; 17:3; Matendo 26:20; 1 Yoh 1:8-9**). Ndani ya Kristo, hatuna hatia ya dhambi wala hukumu kana kwamba tumelipa deni lote la dhambi sisi wenyewewe (**Rum 6:3-7; Gal 2:20**). Kwa kweli, tunapomgeukia Yesu kwa imani, si kwamba anaondoa tu dhambi zetu na kuziweka juu yake na kulipa deni la dhambi zetu ambalo tungepaswa kulipa, bali pia hutupa haki yake ili tuweze kusimama mbele za Mungu (**Isa 53:5-6, 10-11; Rum 10:4; 2 Kor 5:21; Ebr 2:17-18; 1 Pet 2:4; 3:18**).

Tunapoiamini injili na kumgeukia Kristo kama Bwana wetu, kila eneo la maisha yetu hubadilika: (1) Wote waliounganishwa na Kristo kwa imani wana uhakika wa wokovu wao. Kama wokovu ungetegemea hata kwa sehemu juhudi zetu sisi, tusingeweza kuwa na uhakika kwamba "tumefanya vya kutosha" kustahili wokovu. Hata hivyo, kwa sababu Mungu ndani ya Kristo alifanya yale tusiyoweza kufanya, Wakristo wanaweza na wana uhakika ya kuwa wameokoka na milele watakuwa wameokoka (**Yoh 3:36; 6:37, 47; 11:25; 1 Yoh 5:11-12**). (2) Kuokoka na kuunganishwa na Kristo kunabadilisha hadhi ya Wakristo kisheria. "Msalaba unakomboa kutoka katika nguvu ya dhambi, unatuliza ghadhabu ya Mungu, unasafisha hatia na doa la dhambi, huwapatanisha waamini na Mungu, na kuwapatia ushindi kiulimwengu dhidi ya adui wakuu wa kiroho" (Demarest 1997: 196). (3) Kuokoka na kuunganishwa na Kristo huwabadilisha Wakristo kutoka ndani. Mtu anapokuja kwa Kristo, hupokea moyo mpya (**Ezek 36:26; 2 Kor 3:3**), nia ya Kristo (**1 Kor 2:16**), na Roho kutoka kwa Kristo (**Ezek 36:26; Yoh 14:17**). (4) Kuokoka na kuunganishwa na Kristo huwapa Wakristo uhusiano wa ndani na Mungu kupitia Kristo. Wakristo wanaweza *"kukaribia kiti cha neema kwa ujarisiri"* (**Ebr 4:16**; ona pia **Ebr 7:19**) kwa sababu Kristo yu "ndani" ya waamini (**Yoh 14:20; 17:23; Rum 8:10; Gal 2:20; Efeso 3:17; Kol 1:27; 1 Yoh 3:24; Ufu 3:20**) na waamini wako "ndani ya Kristo" (**Rum 8:1; 12:5; 16: 6, 7, 9-10; 1 Kor 1:2, 30; 4:10, 15; 15:18, 22; 2 Kor 1:21; 5:17; 12:2; Gal 1:22; 3:28; 6:15; Efeso 1:3; 2:6, 10; Fil 1:1; Kol 1:2; 1 Thes 2:14; 4:16; 1 Tim 3:13; 2 Tim 3:12; Fil 23; 1 Pet 5:14**). (5) Kuokoka na kuunganishwa na Kristo huwapa Wakristo lengo jipya na sababu ya kiushi. Kwa sababu Kristo yu ndani yetu na tuna moyo mpya, nia mpya, na Roho mpya, viwango vyake na vipaumbele vyake vinakuwa viwango vyetu na vipaumbele vyetu. Anatenda kazi ndani yetu na kupitia kwetu ili atufanye kama yeye alivyo (**Rum 8:29; Fil 2:12-13**). (6) Kuokoka na kuunganishwa na Kristo huumba mtu mpya (**Yoh 3:3; Rum 6:4; 2 Kor 5:17; Gal 6:15**); waamini wameasiliwa ndani ya familia ya Mungu kama watoto wake (**Yoh 1:12; Rum 8:14-17, 23; 9:4; Gal 3:26; 4:5-7; Efeso 1:5; 2:19; 1 Yoh 3:1**) na wanakuwa na mahusiano thabiti kama dada na kaka (mfano, **Math 12:50; Matendo 1:16; 6:3; 11:29; 12:17; 16:40; 18:18; 21:7, 17; Rum 14:10; 1 Tim 5:1-2**). (7) Siku moja, Kristo atarudi na kuifanya upya dunia yote na uumbaji wote (**Rum 8:18-23; 2 Pet 3:3-13; Ufu 21:1-11**). Hiyo, kwa asili, ndiyo injili.

Kuielewa kwa undani na kuitambua injili na mambo yanayohusiana nayo ni jambo la msingi kwa uanafunzi: "Injili ni kwa ajili ya wanafunzi, na si kwa ajili ya 'wenye dhambi tu;' inaokoa na kubadilisha watu katika mahusiano, si tu watu binafsi walio pekee. . . . Uanafunzi unahusiana na kumtegemea Yesu, kuamini injili yake. Ingawaje inaonekana kuwa rahisi hivyo, tatizo ni kwamba sote tunasumbuka katika kuielewa dhana ya kumtegemea Yesu au kuiamini injili hasa kunamaanisha nini. . . . [Agizo Kuu] hulenga katika kuihubiri injili kwa wale ambao hawajawa wanafunzi na kuifundisha injili kwa wale ambao ni wanafunzi tayari. Yesu anaweka injili kwanza, ambayo hupelekea kuwafanya na kuwakuza wanafunzi. Hawaiti watu kuhubiri kwanza, na ndipo kufanya wanafunzi iwe chaguo la pili. Vyote uinjilisti na kuwafanya watu kuwa wanafunzi husukumwa na injili. . . . Yesu alihubiri injili hiyo hiyo kwa makutano na wanafunzi. Hakuwa na mafundisho maalum ya ziada kwa ajili ya wanafunzi wake, injili iliyoongezeka kusoma masomo ya juu zaidi. Injili ni kwa ajili ya wale ambao hawajahitimu na wale ambao wangepaswa kuwa wamehitimu kwa sababu hakuna anayehitimu katika injili. Yesu alihubiri injili ile ile ya ufalme kwa wenye dhambi na watakatifu. Kwa nini? Kwa sababu agenda yake ya neema ndilo jawabu pekee la mashaka tuliyonayo ya dhambi, Kwa Mkristo au asiye Mkristo. Wote wanahitaji nguvu ya injili inayosamehe, inayopatanisha, inayorejeza ili kumjua Mungu na kumfurahia, si mara moja tu bali kwa maisha yote." (Dodson 2012: 17, 19, 36, 38)

Viongozi wengi wa kanisa wana mtazamo dhaifu wa injili: Wanafikiri kwamba ni "ABCs" tu ya Ukristo, ya kwamba ni kwa ajili ya uinjilisti na wenye dhambi, na ya kwamba inahusisha vipengele fulani vichache vya kiimani ambavyo mtu anatakiwa kuwa navyo ili "aokoke." Viongozi wa jinsi hiyo kwa kawaida hutegemea sheria na miongozo ya wanadamu, ushawishi wa madhabahuni, na vitisho vya kuwatenga waumini ili kutawala matendo yao. Mtazamo huu huonyesha kuwa viongozi wa kanisa na wafuasi wao hawaielewi injili kabisa. Kwa kweli, "Injili [ni] ya uwiano wa kiufalme, inahuisha maisha yote. Injili ina madai yanayoizunguka,

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

na kile ambacho injili inadai inakitekeleza." (Ibid.: 37)[14]

Injili inatubadili sisi ndani ili tuishi kwa imani ndani ya Yesu Bwana wa maisha yetu. Darrow Miller anazungumza kuhusu vita ya kiakili ndani ya kanisa "kati ya wale ambao watatoa kipaumbele kwa injili au matendo ya kijamii. Pande zote ziko sawa, na zote haziko sawa. Kufanywa upya ni kupata badiliko hasa, katika Nyanja zote za maisha, kama namna anavyobadilika kiwavi kuwa kipepeo. Si tu badiliko la kidini bali badiliko la mfumo wote wa mwenendo wa maisha ya mtu. . . . Badiliko hili huanzia katika utu wa ndani, ikianzia na vile tunavyoviamini na kuvithamanisha, na hatimaye hutokezea nje katika tabia na matokeo ya yale tunayotenda. Injili ni zaidi sana ya uinjilisti. Wakristo wengi wamekubali tafsiri iliyochakachuliwa, ya agizo la Kristo la kufanya mataifa yote kuna wanafunzi; lakini injili ni mwitikio wa Mungu kwa mahitaji yote ya mwanadamu." (Miller 1998: 73) Badiliko linalofanywa na injili ni kubwa sana na la kina:

- <u>Kuokoka na kuunganishwa na Kristo huwapa Wakristo uhusiano wa ndani na wa kibinafsi na Mungu kupitia Kristo.</u> Mtu anapokuja kwa Kristo, anakuwa *"kiumbe kipya"* (**2 Kor 5:17**). Asili ya uongozi na nguvu ya kuishi maisha yaliyo safi haitokani na vyanzo vya nje (kwa kufuata sheria na mapokeo) lakini kupitia tukio la ndani; chanzo cha msingi cha uongozi na nguvu ni Yesu Mwenyewe, ambaye sasa huishi ndani na kupitia watu wake. Kama **Gal 2:20** inavyosema, *"Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilionao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akijitoa nafsi yake kwa ajili yangu."* Yesu anatupa moyo mpya (**Ezek 36:26; 2 Kor 3:3**), nafsi (**1 Kor 2:16**), na roho (**Ezek 36:26; Yoh 14:17**). Kwa hivyo anatumia Neno lake ndani yetu na kupitia sisi (**Yoh 6:63; 68; 8:31-32; 14:26; 16:13-15; 2 Yoh 9**). Kupitia uwezo ambao Kristo amewapa waamini, Wakristo kwa hakika katika hali inayoendelea wanasafishwa na kubadilishwa katika utu wa ndani ili kwamba wawe *"aliwachagua tangu asili, wafananishwe na mfano wa [Yesu Kristo]"* (**Rum 8:29**).
- <u>Injili hutubadilisha tabia.</u> Msalaba hutukomboa kutoka katika nguvu ya dhambi; hatuendelei kuwa watumwa wake (**Yoh 8:34; Rum 6:16**) bali sasa tumeunganishwa na Kristo (**Efeso 6:6**). Hii huwapa Wakristo sababu na kusudi jipya la kuishi. "Dini huenda kwa kanuni hii 'Ninatii—kwa hiyo Mungu ananikubali.' Bali kanuni inayotumika katika injili ni 'Mungu ananikubali kwa sababu ya kile alichakifanya Yesu—kwa hiyo ninatii.'" (Keller 2008: 179-80) Kama ilivyotajwa hapo juu, mtu anapompokea Kristo na kuingia katika uhusiano wa kuokolewa naye, *bila upendeleo* anapokea vitendea kazi (moyo mpya, nia mpya, Roho mpya) ambavyo humwezesha mwamini kuishi maisha mapya kimaadili yanayompa Mungu heshima. *Kimsingi tunatawaliwa na,* "Kielelezo cha Kristo cha kufa kwa niaba yetu ambacho huachilia nguvu mpya ya kimaadili ambayo hubadilisha mienendo yetu, nia na tabia" (Demarest 1997: 196). Hali hii inafanana na ile ya mtu aliyempenda mwingine: "Upendo wako unakupa shauku ya kutaka umpendaye akukubali. . . . [Unapomwoa umpendaye] Je unasema, 'Safi sana! nimeshampata! Sasa naweza kufanya chochote kile nitakacho'? La hasha. Sasa hata husubiri mpenzi wako akuombe umfanyie kitu fulani. Unakitarajia kila kinachompendeza. Hakuna kushurutishwa wala fikra za wajibu, hata hivyo tabia yako imebadilishwa vilivyo na nafsi na moyo wa mtu unayempenda." (Keller 2008: 183) Ndiyo maana **Rum 6:1-2** inasema, *"Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi?"* Vivyo hivyo, "sisi sote tunahitaji wakati wote kuamshwa na uzuri na utukufu wa Kristo na utoshelevu wa neema yake, ambayo kwa upende mwingine itahimiza utii wa Kristo tunaowiwa" (Dodson 2012: 74).

Hatimaye, uanafunzi ni mchakato wa kumfikisha mwanafunzi kiwango cha *kuamini* injili hasa kiasi ya kwamba inapenya ndani ya moyo, nia, utashi na kila eneo la maisha ya mwanafunzi. Kwa hakika, kama

[14] Katika *The Cost of Discipleship* Dietrich Bonhoeffer alitambulika kwa kutofautisha kile kinachoitwa "neema rahisi" dhidi ya "neema yenye gharama": "Neema rahisi ni kuhubiri msamaha bila kuhitaji toba, ubatizo bila nidhamu ya kanisa, Ushirika bila kukiri, msamaha bila ukiri wa binafsi. Neema rahisi ni neema bila kufanyika mwanafunzi, neema bila msalaba, neema bila Yesu Kristo, akiishi na kukaa ndani. . . . Neema yenye gharama ni Injili ambayo lazima *itafutwe* tena, na tena, kipawa ambacho lazima *kitafutwe,* mlango ambao mtu lazima *agonge*. Neema ya jinsi hii ni ya *gharama* kwa sababu inatuita *tufuate*, na ni *neema* kwa sababu inatuita tumfuate *Yesu Kristo*. Ni ya gharama kwa sababu inamgharimu mtu maisha yake, na ni neema kwa sababu inampa mtu maisha yaliyo maisha kweli. Ni ya gharama kwa sababu inahukumu dhambi, ni neema kwa sababu inamhesabia mwenye dhambi kuwa na haki. Zaidi ya yote, ni ya *gharama* kwa sababu ilimgharimu Mungu kumtoa Mwana wake . . . na kile ambacho kilimgharimu Mungu gharama kubwa hakiwezi kuwa rahisi kwetu. Zaidi ya hayo, ni neema kwa sababu Mungu hakumzuia Mwana wake asiilipe gharama kwa ajili yetu ingawaje alikuwa wa thamani sana kwake, bali alimtoa kwa ajili yetu. . . . Neema ya gharama inatukabili kama wito wa neema kumfuata Yesu, inakuja kama neno la msamaha kwa roho iliyovunjika na moyo wenye toba. Neema ni ya gharama kwa sababu inamshurutisha mtu kujitiisha kwenye nira ya Yesu na kumfuata; ni neema kwa sababu Yesu anasema: 'Nira yangu ni laini na mzigo wangu ni mwepesi.'" (Bonhoeffer 1963: 47-48)

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

Timothy Keller anavyosema, "Matatizo yote, ya kibinafsi au ya kijamii, yanatokana na kushindwa kutumia injili kwa kumaanisha hasa, ni kushindwa kwenda 'sambamba na kweli ya injili'' (Gal. 2:14). Patholojia zote kanisani pamoja na kutokufanikiwa kwake hutokana na kushindwa kuachilia injili kuwekwa dhahiri kwa namna ya kumaanisha hasa. Ikiwa injili itafafanuliwa na kutendewa kazi katika utimilifu wake katika kanisa lolote, kanisa litaanza kuonekana liko tofauti sana. Watu wataona ndani yake nguvu ya kuwagusa ya kimaadili ikipenya katika dhamira zao na pia huruma na uwezo wa kukabiliana na mambo kwa namna tofauti tofauti." (Keller 2000: 9) Biblia mara kwa mara inauelezea mchakato huu wa kuamini na kutenda sawa sawa na injili ya kuwa ni kama "vita" au "kazi ya kutumia nguvu" au "mapambano" (**Kol 1:29; 4:12; 1 Tim 1:18; 4:10; 6:12; 2 Tim 4:7**). "Tunapambana ili tuione sura ya utukufu wa Mungu iking'aa katika uso wa Yesu Kristo. Imani hii haishindani ili kupata ukamilifu, bali kupata kuamini. Tunapambana ili tuamini kwamba Yesu ni wa thamani zaidi, anatosheleza, na kusisimua kuliko chochote kile dunia inachoweza kutupa. Hii ndiyo imani katika injili – tangazo kubwa kwamba Yesu ameshinda dhambi, mauti, na uovu kupitia kifo chake na kufufuka na anayafanya mambo yote mapya, hata sisi. Tunapoiamini injili, tunafikia mahali pa kuzifurahia ahadi za neema ya Mungu, Amani na furaha. Tunapokuwa hatuiamini injili, tunakwenda mbali na vitu hivi. Zaidi ya hayo, tunakwenda mbali na Yesu, ambaye anastahili juhudi zetu zote, kuonakwetu kote, na kuamini kwetu kote." (Dodson 2012: 60). Hii ndio maana injili ni msingi wa uanafunzi.[15]

**C. *Nguvu ya kufanya wanafunzi***

Kuiamini injili na kuelewa na kila kinachohusiana nayo huathiri nyanja zote za maisha ya mwanafunzi. Ndiyo maana, Petro (na Barnaba) walipoacha kula na watu wa Mataifa, Paulo *"alishindana naye uso kwa uso"* (**Gal 2:11**) katika msingi kwamba *"hawakuwa sahihi <u>kuhusiana na kweli ya injili</u>"* (**Gal 2:14**). "unahusisha maisha yote, sharti kanisa kuwafunza watu wake kuhusu maisha yote" (Colson 1992: 287). Inamaanisha uanafunzi na mchakato wa kuadibisha ndivyo ambavyo hutekeleza injili—na kuhusishwa kwa injili katika maeneo makuu ya maisha—kama kiini kikuu (onaCarter, Suh, and David 2014; Vanderstelt n.d.). Yafuatayo ni maeneo muhimu ya Imani na maisha yatokayo katika injili. Haya ni maeneo ambayo kanisa lapaswa kufunza watu wake ili wawe wanafunzi:

1. <u>Kanisa lapaswa kuwapa mafunzo thabiti washirika wake ili wajue wanachokiamini, kwa nini wanaamini, na kuitetea Imani yao kwa wengine.</u> Biblia inafundisha kuwa Yesu Kristo ni Mungu kamili na mtu kamili, inamaanisha Mungu aliyekuja duniani kama mtu. Ukristo pekee ndio unatambua na kutilia maanani "anguko" la wanadamu, uzito halisi wa dhambi, utakatifu na ukamilifu wa Mungu, hali isiyokubaliana ya Mungu na dhambi kuwepo pamoja, ukweli kuwa wanadamu wote wanastahili hukumu kwa sababu ya dhambi zao, na hali ya wanadamu kutoweza kujiokoa wenyewe kwa juhudi zao. Na ndio maana ukweli kwamba Yesu alikuwa mtu kamili lakini pia Mungu kamili si tu ni muhimu lakini pia wa lazima kabisa kwa wokovu. Gleason Archer anasema, "Mungu kama Mungu hakuweza kutusamehe dhambi zetu mpaka malipo kamili yalipofanyika kwa niaba yetu; la sivyo angekuwa mwenye kuruhusu na kutetea ukiukwaji wa sheria yake Takatifu. Ni pale tu alipokuwa kama mwanadamu kwamba Mungu ndani ya Kristo aliweza kwa utoshelevu kulipa gharama ya dhambi za binadamu; kwa kuwa ni mwanadamu, mwanadamu halisi, angeweza kikamilifu kuwakilisha kizazi cha wanadamu. Lakini mkombozi wetu alipaswa kuwa Mungu pia, kwa kuwa ni Mungu pekee angeweza kutoa dhabihu yenye thamani isiyopimika, kugharimia adhabu ya jehanamu ya milele ambayo tulistahili kupata kwa sababu ya dhambi zetu, sawa sawa na matakwa ya haki ya Kiungu." (Archer 1982: 323; ona pia Jadeed 1996-2015: 4). Alichokuwa anafanya Yesu msalabani ni kupokea hukumu, kulipia gharama, na kuchukua juu yake adhabu ambayo ilipasa kiadhibiwe kizazi cha wanadamu wenye dhambi. Kristo alikuja kutufanyia kile ambacho hatukuweza kukifanya kwa ajili yetu—aliishi maisha ambayo tungepaswa kuishi na kulipa gharama ya dhambi zetu ambazo tungepaswa kulipa lakini kamwe tusingeweza; na tunapoamini hayo na kumpokea katika maisha yetu kama Bwana na mwokozi, huingia ndani yetu kwa njia ya Roho Mtakatifu ili aishi maisha yake kupitia sisi, akitubadilisha kutoka ndani

---

[15] Ishara mojawapo ya imani katika Injili ni ubatizo. Andreas Kostenberger anauita ubatizo "kitu muhimu katika uanafunzi ndani ya Ukristo" (Kostenberger 2006: 33). Anasema kwamba katika "Agizo Kuu" (**Math 28:18-20**), kufanya wanafunzi kunahusisha "kubatiza waongofu wapya na kuwafundisha kutii amri za Yesu (ona pia Yohana 4:1). Kanisa linalotii litaichukua moyoni amri ya Kristo aliyefufuka na kuingia katika misheni na uinjilisti wa kuhubiri, likitafuta kusababisha watu kuokoka kutakakosababisha matokeo ya ubatizo, mafunzo, na kukua katika Ukristo. Katika kiwango cha mtu binafsi, wale ambao wameweka tumaini lao kwa Yesu Kristo na wametubu dhambi zao ni lazima wabatizwe ikiwa ni sehemu ya mafunzo yao ya kufanywa wanafunzi ndani ya Ukristo. Japokuwa kunaweza kuwepo kipindi cha kupewa maelekezo kabla ya kubatizwa, mtu ambaye ameshaokoka kwa dhati na anahitaji kubatizwa haipasi kumuwekea kikwazo chochote." (Ibid.)

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

hadi nje ili tuwe kama yeye. Hiyo ni *injili*.[16]

Ukweli kwamba Yesu ndiye vile asemavyo ndiye (Mungu aliyekuja duniani) na ya kuwa dhabihu yake msalabani ilikubaliwa na Baba ilithibitishwa wakati Yesu alipofanya kile ambacho hakuna mtu mwenye kupatwa na mauti angeweza kukifanya, ambacho ni, kufufuka katika wafu na kisha kupaa kurudi mbinguni. Kitabu cha ECLEA kiitwacho *Ukristo na Uislam: Mambo Muhimu ya Kitheolojia* (http://www.eclea.net/courses.html#islam) hujadili na kutoa ushahidi wa kibiblia na kihistoria wa uungu wa Kristo, kusulubiwa kwake na kufufuka, kile alichotenda msalabani, kwa nini kifo cha Kristo msalabani kilikuwa lazima, asili ya Mungu, Utatu, na jinsi ambavyo Biblia yaweza kutegemewa. Kitabu cha ECLEA kiitwacho, *Theolojia ya Kibiblia* (http://www.eclea.net/courses.html#theology) kinaweka kwako simulizi ya msingi ya Biblia, kinaonyesha jinsi AJ linavyooana na AK, na kushughulika na swala la ukuu wa Mungu, wajibu wa ubinadamu, na uwepo wa dhambi na uovu. Kitabu cha ECLEA kiitwacho *1 Timotheo: Dondoo/Mwongozo Mfuypi; Uchambuzi; Kijarida chaMafunzo ya Kiutendaji* (http://www.eclea.net/courses.html#timothy) kinashughulika na maswala muhimu ya imani yetu: wokovu kwa neema kupitia imani ndani ya Yesu Kristo; umuhimu wa maombi; sifa za kuwa kiongozi kanisani; na ukuu wa Yesu. Kitabu hiki pia hushughulika na mambo muhimu ya kiutendaji: mafundisho ya kweli dhidi ya yale ya uongo; namna ya kudhibiti maisha yako kiroho; kushauru na kukemea watu; wajibu wa kanisa kwa maskini na wahitaji; mambo yanayowahusu wazee wa kanisa; na injili na pesa. "Mwongozo wa Mafunzo ya Kusimika" (sehemu ya mwisho ya kitabu cha ECLEA kiitwacho *1 Timotheo*) ni mfululizo wa maswali kutoka katika kila sehemu ya 1 Timotheo, kwa ajili ya majadiliano katika vikundi vidogo, ili kusaidia Wakristo kwa ujumla na viongozi wa kanisa hasa kutathmini maisha yao ya kiroho na hali za makanisa yao. Vitabu hivi na nyenzo nzuri kwa kanisa kutumia kwa ajili ya kuwafunza watu wake katika maeneo haya. Hatimaye, wanafunzi wazuri wanahitaji kufundisha jinsi ya kuitetea imani yao (*utetezi*), si tu wao kujua mafundisho ya Kikristo.

2. <u>Kanisa linapaswa kuwapa mafunzo thabiti washirika wake ili waitumie imani yao katika kuishi maisha yafaayo kuigwa hapa duniani.</u> Biblia kwa kurudiarudia inawaambia waamini waishi kama Yesu alivyoishi, ikimaanisha, *"kuutimiza wokovu wao"* (**Fil 2:12**). Hili linatenda kazi katika maeneo yote ya maisha. Paulo anasema, *"Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lolote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu"* (**1 Kor 10:31**). Yakobo anakwenda mbele zaidi akisema kwamba *"imani pasipo matendo imekufa"* (**Yak 2:26**). Kwa tabia zetu tunapaswa kuwa mfano na wa kumatia Mungu heshima *"mpate kuwa wana wa Mungu wasio na lawama, wala udanganyifu, wasio na ila katika kizazi chenye ukaidi, kilichopotoka; ambao kati ya hao mnaonekana kuwa kama mianga katika ulimwengu,"* (**Fil 2:15**); *"Kwa maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa, nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa;"* (**Tito 2:11-12**). Yesu alitilia mkazo umuhimu wa kuishi maisha imani hadharani: *"Vivyo hivyo nuru yenu naiangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni"* (**Math 5:16**). Paulo pia alihimiza kwamba imani yetu ikamate maisha yetu kiasi kwamba *"kuendelea kwetu kuwe dhahiri kwa watu wote"* (**1 Tim 4:15**). Kubadilisha zile tabia za ndani za namna ya kuwaza na mwenenndo ili kwamba waaminio wawe *"wanafananishwa na mfano wa sura ya [Kristo]"* (**Rum 8:29**) ni mchakato endelevu katika maisha yetu yote. Ndio maana waamini waliokomaa wanapaswa kufunza na kuwa kielelezo cha ukristo kwa Wakristo wachanga.

Walter Henrichsen anasema, "Pamoja na kutumia kielelezo cha mduara kukusaidia kufunza wanafunzi wako [ona hapo chini, sehemu **V. D.** ***Asili na tabia ya wanafunzi waliokomaa***], unaweza

[16] Hili huinua muingiliano muhimu kati ya kufanya wanafunzi, uinjilisti na kuongoka. Setzer na Putman wanataarifu, "miaka kadhaa iliyopita, tulianza kuona mwelekeo wa kufurahisha katika mengi ya makanisa yetu mapya ambayo yalivuta idadi kubwa ya watu wasiofikiwa/wasiohudhuria kanisani. Inaonyesha kwamba kadiri walivyochelewa kuweka imani yao wazi kwa watu, hatari ya wao kurudi nyuma ilikuwa ndogo. Kwa upande mwingine, watu walipokuja na kwa haraka wakatangaza kuwa wamemkubali Kristo hasa, walionekana kupotea kwa haraka kama walivyokuja. Siku za karibuni, katika mahojiano na mmishonari aliyekuwa akirudi kutoka Malaya aliulizwa kuhusu mtindo wake wa kufanya uinjilisti. Alisema haya, katika utamaduni wa nchi ambayo ndiko alikotokea, mtu alipoongoka, walikuwa tayari ameweka mizizi katika Maandiko, mara nyingi anakuwa tayari yuko katika huduma za kijamii na kwa kawaida akiwa pia anajihusisha na huduma fulani ndani ya kanisa. Kufanywa mwanafunzi katika muktadha huu ni tendo ambalo lilianza kitambo kabla ya mtu kuongoka, na kuongoka ilikuwa tu ni hatua ambayo ni sehemu ya mchakato wa kufanywa mwanafunzi." (Setzer na Putman 2006: 104) Ufahamu huu unathibitishwa na timu iliyofanikwa ya waongofu waliotoka katika imani ta Kiislamu katika Mashariki ya Kati ambao wao "hushughulika na kufanya wanafunzi, sio kuwafanya waokoke. . . . Tunajitahidi kufanya watu kuwa wanafunzi kwanza. Tunategemea kwamba mtu anaikubali imanai kiukweli akiwa ameshafundishwa kweli." (Daniel 2010: 40) Makanisa yamaanishe katika kuwaweka washirika wote katika vikundi, sio tu wale waliofanya ukiri wa imani.

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

kutaka kujenga maeneo ya mwenendo, kama vile usafi wa moyo katika maisha, imani, upendo, na uadilifu. Hata hivyo, tunapaswa wakati wote kujikumbusha kwamba utekelezaji wa malengo ya mafunzo lazima ukubaliane na mahitaji ya mtu binafsi. Kwa kuzingatia hayo mahitaji, tengeneza mpango. Wakati wote jiulize maswali matatu: (1) Anahitaji nini? (2) Atapata anachohitaji kwa njia gani? (3) Nitajuaje atakapopata?" (Henrichsen 1988: 103)

3. Kanisa linapaswa kuwapa mafunzo thabiti washirika wake ili wafanikiwe kukabili swala la dhambi katika maisha yao. Mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kwa uaminifu kushughulikia swala la dhambi katika maisha yao. Swala la dhambi liko katika kiini cha injili (dhambi yetu ndiyo ilisababisha Kristo kuja duniani na kufa kwa niaba yetu, mfano, **Math 1:21; 9:13; 26:28; Luka 5:32; Yoh 1:29; 8:24; Matendo 2:38; 10:43; Rum 6:23; 8:3; 1 Kor 15:3; 2 Kor 5:21; Gal 1:4; Kol 1:14; Ebr 1:3; 2:17; 10:12; 1 Pet 2:24; 3:18; 1 Yoh 2:2; 3:5; 4:10; Ufu 1:5**). Kuweza kushughulikia dhambi vilevile ni mwelekeo muhimu sana wa maisha yetu (mfano, **Math 6:12; 18:15-35; Luka 11:4; 15:7; 17:3; Yoh 5:14; 8:11, 34; Rum 2:12; 3:9, 23; 6:1-2, 11-22; 7:14-24; Efeso 4:26; 1 Tim 5:20; 10:26; 12:4; Yak 2:9; 4:8, 17; 5:16; 1 Yoh 1:8-10; 3:6-9**). Hii ndiyo sababu moja kwa nini wanavikundi vya uanafunzi yawapasa kukubaliana katika kanuni za kimsingi za kutegemeana katika uwazi wao kwa wao, kweli ya Neno la Mungu katika jamii, na uwajibikaji katika mabadiliko ya maisha kwa pande zote uliojadiliwa hapo chini. Hili laweza kuwa gumu sana katika tamaduni kama zile za Afrika ya Mashariki ambapo viongozi wa kanisa, na hasa wanaume, hawako tayari kuwa wazi au kukubali makossa yao na dhambi zao wao kwa wao. Kwa kuongezea, kwa sababu ya swala la kushughulikia dhambi maishani mwetu ingekuwa ni vema kwa wanaume kukutana na wanaume na wanawake kwa wanawake ili kuweza kubabili vema maswala mahususi ya kijinsia na dhambi vivyo hivyo.

Bila kujali mipaka ya kiutamaduni, hofu, na kutoaminiana, ili tuwe wanafunzi tunapaswa kufuata Biblia inavyotuambia *"Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa."* (**Yak 5:16**). Dietrich Bonhoeffer anajadili kwa nini hili ni muhimu sana: "Katika kukiri mtu anapenya kuelekea uhakika. Ni kwa nini ni rahisi kwetu sisi kukiri dhambi zetu kwa Mungu kuliko kwa ndugu yako? . . . Lazima tujiulize kama hatukujidanganya wenyewe mara kwa mara kwa ukiri wetu wa dhambi kwa Mungu, endapo badala yake tumekiri dhambi zetu kwetu sisi wenyewe na pia kujipa wenyewe msamaha. Na pengine huenda ikawa ndiyo sababu ya kurudia rudia matendo ya dhambi mara nyingi mno na udhaifu wetu wa kutoweza kutii katika Ukristo wetu kwamba kunatokana na ukweli kwamba tunaishi katika kujisamehe hasa na sio katika msamaha halisi? . . . Nani anaweza kutuhakikishia kwamba, katika kukiri na kusamehewa dhambi zetu, hatushuguliki na sisi wenyewe bali na Mungu aliye hai? Mungu ndiye anayetupa uhakika huu kupitia ndugu yetu. Ndugu yetu anavunja ule mduara wa kujidanganya. Mtu anayekiri dhambi zake mbele ya ndugu anajijua kwamba hayuko peke yake tena; anauhisi uwepo wa Mungu kwa uhalisia wa yule mtu mwingine. . . . Kama vile ambavyo ukiri wangu wa dhambi kwa ndugu unavyonilinda mimi dhidi ya kujidanganya, vivyo hivyo uhakika wa msamaha unaotamkwa kwangu na ndugu kwa niaba ya Mungu. Agizo la kuungamiana dhambi sisi kwa sisi limetolewa kwetu na Mungu ili tupate uhakika wa msamaha wa Kiungu." (Bonhoeffer 1954: 115-17)

Yatupasa kwanza tujue ni dhambi zipi zipo katika maisha yetu ndipo tuweze kushinda dhambi maishani mwetu. "Ili tujue dhambi yetu tunatakiwa tuwe na uelewa na majaribu yetu hasa, maeneo ambayo ni rahisi kwetu kutenda dhambi. Haya majaribu na dhambi yaweza kuwa dhahiri kwa kuonekana au kutoonekana, kwa wazi kama hasira au kwa kificho kama kujihurumia." (Dodson 2012: 122) Ni wazi kabisa, ni lazima tutafakari na kuomba kuhusiana na hili, pamoja na kuwaza ni wakati gani na katika mazingira gani tunajaribiwa zaidi kutenda dhambi. Pia tunahitaji kuwaza ni *kwa nini* tunatenda dhambi fulani tunazozitenda. "Hakuna hata mmoja anayetenda dhambi kama wajibu. Sote tunatenda dhambi kwa sababu tunataka kufanya hivyo, kwa sababu mioyo yetu inataka kitu fulani. Tusipokabili swala la ushawishi nyuma ya dhambi yetu, tutaikabibili juu juu, tunarekebisha tabia zetu, sio mioyo yetu. Mungu hataki marekibisho ya tabia tu; anataka utii wa kupenda kwa mguso!" (Ibid.: 124) Kwa sababu Mungu ametupa mwili wa Kristo kutusaidia, kutuhimiza, kutuonya na kututia moyo, kushinda dhambi kunaweza kutokea kwa mafanikio katika mahusiano ambapo kuna kuwajibika na kuaminiana. Hivi ndivyo vikundi vidogo vya uanafunzi vimekusudiwa kuwa. Hivyo, tunaweza kuuliza washiriki wengine wa kikundi cha uanafunzi "kutaja dhambi wanazoziona katika maisha yako. Mara nyingi, tunashindwa kuona madhaifu yetu. Jamii inayopendana inaweza kutusaidia kwa kutuinulia kioo cha Neno la Mungu ili tuweze kujiona vizuri zaidi." (Ibid.: 123)

Vita yetu dhidi ya dhambi inawezeshwa kwa uielewa injili. Hasa hasa, ingawaje tuko katika mapambano ambayo *"mwili hutamani ukishindana na Roho, na Roho kushindana na mwili;"* (**Gal**

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

**5:17**; ona pia **Rum 7:14-23**), vita yetu inapiganwa dhidi ya ukweli kwamba nyuma ya pazia, msalabani, Kristo alishashinda adhabu, nguvu, na uwepo wa dhambi. "Kamwe hatutabeba adhabu ya dhambi kwa sababu Yesu alibeba adhabu yetu katika kifo chake kulichoichukua hiyo ghadhabu. Nguvu ya dhambi imevunjwa kwa sababu Yesu ametupa maisha mapya. Dhambi itatoweshwa milele mara tutakapokufa au tunapokutanishwa na Yesu wakati wa kurudi kwake." (Ibid.: 126) Kwa kuielewa injili, tutaelewa kwamba Yesu ametuweka huru kutoka katika nguvu ya dhambi; kwa hiyo, hatutarudi katika mfumo wetu wa zamani wa dhambi. Pia tutaelewa kuwa Mungu anatukubali, si kama tulivyo sisi wenyewe bali kama tulivyo ndani ya Kristo; kwa hiyo, tuna kila sababu kupambana kutoka katika utambulisho wetu mpya, tukijua kwamba ndani ya Kristo tuna asili mpya takatifu na watakatifu hawatendi dhambi (**1 Yoh 3:6, 9; 5:18**), wakati ambapo dhambi inayojirudiarudia isiyotubiwa inaweza kutuondoa katika ufalme kwa sababu inadhihirisha "imani" yetu kama wenye kukiri kwa midomo bila kumaanisha (**Gal 5:19-21; Efeso 5:5; Ebr 3:7-13; 6:4-6; 10:26-27; 1 Yoh 3:6, 10**). Tunapambana dhidi ya dhambi kwa sababu tunampenda Yesu hasa, kwa sababu ya ile nafasi yetu ndani ya Kristo, kwa sababu ya kile ambacho alikifanya ndani yetu na kwa ajili yetu, na kile atakachokifanya ndani yetu na kwa ajili yetu. Yeye *"anayafanya yote kuwa mapya"* (**Ufu 21:5**; ona pia **2 Kor 5:17**), hata sisi. Tukiamini hili hasa—na kusaidia, kuhimiza, kuonya, na kuwatia moyo washiriki wengine wa kikundi chetu cha uanafunzi waamini hili—tutaona ushindi mkubwa sana dhidi ya dhambi katika maisha yetu. Tutaona ushindi kwa sababu hatupigani peke yetu lakini tunaweza kumtegemea Bwana wetu kutenda kazi ndani yetu (**Yoh 14:16-17, 26; Rum 8:13-14; F 2:12-13**). Ni mchakato unaoendelea maisha yetu yote, lakini Mungu ametuhakikishia ushindi.

Kipengele kingine cha dhambi ni mwitikio wetu wakati wengine wanapotenda dhambi dhidi yetu na kutusababishia madhara. Hilo hutokea mara kwa mara na ndio maana msamaha na upatanisho ni muhimu sana. Kushindwa kuwasamehe wengine kunaweza kusababisha ugumu wa moyo na matatizo mengineyo mengi. Hili ni suala ambalo watu wote hukutana nalo. Kitabu cha ECLEA kiitwacho *Msamaha na Upatanisho* (http://www.eclea.net/courses.html#forgive) kushughulikia mambo ya msingi ya muhimu ya kimaandiko kuhusiana na msamaha na upatanisho. Kinajadili msamaha na upatanisho ni nini na si nini. Mifano halisi ya jinsi ya kusamehe na namna ya kupatanisha imewekwa. Hii ni dhana nzuri kwa ajili ya matumizi ya kanisa katika kuwafunza washirika wake katika maeneo haya.

4. <u>Kanisa lapaswa kuwapa mafunzo thabiti washirika wake ili wawe na ndoa na familia imara.</u> Familia ndicho kitengo cha msingi ndani ya jamii. Kunapokuwa na tatizo katika Ndoa na mahusiano kati ya watoto na wazazi, jamii inaporomoka. Kitabu cha ECLEA kiitwacho *Ndoa Na Malezi Ya Kibiblia* (http://www.eclea.net/courses.html#marpar) ni ufafanuzi wa kibiblia wenye kiini ndani ya Yesu na utumiaji wa ufunuo wa Mungu kuhusiana na ndoa na malezi, ikielezea taasisi yake, kusudi, majukumu yetu, na wajibu wetu ikiwa na mtazamo maalum kwenye mahusiano, mawasiliano, tendo la ndoa, malezi, uzazi wa mpango, na kuachana. Ni nyenzo nzuri ya kanisa kwa ajili ya kuwafunza washirika wake katika eneo hili.

5. <u>Kanisa lapaswa kuwapa mafunzo thabiti washirika wake ili waweze kutekeleza wito wao kwa ubora na kwa namna inayompa Mungu heshima.</u> "Katika kipindi cha Matengenezo, kusaidia waamini kutambua wito wao ilichukuliwa kama hatua ya kwanza katika uanafunzi. Kwa kuwa kazi yetu ni kumtukuza Mungu, kanisa linapaswa kufundisha mtazamo wa juu kuhusu kazi na tabia za Kikristo za bidii, umakini katika matumizi ya pesa, ubunifu, na kutenda kwa ubora. Kama kanisa halitafundisha maadili bora ya kazi, nani atafundisha? Kanisani pia ndipo mahali pa asili ambapo ushauri wa kitaaluma waweza kutolewa." (Colson 1992: 292-93) Paulo aligundua umuhimu wa maadili mema ya kazi *kama njia ya kumshuhudia Yesu* alipoandika, *"Wo wote walio chini ya kongwa, hali ya utumwa, na wawahesabie bwana zao kuwa wamestahili heshima yote, <u>jina la Mungu lisitukanwe wala mafundisho yetu</u>. Na wale walio na bwana waaminio wasiwadharau kwa kuwa ni ndugu; bali afadhali wawatumikie, kwa sababu hao waishirikio faida ya kazi yao wamekuwa wenye imani na kupendwa. Mambo haya uyafundishe na kuonya."* (**1 Tim 6:1-2**)

6. <u>Kanasa lapaswa kuwapa mafunzo thabiti washirika wake ili wawe mawakili wema wa miili yao, mazingira, muda na fahamu zao.</u> Miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu (**1 Kor 6:19-20**; ona pia **Yoh 14:16-17; 1 Kor 3:16-17; 2 Kor 6:16**). Mungu anamiliki dunia (inamaanisha, mazingira yetu) na kila kitu ndani yake (**Ayubu 12:7-10; Zab 24:1; 50:10-12; 104:1-30; Isa 66:1-2a; Math 5:34-35; Matendo 7:49-50**). "Muda ni maisha. Hauwezi kurudishwa nyuma wala kuwa mbadala wa kitu kingine. Kupoteza muda ni kupoteza maisha yako, lakini kutawala muda wako ni kutawala maisha yako na kupata kila upaswacho kupata." (Lakein 1989: 1) Ni kwa namna gani tunajihusisha na maeneo haya yote huanzia na jinsi tunavyofikiri; kwa hiyo, Biblia inatuagiza *"tugeuzwe kwa kufanywa upya nia zetu"*

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

(**Rum 12:2**). Kitabu cha ECLEA kiitacho *Uwakili wa Kibiblia* (http://www.eclea.net/courses.html#stewardship) kina mijadala ya kina na ya kimatendo kuhusu uwakili wa mtu kwa mwili wake, mazingira, muda, na ufahamu. Ni nyenzo nzuri kwa ajili ya matumizi ya kanisa kuwafunza washirika wake katika maeneo haya.

7. <u>Kanisa lapaswa kuwapa mafunzo thabiti washirika wake kuwa mawakili wazuri wa pesa zao.</u> Pesa ni ya kiroho. Mwenendo wetu na vipa umbele vyetu katika vitu tunavyomiliki ni viashiria halisi vya mwenendo wetu na vipa umbele vyetu kwa Mungu (ona**Yak 2:14-18; 1 Yoh 3:17**). Tusipotawala pesa zetu, hatutawali maisha yetu. Kitabu cha ECLEA, *Uwakili wa Kibiblia* (http://www.eclea.net/courses.html#stewardship) kina sura ndefu inayohusu uwakili wa pesa na vitu, pamoja na maoni ya kiutendaji ya jinsi ya kupanga bajeti na kutawala pesa zako. Hii ni nyenzo muhimu kwa matumizi ya kanisa kuwafunza washirika wake katika maeneo haya.

8. <u>Kanisa lapaswa kuwapa mafunzo thabiti washirika wake ili wawe wabeba Habari Njema wenye mafanikio na wawafikie wale wenye mahitaji maalum kimwili na kiroho.</u> "Waamini wote wameitwa kuwa mashahidi, kwa maneno na matendo. Hivyo, kanisa linahitaji kufunza watu wa kawaida kugundua vipawa vyao vya kiinjilisti na kuvitumia vema masokoni." (Colson 1992: 294) Lazima matendo yetu na maneno yetu viende pamoja. Yesu alikazia kuhusu uhusiano wa asili ya Imani yetu wakati aliposema namna tunavyowatendea *"walio wadogo"* ndivyo, hasa, tunavyomtendea Yesu mwenyewe (**Math 25:31-46**). Kila kijiji na jamii ina watu ambao wengine hujiepusha nao: watu wa makabila mengine, waathirika wa UKIMWI, yatima, makahaba, wafungwa, walevi na waathirika wa madawa ya kulevya, wasio na mahali pa kuishi, mashoga, masikini, wagonjwa, walio katika hali ya kufa. Matendo yetu ya upendo kwa wale ambao hawapendeki hutupa fursa kuwambia watu hao kuhusu Yesu (*"Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza,"* **1 Yoh 4:19**) na pia huyafanya maneno yetu kuaminika.

Zaidi ya hayo, kila darasa la shule ya Jumapili, kundi dogo, kundi la uanafunzi, na makundi mengine ya kanisa (ikiwa pamoja na kikundi cha kusifu na kuabudu na wapigaji wa vyombo) wawe na kitengo cha huduma kwa ajili ya jamii. "Huduma kwa wengine ni hatua ya kwanza, sio udhihirisho wa baadaye wa kiroho. Sote tunajua kwamba tunakua kwa haraka tunapowasaidia na kuwahudumia wengine. Huduma ni mlango ambao wengi wetu ndipo tunapojifunzia mengi kuhusu sisi wenyewe na tunakuja kumwona Mungu akitenda kazi duniani. . . . Kuwasubiri watu wawe 'tayari kutumika' huwa inamaanisha kuwazuia kutumika, kwa kuwa wengi wetu tunajifunza kwa kutenda na kuuliza badala ya kupata mafunzo ndipo tutumwe kufanya kazi. Yesu aliwatuma wanafunzi wake kabla hawajawa 'tayari.' Alijua kwamba njia iliyokuwa ya haraka zaidi ya kuwaimarisha ni kuwaingiza katika huduma hasa. Kisha akawauliza uzoefu wao ili wajifunze kutoka katika huo uzoefu." (McNeal 2009: 105-06) Watu wanapofanya huduma katika jamii au miradi mingine ya kimisheni, inapasa waulizwe mara kwa mara. "Maswali ni pamoja na 'Umejifunza nini? Kuhusu watu? Kuhusu Mungu? Kuhusu wewe mwenyewe? Je kuna maeneo yoyote ya misimamo yako yalipata changamoto? Ni eneo gani la uzoefu huu au ufahamu wa uzoefu huu unaweza kuuhamisha na kuutumia katika maisha yako yote? Maisha yako yatakuwaje tofauti kutokana na uzoefu huu? Tabia ya kuuliza itakuwa na faida za kiroho pia za kuwasaidia watu kuona kuwa Mungu anahusika na maisha yao kila siku katika maeneo yote. Hili ni jambo muhimu sana katika kuwasaidia watu ili waishi maisha yanye kusudi zaidi." (Ibid.: 103) Kazi ya kanisa katika kufunza washirika wake katika maeneo haya ni muhimu. Umuhimu wa mahusiano na kupendana unajadiliwa kwa kina katika sehemu ya "Uwakili wa Mahusiano" katika kitabu cha ECLEA, *Uwakili wa Kibiblia* (http://www.eclea.net/courses.html#stewardship).

**D.** ***Asili na tabia ya wanafunzi waliokomaa***

Wanafunzi wote lazima wawe *"watu waaminifu [Gr. = anthrōpois (inamaanisha, watu wa jinsia zote; wanadamu)] watakaofaa kuwafundisha na wengine"* (**2 Tim 2:2**). "Safari iendayo kwenye uanafunzi wa kweli huanza mtu anapozaliwa mara ya pili" (MacDonald 1975: 4). Kwa hali yoyote, Yesu "hatafuti wanaume na wanawake ambao watampa muda wa mabaki wa jioni—au siku za mwishoni mwa wiki—au miaka yao ya kustaafu. Kwa hakika anawatafuta wale watakaompa nafasi ya kwanza katika maisha yao." (Ibid.: 5) Biblia hutoa sifa kadhaa za mwanafunzi wa kweli:

1. <u>Upendo wa juu Zaidi kwa Yesu kupita hata tunavyowapenda walio karibu nasi.</u> *"Kama mtu akija kwangu naye hamchukii baba yake, na mama yake na mke wake, na mwanawe, na ndugu zake waume na wake; naam, nafsi yake mwenyewe, hawezi kuwa mwanafunzi wangu."* (**Luka 14:26**; ona pia **Math 19:29; Marko 10:29-30; Luka 18:29-30**). Tamko la Yesu kuhusu "kuchukia" familia yake mtu katika

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

**Luka 14:26** haimaanishi kwamba mwanafunzi aidharau familia yake au awaone wao ni maadui wake.[17] Badala yake, tamko lake ni msemo wa Kiebrania wa kulinganisha ukimaanisha kwamba "kulinganisha upendo wako kwangu, hisia zako kwa wengine wote, ikiwa ni pamoja na wale wa karibu sana kwako, iwe kana kwamba unawachukia—Napaswa kuwa wa muhimu kiasi hicho kwako." Upendo mkuu kwa Yesu huja kutokana na kujiona sisi wenyewe kama tulivyo hasa, yaani, watu tuliopinda na wenye dhambi katika kiini cha maisha yetu, ambao hatuwezi kuibadili hali hiyo kwa juhudi yoyote ili, ambao tumegundua kuwa Yesu ndiye tiba pekee. Henrichsen anahoji, "Ukristo ni dini ya kuokoa. Imetengenezwa kwa ajili ya wahitaji hasa. Ni kwa ajili ya watu ambao wana uhitaji wa kitu zaidi ya vile wanavyoweza kupata katika maisha kwa juhudi yao wao wenyewe. . . . Hitaji moja kuu na muhimu kwa mwanafunzi wa kweli ni ile hali ya uhitaji inayowaka katika vilindi vya moyo wake." (Henrichsen 1988: 36-37)

2. <u>Kujikana nafsi ili kumfuata Yesu.</u> *"Akawaambia wote, Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate. Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake ataiangamiza, na mtu atakaye iangamiza nafsi yake kwa ajili yangu ndiye atakayeisalimisha."* (**Luka 9:23-24**; ona pia **Math 10:38-39; 16:24-25**) Tamko la Yesu kuhusu "mtu kuubeba msalaba wake" linaweka wazi kwamba hata maisha ya wanafunzi wenyewe yalikuwa nafasi ya pili na utii kwa Yesu. Jonathan Dodson anabainisha, "Katika dola ya Kirumi ilikuwa ni kawaida kwa wafungwa kubeba misalaba wanapoelekea kwenye eneo la kuuwawa. Kubeba msalaba hadharani ilionyesha *unyenyekevu* wa mhalifu kwa dola, unyenyekevu wake mbele ya mamlaka inayotawala. . . . Kwa mwanafunzi kubeba msalaba wake, wakati huo, haikuwa tu tendo la *kujikana nafsi* lakini, muhimu zaidi, *kujisalimisha* kwa Yesu kama mamlaka inayotawala, kama Bwana wako. Ni kusema hapana kwa mamlaka juu yako mwenyewe, kujifuata mwenyewe, na ndio kwa mamlaka ya Yesu—hapana kwa mapenzi yako mwenyewe na ndio kwa mapenzi yake." (Dodson 2012: 160n.17) George Ladd anaongeza, "Yesu alipofundisha kwamba ili mtu awe mwanafunzi wake lazima ajikane mwenyewe na kubeba msalaba wake mwenyewe (Math. 10:38; 16:24), hakuwa anazungumzia kujikataa au hali ya kubeba mizigo mizito; alimaanisha kuwa tayari kufa kwa ajili ya kule kumwamini. Msalaba haukuwa kitu kingine bali kifaa ambacho kwacho mauti ingewapata. Kila mwanafunzi wa Yesu kwa asili ni mfiadini." (Ladd 1972: 104) Ingawaje idadi kubwa ya Wakristo hawatapitia mateso kimwili hata kuuawa kwa ajili ya imani yao, lazima watarajie na kuwa tayari kuteswa (mfano, **Math 5:10-12; 10:22; Marko 10:30; Luka 6:22; Yoh 15:18-19; 2 Kor 4:8-12; Fil 1:28-30; 2 Tim 2:3; 3:12; 1 Pet 4:12-16; 1 Yoh 3:13**).

Katika maisha yake yote hapa duniani Yesu alifanya yale tu ambayo Baba alimwagiza kufanya (**Yoh 5:19, 30; 6:38; 8:28; 12:49; 14:10**). Hali kadhalika, Yesu akasema, *"Mkinipenda, mtazishika amri zangu"* (**Yoh 14:15**; ona pia **Math 12:50; 28:19-20; Marko 3:35; Luka 17:10; Yoh 14:21, 23-24; 15:10, 14; 1 Yoh 5:3; 2 Yoh 6**). "Kumfuata" Yesu maana yake tunatakiwa tuongozwe na Roho Mtakatifu ili tuwaze kama Kristo alivyowaza, tuhisi kama alivyohisi na tutende kama alivyotenda. Maisha ya jinsi hiyo yatadhihirishwa na *"tunda la Roho"* (*"upendo, furaha, amamni, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, [na] kiasi"*) (**Gal 5:22-23**). Viwango na vipaumbele vya Yesu yabidi viwe viwango na vipaumbele vyetu. Lengo la mwanafunzi wa kweli sharti liwe kama lile ambalo Mungu amelitamka katika Biblia, yaani, "kuutafuta kwanza ufalme wa Mungu na haki yake" (**Math 6:33**). Kuishi maisha ya aina hii ni kipimo halisi kinachoonyesha ya kuwa tuko katika uelewano na sauti ya Roho wa Mungu. Hili linapokuwa kweli katika maisha yetu, mfano, "tunapokaa ndani yake" (**Yoh 15:4-7**), *"tutafananishwa na mfano wa [Yesu Kristo]"* (**Rum 8:29**) *"tutazaa matunda mengi, na kuthibitisha kuwa tu wanafunzi wake"* (**Yoh 15:8**).

3. <u>Kuacha vitu vyote tulivyonavyo ili kumfuata Yesu.</u> *"Basi kadhalika kila mmoja wenu asiyeacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu"* (**Luka 14:33**; ona pia **Math 19:16-26, 29; Marko 10:17-25, 29-30; Luka 18:18-27, 29-30; Matendo 2:44-45; 4:32, 34-35; 2 Tim 2:4**). Kwa kuwa tunapaswa kumpenda Yesu kuliko wale walio karibu na sisi na hata kuliko maisha yetu wenyewe, inakuwa kwamba vilevile tunapaswa kumpenda Yesu kuliko kitu chochote tunachoweza kuwa nacho. Ingawaje kumpenda Yesu kuliko wale tuwapendao na kuliko tunavyojipenda inaonekana kuwa juu zaidi ya kumpenda Yesu kuliko vitu ambavyo tungekuwa navyo, Yesu anajua moyo wa mwanadamu (**Yoh 2:24-25**) na hivyo alisema, *"Kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwa na moyo wako"* (**Math 6:21; Luka 12:34**). Katika kuyajua hayo, zaidi ya miaka 150 iliyopita J. B. Wakeley anabainisha

[17] Kumbuka kwamba tunapaswa "kuwapenda jirani zetu kama nafsi zetu" (**Math 19:19; 22:39; Marko 12:31**) na "kuwapenda adui zetu" pia (**Math 5:44-47**). Matamko hayo huonyesha ni kwa kiwango gani upendo wetu unapaswa kuwa kwa ajili ya Kristo: tunapaswa kumpenda kila mmoja, zaidi ya hayo kumpenda Kristo zaidi, ukilinganisha na upendo wetu kwake, upendo wetu kwa wengine ni kama kuwachukia.

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

kwamba "unapookoka kila kitu ispokuwa pochi ni kutookoka kabisa" (Wakeley 1858: 152). Kwa hiyo, **Luka 14:33** "inaweza kuwa ni kifungu kisichopendwa kati ya vifungu vote vya uanafunzi ndani ya Biblia. . . . Kuacha vyote inamaanisha nini? Inamaanisha kuacha vitu vyote ambavyo si vya lazima na ambavyo vinaweza kutumika katika kueneza injili. Mtu anayeacha vyote hawi lofa asiyejimudu; anafanya kazi kwa bidii kwa ajili ya mahitaji yake na ya familia yake. Lakini kwa kuwa shauku ya moyo wake ni kuendeleza ujumbe wa Kristo, anawekeza kila kitu kilicho juu ya mahitaji yake kwenye kazi ya bwana na kuuacha wakati ujao mikononi mwa Mungu." (MacDonald 1975: 9) Na ndio maana Yesu alikazia umuhimu wa kuhesabu gharama ya kuwa mwanafunzi kwa makini kabla ya kudiriki kuwa mwanafunzi (ona **Luka 14:28**). Maana ya kiroho ya mwenendo wetu kuhusiana na maswala ya pesa na umiliki wa vitu ni jambo muhimu sana kuliko tunavyoweza kulielezea. Paulo analiweka hivi, *Maana wengi huenenda, ambao nimewaambiaeni mara nyingi habari zao, na sasa nawaambia hata kwa machozi kuwa ni adui za msalaba wa Kristo; mwisho wao ni uharibifu, mungu wao ni tumbo, utukufu wao u katika fedheha yao, waniao mambo ya dunia"* (**Fil 3:18-19**; ona pia **Yak 4:4; 1 Yoh 2:15**). Kwa maneno mengine wale *"waniao mambo ya dunia"* ni *"maadui wa msalaba wa Kristo,"* na *"mwisho wao ni uharibifu."*

4. <u>Upendo mkubwa kwa wale wote walio wa Kristo.</u> *"Amri mpya nawapa, Mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo. Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi."* (**Yoh 13:34-35**; ona pia **Yoh 15:12, 17; 1 Yoh 2:9-10; 3:14**) Charles Colson anaeleza, "Tupofanyika kuwa wafuasi wa Kristo, tunakuwa washirika wa kanisa lake—Kujitoa kwetu kwa kanisa hakutofautishwi na kujitoa kwetu kwake [ona **Math 16:15-18; 22:36-40; 25:31-46; Matendo 20:28; 1 Kor 12:12-27; Gal 6:10; 1 Yoh 3:14; 4:19-20**]" (Colson 1992: 64-65). Sababu ya hili ni kwamba waamini wote wamefanywa kuwa wana katika familia ya Mungu (**Rum 8:15, 23; 9:4; Gal 4:5; Efeso 1:5; 2:19**). Kwa hiyo, kanisa ni familia (**Gal 6:10; 1 Tim 3:15; 5:1-2; Ebr 3:6; 1 Pet 4:17**). Lewis analieleza kwa namna hii, "Kanisa si *kama* familia; *ni* familia. . . . Hii inaweza kuonekana kwa ukweli kwamba neno *mwanafunzi*, lililoenea sana katika kanisa la kwanza, linapotea baada ya kitabu cha Matendo ya Mitume. Nafasi yake inachukuliwa na neno *ndugu* katika maandiko ya Biblia yaliyofuata baada ya hapo." (Lewis 2015: n.p.)

Familia zinapendana na kuhudumiana. Hata hivyo, makanisa mengi *hayaishi* kama familia. Ukabila, matengano kati ya maskini na matajiri, na migongano kati ya vikundi itokanayo na sababu mbali mbali ni hali inayojidhihirisha kwa kawaida katika makanisa mengi ya mahali pamoja. Tatizo haliishii tu katika matengano yaliyomo katika makanisa ya mahali pamoja. Bali zaidi sana, tatizo la matengano ni baya zaidi miongoni mwa madhehebu tofauti. Hali hii inaathiri ushuhuda wa kanisa kwa dunia kwa kiwango kikubwa. Umoja wetu au kukosa umoja kwetu moja kwa moja huathiri ile hali ya dunia kuamini kwamba Yesu ni Masihi wa Mungu (ona **Yoh 17:21, 23**). Kama kanisa haliwatendei washirika wake, na makanisa mengine, kama ndugu wapendwa wa familia moja, basi dunia itaendelea (kihalali) kulidhihaki kanisa na kuuliza: "Kwa nini tuwe Wakristo, wakati ninyi Wakristo wenyewe hampendani?"

5. <u>Moyo wa kiutumishi.</u> *"Lakini Yesu akawaita, akasema, Mwajua ya kuwa wakuu wa Mataifa huwatawala kwa nguvu, na wakubwa wao huwatumikisha. Lakini haitakuwa hivyo kwenu; bali mtu yeyote atakaye kuwa wa kwanza kwenu awe mtumwa wenu; kama vile mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi."* (**Math 20:25-28;** ona pia **Marko 10:42-45**) *"Wala msiitwe viongozi; maana kiongozi wenu ni mmoja, naye ndiye Kristo. Naye aliye mkubwa wenu atakuwa mtumishi wenu."* (**Math 23:10-11;** ona pia **Marko 9:35-37**) *"Ninyi mwaniita, mwalimu, na, Bwana; nanyi mwanena vema, maana ndivyo nilivyo. Basi ikiwa mimi, niliye Bwana na Mwalimu, nimewatawadha miguu, imewapasa vivyo kutawadhana miguu ninyi kwa ninyi. Kwa kuwa nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo."* (**Yoh 13:13-15**)

Yesu alisema kwamba amri mbili—mpende Mungu kwa moyo wako wote, nafsi, na akili na mpende jirani yako kama nafsi yako (**Math 22:36-40; Marko 12:28-34; Luka 10:25-28**)—ni misingi kwa Biblia yote. Mungu hadanganywi na maneno yetu. Kwa hiyo, ametupa kipimo ambacho kwacho, sisi na kila mtu mwingine, na Mungu mwenyewe tunaweza kuona wazi wazi endapo, kwa kweli, tunampenda Mungu kwa moyo, nafsi, na akili. Kipimo ni hiki: namna tunavyotekeleza "amri ya pili" (inamaanisha, kwa namna gani tunawapenda watu) ni ushahidi kwamba tunatekeleza "amri ya kwanza" (inamaanisha, kumpenda Mungu). Hata Yesu alipomkabili Petro na kuumuliza mara tatu *"Wanipenda?"* Yesu hakukubali majibu ya Petro kirahisi, *"Naam, Bwana, wewe wajua kuwa nakupenda."* Badala yake, Yesu hatimaye anamwambia Petro, *"Lisha wana-kondoo wangu"* (**Yoh 21:15-17**). Kile ambacho Yesu alikuwa anamwambia Petro ni hiki: "Ikiwa kweli unanipenda, basi

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

utathibitisha upendo wako kwa kuwahudumia kondoo wangu."

Kusudi la Mungu kusimika vipawa vya kiroho mbalimbali na viongozi ni *"kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu hata kazi ya kuduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe"* (**Efeso 4:12**). Wale wenye moyo wa utumishi "huwalenga wengine, si wao wenyewe. Huu ni unyenyekevu wa kweli: si kujifikiria kwamba hatuwezi bali kutoufikiria *ukosefu* wetu. . . . Hii ndiyo maana ya 'kuipoteza nafsi yako'—kuisahau nafsi yako unapowahudumia wengine. Tunapoacha kuona mahitaji yetu, tunapata kuelewa mahitaji yanayotuzunguka." (Warren 2002: 265) Katika kuelewa hili, mifano kadhaa ya Yesu kuhusiana na ufalme wa mbinguni huonyesh kwamba hukumu ya mwisho itahusika na yale tunayotenda, hasa kuhusu namna tunavyowahudumia na kuwatendea wengine katika maisha haya (**Math 18:23-35; 21:28-32; 21:33-44; 24:45-51; 25:1-13; 25:14-30; Marko 12:1-12; Luka 12:42-48; 16:1-9; 19:12-27; 20:9-18**). Hii ni kwa sababu kile tunachofanya, namna tunavyowatumikia na kuwatendea watu wengine hudhihirisha kile hasa tunachofikiri kuhusu Yesu. Yesu alisema, *"kwa kadiri mlivyomtendea* [inamaanisha, mlionyesha huruma na kuhusika] *mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea Mimi"* (**Math 25:40**), na *"Kadiri msivyomtendea mmojawapo wa hao walio wadogo, hamkunitendea mimi"* (**Math 25:45**). "Hakuna ambacho kingedhihirisha kwa uwazi zaidi kuliko jinsi matendo ambayo Mungu anayakubali yanapotendwa kwa kawaida kutokana na uhusiano mzuri na Mungu. Ni kile anachofanya mtu pasipo kutaka kutambuliwa ndicho huonyesha moyo wake kwa kweli." (Travis 1982: 191)

Moyo huu wa kiutumishi na mtindo wa maisha wa mwanafunzi aliyekomaa, ambaye hutumikia bila kuhitaji kutambulika, kujengeka kadiri mtu anavyozidi kumpenda Yesu na anavyoendelea kuuona utambulisho wake ndani ya Yesu. Mwanafunzi anajua kwamba kwa sababu kila mwanadamu ameumbwa kwa "mfano wa Mungu" (**Mwz 1:26-27; 5:1-3; 9:6; Efeso 4:24; Kol 3:10; Yak 3:9**), namna tunavyoutendea mfano wa Mungu huonyesha jinsi tunavyomfikiria Mungu. Kadiri Yesu anavofanyika fokasi yetu, tunaanza kufikiri kama Yesu alivyofikiri na kutenda kama Yesu alivyotenda. Hivyo, *"kama vile mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika"* (**Math 20:28**), vivyo na sisi—na Mungu atamkumbuka na kumheshimu wanafunzi wake wanaowatumikia wengine kwa mioyo ya upendo na uhiari (**Zab 100:2; Yoh 12:26; Ebr 6:10**). Henrichsen anahitimisha, "*Mwanafunzi ni yule ambaye wakati wote ana mahusiano na watu wenye mahitaji.* Kama mwanafunzi wa Yesu, je unatatua mahitaji ya watu wengine wakati wote?" (Henrichsen 1988: 32, mkazo kwenye nakala ya asili)

Mfano rahisi, ingawa wenye utata kiutamaduni, ni hasa kuhusu waume kuwasaidia wake zao wanapokuwa katika hali ya maumivu ya kujifungua, kwa sababu **Efeso 5:28** inasema kwamba "*waume nao kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe."* Katika tamaduni nyingi, wanawake wanatarajiwa kufanya kazi zaidi za nyumbani mbalimbali kwa ajili ya familia (kwa mfano, kuleta kuni, kuteka maji, usafi wa mazingira, pamoja na kuzaa na kulea watoto wengi). Hii huchosha na ni ngumu kwa mwili wa mwanamke. Ikiwa waume *"wanawapenda wake zao kama wanavyoipenda miili yao"* kiukweli, wasingewafanyisha kazi ngumu, kuumiza miili yao. Badala yake, wangefanya baadhi ya hizo kazi wao wenyewe. Itasaidia kuutunza mwili wa mwanamke, kazi itafanyika kwa haraka, na kawapa fursa mume na mke kuwa na muda Zaidi wa kujenga mahusiano yao katika kipindi ambacho hakuna kazi ya kufanya.

6. Kuendelea katika Neno la Mungu. *"Ninyi mkikaa katika Neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli"* (**Yoh 8:31**; ona pia **Yoh 14:26; 2 Yoh 9**). Neno la Mungu ni kweli (**Yoh 17:17**). Maneno ya Mungu *"ni uhai kwa wale wazipatao"* (**Mith 4:22**). Ni *"furaha kwangu, na shangwe ya moyo wangu"* (**Yer 15:16**). Neno lake ni taa na nuru inayoongoza (**Zab 119:105**). Mungu ameliinua Neno lake na Jina lake juu ya vitu vyote (**Zab 138:2**). *"Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema"* (**2 Tim 3:16-17**). Kwa kuwa Kristo "ni uzima wetu" (**Kol 3:4**), twapaswa "kukaa ndani yake" na maneno yake "yakae ndani yetu" (**Yoh 15:7**). Kukaa kunamaanisha kuvumilia. Yesu mwenyewe alitekeleza haya kimatendo yeye ambaye aliyajua maandiko "kwa kwenda mbele na kwa kurudi nyuma." Yesu alinukuu kutoka katika mistari tofauti ya Maandiko isiyopungua 60 (ikimaanisha, AK) na kutoa dokezo angalau mara mbili hiyo pamoja na nukuu za kiujumla (Moyise 2010: 3-4). Hata alipokuwa akifa, Yesu alinukuu Maandiko (**Math 27:46; Marko 15:36**, akinukuu **Zab 22:1; Luka 23:46**, akinukuu **Zab 31:5**). Kwa kuwa hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa Yesu, si zaidi sana ingepasa kuwa hivyo kwetu sisi. Hivyo inatupasa kujiuliza: Je tunasikia Biblia ikifafanuliwa kwa usahihi kanisani? Je tuna vipindi vya kusoma Biblia mara kwa mara? Je tunajifunza Maandiko kimpangilio? Je tunakariri Maandiko? Je tunatafakari yale tunayoyasoma? Kiu yetu ya Biblia ni kubwa mno kiasi ambacho haiwezi kutoshelezwa? Mchoro

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

hapo chini unatuongoza kwa kifupi jinsi mwenendo wetu kuelekea na kuwa na mahusiano na Biblia kwa kuilinganisha hali hiyo na vidole vitano vya mkono. Tunahitaji: *kusikia* neno likihubiriwa (**Matendo 10:17**, kidole kidogo); *husoma* Neno (**Ufu 1:3**, kidole cha pete); *kujifunza* Neno (**Matendo 17:11**, kidole cha kati); *hukariri* Neno (**Zab 119:9, 11**, kidole cha shahada); na *kutafakari* Neno (**Zab 1:2-3**, kidole gumba) (Navigators 2004: "The Word Hand").

"Kukaa" katika Neno la Mungu inamaanisha zaidi ya ustahimilivu wa kusikia, kusoma, *kujifunza*, kukariri, na kutafakari Maandiko; kukaa maana yake ni kuliishi Neno katika maisha yetu. Kwa maana nyingine, Biblia itufinyange—mioyo yetu, fahamu, na vitendo—na iwe kipimo ambacho kwacho tunayatambua yaliyo sahihi na yasiyo sahihi na yepi tufanye na yepi tusifanye. Henrichsen anasema, "*Mwanafunzi ni yule ambaye huongozwa na Biblia katika kila eneo la maisha yake katika kuamua yale yaliyo sahihi na huyaishi hayo wakati wote* badala ya kuruhusu matukio yatengeneze mwenendo wake" (Henrichsen 1988: 32, mkazo kwenye nakala ya asili). Yesu alisema, *"Basi kila asikiae hayo maneno yangu, na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake kwenye mwamba; mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, isianguke; kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba. Na kila asikiaye hayo maneno yangu asiyafanye, atafananishwa na mtu mpumbavu, aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga; mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, ikaanguka; nalo anguko lake likawa kubwa."* (**Math 7:24-27**; ona pia **Luka 6:47-49**) Yakobo anaiweka hivi, *"Lakini iweni watendaji wa Neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu. . . . Lakini aliyeionasheria kamilifu iliyo ya uhuru, na kukaa humo, asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake."* (**Yak 1:22, 25**; ona pia **Rum 2:13**)

Mchoro kiongozi unaainisha maisha yaliyo na mpangilio, na yenye afya kiroho ya mwanafunzi wa Kristo kama gurudumu, kwa namna hii:




Kitovu ni Kristo—kiini cha kila kitu, inamaanisha, hali ya kujiachia kabisa katika mamlaka yake. Ukingo ni kujiachia kabisa katika ubwana wake na mamlaka yake. Ukingo ni utii wetu kwa Kristo katika maeneo yote maisha yetu (kupitia, maneno, na matendo). Njukuti za wima (Neno na Maombi) ni namna tunavyohusiana na Mungu. Njukuti mlalo (kushuhudia na ushirika) ni namna tunavyohusiana na wengine (Navigators 2006: "Gurudumu").

## VI. <u>Mambo Muhimu kuhusu Mafunzo Bora ya Kufanya Wanafunzi</u>

"Hakuna afanyaye wanafunzi kwa bahati. Kufanya watu kuwa wanafunzi ni kazi ya makusudi. . . . Neno la Kiyunani la 'mwanafunzi' [ni] *mathetes.* Ikitafsiriwa moja kwa moja, inamaanisha *anaejifunza.* Hapa Maandiko yanatuambia kitu fulani, kitu fulani kuhusu kuyapanga maisha yetu kwa namna ya kuwa *wajifunzaji wa Yesu wa maisha.* . . . Inaonekana kuna njia tatu tofauti ambazo kwazo twajifunza, lakini kwa upande mwingine tunajifunza vizuri zaidi kunapokuwa na mwingiliano kati ya zote tatu kwa wakati mmoja:

(1) Darasani/Mhadhara wa kuhamishia maarifa
(2) Uanagenzi
(3) Mzamo

Ujifunnzaji wa darasani ni wakati taarifa, michakato na kweli hufundishwa kutoka kwa mwalimu kwenda kwa wanafunzi katika mfumo uliozoeleka wa mhadhara. Uanagenzi ni wakati mtu anapojifunza taaluma fulani kwa kujiambatanisha na mtu mwenye taaluma hiyo. Mzamo ni wakati mtu anapowekwa katika mazingira, mfumo au tamaduni na anajifunza kwa uzoefu wa kile anachoona au kupitia." (Breen 2011: 20-21, mkazo kwenye nakala ya asili)

Kujifunza kweli, fundisho, na habari kuhusu Kristo na Ukristo ni *muhimu* hakika, lakini hiyo hiyo *haitoshi* kumfanya watu wawe wanafunzi wazuri.. "Tunapomsikiliza mwalimu au mnenaji wa Biblia mwenye kipawa, tunaweza kutoka tumehuishwa na kutiwa moyo. Tunaweza hata kuwafunza wengine katika mazingira haya. . . . Lakini kumbuka, uanafunzi unahitaji zaidi ya mabadiliko ya kichwani. Yesu alisema katikaMathayo

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

4:19 ya kuwa atatufanya kuwa kitu kingine tofauti kabisa—ya kwamba tutakuwa na mabadiliko moyoni na katika mikono pia. . . . Watu wengi si wajifunzaji wasikivu na hupata shida kuwa na foksi wakati wowote ule, hasa hasa katika nyakati hizi ambazo watu wanataka vitu vitendeke kwa haraka. Wakufunzi wa wanafunzi wenye mafanikio kamwe hawataacha utaratibu wao wa kutoa maelekezo, lakini wanaelewa mipaka yake." (Putnam 2010: 48)

Kwa Yesu, *mahusiano* yalikuwa ndicho kiini cha kuadibisha wafuasi wake. "Yesu alikuwa kielelezo cha umuhimu wa mahusiano kwa namna alivyowafunza wanafunzi wake. . . . Alizungumza kuhusu kweli walipokuwa wakila na walipokuwa wakilala. Yesu alikuwa *na* wanafunzi wake kwa sababu uhusiano wake nao ulikuwa ndio mfereji wa kupitishia vyote walivyokuwa wanahitaji. . . . Aliwekeza katika maisha ya Kumi na wawili. Alichagua kuwa katika mahusiano na wanafunzi wake kwa sababu alielewa kwamba tabia huambukizwa kwa urahisi zaidi kwa matendo kuliko kufunzwa kwa maneno." (Ibid.: 48-49) Na kilichotokea baada ya kutumia muda wake nao, na kuwafunza kwa njia rasmi na zisizo rasmi, na kuwa kielelezo kwao, wanafunzi wa Yesu hatimaye walikuwa kama yeye na *"walioupindua ulimwengu"* (**Matendo 17:6**, NKJV). Kama wale Kumi na wawili, wanafunzi wazuri hutengenezwa wanapotendea kazi waliyojifunza na kuyaishi yale wanayoyaamini. Breen anaielezea hivi: "Je utamwamini daktari mwenye elimu ya darasani tu bila uzoefu wa kimatendo akufanyie upasuaji wa moyo? *Hata hivyo ndivyo ambavyo tumeuweka mfumo wa mchakato wa uanafunzi!"* (Ibid.: 26, mkazo kwenye nakala ya asili)

Ili utengenezaji wa wanafunzi ufanikiwe, uongozi wa kanisa lazima uone umuhimu wa kutengeneza wanafunzi na uweke nguvu zake katika hilo na kujihusisha kikamilifu katika mchakato wa uanafunzi. Kama ambavyo shirika la uanafunzi la Churches Alive linavyoelezea, "Mafanikio ya huduma ya kufanya wanafunzi hatimaye yanahusiana na baraza lako la utawala na umiliki wao wa huduma. Ikiwa kuwafanya wanafunzi kutachukuliwa kama kipindi kimojawapo cha kanisa, mpango huo hautafanikiwa. Kama itachukuliwa kama ndio sababu ya kanisa kuwepo, itakuwa, itafanikiwa na kulibadili kanisa kwa kuilea kwa makini. Ili kuwa kanisa linalotengeneza wanafunzi inahusisha kuhamisha mtazamo kutoka katika kulifanya kanisa liwepo na kuwa kituo cha kutengeneza wanafunzi. Hili ni badiliko la kusisimua. Badiliko kutoka Agano la Kale pamoja na mkazo wake wa zama hizo wa nguvu kwa wachache, hadi kanisa la karne ya kwanza ambalo kawaida ilikuwa ni kwamba nguvu za Roho Mtakatifu zilikuwapo kwa waamini wote halishangazi." (Churches Alive 1996: 1.8) Hii inamaanisha uongozi uliopo wa kanisa unahitajika kimatendo utegemeze na kutia moyo (kwa vitu, kwa njia ya maombi, na kwa namna nyinginezo), na kuwa karibu na wale wanaoongoza huduma ya kufunza wanafunzi,[18] na kuwajuza washirika wa kanisa umuhimu wa uanafunzi mara kwa mara.

**A.** ***Vikundi vya kufanya wanafunzi***

Tukio la kufunza wanafunzi linaweza kufanyika katika mazingira yoyote: mtu kwa mtu; kikundi kidogo cha watu wawili hadi wanne[19]; au hata katika chumba kikubwa cha darasa/mihadhara. Hata hivyo kielelezo cha Yesu cha kufunza wanafunzi kilikuwa mtu kwa mtu lakini si kila mmoja alipata nafasi ya kuwa karibu naye sawa na mwingine. Alichagua timu ya wanaume kumi na mbili, lakini hata kati ya timu alikuwa na uhusiano uliokuwa wa karibu zaidi na Petro, Yakobo na Yohana. Zaidi ya wale kumi na mbili walikuwepo sabini na wawili, halafu wale mia na ishirini, na tena walikuwepo makutano. . . . Kwa lugha rahisi, tunawakaribisha watu wachache tu kwenye mahusiano ya kuadibishana nasi. Ikiwa Yesu alikaribisha watu kumi na mbili, tunaweza kusema [kwamba] hatuwezi kufanya zaidi ya alivyofanya yeye." (Breen 2011: 38) Hii inaashiria kwamba kanisa la mahali pamoja lapaswa kuwa na vikundi vya ukubwa tofauti kwa ajili ya majukumu mbali mbali. Kwa mfano, kanisa moja liligundua kwa ukuaji wa kiroho na ukomavu wa waumini wa kanisa uliongezeka kwa kasi baada ya kuanzisha vikundi vya watu 3-4. "Kama wale watu watatu waliokuwa karibu sana na Yesu (Petro, Yakobo, Yohana), kikundi cha Uanafunzi chenye matokeo mazuri huundwa na watu 3 na si zaidi ya waamini 4

[18] Uongozi uliopo wa kanisa unapaswa kufanya mambo yale yale na viongozi wa kufanya wanafunzi kama viongozi wa kufanya wanafunzi wanavyofanya wao kwa wao wanapokutana (ona namba.23, chini).

[19] Ikiwa kanisa lako litaamua kuwa na makundi yenye watu wengi zaidi ya 3-4, hasa ikiwa kundi lina wanaume na wanawake, uzingatie kuwa na viongozi wa kiume na kike wakitenda kazi pamoja: "Uzoefu unaonyesha kwamba kuwatumia mke na mume kama vingozi watendao kazi pamoja katika kundi la kukuza wanafunzi huwa na mafanikio sana. Hii inakubaliana na simulizi ya Mwanzo ya mwanamke kumkamilisha mwanamume na vile vile katika Agano jipya mfano wa kuwatuma wanafunzi wawili wawili. Mwanamume na mwanamke ambao hawajaoana pia wanaweza kuongoza. Lengo lako ni kuchagua viongozi walio bora kabisa ambao unao. Unapokuwa na viongozi wawili unakuwa na jozi mbili za macho na masikio ambazo zitashughulika na masuala ya kikundi. Mtu mmoja anapozungumza, wengine wanaweza kusikiliza. Mmoja anapokuwa amezama katika kuongoza majadiliano, mwengine anaweza kuyaweka majadiliano katika uelekeo unaotakiwa na kusimamia muda. Wawili wanaweza kushauriana na kila mmoja ni chanzo cha wazo la ziada. Wanaweza pia kutegemezana kwa kuombeana na kutiana moyo." (Churches Alive 1996: 4.3)

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

wa jinsia moja ambao wana kusudi la kukua katika Mungu na katika uhusiano wa wao kwa wao. Kiini ni mchakato wa Kibiblia ambao unaweza kujenga na kubadilisha maisha, mtandao wa kufanya wanafunzi wa kiroho na jamii ya watu wa kanisa lako kwa namna ambayo hakuna anayesimama peke yake, anayepambana peke yake, anayejijenga peke yake au kukua peke yake. Tunauita Mchakato Kiini wa Meno 3 wa Kufanya Wanafunzi (K3 = Kundi + Kikundi + Kiini). Huu mchakato wa Kufanya Wanafunzi wa Meno 3 si kitu kipya. Huduma ya Kristo ilikuwa kwa makutano, wale 12, na wale watatu (Kundi + Kikundi + Kiini).” (Kufanya Wanafunzi Kiini au: “Kiini cha Meno 3”) Kanisa moja kubwa lina vikundi vya ukubwa tofauti kwa ajili ya kazi mbali mbali, kama inavyoonekena hapo chini (Mosaic 2016: 7-12):

| **Muktadha** | **Idadi** | **Fokasi** | **Kujifunza kutoka kwa Yesu** | **Mwitikio wa Kanisa** | **Matokeo** |
|---|---|---|---|---|---|
| Hadhara | 100 (mamia) | Kuhubiri, Kweli, Kuabudu | Yesu na makutano | Makusanyiko, Matukio | Mvuto, Kusherehekea, Mwendo |
| Jamii | 20-70 | Kuchunga, Kufunza, Kuhamasisha | Yesu na wale 70 | Makundi mbali mbali, Timu za Huduma, Madarasa ya Kufunza | Kuzidishwa, Misheni, Mguso |
| Binafsi | 12-18 | Kutegemeza, Kutia changa moto, kutendea kazi | Yesu na wale 12 | Jamii za Kimisheni, Makundi ya Wanaume/Wanawake, Makundi ya Kutegemeza | Kujitoa, Misheni, Jamii |
| Hali ya uwazi | 2-5 | Kujihatarisha, Uwajibikaji, Kukua | Yesu na wale 3 | Marafiki wa kina, Ndoa, Makusudi Uanafunzi | Mahusiano ya karibu sana, Kubadilishwa, Ukomavu |
| Uungu | Pekee na Mungu | Kuwa na Muumba na Mkombozi wako | Yesu na Baba | Mwindo wa binafsi | Mahusiano ya karibu sana, Utambulisho, Kujitoa |

Utafiti zaidi ya mmoja unaonyesha kwamba *muktadha bora* wa uanafunzi wanye kubadilisha maisha ni ule wa mwalimu na wanafunzi 2-3 (wanaojifunza).[20]

1. <u>Biblia imetilia mkazo umuhimu wa “wawili au watatu” kwa kurudiarudia</u> Biblia inaonyesha kwamba yafuatayo yote yana nguvu zaidi katika makundi ya watu 2-3: jamii (**Mhubiri 4:9-12**); uwajibikaji (**1 Tim 5:19**); utawala wa fedha (**2 Kor 8:16-24**); utunzaji wa siri (**Math 18:15-17**); uwezo wa kuhilimi mabadiliko (**Math 18:20**); mawasiliano (**1 Kor 14:26-33**); uelekeo (**2 Kor 13:1**); uongozi (**1 Kor 14:29**); umisheni (**Luka 10:1; Matendo 13:2-4**) (ona Cole 2011: n.p.).

2. <u>Faida za kundi dogo (watu 3-4) ni pamoja na hizi zifuatazo:</u>
   - “Kuna kuhama kutoka shinikizo lisilo asili kuelekea kwenye ushiriki ambao ni asili wa mwalimu. Mtu wa tatu au wa nne anapoongezwa, mwalimu hawi tena fokasi, bali wao ni sehemu ya mchakato wa kundi.”
   - “Kuna kuhama kutoka ngazi za mamlaka na kwenda kwenye mahusiano ya kiwenza. Seti ya watu watatu/wanne kwa kawaida hutengeneza hali iliyo rahisi ya safari ya kwenda na mtu sambamba. Fokasi haiko sana kwa mwalimu kama ambavyo iko kwa Kristo ambaye sote tunaelekeza maisha yetu kwake.”
   - “Kuna kuhama kutoka mjadala na kwenda kwenye kubadilishana kuliko na nguvu. Katika jaribio langu la awali na seti za watu watatu, mara nyingi nilitoka katika nyakati hizo nikijiambia, ‘Ni nini kilifanya mabadilishano yale kuwa hai na yenye nguvu namna ile?’ Uwepo wa Roho Mtakatifu ulionyesha kuhusika. Uhai na nguvu ulisababisha mabadiliko. Kwa kadiri ambavyo nimeielewa nguvu ya kundi, mtu kwa mtu si kundi. Ni wakati tu unapoongeza mtu wa tatu ndipo hapo unapokuwa na alama ya kwanza ya kuwa na kundi (Fikiria Utatu).”
   - “Kuna kuhama kutoka uingizaji wenye mipaka na kwenda kwenye hekima ndani ya namba. Kitabu cha Mithali kinazungumzia kuhusu hekima ambayo hutoka kwa washauri wengi (Mithali 15:22). Mara nyingine wale wanaodhaniwa kuwa ni wadogo au wachanga katika imani ndiwo kwao

---

[20] Kama tutakavyoona katika sehemu **B. *Sifa za kundi zuri la ufunzaji wanafunzi*** na **D. *Mchakato wa kufanya wanafunzi wapaswa kujizalisha wenyewe***, uhusiano kati ya mwalimu na wanafunzi si wa ngazi za kimamlaka. Badala yake, ni uhusiano wa ushirikishanaji wa majukumu na wajibu ambao kwa huo wanafunzi hupewa ziada ya mamlaka kwa ajili ya kuongoza kundi.

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

hekima kubwa hutoka, au cheche mpya za uhai au maswali makubwa."

- "Kuna kuhama kutoka kuongezeka na kwenda katika kuzidishwa. Kwangu mimi hakuna furaha iliyo kuu kuliko ile ya Mkristo kuzaa tunda la kiroho. Hayo yote hapo juu yakijumlishwa tunapata kitu kinachoitwa kutiwa nguvu. Kwa sababu zaidi ya miongo miwili, nimeona kiasi cha uzalishaji cha 75% ambacho ni adimu kupitia seti za watu watatu/wanne za muundo wa kufanya wanafunzi."
- Kwa kifupi, kundi dogo huhamasisha uzidishaji kwa sababu linapunguza kwa kiasi kikubwa ngazi za kimamlaka na kuongeza hali ya muundo wa malezi ya kiwenza. Kwa kutoa mtaala wa 'Kufanya Wanafunzi' ambao umeandaliwa mahususi kwa kujenga mahusiano ya karibu, inafanya muundo rahisi wa uzalishaji, ambao karibu kila mwamini anayekua anaweza kuuongoza. Uongozi katika haya makundi unaweza kuwa wa kupokezana mapema tu kwani ukubwa wa kundi hurahisisha mwingiliano usio rasmi na mtaala unatoa mwongozo wa kuufuata." (Ogden 2007: 4-5)

3. <u>Kundi dogo (watu 3-4) linafaa zaidi kwa uadibishaji wa mtu kwa mtu kwa sababu zifuatazo:</u>
   - Katika mfumo wa mtu kwa mtu mwalimu ndiye mwenye kuwajibika kabisa kwa maswala ya kiroho ya huyu mwingine.
   - Uhusiano wa mtu kwa mtu huweka mfumo wa ngazi za mamlaka ambazo hupelekea kutegemeana.
   - Mfumo wa mtu kwa mtu huweka mipaka ya mahojiano na kubadilishana mawazo.
   - Mfumo wa mtu kwa mtu hutengeneza mtazamo wa aina moja.
   - Mfumo wa mtu kwa mtu kiujumla kwa kawaida hauzalishi (Ogden 2007: 3).
4. <u>Kundi dogo (watu 3-4) ni bora pia kuliko kundi kubwa kwa sababu kadiri kundi linavyokuwa kubwa ndivyo ambavyo nyanja tatu zifuatazo ambazo hupelekea uletaji wa mabadiliko hudhofishwa:</u>
   - *Kweli*—"Kiwango cha ujifunzaji huwa sambamba na kiwango cha uwezo wa kuipata kweli, jambo ambalo huwa gumu sana ikiwa kuna sauti nyingi zinazochangia katika kutoa ile kweli. Na inakuwa vigumu zaidi kuweza kufuatilia hali na kiwango cha ujifunzaji, kwa kadiri kundi linavyozidi kuongezeka."
   - *Mahusiano yenye uwazi*—"Hali ya kuwa wazi ni muhimu sana ili kuleta mabadiliko, uwazi unakuwa mgumu kwa kadiri kundi linaavyokuwa kubwa. Tunapokosa uhuru wa kueleza yale yanayotusonga, Roho hataweza kuwatumia wana kikundi kwa ufanisi kuhudumia wale wenye mahitaji."
   - *Kuwajibika kwa pamoja*—"Kwa kadiri kundu linavyokuwa kubwa ndivyo inakuwa rahisi kwa mtu kujificha. Uwajibikaji huhitaji kuona andapo watu wanatekeleza majukumu waliyopangiwa, au watu bado wanajitoa kutii. Idadi kubwa hupunguza ule uwezo wa kufuatilia maisha ya mtu mmoja mmoja." (Ogden 1998: 11)

**B.** ***Sifa za vikundi vizuri vya kufanya wanafunzi***

Sababu mbalimbali zinazofanya kikundi cha uanafunzi kiwe kizuri:

1. <u>Mahusiano katika kufanya wanafunzi yanaonekana kwa urafiki wa karibu sana, wakati ambapo programu huwa na hali ya kujihusisha na habari zaidi.</u> "Programu hutenda kazi kwa kuamini kwamba ikiwa mtu ana habari zaidi basi hiyo moja kwa moja itamfanya kubadilika. Kwa maana nyingine fundisho sahihi litazalisha maisha sahihi. Kuwajaza watu maandiko kichwani na kanuni za kibiblia kutasababisha mabadiliko ya nwenendo, viwango na moyo wa Mungu." (Ogden 2007: 6) Kuelewa Biblia na kanuni za Biblia ni sawa na muhimu; hata hivyo, hilo pekee halitoshi kutengeneza wanafunzi wazuri. Utengenezaji wa wanafunzi unahitaji mahusiano. Yesu hakufundisha tu Biblia kwa wanafunzi wake bali alikuwa na mahusiano ya karibu nao na akawa kielelezo cha yele aliyokuwa akiwafundisha kutoka katika Biblia. Robert Coleman anaielezea kwa namna hii: "Kuwahubiria makutano, ingawaje ni muhimu, kamwe haitalingana na kazi ya kuwaandaa viongozi kwa kazi ya uinjilisti. Wala maombi ya vipindi na madarasa ya wakristo watenda kazi vile vile hayawezi. Kuwajenga watu si kazi nyepesi. Inahitaji ufuatiliaji wa karibu ambao unaendelea, kama ule ambao baba hufanya kwa watoto wake. . . . Mfano wa Yesu unatufundisha kwamba inawezekana tu kwa mtu kukaa karibu na wale anaotaka kuwaongoza." (Coleman 1964: 47)

Matokeo muhimu ya jambo hili ni kwamba wewe (mfunzaji) unahitajika kuwapa watu walio katika kundi lako la kufanya wanafunzi "*nafasi* kubwa kuyaona maisha yako kuliko ile ambayo unawapa watu wengine au kuliko ile ambayo kwa kawaida unawapa wale unaowaongoza kwa wakati ule. . . . Kwa kawaidi ni kama tu kuwakaribisha kufanya kile ambacho tayari unakifanya. Wakaribishe na familia zao kula chakula na familia yako. Mara nyingi tunasahau kwamba hata kama unaweza usiite kuwa ni 'wakati wa kufunza wanafunzi' haimaanisha kwamba hatuwafunzi watu maana ya kumfuata

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

Yesu. Watu watakapokuja nyumbani kwetu watachunguza namna tunavyopendana, namna tunavyolea watoto wetu na namna tunavyoishi. Tunawaingiza katika maisha yetu. Ili hili litokee ni lazima tuwape watu nafasi ya kuyaona maisha yetu ya siku kwa siku. *Ndio maana ni muhimu tuwe na aina ya maisha ambayo yanastahili kuigwaa!*" (Breen 2011: 40, mkazo kwenye nakala ya asili) Kwa kifupi, "Kufanya wanafunzi kunahitaji si tu 'kushiriki imani moja,' bali pia kushiriki maisha yetu—kushindwa na mafanikio, kutotii na kutii" (Dodson 2012: 15).

2. Mahusiano ya kufanya wanafunzi yanalenga katika mchakato wa ukuaji wa kipekee wa mtu mmoja, wakati ambapo programu inakazia utendaji wa kundi kimtandao uthabiti wa usimamizi. "Mahusiano ya kufanya wanafunzi ni muhimu yatofautiane katika urefu wa muda, kwa sababu hakuna watu wawili ambao hukua kwa mwendo unaolingana. Si swala tu la kupitia mtaala kwa usawa, bali mtazamo wa mtu kwa mtu ambao huzingatia mahitaji binfsi ya kila mhusika katika kukua." (Ogden 2007: 7) Walimu wazuri wa kufanya wanafunzi wanahitaji kuweza kutathmini ni wapi kila mwanachama wa vikundi vyao vya kufanya wanafunzi yupo katika safari yake ya kiroho. Jim Putnam anashauri kwamba, ingawaje Wakristo wote wana *thamani* iliyo sawa, si Wakristo wote *wanatumika* sawa katika makusudi ya Bwana. Tofauti iko katika Viwango vyao vya *ukomavu.* (Putnam 2010: 42) Putnam anaona hatua tano za ukuaji wa mwanafunzi (Ibid.: 41-42; ona pia Follwers 2010: "Maisha Halisi" kwa ajili ya chati ambayo inaainisha sifa za ujumla, itikadi za kiimani, tabia, mwenendo, mahitaji ya kiroho, na matamko ambayo huonyesha jinsi kila moja ya hatua hizo tano za kuendelea kiroho zilivyo):

- Hatua 1: *Ufu wa Kiroho*. Mtu hajazaliwa mara ya pili bado. Watu hawa wako katika hali ya kutokuamini, au wanaweza kujua lugha ya Kikristo na hata kwenda kanisani, lakini kutokuamini kwao kutawekwa wazi na kauli wanazotoa, itikadi wanazozishikilia na mambo wanayofanya.
- Hatua 2: *Uchanga Kiroho*. Wakristo wapya wote huanza kama watoto wachanga. Wanaweza kuwa moto sana katika imani yao lakini bado hawajui mambo mengi. Mkristo mpya ni mtoto mchanga hata kama amekuwa akihudhuria kanisani kwa muda mrefu kabla ya kuzaliwa mara ya pili. Watu hawa wanaweza kujua mafundisho mbali mbali ya Kikristo, lakini mafundisho hayo bado hayajakuwa na faida yoyote ya kuwafaa hata kuleta mabadiliko katika maisha yao.
- Hatua 3: *Utoto wa Kiroho*. Wachanga wa kiroho wanapokua, wanakuwa watoto wa kiroho ambao huanza kuelewa lugha za msingi za imani. Mara nyingi wanaweza kuwa wabinafsi kwa mfano wanaweza kufanya jambo sahihi ili kupata kitu fulani wanachotaka au wanaweza kukwepa kitu fulani kwa kuogopa matokeo wasiyoyataka.
- Hatua 4: *Vijana wa Kiroho.*Watoto wa kiroho hukua na kuwa vijana wa kiroho. Wamekua sana na wanaweza kutumika kwa kuamua lakini bado hawawezi kufanya wanafunzi ambao wanaweza kufanya wanafunzi wengine.
- Hatua 5: *Wazazi wa Kiroho.* Hii ni hatua ya mwisho ya kukua. Ukiachilia mbali wazazi wa kiroho ambao *wanaweza* kufanya wanafunzi lakini hawafanyi hivyo, wazazi wa kiroho wameweka kipaumbele katika maisha yao katika misheni ya Yesu kwa kuamua wanafanya wanafunzi wapya.[21]

Kwa sababu mchakato wa kufanya wanafunzi umekusudiwa kumsaidia mwanafunzi kukomaa kiroho, kazi moja ya kiongozi anayefunza ni kuchunguza na kupima ukuaji wa wana kikundi. Hii haipaswi kuwa dhana ngumu: walimu hupitia na kupima maendeleo ya wanafunzi; wasimamizi kupitia na kupima maendeleo ya wafanyakazi; wazazi hupitia na kutoa mrejesho kwa watoto. Kiongozi wa wanafunzi anapaswa kujenga "kumbukumbu ya ukuaji wa kiroho" ili aweze kufuatilia maendeleo ya ukuaji wa wanachama wa kikundi chake cha wanafunzi. Kumbukumbu hiyo inaweza kutegemea upimaji na matokeo kama yalivyojadiliwa hapo nyuma katika sehemu **V.C. *Nguvu ya kufanya wanafunzi*** na ***D. Asili na tabia ya wanafunzi waliokomaa*** pamoja na vipimio vingine kama vile uwezo wa kuwasiliana na sifa za kibinafsi (kufundishika, huruma, uwezo wa kushirikiana na wengine, nk. Ambao hudhihirika wakati wa mchakato wa ujifunzaji). Kumbukumbu hizo zitatambulisha maeneo ya uwezo na maendeleo ili kwamba mwanafunzi atiwe moyo; na pia itaonyesha maeneo ambayo yanahitaji kuongeza bidii.

3. Mahusiano katika kufanya wanafunzi huhusisha mapatano kamili ya kuwajibika ya washiriki, wakati

[21] Hammond na Cronshaw huzungumzia mchakato wa kukua kama huu (ukianzia wakati wa kutubu/uchanga wa kiroho): (1) *Kutokujielewa na kutokuwa na ujuzi*. Watu walio katika hatua hii hawaelewi hata kinachoendele; hawana ujuzi na hata hawajui hivyo. Kiongozi inabidi awajulishe na kuanza mchakato wa kuwafunza. (2) *Kuelewa kwamba huna ujuzi.* Wanafunzi wanatambua mambo na pia wanatambua hali yao ya kutokujua na wataishughulikia ipasavyo. Wakijizoeza na "kuacha" njia za zamani ni muhimu ili kuendelea mbele. (3) *Kuelewa unachojua.* Watu sasa wanaelewa mambo ya msingi ya mabadiliko lakini wanahitaji kuwa na msimamo ili watende vema; si "asili ya pili" kwao bado. (4) *Kutoelewa unachojua.* Katika hatua hii watu wamejifunza na kuwa na mabadiliko ya kimilele ambayo yamekuwa asili ya pili kwao. Sasa wanaweza kufundishana wao kwa wao na kuwa kielelezo kwa wengine. (Hammond na Cronshaw 2014: 7-8)

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

ambapo programu huwa na mmoja au wachache ambao hufanya kwa niaba ya wengine wengi. "Programu nyingi zimeandaliwa kwa mfumo unaolenga mtu au wachache ambao ni nguzo nao hufanya kazi ngumu ya kuandaa na wengineo huja kama wapokeaji tu wasioshiriki katika mchakato wa kazi. . . . Katika mahusiano ya kufanya wanafunzi wadau hushiriki nafasi sawa ya majukumu katika kuandaa, kujiweka wazi na katika agenda ya kubadili maisha. Hili si swala linalomhusu mtu mmoja ambaye ni mwalimu mwenye uelewa, ambapo wengine ni wajifunzaji wanaochukuwa ujuzi wa mmoja mwenye hekima ambayo imewazidi wote. Kwa hakika viwango vya ukomavu vitatofautiana, lakini matarajio ya msingi ni katika mahusiano ya kutoa na kupokea, Yule aliye mwalimu na ambaye ni mwanafunzi waweza kubadilika kutoka wakati mmoja hadi wakati mwingine." (Ogden 2007: 6)

"Wachanga wa kiroho hawaelewi sheria za mchezo mpya wanaoucheza. Hawajui kwamba vita ya kiroho inapiganwa na ya kuwa wana adui mpya ambaye ana lengo la kuwaua na kuwaangamiza (ona Yoh 10:10; 1 Petro 5:8)." (Putnam 2010: 53) Kwa hiyo, wanafunzi, hasa hasa waamini wapya, wanahitaji mchungaji, mshauri, mwalimu wa wanafunzi ambaye atawalinda, kuwaongoza, kuwafundisha, kuwa nao, kuwaelekeza, na kuwafuatilia. Wakati huo huo, *wanafunzi wanaandaliwa kuongoza vikundi vyao na 'kufanya wengine kuwa wanafunzi'*. Hivyo, mapema katika mchakato wapewe jukumu la kuandaa na kuongoza mjadala kuhusu yale wanayojifunza katika kundi.[22] Putnam anauelezea mchakato: "Mwalimu wa wanafunzi mwenye mafanikio wakati wote atawachukuwa wafuasi wake katika mchakato. Inaanzia na 'Wewe tazama; mimi ninafanya' na kwenda kwenye 'Tufanye pamoja' na kuelekea kwenye 'Wewe unafanya; mimi nakutazama.' Hatimaye, mwanafunzi anaanza mchakato huu pamoja na mtu mwingine—mtu ambaye atakuwa anaonawakati mwanafunzi akifanya." (Ibid.: 59)

4. Fokasi ya mahusiano katika kufanya wanafunzi ni uwajibikaji katika mabadiliko ya maisha, wakati ambapo fokasi ya program ni uwajibikaji kuhusiana na mada zilizopo. "Kukua ili kumfanania Kristo ndio lengo kuu. Kipimio cha uwajibikaji katika programu kina hali ya kupima kirahisi, tabia ambazo ni rahisi kuziona kama vile kukariri maandiko, kumaliza mistari ya kusoma kwa wiki na kujitiisha katika nidhamu ya kiroho. Katika mahusiano ya kufanya wanafunzi fokasi ya uwajibikaji ni ujifunzaji 'kuona na kutii yale yote ambayo Yesu ameagiza' (Math. 28:19). Kwa mfano, kunatofauti kubwa kati ya kujua kwamba Yesu alifundisha tuwapende adui zetu, na kuwapenda adui zetu kiukweli. Kiini cha mahusiano ya kufanya wanafunza ni kuhusisha maisha ya Yesu katika kila eneo la maisha yetu na yale tunayotenda." (Ogden 2007: 7)

5. Bila kujali ukubwa, makundi yote ya kufanya wanafunzi yana msingi katika kanuni ambazo ndizo kiini. Ingawaje ufanyaji wa wanafunzi unatekelezeka katika vikundi vidogo, "si vikundi vinavyofanya wanafunzi; wanafunzi hufanya wanafunzi" (Cole 2011: n.p.). Zaidi ya hapo, "wanafunzi hufanywa katika mahusiano, sio programu" (Ogden 2007: 5). Ili kufanikiwa, washiriki wote wa kikundi cha kufanya waanfunzi sharti wakubaliane kanuni za msingi:

- Kutegemea uwazi wa kila mmoja. "Uwajibikaji wa karibu wa kimahusiano na waaminio wengine ni jambo la msingi kwa ukuaji katika uanafunzi. . . . *Kiwango kile ambacho tutaruhusu wengine waone kama maeneo ya maisha yetu ambayo tunahitaji tochi ya Mungu kuingilia na kutubadilisha ndicho kiwango ambacho tunamkaribisha Roho Mtakatifu kutufanya wapya.* Uhiari wetu wa kuingia katika mahusiano ya ndani ya mtu kwa mtu ni ukiri wa shauku yetu ya kweli mbele za Mungu ya utayari wetu kumkaribisha Bwana kututengeneza upya maishani mwetu." (Ogden 2007: 8, mkazo kwenye nakala ya asili) Kuaminiana hakutokei kwa ghafla bali huchukua muda na gharama ya kuwa pamoja. Kundi dogo linapoanza kutengeneza ukuaji wa kuaminiana kwa sababu hakuna mahali pa kujificha. **Yak 5:16** inasema, *"Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa."* "Kuleta aibu ya hatia yetu mbele ya washiriki wa mwili wa Kristo tunaowaamini hiyo peke yake yaweza kuleta matokeo yanayokomboa. Jambo linapokuwa limewekwa wazi kwa wengine, huanza kupoteza nguvu zake za kutawala. Dhambi hupenda giza, bali nguvu yake hudhoofika katika nuru." (Ibid.)
- Kweli ya Neno la Mungu katika jamii. "Ni jambo muhimu hasa katika wakati wetu huu ya kwamba mwanafunzi awe na fursa ya kujifunza mafundisho ya msingi ya maisha ya Kikristo katika mfumo ulio na mpangilio fasaha. Tunaishi katika kipindi ambacho mtu wa kawaida huwa ana kiwango kidogo cha msingi wa uelewa wa imani yake ya Kikristo." (Ogden 2007: 9) Mshiriki mmoja katika kikundi kidogo cha uanafunzi alisema, "Nimegundua kadiri tulivyokuwa tunajifunza

[22] Hili limejadiliwa kwa ufasaha zaidi hapo chini katika sehemu **VI.D.** ***Mchakato wa kufanya wanafunzi unapaswa kuwa wa kujizidisha wenyewe***.

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

imani yetu kwa mpangilio na mtiririko ulioratibiwa vema ilikuwa kama mpangilio wa picha. Nilikuwa na vishada vya vigae vikiwa na nafasi zilizo wazi katika maeneo fulani. Mtazamo huu umeniwezesha mimi kujaza nafasi zote zilizokuwa wazi na vigae vyake Kwa sasa ninaona kwa mtazamo mpana jinsi imani ya Kikristo ilivyo ya kuelewaka kwa urahisi." (Ibid.: 9-10)

- Makubaliano ya uwajibikaji uletao mabadiliko ya maisha. "Uhusiano uliopo kati ya wale ambao wako pamoja katika safari ya uanafunzi ni wa kiagano. Agano ni nini? Agano ni makubaliano ya pamoja yaliyoandikwa kati ya pande 2 au zaidi ambayo hueleza kwa ufasaha matarajio na wajibu katika uhusiano. Kinachoonekana katika tafsiri hii ni kwamba wadau wa kiagano hupeana mamlaka ya kuwazui kwenye agano ambalo wamekubaliana wao kwa wao." (Odgen 2007: 10) Uwajibikaji wa pamoja "hutuleta tena katika kiini cha maana ya kuwa mwanafunzi wa Yesu" kwa sababu "mwanafunzi ni yule aliye chini ya mamlaka" (Ibid.).

"Uwajibikaji sio chaguo katika mchakato wa kuadibisha. Hakuna anayealazimishwa kuwa katika Kundi la Kukua, lakini wale wanaojiunga hufanya hivyo kwa sababu wanajua wanamhitaji mtu mwingine kuwasaidi kuwa na nidhamu zaidi katika safari yao ya rohoni. Wanapoomba kuwa chini ya mamlaka yako, na ukakubali kuwaongoza, wanahaki ya kutarajia uongozi wa kiungu. . . . Ikiwa mwanachama atakosa kuhudhuria mikutano mara kwa mara au atashindwa kumaliza masomo yake ya Biblia, utahitajika ukutane na mtu huyo umsaidie kutatua matatizo yoyote aliyonayo. . . . Kadiri tatizo linavyotatuliwa mapema, ndivyo inavyokuwa rahisi zaizi kulisahihisha. Wanachama wengine katika kundi watakuwa wakijua pia kuhusu udhaifu huo wa mahudhurio wa mwanachama na/au ushiriki kama ujuovyo wewe; ikiwa mtaachia tatizo hilo liendelee litaathiri kundi lote. Ukosefu wa uwajibikaji utaharibu umoja wa kundi na mchakato wa kufanya wanafunzi. . . . Vitendo vya uadibishaji ni zana muhimu kwa kuwafanya viongozi kuwa wanafunzi. . . . Vitendo vya uadibishaji ni kitu tunachofanya kwa ajili ya watu si kile unachokifanya kwa watu. Katika maana yake iliyo rahisi, kitendo cha uadibishaji ni kitendo ambacho kinafanywa na wewe kumsaidia Mkristo mwenzako dada au kaka, afanye kile ambacho aliahidi kuwa atafanya." (Churches Alive 1996: 4.6-7) Kuwajibika kunaweza kuwezeshwa na chati ya mahudhurio pamoja na fomu za ripoti ya maendeleo ambayo kiongozi wa kikundi hujaza wanapokutana kama viongozi na pamoja na bodi ya uongozi wa kanisa.[23]

### C. *Mchakato wa kufanya wanafunzi*

Kwa kawaida vikundi vya kufanya wanafunzi hupaswa kukutana kila wiki au kila baada ya wiki moja ili kudumisha mwndelezo. Vikundi vya kufanya wanafunza hukutana kutiana moyo na kuimarisha wanachama katika injili. Kwa hiyo, havishughuliki tu na swala la wanachama kushirikishana simulizi za maisha yao, matatizo yao, na ushindi wao tangu wakutane mkutano wa mwisho. Kwa hakika jambo hilo linapaswa kutokea. Kwa hali yoyote, kuhamasisha na kuimarisha wanachama katika injili, mikutano iwe na mtaala ambao wanachama wote watausoma na kuujadili. Mtaala unaweza ukahusisha kujifunza vitabu tofauti tofauti vya Biblia au kujifunza vitabu vingine vya uanafunzi. Hapa kuna maoni machahe:

1. Kutumia Biblia. "Kila mwanafunzi anapaswa kubadili mtazamo wa kidunia (ambao yeye anaanza nao) kwa mtazamo wa Mungu. Tunahitaji mtazamo wa Kibiblia wa dunia. Biblia ni brashi ya Mungu ya kutusugulia, ambayo imeandaliwa kututakasa (kutusafisha) (ona Yoh 17:17). Neno lake pia ni chakula cha kiroho ambacho huyatunza maisha yetu ya kiroho (ona Mathayo 4:4). Linatia nuru njia yetu (ona Zaburi 119:105), na sisi tunapaswa kuhifadhi neno la Mungu mioyoni mwetu ili tusimtende Mungu dhambi (ona Zaburi 119:11). Pia ni upanga wetu wa Roho, ambao tunautumia kupambana na adui wetu shetani (ona Waefeso 6:17)." (Putnam 2010: 52)

    Kama wanachama wa kikundi cha kufanya wanafunzi (hasa kiongozi au mwalimu) hajasoma kitabu au kujifunza kuhusu kutafsiri Biblia (wakati mwingine inaitwa Elimu ya Kutafsiri Maandiko), itasaidia sana ukifanya hivyo ili uweze kuelewa Biblia katika muktadha wake na uwe na ufahamu wa Biblia ambao kiini chake ni Kristo. Kitabu cha ECLEA kiitwacho *Tafsiri ya Biblia*

---

[23] Churches Alive inasema, "Kwa sababu ya ile hali ya kuweka malengo bila ya kufikiria kiwango cha kazi yote itakayo hitajika kufanyika ili malengo yatimie, taarifa zinahitajika . . . ili kuhakikisha kwamba kuna maendeleo yamefanyika baada ya kuweka malengo. Mfumo wa kutoa taarifa hauhitaji kuwa wa kuchanganya. Ile tu hali ya kujua kwamba taarifa inahitajika inatosha kuwa kichocheo cha kuhimiza utekelezaji wa malengo yaliyokusudiwa." (Churches Alive 1996: 5.3)

*Viongozi* wa kundi la wanafunzi hukutana pamoja mara kwa mara kujadili kuhusu masomo watakayofundisha, na kuwajibishana, kujadili mipango, kuuliza maswali, kushirikishana ujuzi, kutatua matatizo wanayokutana nayo, kuombeana na kutiana moyo, kupeana mawazo mapya kwa ajili ya maendeleo, kuratibu shughuli, na kufunzana ili kwamba kazi ya kufanya wanafunzi kanisani iwe na matokeo makubwa kadiri inavyowezekana.

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

(http://www.eclea.net/courses.html#interpretation) na *Mahubiri ya Ufafanuzi* (http://www.eclea.net/courses.html#preaching) vyote hushughulika na swala la kuielewa Biblia katika muktadha na kutendea kazi kile ambacho Biblia inasema. Kitabu cha ECLEA kiitwacho *Theolojia ya Kibiblia* (http://www.eclea.net/courses.html#theology) kinaonyesha ule msingi wa simulizi ya kibiblia na kinaonyesha jinsi AK linavyoingiliana na kuhusiana na AJ. Vitabu hivi ni zana nzuri kwa vikundi vya kufanya wanafunzi kutumia.

Unapotumia Biblia kama mtaala, "kila mtu lazima ajitoe kusoma sura ile ile ya Biblia kila wiki. Mnaposoma, muwe mnamuuliza Roho Mtakatifu awape kujua ni kitu gani anataka kutekeleza ndani yenu. Roho Mtakatifu anaweza kuwaonyesha dhambi ili muitubie, kufurahia ahadi fulani, kutafakari kuhusu ufunuo fulani, au kumsifu Mungu kwa ajili ya matokeo fulani. Kila wiki, mnapokutanika, anzeni kwa kuweka fokasi kwenye kifungu kwa kushirikishana vile ambavyo Roho amewagusa kupitia Neno kuwabadilisha." (Dodson 2012: 137) Kikundi pia kipitie kifungu kwa pamoja, ili kipate kujua ujumbe kiini wa kifungu na sura. Wana kikundi wanapaswa kuuliza, "Injili inaonekana wapi katika kifungu hiki?" kikundi kinapaswa kutambua maeneo yanayowapa shida na waliyofanikiwa wanapokuwa wakiendelea kujifunza kifungu. "Ulizaneni maswali. Kwa neema mpeane shinikizo mmoja kwa mwingine ili kutambua misukumo isiyo ya kiungu na kupata misukumo ya injili. . . . Shirikishaneni maisha yenu, si tu yale mnayotambua. . . . Mwisho, hakikisheni mnashirikishana majina ya watu ambao mnajaribu kuwabariki kwa injili. Ombeni kama kikundi, Mkimwomba Mungu awasaidie kutegemea ahadi zake na pia kuwapa wasioamini walio katika maisha yenu kipawa kile kile cha imani alichowapa ninyi!" (Ibid.: 138)

David Garrison anaelezea jinsi Huduma Ya Kupanda Makanisa ya Bangalore, India, inavyopanga mikutano yake ya wiki ya kujifunza Biblia kwa kuona "maswali manne ya Paulo ya kufanya wanafunzi [kutoka **2 Tim 3:16-17**]:

1) Mungu anatufundisha nini (nini fundisho au kitu cha thamani ambacho Mungu anakionyesha katika kifungu hiki)?
2) Mungu anakemea nini (ni nini kisicho cha kimaadili au fundisho potofu ambalo Mungu anapinga katika kifungu hiki)?
3) Mungu anasahihisha nini (ni kitu gani katika maisha yangu ambacho kinahitaji kurekebishwa kutokana na kile ambacho nimesoma au kusikia katika kifungu)?
4) Ni lipi funzo langu katika haki (ni kipi ambacho Mungu ananitaka nikifanyie kazi katika maisha yangu wiki hii, kama matokeo ya kile ambacho nimesoma katika Maandiko)?

Wakati mwingine tutaona haya kama 'Maswali ya usahihi:'

1) Kipi ni sahihi? -- *fundisho*
2) Kipi si sahihi? -- *kemeo*
3) Nawezaje kuwa sawa? -- *sahihisho*
4) Nawezaje kubaki sawa? – *funzo katika haki*

Kuuliza maswali haya ya Roho Mtakatifu pamoja na jamii ya kaka na dada ndani ya Kristo ambao mmeshibana hakika ni njia ielekeayo kwenye kukua na kuwa kama Kristo. Kilicho bora kabisa katika program ya kufanya wanafunzi, ni uhakika wa kuwaacha 'wanaume (na wanawake) wa Mungu wakiwa wameandaliwa kikamilifu kwa ajili ya kila kazi njema.'" (Garrison 2010: n.p.)

2. <u>Simulizi za Kibiblia.</u> Vikundi vidogo vidogo vya kufanya wanafunzi vya Jim Putnam katika huduma iitwayo Real Life Ministries hutumia Biblia kama mtaala wao wa kufanya wanafunzi, lakini wanafanya hivyo kwa mtindo wa kufurahisha uitwao "Simulizi za Biblia." Kwa kila kifungu cha Biblia, kiongozi wa kikundi hujifunza hicho kifungu (simulizi) au anampangia mmoja wa wana kikundi kujifunza na *kukielezea kama simulizi bila ya kusoma*—si neno kwa neno bali kwa namna ambayo ukweli wa simulizi unabaki kama ulivyo halisi. "Wakati msimuliaji anaposimulia simulizi, wana kikundi wanasoma ili kuona kama kuna anachoacha katika kusimulia. Simulizi inapoisha, msimuliaji au kiongozi wa kikukndi ataijenga tena simulizi akigusia yale ambayo yameachwa. Mara kwa mara kiongozi anamwomba mtu mwingine asimulie tena bila kusoma. Hakuna ajuae atakayechaguliwa, kwa hiyo kila mmoja anakuwa msikivu na kuwa tayari endapo atachaguliwa." (Putnam 2010: 158) Baada ya kufanya haya, kiongozi anauliza maswali ili kukazia kweli inayofundishwa katika simulizi. Maswali hayo ni kama haya:

- Kitu gani kipya umekigundua katika simulizi ambacho hukukijua kabla?
- Umejifunza nini kuhusu Mungu?
- Umejifunza nini kuhsu watu?
- Ni nani katika simulizi ambaye kwa sehemu kubwa ni kama wewe?

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

- Ni kitu gani utatoka nacho katika mjadala huu?
- Utakifanyia nini ulichojifunza?

Putnam anahitimisha kwa kusema simulizi za Biblia ni njia iliyo bora ya kutoa ujumbe wa Biblia kwa sababu: (1) Inasaidia watu kujua Biblia (haiogopeshi na simulizi hubaki katika fahamu za watu); (2) Inasaidia kuandaa viongozi (watu wengi hawadhani kwamba wana sifa za kufundisha Biblia kwa sababu ya kukosa elimu ya Kitheolojia, lakini kila mtu anajua jinsi ya kusimulia simulizi na kuuliza maswali); (3) Ni nzuri kwa mafunzo halisi (kwa sababu wasikilizaji wanashiriki, wanakumbuka simulizi); (4) Inawaimarisha watu kwa huduma (simulizi zinaweza kutumika katika maeneo mengi ya maisha); (5) Inasaidia watu kufanya watoto wao kuwa wanafunzi (wazazi wanaposimulia mambo ya watoto wao, kuna mguso mkubwa kwa familia za wengine); (6) Inasaidia viongozi kutathmini hali ya kiroho ya watu wao (mtindo wa kusimulia husababisha watu kuzungumza kitu ambacho husababisha iwe rahisi kutathmini mahali walipo katika safari yao ya kiroho); (7) Inasababisha vikundi vidogo visichoshe (muda huonekena kwenda haraka mtu anaposimulia kuliko anapofanya mhadhara); (8) Watu huweza kufahamiana (muingiliano wa simulizi na maswali huhamasisha hali ya kujuana kwa karibu). (Ibid.: 159-62) Mtindo huu wa simulizi za Biblia unafaa sana kwa vifungu vya Biblia ambavyo ni hadithi, mfano, sehemu kubwa ya AK, Injili na kitabu cha Matendo ya Mitume.

3. Kozi za Uanafunzi na vitendea kazi. Kuna vitabu vingi sana vya kufanya wanafunzi na zana nyingine zinapatikana katika mtandandao, kwa kununua au bure. Pia ziko *kozi za uanafunzi za bure* mtandaoni, ambazo zina masomo, vifungu vya kusoma na amswali ya majadiliano, hiyo inaweza kutumika kama sehemu ya mchakato wa kikundi kidogo cha kufanya wanafunzi. Mwisho wa kitabu hiki, **KIAMBATISHO 2—KOZI ZA KUFANYA WANAFUNZI NA NYENZO** inaorodhesha nyingi ya zana hizi za kwenye mtandao na kozi ambazo kanisa linaweza kutumia kuendesha kozi zake za kufanya wanafunzi.

Inasaidia kutumia nyenzo kama hizi, hasa hasa unapofokasi kwenye mambo fulani amabayo yamejadiliwa juu (mfano, jinsi injili inavyohusiana na utawala wa pesa, kulea, msamaha na upatanisho). ECLEA ina vitabu kwa kila moja ya mambo hayo na zaidi, unaweza kuvipata bure katika tovuti ya ECLEA (http://www.eclea.net/courses.html). Unapotumia nyenzo kama hizi, ni hekima zaidi kutumia vitabu vya Biblia na vitabu vingine vya kufanya wanafunzi kwa kubadilishana ili Biblia na injili vibaki kuwa kiini katika maisha ya wanafunzi
.

**D.** ***Mchakato wa kufanya wanafunzi unapaswa kuwa wa kujizidisha wenyewe***

Kuna maeneo matatu ambapo uzidishaji wa wanafunzi hutokea: (1) ndani ya kanisa la mahali pamoja; (2) kati ya makanisa ya mahali pamoja; na (3) kupanda makanisa.

1. Uzidishaji katika kufanya wanafunzi ndani ya kanisa la mahali pamoja. "Mchakato wa mafunzo ya [kufanya wanafunzi] hauhusiki tu na kushirikishana taarifa. Bali, unahusisha kuwasaidia watu na 'jinsi ya' katika kufanya wanafunzi ili kwamba wawezi kutekelaza maono. Tunapofahamu hili, mapema iwezekanavyo matie moyo mwanafunzi wako kuanza kufanya mwanafunzi mwengine." (Henrichsen 1988: 104) Kwa mfano, Mike Breen anasema kwamba kipindi cha muda uliokubalika [mara nyingi miezi sita-kumi na mbili] wanafunzi wanaanza kuunda vikundi vyao vya kufanya wanafunzi na kuwafunza wengine (Breen 2011: 39). Vivyohivyo, Jonathan Dodson (ambaye anashauri vikundi vya kufanya wanafunzi vya watu wawili au watatu) anasema, "Kama kundi litakua zaidi ya watu watatu, ni muhimu kwamba mwanachama mpya ashiriki mara kadhaa kupata wazo na baadaye kuanza kundi jipya. Hii inabakisha ile hali ya kushibana na kutegemeana iliyojengwa ndani ya kundi la kwanza, wakati huo huo ukilea uzalishaji." (Dodson 2012: 136) Kwa kifupi, "Kuwa mwanafunzi maana yake ni *kufanya* wanafunzi" (Ibid.: 15).

Kufanya uzidishaji wa binafsi kuwa kiungo muhimu cha mchakato wa kufanya wanafunzi kuna angalau matokeo matatu kwa mwanafunzi:

- Itaimarisha imani ya mwanafunzi mwenyewe. "Mwanafunzi anapoanza kumshirikisha mtu mwingine kweli za Kikristo, anaulizwa maswali amabayo yanapenya ndani yake. Utengenezaji wake wa majibu husababisha kusiliba kweli ndani ya moyo wake pia wakati anapomsaidia mtu mwingine." (Henrichsen 1988: 105)
- Inampatia maabara kwa ajili ya ukuaji wake mwenyewe. "Anapoyajenga maisha ya mwanafunzi mwingine, anapata fursa ya kuona kama kile ambacho yeye mwengewe anafanya kinaweza kutumika kwa wengine" (Henrichsen 1988: 105).
- Humfanya mwanafunzi awe wa kufundishika awe na shauku ya kujifunza. Mwanafunzi anapojua ya kwamba yeye naye atakuwa na jukumu la kuwafanya wengine kuwa wanafunzi katika

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

muda mfupi ujao, na kwa kweli yeye anapokuwa ana wafanya wengine kuwa wanafunzi akiwa yeye ona katika hatua za yeye kufanywa kuwa mwanafunzi, mtaala wa kufanya wanafunzi na mchakato unapungua kuwa wa kitaaluma au wa kufikirika; unafanyika kuwa "halisi." Mwanafunzi anajua ya kuwa anatakiwa kuelewa anachofunzwa na kwa ukweli "kukifanywa kuwa chake", kwa sababu mwanafunzi anajua kwamba muda si mrefu na yeye atakuwa anatoa ujumbe ule kwa wengine.

2. Ushirikiano wa makanisa. Nyanja moja ya kuzidisha wanafunzi ambayo huenda makanisa hawaionai kwa karibu ni *kusaidia makanisa mengine na madhehebu mengine* kuwa vituo vya kufanya wanafunzi. "Makanisa ambayo 'yamekuwa vituo kwa msaada wa mengine' hupata nguvu ya mguso ambayo haiwezi hufikiwa kwa njia nyingineyo yote. Maandiko kamwe hayaweki tofauti za madhehebu au za kijografia yanapotuagiza 'tuwafanye watu wa mataifa yote kuwa wanafunzi.' Makanisa yaliyoko katika eneo la utawala wako ikiwa ni pamoja na yale ya madhehebu mengine yanaweza kuwa miongoni mwa yale ambayo Mungu anataka uyafikie. Kuhusiana na swala la matokeo na gharama za uwekezaji huo, linaweza kuwa jambo la kupendeza sana kulisaidia kanisa jingine kuwa kanisa linalofanya wanafunzi badala ya kujaribu kuwavuta kwako, kuwachukuwa kanisani kwako na kuwafanya wanafunzi wako." (Churches Alive 1996: 1.13)

3. Kupanda makanisa. Tunahitaji makanisa na Wakristo wengi zaidi wenye afya, ili tuweze kufanya wanafunzi wengi zaidi. Timothy Keller anasema, "Hali ya nguvu, ya kuendelea, kupanda makanisa mapya ni mkakati mmoja muhimu kwa ajili ya (1) ongezeko la idadi katika mwili wa Kristo katika jiji na (2) kuendelea kwa hali ya uamsho wa makanisa yaliyopo kwa pamoja katika jiji. Si kitu kingine—si mikutano ya injili, programu za kuwafikia watu, huduma za makanisa, makanisa makubwa yanayokua, ushauri wa makusanyiko, wala michakato ya uamsho wa makanisa—itakuwa na mguso unaoendelea na wenye nguvu, kama upandaji wa makanisa unaoendelea. Hili ni tamko la kushtusha, lakini kwa wale ambao wamefanya ufuatiliaji kwa kiasi fulani, halijipingi kamwe." (Keller 2002: 1) Sehemu iliyobaki katika Makala yake huchambua sababu zilizopeplekea kutoa tamko hilo.

Mungu, kwa kweli, ukuaji wa haraka wa Makundi ya Upandaji wa Makanisa (MUM) duniani kote. MUM "ni mpango wa upandaji wa makanisa wa haraka katika maeneo ya wenyeji ndani ya eneo la jamii ya watu au eneo la idadi fulani ya watu" (Garrison 1999: 7). David Garrison amezielezea na kuzifanyia uchambuzi hizi MUM mwaka 1999 katika kijitabu chake (Garrison 1999; ona pia Garrison n.d. [2-ukurasa wa ufupisho]) ametoa matokeo ya utafiti wake katika kitabu chake cha mwaka 2004 (Garrison 2004). Katika MUM, "kufanya wanafunzi huwa ni swala la uhai kuhamishwa kwa uhai mwingine badala ya kuwa swala la kujifunza darasani tu" (Garrison 2010: n.p.). Kiini cha mchakato wa kufanya wanafunzi unaoweza kutumika katika mfumo wa upandaji wa makanisa wa aina yoyote ile "unatumia kujifunza Biblia kwa pamoja na vikundi vya kuabudu, unakazia utii kwa Biblia kama njia pekee ya mafanikio, unatumia viongozi wasiolipwa ambao hawako katika mfumo wa vyeo au madaraka na wanakutana katika vikundi vidogo vidogo au Makanisa ya Nyumbani" (Garrison 1999: 36).

Kuna miundo mingine mbali mbali ya upandaji wa makanisa licha ya hii ya MUM (ona, mfano, Stetzer 2015; Discipleship Ministries 2017). Kitabu hiki hakiwezi kuelezea mchakato wote wa upandaji makanisa kwa kina kwani hilo litakuwa ni somo jingine pekee. Hata hivyo kuna vitabu vingi vya upandaji wa makanisa kwenye mtandao, pamoja na: Makundi ya Upandaji wa Makanisa 2015; Rapidly Advancing Disciples 2011; Rapidly Advancing Disciples 2016; e3 partners Ministry 2011; Cheney, Putnam, and Sanders 2003; Shank 2014; Exponential.org 2017; T4Tonline.org 2017.

**E. *Kufanya wanafunzi: hitimisho***

"Kufanya wanafunzi kunachukua muda. Haiwezi kutekelezwa kwa njia ya kutoa mihadhara na semina za mafunzo kanisani, wala haiwezi kufanywa kwa kusoma kitabu. Haiwezi kuharakishwa. . . . Wanafunzi wanafanywa, lakini si kiujumla. Kila mmoja hufinyangwa na kutengenezwa kibinafsi na Roho wa Mungu. Itachukuwa muda gani ni swala lisilo hakika kwani huwa kuna tofauti katika ya mtu na mtu, kwa kutegemea kwa kiwango kikubwa wako wapi wanapoanza mchakato wa mafunzo. Lakini jambo ambalo ni hakika ni hili; inachukuwa muda. Bwana Yesu alianza na 12 ambao walikuwa na misingi ya imani ya Mungu mmoja, wenye hofu ya Mungu, ambao walitoka kwenye nyumba zenye kiwango fulani cha malezi ambacho si kibaya. Alijitoa muda wote kuwafundisha na kuwaendeleza. Alikuwa mahiri katika ujuzi wa kufunza, hata hivyo ilimchukua miaka mitatu kamili. Sitaraji kama ni rahisi kufanya kwa muda mfupi zaidi." (Henrichsen 1988: 107; ona pia Coleman 1964: 48) Kwa kweli, kukua katika uanafunzi ni mchakato wa maisha yote. Kwa sababu vikundi vya kufanya wanafunzi vina misingi katika kuaminiana, urafiki, na uwajibikaji, vinaweza kudumu bila kuwa na wakati wa ukomo.

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

## VII. <u>Huduma Ndani Ya Kanisa</u>

Kanisa si kuhusu sisi; ni kuhusu Kristo. Kanisa ni mwili wake, sio wetu. Tunapaswa kuhakikisha kwamba kanisa linaongozwa sawa sawa na waume na wake ambao wana sifa za kufanya kazi hiyo (**1 Tim 3:1-13**). Kwa njia hiyo, jambo lolote likimpata mchungaji au kiongozi mwingine yeyote, kanisa linaweza kuendelea viruzi bila shida, kwa sababu limejengwa kwenye msingi imara wa kiuongozi. Utendaji sahihi wa kanisa, huduma ndani ya kanisa, na uwekaji wa viongozi wapya, unahusiana moja kwa moja na kufanya wanafunzi: "Ikiwa kanisa litamaanisha katika kufanya wanafunza kama Biblia inavyofundisha, na ni kazi nzuri, kila hitaji la kanisa litatekelezwa. Tunapowafanya watu wetu kuwa wanafunzi, kwa kawaida viongozi watajitokeza kutoka miongoni mwao." (Putnam 2010: 23)

### A. *Kazi ya kanisa, na hasa ya viongozi wa kanisa, ni kuandaa na kuwawezesha watu ndani ya kanisa kufanya huduma zao*

Alama ya *kiongozi* mzuri inaonekana kimsingi katika *wafuasi* wake: Je wanajifunza? Je wanatumika? Je wanafikia viwango vyao vya juu vya utendaji? Ja wanabadilika na kuweza kusimamia migogoro kwa neema? Je wanaonyesha sifa na tabia za wanafunzi wa Kristo wakomavu? Je wanaonyesha "tunda la Roho" (**Gal 5:22-23**)? Je wanafanya wengine kuwa wanafunzi na kuinua viongozi wapya?

Ukweli kwamba uongozi wa kanisa unahitaji *kutenda* na unahusika na *uwajibikaji* wa kiongozi, sio cheo, unaonekana katika **Efeso 4:11**, ambayo inasema, *"Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii, na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na walimu."* Kila moja ya vipawa hivi humaanisha *utendaji* unaoonekana. Kuna kiwango fulani cha mwingiliano kati ya kazi hizi na uongozi wa kanisa ulio rasmi wa mzee, mwonazi, askofu, mchungaji, na shemasi, lakini haufanani.[24] Hivyo, wakati wachungaji wote, kwa tafsiri, ni walimu, [25] na wazee wote na waonazi wanapaswa kuwa na uwezo wa kufundisha (**1 Tim 3:2**), si wote walio na kipawa na uwezo wa kufundisha wana uwezo na kipawa cha kuchunga; kwa maneno mengine, wachungaji wote ni walimu pia, lakini si walimu wote ni wachungaji. Zaidi ya hapo, si lazima kwamba wale walio katika nafasi za uongozi rasmi wa kanisa (yaani, wazee, waonazi, maaskofu, wachungaji, na mashemasi) watakuwa na vipawa vya kuwa mitume, manabii, au wainjilisti. Maelezo mafupi kuhusu kazi zao katika **Efeso 4:11** yapo katika mpangilio:

- <u>Mtume.</u> "Mtume" ni mtu ambaye ametumwa kwa mamlaka na amepewa wajibu maalumu wa kutekeleza kwa kusudi maalum halisi. Ni nomino *apostellō* kwa Kiyunani ("kutuma"). Maana halisi ya "mtume" inaelezewa na maneno kama "balozi," "mwakilishi," au "mjumbe." AJ huwatambua aina mbili ya mitume: (A) Mitume wa *msingi*; na (B) Mitume ambao *wametumwa na kanisa*. Mitume wa "Msingi" ni wale ambao walikuwa pamoja na Yesu, mashahidi wa ufufuo, na waliitwa bayana kuwa mitume na kuwa mashahidi wa Yesu (ona **Math 10:1-5; Marko 6:7, 30; Luka 6:13; Yoh 15:27; Matendo 1:21-22**). Waliweza kuthibitisha umaalumu wa kile ambacho wao ndiwo kwa kufanya miujiza (ona **Math 10:1-8; Marko 6:7; Matendo 2:43; 2 Kor 12:12**). Mitume wa msingi walikuwa viongozi wa kanisa la kwanza na "msingi" wa kanisa lenyewe (**Efeso 2:19-20**). Kama tujuavyo, wale ambao wana mamlaka ya kitume ya msingi hawako tangu wale mitume wa kwanza wafe (ni msingi mmoja tu unawekwa kwa ajili ya jengo). Mitume "Wanaotumwa na Kanisa" ni wale wanaume na wanawake ambao wametumwa na kanisa kwenda na kuhubiri injili, kupanda makanisa mpya, na kulijenga kanisa (ona **Matendo 13:1-3; 14:14; Rum 16:7; 1 Kor 9:5-6; 12:28; 1 Thes 1:1; 2:6**). Mitume hao wote umoja kupitia mtu kama Paulo (ona **Matendo 9:1-16; 13:1-3; 1 Kor 9:1; 15:6-10; Gal 1:11-17; 1 Tim 2:7**). Mitume wanaotumwa na kanisa hawawezi kuwa na mamlaka kuu zaidi ya ile iliyowekwa juu yao na kanisa. Kanisa ni mwili wa Kristo duniani (**1 Kor 12:27; Efeso 1:22-23; 4:15-16; Kol 1:18**). Kanisa ni hekalu la Roho Mtakatifu (**1 Kor 3:16-17**). Kristo amelitia mafuta kanisa na kulipa mamlaka yake (**Math 16:18-19**). Vivyo hivyo, Kristo anatarajiwa kutenda kazi kupitia kanisa lake, si kibinafsi nje yake. Kwa kuwatuma mitume, kanisa pia huwawezesha na kuwataka wawajibike, kwa niaba ya kanisa na machoni mwa wanadamu.

  Inabibidi kanisa liwapime watu wanaojiita mitume ili kujua kama ni mitume wa kweli au wa uongo (**1 Yoh 4:1-6;** ona pia **2 Kor 11:3-4, 13; Ufu 2:2**). Watu wengi siku za leo wanapenda kujiweka wao wenyewe kuwa "mitume." Hii ni kinyume na mfumo wa AJ (Mitume wa AJ hawakujiita wao wenyewe kuwa mitume). Wengi wa hawa "mitume" wa kujiita hujigamba kuwa nia watenda miujiza. Hata hivyo, hata tendo la kufanya miujiza pekee si lazima iwe ishara kwamba mtu ameitwa na Mungu (**Matt 7:15-23; 2 Tim 3:1-9**

---

[24] Suala la uongozi wa kanisa limejadiliwa hapo nyuma katika sehemu ya **II.B. *Muundo wa Uongozi wa Kanisa*** na sifa za viongozi zimezungumziwa katika sehemu ya **II.C. *Uongozi wa Kanisa***.

[25] Mjadala wa Recall Grudem kuhusiana na hili katika sehemu ya **II.B. *Muundo wa Uongozi wa Kanisa***, ambapo alisema kwamba "mstari huu ungeweza kutafsiriwa vizuri zaidi kama 'mchungaji-walimu' (kundi moja) badala ya 'wachungaji na walimu' (ikimaanisha makundi mawili) hii inatokana na uundaji wa sentensi wa Kiyunani" (Grudem 1994: 913).

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

[ona **Kut 7:10-12, 20-22; 8:6-7, 16-19**]). Hapa Afrika, "kuinukia kwa mitume na manabii wa kiafrika kulisababisha kutangazwa kwa usawa wa kiimani kati ya wazungu na watu weusi katika huduma (Gal 3:28; Kol 3:11). Pia iliweka msingi wa kanuni ya kutenganisha imani ya Kikristo na uhusiano wake na utawala wa kisiasa wa wakoloni." (Ouedraogo 2006: 1434) Kwa bahati mbaya, hata hivyo, "imani ya wengi wa mitume wa kiafrika haisimamii Biblia kama msingi wa imani yao na mwenendo wao wa maisha. . . . Wanadai [kile wanachotamka ni ufunuo utokao kwa Mungu moja kwa moja] kama nyongeza ya Biblia. Hata hivyo, Biblia inaonya dhidi ya kufanya hata nyongeza kidogo katika neno la Mungu (Ufu 22:18-19). . . . Vile vile wengi wa mitume wa Afrika hujihushisha na imani potofu. . . . Hata wengine wanadiriki kusema wao ndio wanamrithi Kristo na hata wengine wajiita Kristo. Madai ya jinsi hiyo hufanya watu wawaabudu. Chakusikitisha, wengi wao kuchukuwa fahamu zote za wafuasi wao na kutawala mawazo yao kabisa. AJ linatuonya dhidi ya watu kama hao (Math 24:11; Yuda 4-16)." (Ibid.) "Mitume" wa siku hizi yabidi tuwapime kwa yale wanayofundisha (ona **Matendo 17:11; 1 Tim 6:3-5**) na namna wanavyoishi (ona **Math 20:25-28; Marko 10:42-45; Luka 22:24-27; Yoh 13:12-17; Matendo 18:3; 1 Kor 9:11-18; 2 Kor 11:7; 12:13**).

- <u>Nabii.</u> Kuna kufanana kati ya manabii na mitume, ina maana, walikuwepo manabii wa *msingi* (**Efeso 2:20**), na kuna wale ambao Grudem anawaita manabii wa *kusanyiko* (Grudem 1994: 1055; ona **Matendo 21:9; Rum 12:6; 1 Kor 11:5; 12:28-29; 14:29-33, 37-38; 1 Thes 5:19-21; 1 Tim 4:14**). Ingawaje kumekuwako na mjadala kuhusiana na asili ya manabii wa sasa na unabii (ona Grudem 1994: 1049; Hodge 1993: 388-89; Kell 2006: 11-13), "Kwa kawaida unabii, katika maandiko yote, unakuwa na kusudi na ni bayana" (Kell 2006: 46). Hali ya kusudi ya unabii inaonyeshwa katika **1 Kor 14:3** ambayo inasema kwamba *"yeye ahutubuye husema na watu maneno ya kuwajenga na kuwafaiji na kuwatia moyo"* (ona pia **Matendo 15:32** ambayo inasema Yuda na Sila, ambao walikuwa manabii, , *"<u>wakawausia</u> [au wakawatia moyo] na <u>wakawathibitisha</u> ndugu"*; na **1 Kor 14:31** [*"Kwa maana ninyi nyote mwaweza kuhutubu mmoja mmoja, ili wote wapate <u>kujifunza</u>, na wote <u>wafarijiwe</u>"*]). Pengine tafsiri iliyo bora zaidi ya nabii wa sasa na unabii wa sasa inatolewa na Charles Hodge: "Karama ambayo Paulo anaizungumzia hapa, si, kwa hivyo, ile idara ya kubashiri mambo ya wakati ujao, bali yale ya wakati tulionao uliopo kwa uvuvio, akimwongoza msikiaji kupokea, kama kutoka katika mdomo wa Mungu, ujumbe mahususi alioupokea, ikiwa kutiwa moyo, au maagizo, au faraja." (Hodge 1993: 389-90; ona pia Kell 2006: 53 [manabii ni "wajumbe ambao hupokea kweli iliyovuviwa kutoka kwa Mungu kwa manufaa ya wale watakaosikia"]; Grudem 1994: 1057-58 ["unabii hutokea wakati ufunuo kutoka kwa Mungu unatolewa na nabii kwa kutumia maneno ya kawaida ya (kibinadamu). . . . Ni mpaka mtu apokee 'ufunuo' moja kwa moja kutoka kwa Mungu vinginevyo hakuna unabii"]).

Pengine ili kuwakatisha tamaa watu ili wasijiite "manabii" kwa lengo la kuwatawala watu isivyostahili (au kuchukua pesa zao), katika AJ imerudiwa rudiwa mara kwa mara ikionya dhidi ya "manabii wa uongo" (**Math 7:15; 24:11; Marko 13:22; Luka 6:26; Matendo 13:6; 2 Pet 2:1; 1 Yoh 2:18; 4:1; Ufu 2:20**). Biblia inasema "uvuvio wa nabii ni wa muda fulani rasmi na wa kupita" (Hodge 1993: 389) na anasema kwamba nabii na ujumbe wake *vipimwe* na kusanyiko (**1 Kor 14:29-33; 1 Thes 5:20-21; 1 Yoh 4:1**).

1. *Hitaji la hukumu:* "Nabii anaposimama kati ya Mungu na watu wake, lazima iwepo hali ya kuwajibika kwa kile kitakochosemwa. Kusema kwamba mtu anayesema 'maneno kutoka kwa Mungu' asiwe na hatia ya kiwango fulani cha hukumu kwa hakika inapingana na mkazo wa uwajibikaji ambao umewekwa katika maandiko. . . . Uhalisia ni kwamba manabii wa uongo na jumbe za uongo huweka mazingira ya uhitaji wa kuhukumu wale wanaodai kuwa wana 'maneno kutoka kwa Mungu.' (1 Thes 5:20-21 na 1 Kor 14:29). Ikiwa Mungu hakusema na mtu kiukweli, basi ni lazima tuwe na uwezo wa kupambanua hilo na kuchukua hatua ili kuilinda kweli na kusahihisha uopotovu." (Kell 2006: 9, 23) "Kuhumu ilipaswa kufokasi kwanye yale maneno ya unabii zaidi, ingawaje tathmini yake itamuathiri sana nabii kuhusiana na kupewa fursa zaidi hapo baadaye ya kutoa ufunuo katika jamii. Hukumu ilipaswa kuwa ni ya kijamii zaidi, ingawa kwa kiwango kikubwa iwe imeongozwa na wazee, manabii wengine, au mitume ikiwa walikuwepo." (Ibid.: 31-32)
2. *Kipimo cha hukumu:* Hatimaye, Biblia ndicho kipimo cha kumhukumu anayejifanya kuwa 'nabii,' kwa sababu nabii wa kweli hawezi kusema kinyume na kile ambacho tayari Mungu amefunua katika Neno lake. Ndio maana ni muhimu kwa viongozi wa kanisa kujua Biblia vizuri na kwa watu ndani ya kanisa kuwa katika maadili mema. Tukiwa na viwango hivyo, "Ufunuo ambao mwelekeo wake uko nje ya misingi ya Biblia utakataliwa moja kwa moja. . . . Ikiwa mtu au kikundi ambao hudai kuwa wao ni manabii, kama watasema matamko ambayo kwa kiwango fulani hushusha hadhi ya Mungu Baba, mwana Yesu Kristo au Roho Mtakatifu; basi hao watakuwa wakinena kama manabii wa uongo. . . . Ikiwa ufunuo fulani wa nabii unapingana wazi wazi na kifungu fulani cha Maandiko, ujumbe wa huyo

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

nabii ukataliwe kwamba ni wa uongo [**Matendo 17:10-11; 1 Kor 14:37-38; 1 Yoh 4:6**]. . . . Ikiwa ufunuo hauna faida ya 'kuwajenga na kuwafariji na kuwatia moyo' (Matendo 15:32, 1 Kor 14:3), yabidi ukataliwe. . . . Ikiwa mtu atatoa matamko anayodai kuwa ni ya kinabii kwamba kuna jambo fulani [litatokea] na halikutokea, matamko hayo yatajwe kwamba ni uongo." (Kell 2006: 41, 43, 45, 46) Tukiwa tunatambua kwamba Biblia ndiyo kipimo kikuu cha kupima tamko linalodaiwa kuwa "ufunuo" au "unabii," lazima tuelewe kuwa Biblia haijafikia ukaribu wa kubainisha namna ya kushughulikia kila elementi ya maelfu kwa maelfu ya matukio ambayo watu hudai kupokea ufunuo" (Ibid.: 47). Katika mazingira kama hayo, "kipimo cha muda, maombi, na ushauri vyote ni muhimu ili kuweza kutathmini madai ya ufunuo. Kabla mtu hajaukubali huo unaoitwa unabii, achukuwe muda kuomba kuhusiana na swala hilo kisha alilete mbele ya wengine, ikiwezekana hata kwa viongozi wa kanisa, ambao wataweza kutoa mwelekeo sahihi wa kibiblia. Ikiwa unabii umetolewa kuhusiana na tukio la wakati ujao, kanisa yabidi lisubiri ili kuona kama kweli jambo lile litatukia." (Ibid.: 48)

Biblia pia imeweka wazi kuhusiana na mtindo wa maisha wa Mkristo wa kweli kimwenendo, kimaadili, vipaumbele, sababu zile za ndani zinazomfanya afanye kile anachofanya (na, hivyo, nabii wa kweli) yabidi awe hivyo. *Didache* (c. 70-110) inakazia umuhimu wa kutathmini sababu za ndani za mtu kufanya anayoyafanya na mtindo wake wa maisha ili kupambanua kama yeye ni nabii au mtume wa uongo. Inasema: "Sasa kuhusiana na mitume na manabii, shughulikeni nao kama ifuatavyo kulingana na uongozi wa injili. Na mtume ajaye kwenu na apokelewe kana kwa kwamba yeye ndiye Bwana. Lakini asikae zaidi ya siku moja, isipokuwa kama kuna uhitaji, na katika mazingira kama hayo anaweza kukaa siku nyingine moja zaidi. Lakini akikaa siku tatu, yeye ni nabii wa uongo. Na mtume anapoondoka, asichukuwe chochote ispokuwa chakula kitakocho mfikisha kwenye malazi yake mengine. Lakini akiomba fedha, yeye ni nabii wa uongo.

Pia, msimpime au kumtathmini nabii yeyote asemaye katika roho, kwa maana kila dhambi itasamehewa, lakini dhambi hii haitasamehewa. Hata hivyo, si kila asemaye katika roho ni nabii, ispokuwa tu aonyeshe mwenendo kama wa Bwana. Kwa tabia zake, hivyo, nabii wa kweli na yule wa uongo watatambulika. Zaidi ya hayo, nabii yeyote anayeagiza chakula akiwa katika roho hatakila; ikikila, yeye ni nabii wa uongo. Ikiwa nabii yeyote anafundisha kweli, lakini yeye hatendi kama anavyofundisha, yeye ni nabii wa uongo. Lakini nabii yeyote aliyethibitishwa kwamba ni wa kweli anapofanya kitu ambacho kinaonekana kuwa ni cha kidunia ikiwa ni ishara ya kanisa (ili mradi tu hawafundishi ninyi kufanya yale ambayo yeye anafanya) asihukumiwe na ninyi, kwa maana hukumu yake iko kwa Mungu. Zaidi ya hayo, manabii wa kale pia walifanya mambo ya jinsi hiyo. Lakini mtu akisema katika roho, 'Nipe pesa,' au chochote kile, usimsikilize. Lakini akikuambia utoe kwa ajili ya wengine ambao ni wahitaji, mtu yeyote asimhukumu." (*Didache* 1989: 11.3-.12)

Waraka wa Mkristo wa siku za kale *The Shepherd of Hermas* (c. 95-154) vile vile unaweka mkazo katika kuona mwenendo wa mtu katika kutathmini kama yeye ni nabii wa kweli au wa uongo: "Mtambue mtu mwenye Roho wa kiungu kwa mtindo wa maisha yake. Jambo la kwanza yule mwenye Roho wa kiungu ni mpole, mtulivu na mnyenyekevu na hujiona yeye si kitu kuliko wengine, na hajibu aulizwapo. Wala hazungumzi mwenyewe (wala Roho Mtakatifu hazungumzi wakati mtu yule anapotaka kuzungumza), lakini huzungumza Mungu anapomtaka kuzungumza. . . . Sasa sikia, alisema, kuhusiana na roho wa kidunia asiye na faida, ambaye hana nguvu bali ni mjinga. Kwanza, mtu yule anayejidhania kuwa ana roho hujiinua na anataka apewe kiti cha heshima, na mara tu ana majivuno, hana aibu na mwenye maneno mengi na mwenye kujawa na wingi wa vitu vya anasa na starehe nyingi na hupokea fedha kwa unabii anaoutoa. Sasa, je Roho wa Mungu anaweza kupokea fedha na bado atabiri? Nabii wa Mungu hawezi kufanya hivi, lakini roho za manabii wafanyao hivyo ni ya kidunia." (*Shepherd of Hermas* 43.7-.8, .11-.12)

3. *Namna ya kushughilika na manabii wa uongo:* Mtu anapodai ameagizwa na Mungu kusema jambo wakati hakuagizwa kusema hilo si swala dogo (**Yer 14:14-16; Ezek 22:28; 1 Yoh 4:1-3**). Kuruhusu nabii zisizo sawa ziendelee bila kuzipima au kuzihoji, na kuwaruhusu watu wajiite "manabii" wakati hawamwakilishi Mungu na Neno lake, huweza kutupeleka kwenye kuchanganyikiwa na kuwaongoza watu kubaya (**Matendo 20:29-30; 1 Kor 11:3; 1 Tim 1:4; 4:1-2; 6:20-21**). Ikiwa kile kinachoitwa "unabii" si sahihi, huyo anayeitwa "nabii" yapasa akabiliwe kwa ajili ya kumuadibisha kikanisa; lengo kuu ni kulitengeneza kanisa na kulirejesha katika kweli ya maandiko na jamii (**Math 18:15-20; Gal 6:1; Yak 5:19-20**). Ikiwa mtu huyo atakuwa mwenye toba, muelewa, na anayetaka kujifunza, kama Apolo—ambaye alifundisha kwa usahihi lakini kimapungufu ila alikubali kusahihishwa na Akila na Prisila—Mungu anaweza kumtumia mtu huyu hapo mbeleni (ona **Matendo 18:24-28**). Hata hivyo, kama mtu huyo hatakubali kutubu na akaendelea kunena upotofu kwa jina la Mungu, lazima aletwe

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

mbele ya kusanyiko na kutengwa na ushirika kama nabii wa uongo (Math. 18:17; 2 Kor. 11:4, 2 Yn. 9-11). Lengo la kuchukua hatua kali namna hii si kuweka mazingira ya hofu ya kumtumikia Mungu, bali ni kuweka usalama katika jamii ya kanisa ili watu wawe na hofu ya kusema tofauti na maagizo ya Mungu (1 Kor. 5:1-5, 13; 1 Tim 5:20)." (Kell 2006: 51; see also **Gal 1:8** [*"Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yoyote isipokuwa hiyo mliyoipokea, na alaaniwe"*])

- <u>Mwinjilisti.</u> Mwinjilisti ni yule ambaye hupeleka injili kwa watu, hasa kwa wale ambao hawajasikia bado. Uinjilisti—kuitangaza injili—ni zaidi ya kule kumtangaza Yesu, ya kwamba alikufa kwa ajili ya dhambi zetu na alifufuka kutoka kwa wafu, na kwamba watu wanahitaji kutubu na kumjia kama Mwokozi na Bwana. Injili imekusudiwa kuathiri maisha yetu yote. Kwa hiyo, Kongamano la Lausanne kuhusiana na Kuihubiri Dunia huuelezea "uinjilisti" namna hii: "Kufanya uinjilisti ni kutangaza habari njema kwamba Yesu Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu na alifufuliwa kutoka kwa wafu kama yanenavyo Maandiko, na ya kuwa Bwana anayetawala sasa anatoa msamaha wa dhambi na vipawa vya Roho ya kuwaweka huru wote wanaotubu na kuamini. Uwepo wetu hapa duniani ni muhimu kwa ajili ya uinjilisti, na vivyo hivyo mjadala wa aina hiyo ambao lengo lake ni kusikiliza kwa makini ili kuelewa. Lakini uinjilisti wenyewe ni kumtangaza Yesu wa kihistoria wa Biblia ambaye ni Mwokozi na Bwana, kwa mtazamo wa kuwashawishi watu kumjia kibinafsi ili kupatanishwa na Mungu. Tunapowaita watu kupokea wito wa injili hatupaswi kuficha habari kuhusu gharama ya kuwa mwanafunzi. Yesu bado anawaita wote ambao watamfuata kujikana nafsi zao, na kubeba msalaba wao, na kujitambulisha wao wenyewe na jamii yake mpya. Matokeo ya uinjilisti ni pamoja na utii kwa Kristo, kujiunga na kanisa lake na kutumika kikamilifu duniani." ("Lausanne" 1974: n.p.) Watu wengi wanaojiita wainjilisti wana "uwepo wa dunia" kidogo "hawajadili" au "kusikiliza kwa makini ili waelewe" huficha habari kuhusu "gharama ya kuwa mwanafunzi," na hawawaiti watu "kujikana wenyewe, na kubeba misalaba yao, na kujitambulisha na jamii yake mpya." "Uinjilisti" wa jinsi hii uko kinyume na Kristo mwenyewe ambaye aliweka mkazo "kuhesabu gharama" kujitoa kwake tu (ona **Math 10:37-39; 16:24-25; Marko 8:34-35; Luka 9:23-24; 14:26-33**).
- <u>Mchungaji-Mwalimu.</u> Mchungaji–mwalimu ameshaelezewa hapo nyuma katika sehemu ya **II.B. *Muundo na uongozi wa kanisa***. Mchungaji anayo majukumu mengi. Lazima ahubiri, afundishe, ahusike na utawala wa kanisa na sakramenti, kuadibisha na kushauri, kutembelea wagojwa, kufariji wafiwa, kufungisha ndoa na kuzika, na kusimamia matukio mengine. Huu wito wenye majukumu mengi umetajwa kwa neno la Kiyunani (*poimēn*) "mchungaji" lililotumika katika **Efeso 4:11**. *Poimēn* kwa kawaida hutafsiriwa kama "mchungaji (wa wanyama)." Yesu ndiye mchungaji mkuu. Alisema, *"Mimi ndimi mchungaji mwema. Mchungaji mwema huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo. . . . Kondoo wangu waisikia sauti yangu; nami nawajua, nao wanifuata."* (**Yoh 10:11, 27**) Kama Yesu, mchungaji anapaswa "kujua" kundi lake—anapaswa kuwa na muda nao; yeye ni mtumishi wao, akiyatoa maisha yake kwa ajili yao (ona **Math 20:25-28; Marko 10:42-45; Yoh 13:5-15**).

Ukweli kwamba uongozi wa kanisa unahusu utendaji wa majukumu, na sio cheo, pia inaonekana katika **Efeso 4:12**, ambayo inasema kwamba *kusudi* la Yesu kuwapa watu fulani vipawa fulani na nafasi za kuongoza ni *"kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata mwili wa Kristo ujengwe."* Kwa maneno mengine, wale ambao ni mitume, manabii, wainjilisti, na wachungji-walimu wanatakiwa kuhusika na washirika wa kanisa na wanatakiwa kufunza na kuandaa washirika wa kanisa ili na wao wawe mitume, manabii, wainjilisti, na wachungaji walimu. Hii inamaanisha kwamba, wakati Roho Mtakatifu anapogawanya vipawa vya rohoni *"kwa kila mtu kama apendavyo"* (**1 Kor 12:11**), na sio wote ni mitume, manabii, walimu, nk. (**1 Kor 12:29**), vipawa na ujuzi wa mitume, manabii, wainjilisti na wachungaji walimu vyaweza kufundishwa na kujifunza na watu wanapaswa kuvitamani (ona **1 Kor 12:31; 14:1**). *"Kuwezesha watakatifu"* kunahusisha mambo kadhaa:

1. Kutambua karama, vipawa, na uwezo wa washirika wa kusanyiko, kuwezesha matumizi ya hizo karama, vipawa, na uwezo (ona **Rum 12:6-8; 1 Kor 12:7-31; 14:12; 1 Pet 4:10-11**).
2. <u>Kufundisha, kuagiza, kuhimiza, kufariji, na kuonya kundi kutoka katika Neno la Mungu kuhusiana na mambo muhimu ya mafundisho ya Ukristo na maisha—kwa kifupi, kufunza wanachama wa kanisa kuwa *wanafunzi wakomavu* (ona sehemu **V. KUFANYA WANAFUNZI** na **VI. Mambo Muhimu kuhusu Mafunzo Mazuri ya Kufanya Wanafunzi**, huko nyuma; ona pia **Matendo 2:42; 5:42; 1 Kor 14:19; 2 Kor 1:34; 4:5; 10:8; 1 Thes 4:1; 5:12-14; 1 Tim 4:1-6, 11, 13, 16; 6:2b; 2 Tim 2:2; 3:16-17; 4:1-4; Tito 2:1**).</u>
    a. Ili mchungaji aweze kufundisha vizuri, inabidi awe na zana za kibiblia, kama vile vitabu vyenye kutoa ufafanuzi, vitabu vyenye orodha ya maneno ya Biblia na maana zake na yalipo katika Biblia, nafasi ya kuhudhuria semina na mafundisho mbalimbali ya kithiolojia na masomo ya Biblia yanayopatikana kwake.
    b. Kwa sababu hivi vyote hugharimiwa kwa pesa, kanisa litenge kiasi cha pesa katika bajeti

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

yake kwa ajili ya zana hizi.

c. Kwa sababu makanisa mengi, hasa yale ya vijijini, hayana pesa za kutosha, ofisi ya wilaya ya madhehebu hayo au dayosisi iwe na bajeti kwa ajili ya kuanzisha maktaba katika ngazi ya wilaya au dayosisi ambayo itatumiwa na wachungaji woa wote.

3. Kutambua na kukuza viongozi ndani ya kanisa (ona **Kut 18:17-26; Kum 34:9; 2 Waf 2:1-15; Yoh 17:18; Matendo 1:15-25; 6:1-7; 14:23; 2 Kor 8:16-22; 1 Tim 3:1-13; Tito 1:5**). Hapa inatakiwa viongozi waliopo kuwajua watu wao vizuri na wawe na muda nao, na wanatarajiwa, kuwafundisha na kuwafinyanga ili wawe viongozi wa Kikristo.

4. Kuadibisha wale wanaosababisha matengano, kufundisha uzushi, au wanahusishwa na kashfa za uzinzi (ona **Math 18:15-17; Rum 16:17-20; 1 Kor 5:1-8, 12-13; 1 Tim 1:3; 2 Tim 2:14-18**). Baraza la kanisa, na kanisa kama mwili, lahitajika kuhusika katika hatua za kuadibisha (ona **2 Kor 2:6**). Adhabu hutolewa kwa faida ya mkosaji (**1 Kor 5:5; 1 Tim 1:20**) na kwa faida ya kanisa lenyewe. Kanisa linapohusika katika mchakato wa kuadibisha, watu hujisikia kuwa wana nafasi katika maisha ya kanisa, kushiriki majukumu yao kama Wakristo kwa kumaanisha zaidi, na kuletwa karibu zaidi na kanisa.

5. Kurejesha ushirika kwa wale ambao wamekuwa wahanga wa kuadibishwa kanisani, wametubu, na kubadilika katika tabia zao (ona **2 Kor 2:5-11; 7:8-12; Gal 6:1**).

**B. *Huduma inahusisha watu wote ndani ya kanisa, sio wachungaji tu***

1. Makanisa mengi huendeshwa kwa namna ambayo mchungaji hufanya kila kitu—ndiye mamlaka ya juu zaidi na huamua nini kifanyike au kisifanyike. Watu wapo tu—wanakuja tu na "kuabudu" Jumapili. Kanisa la jinsi hiyo si la Kibiblia:

a. Ingawaje katika AK ulikuwepo ukuhani wa watu maalum, katika AJ waaminio wote wanatambulika kuwa ni "makuhani" (**1 Pet 2:9; Ufu 1:6**).

b. Waaminio wote wamepewa karama ambazo yapaswa zitumike kwa faida ya mwili wote (**Rum 12:6-8; 1 Kor 7:7; 12:7-11, 28; 14:12; Efeso 4:7-8; 1 Pet 4:10-11**).

c. Ingawaje kuna kiwango kikubwa cha uhuru wa kutumika katika AJ kuhusiana na uongozi wa kanisa, si kila mtu ameitwa kuongoza, mfumo wa mamlaka ya kanisa wakati wote uko juu ya wazee zaidi ya mmoja au viongozi ndani ya kanisa, sio mtu mmoja (**Matendo 11:30; 14:23; 15:2-6, 22-23, 28; 16:4; 20:17-18; 21:18; Fil 1:1; 1 Tim 5:17; Tito 1:5; Yak 5:14; 1 Pet 5:1**).[26]

2. Maana ya msingi ya "huduma" ni "utumishi."

a. *Neno kuu la Kiyunani la "huduma" katika AJ ni diakonia ambalo humaanisha "utumishi"* (ona **Matendo 1:17, 25; 6:4; 12:25; 20:24; 21:19; Rum 11:13; 12:7; 1 Kor 16:15; 2 Kor 4:1; 6:3; 8:4; 9:1; Efeso 4:12; Kol 4:17; 1 Tim 1:12; 2 Tim 4:5, 11**).

b. *Neno kuu la Kiyunani la "mhubiri" katika AJ ni diakonos ambalo lina maana "mtumishi"* (ona **Math 23:11; Marko 9:35; 10:43; Yoh 12:26; Rum 16:1; 1 Kor 3:5; 2 Kor 3:6; 6:4; Efeso 3:7; 6:21; Kol 1:7, 23, 25; 4:7; 1 Thes 3:2; 1 Tim 4:6**), na *doulos* lenye maana "mtumwa" (ona **Math 24:45, 46, 48, 50; 25:14, 19, 21, 23, 26, 30; Marko 10:44; Luka 17:10; Yoh 13:16; 15:20; Matendo 2:18; 4:29; Rum 1:1; 2 Kor 4:5; Gal 1:10; Efeso 6:6; Fil 1:12 Tim 2:24; Tito 1:1; Yak 1:1; 1 Pet 2:16; 2 Pet 1:1; Yuda 1:1; Ufu 1:1**).

c. *Umuhimu wa maneno haya kwa viongozi ndani ya kanisa uko sehemu mbili:*

(1) AJ kwa makusudi kabisa hukwepa kuwapa viongozi wa kanisa majina ya vyeo ambayo humaanisha nguvu, heshima, na uwezo wa utendaji wa "kikuhani".

(2) Kristo alikazia kwamba viongozi wa kanisa, pamoja na mitume wake, walitakiwa kuutumikia mwili (**Math 18:1-4; 20:25-28; 23:8-12; Marko 9:33-35; Luka 9:46-48; 22:24-27**).

d. Matumizi ya maneno haya pia hukazia kwamba, kwa kuwa waaminio wote ni watumishi na watumwa wa Kristo, waaminio wote ni "wahubiri" na wana "huduma" ya kutumika katika ufalme.

**C. *Huduma ndani ya kanisa inahusisha huduma katika eneo la "kimwili" na pia katika eneo la "kiroho"***

"Kutumika kunapingana na mwelekeo wetu wa asili. Mara nyingi tunataka zaidi *'tutumikiwe'* kuliko *kuhudumia*. Tunasema, 'Ninatafuta kanisa ambalo litanipatia mahitaji yangu na linanibariki,' sio 'Ninatafuta mahali ili nitumike na *kuwa* baraka.' Tunatarajia watu wengine watutumikie, sio kinyume chake. Lakini

[26] Hili lilijadiliwa hapo juu katika sehemu **II.B.** ***Muundo na uongozi wa kanisa***.

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

tunapokomaa katika Kristo, fokasi ya maisha yetu lazima ibadilike kwa kiwango kikubwa kuelekea kwenye kuishi maisha ya kutumikia wengine. Wafuasi wa Kristo waliokomaa huacha kuuliza, 'Nani atakutana na mahitaji yangu?' na huanza kuuliza, 'Ni mahitaji ya nani naweza kuyatimiza?' Je wewe huwa unauliza swali hilo?" (Warren 2002: 213)

1. <u>Katika mambo waliyofundisha na kutenda, wote Yesu na mitume, walikazia umuhimu wa kujali usalama wa mambo ya mwilini na pia wa yale ya rohoni wa ndugu waaminio.</u>

a. *"Amri mpya" ya Yesu ya "kupendana ninyi kwa ninyi kama vile nilivyowapenda ninyi," ilitolewa kwa wanafunzi (**Yoh 13:34**).* Upendo wao waliounyesha *wao kwa wao* ulikuwa ishara ambayo kwayo *"watu wote wanatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu"* (**Yoh 13:35**).

b. Tamko la Yakobo kwamba *"imani pasipo matendo imakufa"* (**Yak 2:26**) lilitolewa katika muktadha wa *"ikiwa ndugu mwanamume au ndugu mwanamke yu uchi na kupungukiwa na riziki"* (**Yak 2:15**).

c. *Paulo aliagiza kanisa kutoa pesa ili kuwasaidia ndugu waaminio (**2 Wakorintho 8-9**).* Kanisa la kwanza lilijihusisha na mahitaji ya kimwili ya waaminio (**Matendo 2:44-45; 4:32-37**). Kwa hakika, kanisa la kwanza lilianza huduma ya shemasi kwa usahihi ili kuweza kuhudumia mahitaji ya waaminio ya kimwili vizuri na bila upendeleo (**Matendo 6:1-6;** ona **1 Tim 3:8-13**).

d. *Kuwapatia waaminio mahitaji yao kuna matokeo yenye maana kubwa sana kiroho.* **Matendo 4:33-35** inasema, *"[33] Na mitume wakatoa ushuhuda wa kufufuka kwake Yesu kwa nguvu nyingi, na neema nyingi ikawa juu yao wote. [34] Wala hapakuwa na mtu mmoja miongoni mwao mwenye mahitaji; kwa sababu watu wote waliokuwa na viwanja au nyumba waliviuza, wakaileta thamani ya vitu vile vilivyouzwa, [35]wakaiweka miguuni pa mitume; kila mtu akagawiwa kwa kadiri ya alivyohitaji."* Mitume waliweza kuhubiri *"kwa nguvu nyingi,"* na *"neema nyingi ilikuwa juu yao wote,"* <u>kwa</u> (au <u>kwa sababu</u>) *"hakuwepo mtu hata mmoja mwenye mahitaji kati yao."* Kilichosababisha asiwepo mwamini hata mmoja mwenye mahitaji ilikuwa <u>kwa kuwa</u> (au <u>kwa sababu</u>) wote waliokuwa na mali waliuza, na pesa walizopata *"ziligawanywa kwa kila mwenye hitaji."* Hivyo, waaminio walihudumiana mahitaji ya kimwili wao kwa wao. Hii ilimaanisha kwamba wasioamini waliona kilichokuwa kikitokea, ya kwamba ndani ya kanisa, Wakristo walikuwa na mtindo tofauti wa maisha—mtindo bora wa maisha. Wakristo na kanisa wanapoenda kama wanavyopaswa, inaonyesha tofauti ambayo kila mtu anaweza kuiona. Matendo ya waamini kuuza mali zao na kuwasaidia ndugu walio wahitaji yalithibitisha mahubiri ya mitume, hii ndio maana ushuhuda wa mitume ulikuwa na nguvu sana. Makanisa yetu ya leo yatapata matokeo yayo hayo ikiwa tutafanya kama walivyofanya kanisa la kwanza.

2. <u>"Karama za rohoni" ni pamoja na karama ambazo zinahusisha mambo ya mwili moja kwa moja katika maisha.</u> Karama za "rohoni" ni pamoja na vitu kama: hudumu na kuhudumu (**Rum 12:7**); kutoa (**Rum 12:8**); kurehemu (**Rum 12:8**); uponyaji (**1 Kor 12:9, 28**), masaidiano (**1 Kor 12:28**), na mambo ya utawala (**1 Kor 12:28**). Hii inatuonyesha kwamba Mungu nahusika na kila mambo yote yanayohusu maisha yetu. Hivyo, tunapaswa kuhusika na mambo yote yahusuyo maisha ya ndugu zetu wa kiroho. Ni muhimu kukumbuka kwamba "kwa kuwa uwezo wako wa kufanya vitu katika mwili kiasili unatoka kwa Mungu, ni wa muhimu na wa 'kiroho' kama karama za rohoni. Tofauti ni moja tu ni kwamba uwezo huo ulikuwa nao tangu kuzaliwa." (Warren 2002: 242)

3. <u>Mambo muhimu ya huduma ndani ya kanisa yahusiyo maswala ya "mwili".</u> Watu waliomo kanisani wana mahitaji, lakini watu waliomo kanisani pia ni vyanzo vya kukidhi mahitaji. Kanisani ndipo mahali pa kwanza ambapo mtu anapaswa kupafikiria anapokuwa na uhitaji au anapokuwa anataka kusaidia wale wenye uhitaji. Kuwajali masikini, wagonjwa, wenye mahitaji maalum kimwili na kiakili, waliotengwa ni muhimu sana: "Kuwatenga walio dhaifu na wasio na kitu, wanaoonekana kuwa ni watu wasio na faida, katika jamii ya Kikiristo kutamaanisha kwamba ni kujitenga na Kristo; ndani ya yule ndugu maskini Kristo anagonga mlangoni. Kwa hiyo, lazima tuwe makini sana kuhusiana na swala hili." (Bonhoeffer 1954: 38) Eneo hili la huduma limesemwa na Yesu na mitume kwa kurudiwarudiwa na mkazo na kanisa la kwanza walilitekeleza kimatendo (ona **Math 5:31-46; Matendo 2:44-45; 4:32-35; 11:27-30; Rum 12:16; 15:26-27; 1 Kor 16:1-2; 2 Kor 8:1-9:15; Gal 6:10; Yak 1:27; 2:14-17**). Maskini na wahitaji ni pamoja na wale ambao wanapungukiwa mahitaji muhimu ya maisha lakini pia na wale ambao wana mahitaji ya kiroho, kimahusiano na mahitaji mengine. Yafuatayo ni baadhi ya mapendekezo:

- <u>Kuwasidia maskini wa kipato na wahitaji waweze kijikimu:</u>
  (A) *Watu wengi walio wahitaji wangependa waweze kujikimu kuliko kuomba misaada kila siku.*

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

Kanisa linaweza kuwasaidia ili wweze kujikimu. Baadhi ya mapendekezo ni pamoja na: (1) Kutoa mikopo midogo kwa wahitaji. Hili litahitaji kwamba anayepewa awe na mradi alioukusudia tayari. Pia utaratibu wa ufuatiliaji na uwajibikaji utahitajika kuwepo. Tatizo moja kubwa ni kutokulipwa kwa mikopo. (2) Wahitaji wapewe kazi. Hili litahitaji kujua ni nani katika kusanyiko ana biashara, anahitaji msaada nyumbani kwake au anaweza kuajiri watu. Kanisa lenyewe linaweza kuwalipa kwa kufanya usafi wa jengo na mazingira au kazi nyinginezo za kanisa. Dhana ya "utaratibu wa wajane" ni wazo jingine. (3) Toa misaada isiyohusisha fedha. Kanisa linaweza kuwa "ghala" kama lilivyokuwa hekalu la kale (ona **Mal 3:10**) la nguo, chakula kisichoharibika, au vitu vinginevyo vinavyohitajika na wahitaji. Kanisa moja la PAG pale Uganda lilikuwa na wajane 43. Badala ya kuwapa fedha, waliwanunulia mbuzi. Baada ya miaka miwili wale mbuzi 43 waliongezeka na kuwa 281. Wale wajane waliweza kujikimu. Walikuwa na maziwa. Waliweza kuwauza mbuzi na kupata hela. Baadhi ya wajane walinunua ng'ombe baada ya kufanya biashara ya mbuzi. Matokeo yake, wale wajane walivutwa karibu kanisani na wengi wao wamekuwa "mashujaa wa maombi" waaminifu na wanatoa kanisani. Protais Nshogoza wa Rwanda anatoa mfano mwingine: "Mimi na familia yangu tuliondoka Kigali mwaka 2008 kwenda wilaya ya Gicumbi kwa kuitikia wito wa Mungu. Watu wa kwanza niliokutana nao walikuwa wanawake waishio na VVU. Walikuwa hawana tumaini wala msaada. Nilianza kuomba nao na kuwafundisha Neno la Mungu; hilo likaleta tumaini katika maisha yao. Kisha nikaona kwamba umasikini ulikuwa ndisho kikwazo kinachowafanya washindwa kujikimu kimaisha. Nikawapa vitoto vya nguruwe kumi na baada ya miezi sita walikuwa na nguruwe 80. Kila mwanamke aliweza kugawa robo ya wanaozaliwa kwa mjane mwingine na baada ya miaka nane zaidi ya wanaweke 150 walikuwa wamefaidika na Baraka ile na waliweza kutunza familia zao vema, wakakarabati nyumba zao, walilipa ada za shule za watoto wao, na walilipa bima ya afya ya kila mwaka. Sasa nahitaji kuwaletea mbegu za kisasa ambazo huzaa sana ili waweze kukuza biashara yao ya ufugaji wa nguruwe. Hii itakuwa hatua kubwa ya kufanya wanafunzi kwa wanawake ambao walikuwa katika maisha hatarishi katika eneo hili."

(B) *Kanisa linapaswa kutambua vyanzo vingine vya kutegemeza.* Kanisa la mahali halina uwezo wa kukidhi kila hitaji la watu wake. Hata hivyo, linaweza kushirikiana na au kupeleka wale wahitaji kwenye mashirika mengine ambayo yanaweza kutoa vitu au huduma ambazo kanisa haliwezi kutoa. (1) Vyanzo vingine vya msaada wa vitu ni pamoja na: NGOs; mashirika mengine ya misaada ya Kikiristo. (2) Madhehebu mbali mbali yana huduma za kutoa misaada na mawakala wanaoshughulika na ustawi wa jamii. Kanisa Anglikana lina "Umoja wa Kina mama." Kanisa la PAG la Uganda lina "PAG Planning and Development Secretariat." (3) Makanisa mbali mbali, na makanisa ya madhehebu tofauti, yanapaswa kufanya kazi pamoja ili kutatua matatizo yatokanayo na mahitaji yaliyopo katika maeneo yao. Kwa kufanya hivyo watakuwa pia wameonyesha umoja, ambao ni misheni na kusudi la msingi la kanisa.

- Kusaidia wasio na kazi kupata kazi—ikiwa ni kazi za kuwapatia kipato nje ya kanisa au huduma ndani ya kanisa. "Kazi ni wito wa Mungu juu ya maisha ya kila mtu. Ndio mduara ambao kwao, na situ ndani ya huo, Mkristo anamtumikia Kristo na ufalme wake. Ni jukumu la kumshughulisha—jukumu kuu la maisha ya mtu—kupitia hilo anamiliki eneo fulani la utendaji (Luka 19:13) kwa ajili ya Yesu Kristo." (Miller 2002: 9) Biblia inawaagiza Wakristo kuwa na kazi za kuwapatia kipato (**Efeso 4:28; 2 Thes 3:10**). "Katika jamii ya Kikristo kila kitu hutegemea ikiwa kila mmoja huhitajika kiasi gani katika ule mnyororo. Ni mpaka kila mmoja awe ameunganishwa kikamilifu katika ule mnyororo hata yule mdogo kabisa ndipo mnyororo hauwezi kukatika. Jamii inayoruhusu kuwepo kwa wasiofanya kazi miongoni mwa wanachama wake itaangamia kwa ajili yao. Kwa hiyo, itakuwa ni vema, ikiwa kila mwanachama atapewa jukumu lake la kutenda kwa ajili ya jamii, ili atambue pasipo shaka kwamba, yeye pia ana kitu cha kuchangia katika jamii." (Bonhoeffer 1954: 94) Ikiwa kuna watu wanaohitaji kazi ndani ya kanisa, wanachama wengine wa kanisa wanaweza kuwa wamiliki wa biashara wanaohitaji wafanyakazi. Viongozi wa kanisa wanatakiwa kuwajua watu wao na waweke mpango wa kuwaunganisha wale wenye mahitaji na wale wanaoweza kutatua mahitaji hayo.
- Kuomba na kuombeana mmoja kwa mwingine. "Ushirika wa Kikristo huwapo na kuwa hai kupitia maombezi ya wanachama wake kati ya wao kwa wao, vinginevyo hautasimama. Siwezi kumhukumu au kumchukia ndugu ambaye ninamuombea, bila kujali ni kiasi gani cha matatizo amenanisababishia. Uso wake, ambao unaweza kuwa mgeni na nisioweza kuuvumilia, unabadilishwa katika maombezi na unakuwa ni uso wa ndugu ambaye Kristo alimfia, uso wa mwenye dhambi aliyesamehewa. . . . Maombezi ni bwawa la kujisafisha mtu na ushirika lazima

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

waingie kila siku. Shida tunayoipitia na ndugu yetu katika maombezi inaweza kuwa ngumu, lakini shida hiyo ina ahadi kwamba itatekeleza lengo lake." (Bonhoeffer 1954: 86; ona **Yak 5:16**) Henry Blackaby na Claude King vile vile wanasema, "Mengi ya makanisa yetu hayajajifunza namna ya kuomba pamoja. Chanzo kikuu cha nguvu ninachokijua ambacho bado hakijatumiwa ni maombi ya umoja ya watu wa Mungu. Yesu, akinukuu kutoka Isaya 56:7, alisema, 'Nyumba yangu ni nyumba ya sala' (Luka 19:46). Kulisaidia kanisa lako kuwa kanisa la watu wanaoomba litakuwa jambo lenye matokeo yanayolipa. Kila kanisa linapaswa kuwa kanisa la watu wanaoomba!" (Blackaby and King 1994: 308-09)

- <u>Kusameheana.</u> **Efeso 4:32** na **Kol 3:13** yote hutuamuru sisi kusameheana. Yesu aliendelea kwa kusema, *"Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi makosa yenu. Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu wa mbinguni hatawasamehe ninyi makosa yenu."* (**Math 6:9-15**; ona pia **Math 18:21-35; Marko 11:25-26**) Kutosamehe humpa shetani fursa na nafuu ya kutenda kazi kupitia kwetu na kinyume chetu, kibinfsi na kama kanisa (**2 Kor 2:10-11**). Kusamehe huugusa moyo wa Mungu Baba na asili na misheni ya Kristo (**Kut 34:6-7; Math 9:2-8; Marko 2:3-12; Luka 5:17-26; 7:48-50**). Hivyo, kwa kuwa tunapaswa *"kufananishwa na mfano wa [Kristo]"* (**Rum 8:29**), kwetu sisi kuwasamehe wengine ni alama muhimu ya *utakaso.* Ni ishara ya utendaji kazi wa Roho Mtakatifu ndani yetu wa kutubadilisha kwa mfano wa Kristo na kutukamilisha. Ndio maana Kristo alihusianisha msamaha na upendo (**Luka 7:36-50**) na maombi (**Marko 11:23-26**). Kitabu cha ECLEA kinachohusu *Msamaha & Upatanisho* (http://www.eclea.net/courses.html#forgive) huelezea msamaha na upatanisho kwa kirefu, pamoja na mifano hai ya jinsi ya kusamehe na kupatana. Ni msaada mzuri kwa kanisa kutumia kwa ajili ya kuwafunza watu wake katika eneo hili.
- <u>Kutiana moyo, kuwa na mwingine, vile vile kubebeana na kushirikishana mizigo.</u> *"Mchukuliane mizigo na kutimiza hivyo sharia ya Kristo"* (**Gal 6:2**; ona pia **Kol 3:13**). "Sheria ya Kristo ni sheria ya kuchukulia. Kuchukulia maana yake ni kustahimili na kuvumilia. Ndugu ni mzigo kwa Mkristo, kwa sababu ni Mkristo. . . . Ni mpaka atakapokuwa mzigo ndipo hapo mtu mwingine anapokuwa kweli ndugu na sio tu chombo cha kuchezewa. Mzigo wa watu ulikuwa mzito sana kwa Mungu mwenyewe kiasi kwamba aliustahimili msalaba. Hakika Mungu pia alibeba mzigo wa wanadamu katika mwili wa Yesu Kristo. Lakini alibeba kama mama abebavyo mtoto wake, kama mchungaji amkumbatiavyo mwana kondoo alieonekana baada ya kupotea. . . . Ni sheria ya Kristo ambayo tunatekeleza msalabani. Na Wakristo ni lazima washirikiane katika sheria hii. Ni lazima wabebe ndugu wao, lakini, kilicho muhimu zaidi, sasa kwa kuwa sheria ya Kristo imekwishatekelezwa, wanaweza *kubeba* mzigo na ndugu zao. . . . Ni ushirika wa msalaba kuchukua mzigo wa mwingine. Ikiwa mtu hapitii hayo, ushirika ambao yuko si wa Kikristo. Ikiwa kuna mwanachama ambaye atakataa kushiriki kubeba mzigo, anaikana sheria ya Kristo." (Bonhoeffer 1954: 100-101)
- <u>Kuwa na wakati wa pamoja, kuwa na ushirika sisi kwa sisi, na pia kushiriki katika kulibadilisha kanisa kuwa familia ya kweli yanye upendo.</u> **Matendo 2:42, 46-47** hulielezea kanisa la kwanza kama ifuatavyo: *"Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali. . . . Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na moyo mweupe, wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote."* Alama zaidi zinazoonyesha maisha ya kujaa Roho Mtakatifu zinapatikana katika jamii, si tu kibinafsi. **Efeso 5:19-21** (ESV) huzungumzia ishara za kujazwa na Roho kuwa ni *"mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu; na kumshukuru Mungu Baba siku zote kwa mambo yote, katika jina lake Bwana wetu Yesu Kristo. Hali mnanyenyekeana katika kicho cha Kristo."*

AJ mara kadha wa kadha huhimiza waaminio kupendana (**Yoh 13:34-35; Rum 13:8; 1 Thes 3:12; 4:9; 1 Pet 3:8; 4:8; 1 Yoh 3:11, 23; 4:7, 11-12; 2 Yoh 5**), farijianeni (**1 Thes 4:18; 5:11; Ebr 3:13; 10:24-25**), fundishaneni na kuonyana (**Rum 15:14; Col 3:16**), hudumianeni (**Yoh 13:14-15; Gal 5:13; 1 Pet 4:10**), muwe na subira, wavumilivu, mkichukuliana kwa upendo (**Rum 15:7; Efeso 4:2**), muwe na huruma, wakarimu, na mkihudumiana (**1 Kor 12:25; Efeso 4:32; 1 Pet 4:9**), mpatane nia na muwe na amani ninyi kwa ninyi (**Marko 9:50; Rum 12:16; 1 Pet 3:8**), na mheshimiane kwa kuwaona wengine kuwa ni bora kuliko wewe (**Rum 12:10; Fil 2:3**). Kwa kifupi, waaminio wanapaswa *"Kwa pendo la udugu, kupendana wao kwa wao"* (**Rum 12:10**). AJ huelezea kanisa kama familia (ona **Marko 10:29-30; Rum 8:14-17; 2 Kor 6:18; Efeso 1:5; 2:19; Gal 3:26-4:7; 1 Tim 3:15; 5:1-2**). Hizi zote ni sifa za familia nzuri, inayotenda kazi vema. Kanisa

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

linahitajika kuonyesha, kwake na kwa dunia, ya kuwa ni, familia njema, inayotenda kazi vema. Hii ni huduma; ni maisha katika roho; ndivyo muonekano wa maisha katika mwili unavyopaswa kuwa.

## VIII. MISHENI

- "Ni nani atakayemwamini Mungu ambaye atayafanya mambo yote kuwa mapya hapo baadaye ikiwa hakuna kinachoonekana dhahiri katika maisha ya wale wanaomtaraji ya kwamba tayari amesha anza kufanya kila kitu kipya *sasa*—ikiwa haiko dhahiri sasa kwa hili tumaini la yale yajayo linaweza *sasa* kubadilisha mwenendo wa historia uwe na matokeo bora? . . . Itabidi ieleweke wazi kutokana na utendaji thabiti wa maisha ya Kikristo ya kwamba Mungu [kwa kweli] hujidhihirisha kama ambaye nguvu zake zinaweza kuleta maisha mapya katika wakati ujao." (Schillebeeckx 1968: 183-84)
- "Si kwamba msalaba wa Kristo unamaanisha wokovu tu kwa mtu, lakini ni kiini cha tahakiki inayokuwezesha kuonamambo ya kisiasa, kiuchumi, kijamii katika upeo mwingine. Toba na kubadilishwa kwa watu ni lazima kulete matengenezo ya utamaduni na kujengwa upya kwa jamii." (Miller 2001: 22)
- "Kipekee, kanisa hutangaza dunia iliyobadilika kama matokeo ya kubadilika kwa watu. Mtu mwenye fikra huleta falsafa mpya; ni mtu aliyebadilika pekee ndiye aliyekamata siri ya jamii ambayo ni mpya hasa." (Rees 1964: 9)
- "Kwa kusudi hili [Kristo] alikuja, kuleta Amani kwa maadui wa Mungu. Kwa hiyo Wakristo pia, hawako katika maisha yaliyojitenga bali wako katikati ya maadui." (Bonhoeffer 1954: 17) "Kanisa ni kanisa tu pale ambapo lipo kwa ajili ya wengine. . . . Kanisa lazima lishiriki katika matatizo ya kawaida ya kimaisha ndani ya jamii, si kwa kutawala bali kwa kusaidia na kuhudumia. Lazima litoe ujumbe kwa watu wa kila Nyanja ili wajue nini maana ya kuishi kwa ajili ya Kristo, yaani kuishi kwa ajili ya wengine." (Bonhoeffer 1971: 382-83)
- "Watu wa kanisa hufikiri kuhusu namna ya kuwaingiza watu wa duniani kanisani; watu wa Ufalme hufikiri kuhusu namna ya kuliingiza kanisa duniani. Watu wa kanisa wana wasiwasi kwamba dunia italibadilisha kanisa; Watu wa Ufalme hutenda kazi ili kuona kwamba kanisa linabadilisha dunia." (Snyder 1996: 11)
- "Njia ya mafanikio kwa makanisa ambayo yanataka kuikamata nafasi yao kwa upya katika jamii itakuwa ni kupitia kuhudumia na kujitoa dhabihu. . . . Kanisa la kimisheni ni *watu wa Mungu wanaofanya kazi na Mungu katika misheni yake ya kuikomboa dunia.* . . . Kazi yetu si 'kufanya kanisa' vizuri lakini ni kuwa watu wa Mungu kiuhalisia duniani. . . . Ni lazima tuwe tofauti katika lile tumaini tunalowapa watu, katika neema tunayoionyesha, na katika dhabihu ya upendo ulio wazi tunayouonyesha tunaposhughulika na wengine. . . . Wazo ya kwamba kanisa linaweza kuwa na mafanikio bila dunia ambayo imeendelezwa huonyesha utengano na misheni ya Mungu na pia huleta swali kwamba 'je watu wenye mtazamo kama huo wanatambuliwa na Mungu kama watu wake'." (McNeal 2009: 6, 24, 37, mkazo kwenye nakala ya asili)
- "Kuabudu . . . ni mafuta na lengo la umisheni. Ni lengo la umisheni kwa sababu katika umisheni tunakusudia kuyaleta mataifa kwenye kuufurahia utukufu wa Mungu. . . . Ikiwa lengo haliwi kuutafuta utukufu wa Mungu bali kutafuta matakwa ya watu yanayoendana na mapenzi ya moyo na vipaumbele vya kanisa, basi, mtu hatakuwa amehudumiwa sawa sawa, na Mungu hatakuwa amepewa heshima stahiki. . . . Moto wa kuabudu unapowaka ukiwa na joto la thamani halisi ya Mungu, nuru ya umisheni itang'ara hata kuwafikia wale wote walio katika giza nene kabisa duniani kote. . . . Mahali ambapo shauki ya Mungu ni dhaifu, ari ya umisheni itakuwa dhaifu." (Piper 2010: 35-36)
- "Wito wa wokovu ni wito wa kuwa katika misheni na Mungu anapokuwa katika kuipatanisha dunia iliyopotea na yeye mwenyewe kupitia Kristo. . . . Utakapokuwa na mahusiano ya upendo halisi na Mungu, atakuonyesha kile anachokifanya. Kazi yako kama mtumishi ni kufuata mfano wa Yesu: Fanya kile ambacho anakifanya Baba tayari—*ona ni wapi ambapo Mungu yuko kazini na ungana nae!"* (Blackaby na King 1994: 58, 84, mkazo kwenye nakala ya asili)

### A. *Msingi wa maandiko*

Misheni na kusudi la kanisa linaonekana katika kuwafikia na kuwahudumia wale walio nje ya kanisa. "Agizo kuu" la kanisa linapatikana katika **Math 28:18-20:** ***18***_Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, "nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani._ ***19***_Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu,_ ***20***_na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, niko pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."_[27]

---

[27] Robert Coleman anafafanu, "Maneno 'enendeni,' 'mkawabatize,' na 'kuwafundisha' yote yako katika wakati mtimilifu ambayo hupewa nguvu na kitenzi kinachotawala 'mkawafanye kuwa wanafunzi.' Hii inamaanisha kwamba agizo kuu si tu

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

Vile vile vifungu vya Biblia ambavyo hutia mkazo umuhimu wa kuwashuhudia wengine habari za Kristo ni pamoja na **Math 9:35-38; Marko 16:15; Yoh 17:18-21; Matendo 1:8; 5:27-32; 10:34-43; Rum 10:14-17; 15:18-21; 1 Kor 1:21-25; 2 Kor 4:4-13; 2 Tim 4:1-2; 1 Yoh 1:1-3.** Kitabu cha **Matendo** hutoa mifano kwa mifano ya jinsi waaminio wanavyowashuhudia wengine katika mazingira mbalimbali. Kama ambavyo kufanya wanafunzi huhusisha nyanja za kimwili na kiroho, vivyo hivyo umisheni wa kanisa huhusisha huduma na kuwafikia wengine katika nyanja zote za maisha (**Math 5:13-16; 22:36-40; 25:31-46; Yoh 13:4-15, 34-35; 20:21; Gal 6:10; Efeso 2:10; 1 Tim 6:17-18; Yak 1:27; 2:14-26; 1 Yoh 4:20-21**).

**B. *Kanisa limeitwa ili kufanya wanafunzi duniani kote***

Umisheni na kufanya wanafunzi ni vitu vilivyoungana. Watu wanapofanywa kuwa wanafunzi, vipawa vyao vya huduma vitajulikana nao watatiwa moyo kujiunga na huduma zilizopo au kuanzisha huduma mpya, ndani na nje ya kanisa. Vivyo hivyo, huduma yako ya kuwafanya wengine kuwa wanafunzi itatambua au itataka kutambua maeneo ya kiroho yanayo hitaji msaada na kutoa msaada huo. Kila mwamini amepewa kipawa kimoja au zaidi kwa ajili ya kujenga mwili na huduma za wengine. Hizi ni rasilimali ambazo ni za thamani sana – Zawadi za Krismasi alizotupa Mungu – zikisubiri kufunguliwa na kufurahiwa." (Churches Alive 1996: 6.2)[28] Mike Breen anaielezea namna hii: "Hatuna tatizo la 'kimisheni' au tatizo la kiuongozi katika kanisa la Magharibi. Tuna tatizo la kuwafanya watu kuwa wanafunzi. Kama unajua namna ya kuwafanya watu kuwa wanafunzi kwa usahihi, utapata misheni wakati wote. Wakati wote. . . . Kama unajua namna ya kufanya wanafunzi, utawafikia watu wasiomjua Yesu. Kwa sababu hicho ndicho wanafunzi wanachokifanya. Huo ndio ulikuwa mpango mzima wa Yesu. Kama unafanya watu kuwa wanafunzi, wakati watu hawa wanafanya umisheni wanapokua na kwenda kila siku, pamoja na kazi ya Roho ya kuwafinyanga hali ya wakati ujao ya kanisa itajionyesha. . . . Kila mwanafunzi hufanya wanafunzi. Huwezi kuwa mwanafunzi kama huko tayari kuwekeza katika kuwafanya wengine kuwa wanafunzi. Kimsingi huo ndio wito wa Agizo Kuu." (Breen 2011: 12, 39) Matokeo yake ni kubadilishwa: "Matendo ya huduma na urejesho tunayoyafanya [ni] Baraka kwa wengine na picha ya urejesho ambao Mungu anaufanya. Lakini hatimaya familia, majirani, biashara, miji au mataifa hurejezwa wakati Yesu akiokoa na kurejeza watu waliomo ndani yake. Kwa hiyo kama wanafunzi wa Yesu misheni yetu ni kuwafanya wengine zaidi kuwa wanafunzi ili na wao wafanye wanafunzi zaidi. Kwa kufanya hivyo, watu na vitu hurejezwa. Lakini hapa jambo muhimu ni hili–kwa kiwango kikubwa dunia itajaa...Yesu!" (Kalinowski na McBee 2013: 17)

1. <u>Ukristo ni dini ya "nenda kawambie". Waaminio wote wameitwa kuwa mashahidi kwa ajili ya Kristo.</u>
   a. *Wajibu wa kuwa mashahidi hauko mabegani mwa wale tu wenye ofisi au karama maalum ya uinjilisti.* Ndio maana, katika **Efeso 4:11-16,** wale ambao Mungu amewaita kuwa 'wainjilisti,' wanapaswa kutumia kipawa chao na wito wao *"kuwaandaa watakatifu"* ili kwamba, na wao, wawe mashsahidi wazuri.
   b. *Kanisa limeagizwa "kutuma" watu kwenda kutangaza habari njema na kuwafanya watu kuwa wanafunzi (**Rum 10:14-15**).* Hivyo, pesa ya kuwezesha mahitaji ya kuwafikia wengine wahitajika kuwa sehemu ya bajeti ya kanisa.
2. <u>Kanisa limeitwa kufanya "wanafunzi," si tu "walioongoka" (**Math 28:18-20**).</u>
   a. *Mwanafunzi ni mtu anayejifunza, mtu aliyeamua kuwa na mwalimu au bwana (katika mazingira haya, kuwa na Yesu), ili kuwa kama mwalimu au bwana.* Mwanafunzi anachukuwa asili na tabia ya bwana au mwalimu, na anafanya kama bwana au mwalimu anavyofanya (ona Willard 1997: 282-310).
   b. *Ukweli kwamba tunatakiwa kuwafanya wengine kuwa wanafunzi, na sio tu waongofu, katika mataifa yote huonyesha kwamba "Agizo Kuu" linahusu kitu kikubwa zaidi sana kuliko uinjilisti.* Kuongoka ni mwanzo tu wa maisha yakuendelea ya uanafunzi. Kufanya wanafunzi ni kitu kamili. Kufanya wanafunzi kunahusisha utakaso wa watu, si tu ile hali yao ya kuhesabiwa haki.

---

kwenda miisho ya dunia kuhubiri Injili (Marko 16:15), wala kubatiza waongofu wengi katika jina la Utatu wa Mungu, wala kuwafundisha kanuni za Kristo, lakini 'kufanya wanafunzi'—kujenga watu wawe kama wao ambao walilazimishwa na agizo la Kristo kiasi kwamba si tu walifuata, bali pia waliwaongoza wengine kuifuata njia Yake. Ni mpaka pale walipofanya wanafunzi ndipo na shughuli zinginezo zinazohusu lile agizo ziliweza kufanyika ili kutimiza kusudi. . . . Kitu kilicho muhimu katika mwisho wa uendelezaji wa kazi yetu ni uaminifu ambao wanafunzi wetu huondoka nao na wao kuendeleza ule wito wakufanya wanafunzi na viongozi kutokana na wanafunzi wao, na si tu kuwa na wafuasi zaidi." (Coleman 1964: 108-10)

[28] Churches Alive huongezea tahadhari hii kuhusiana na karama za rohoni: "Utambulisho wa karama, ingawaje unaweza kuwa wa msaada sana, ni lazima wakati wote tuzingatie uwezo wa Roho Mtakatifu kuwatia nguvu wanafunzi kwa karama nyinginezo, na kuondoa karama ambazo hazitumiki tena" (Churches Alive 1996: 6.2).

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

Kufanya wanafunzi kunahusisha maisha yote ya mtu. Hivyo, Agizo Kuu linahusisha maisha yote ya watu

3. Agizo la Kristo la kufanya "wanafunzi" linahusisha pia "kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi." Kuna maana mbili katika hili kuhusiana na kanisa la mahali pamoja:

a. *Wale ambao ni viongozi wa kanisa wanahitajika wawe walimu wazuri wa injili na wanatakiwa wawe vielelezo wao wenyewe.* Washirika wa kanisa wanatakiwa wawe na uelewa ulio wazi kuhusu maana ya Ukristo, misingi ya imani ni nini, na namna Wakristo wanavyotakiwa kuishi. Ndio maana moja ya sifa za kuwa kiongozi kanisani ni pamoja na *"kuwa na uwezo wa kufundisha"* (**1 Tim 3:2; 2 Tim 2:24**). Kuhusiana na namna mbali mbali za kufundisha na kushawishi, tabia na [*maadili*] ya mtu huwa na nguvu kubwa sana" (Cooper 1932: 9). Hivyo, tena, kufanya wanafunzi ni kitu kamili; inahusisha maisha yote ya mtu.

b. *Kanisa la mahali pamoja linapaswa kuwaka utaratibu uliopangiliwa wa "kuwafanya watu kuwa wanafunzi" waamini wapya—kuwazamisha katika imani na kuweka kina cha ufahamu wao.* Badala tu ya kuridhika kuwa na waamini wapya na kuwabatiza na kuwafanya kuhudhuria ibada za Jumapili, inabidi yawepo "madarasa ya kufanya wanafunzi." Kupanga watu waliomo kanisani katika vikundi vidogo vidogo vinavyokutana mara kwa mara kwa ajili ya maombi, Kujifunza Biblia, na ushirika ni njia mojawapo nzuri kwa Wakristo kukuwa katika imani yao na katika kujitoa kwao kwa wengine na kanisa.

4. Sehemu mojawapo ya kutekeleza "Agizo Kuu" ni kuanzisha makanisa mapya ya mahali pamoja. Kanisa si tu ushirika wa waaminio ndani ya Kristo duniani lakini pia lina ushirika wa mahali pamoja. Mfumo ambao umeandikwa katika kitabu cha **Matendo** ni kwamba waamini walihubiri injili katika sehemu mbali mbali; wakawafanya waamini wapya kuwa wanafunzi, na kuwajenga katika imani; na kisha wakaanzisha makanisa ya mahali pamoja (ona **Matendo 14:21-23**).

***C. Kanisa limeitwa ili kuwa ushuhuda wa Kristo kwa kuwa mfano na kuwahudumia wengine kwa kutenda mema duniani***

1. Tunachofanya kwa vitendo huzungumza kwa ufasaha kuliko tunachosema na kudhihirisha kweli ya kile tunachoamini. Katika **Math 5:13-16** Yesu alituambia kwamba tunapaswa kuwa mfano kwa yale tutendayo tunapaswa kuwa mfano wa upendo wake duniani: "[13]*Ninyi ni chumvi ya dunia; lakini chumvi ikiwa imeharibika itatiwa nini hata ikolee? Haifai tena kabisa, ila kutupwa nje na kukanyagwa na watu.* [14]*Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima.* [15]*Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango; nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani.* [16]*Vivyo hivyo nuru yenu iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yetu aliye mbinguni."*

Kila mwanadamu ameumbwa kwa "mfano wa Mungu" (**Mwz 1:26-27; 5:1-3; 9:6; Efeso 4:24; Kol 3:10; Yak 3:9**), namna tunavyoutendea mfano wa Mungu huonyesha kile hasa tunachofikiri kuhusu yeye. Kueleza hilo kwa namna nyingine: "Matendo huthibitisha ulivyo." Hivyo, mtume Yohana anakataa kabisa kwamba "*utu* wa rohoni" unaweza kutenganishwa na *matendo* ya mwili. Kwa kweli, Yohana, anasisitiza kwamba inabidi utu wa rohoni uthibitishwe na matendo ya mwilini, vinginevyo utu wa rohoni si halisi. Hicho ndicho tilichokiona katika 1 Yohana 3:7: 'Watoto wadogo, mtu na asiwadanganye; atendaye haki yuna haki, kama yeye alivyo na haki.' Wadanganyifu walikuwa wakisema: Unaweza *kuwa* mwenye haki na bado *usifanye* matendo ya haki. Yohana anasema: Watu *walio* na haki ni wale *watendao* haki. Kutenda kunathibitisha kuwa." (Piper 2009: 146-47) Hili linaonekana mara nyingi katika Biblia yote:

- Namna *tunavyofanya* kile anachotuagiza Mungu ni muhimu sana kuliko taratibu zetu za kuabudu katika dini zetu (**1 Sam 15:22-23; Zab 51:14-17; Isa 29:13-16; Yer 6:16-20; 7:21-23; Hos 6:6; Rum 12:1; Kol 3:23-24; Tito 1:16; 1 Yoh 5:3; 2 Yoh 6; Ufu 19:7-8**).
- Kufanya kwetu kile ambacho Yesu ametuagiza ni ishara kwamba tunampenda kiukweli (**Yoh 14:15, 21, 23; 15:9-10**);
- Ishara ya msingi ya utii na uaminifu kwa Mungu ni *namna* tunavyowatendea watu (**Mith 14:31; 19:17; 21:3; Mika 6:6-8; Math 25:34-40; Marko 12:28-34; Yoh 13:34-35; Yak 1:27; 2:18-26; 1 Pet 3:7; 1 Yoh 2:10; 14, 18-19, 23; 4:7, 11-12, 21**).
- Vivyo hivyo, ishara ya ukosefu wa uaminifu na utii kwa Mungu ni *namna* tunavyowatendea watu (**Mith 14:31; Isa 1:10-17; Ezek 16:48-50; Math 12:1-8; 15:3-9; 23:23; 25:41-46; Yak 2:14-17; 1 Yoh 2:9; 3:10, 15, 17; 4:8, 20**).

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

2. Mifano ya Yesu ya "chumvi" na "nuru" katika **Math 5:13-16** inaonyesha kuwa kanisa linapaswa kuhusika na maisha yote kwa ujmla wake, si tu kufungwa na swala la "kuhubiri na kusifu" siku za Jumapili.

a. *Chumvi hufanya kazi ya kuhifadhi.* Kanisa linapaswa kufanya kazi kama linalohifadhi dhidi ya momonyoko wa maadili maswala ya kiroho. Chumvi pia huweka ladha; kanisa linapaswa kutoa ladha ya uzima wa milele na mfano wa ladha ya mbinguni katika dunia hii yenye magumu. Sababu hizi zote, "Wakristo" watalazimika 'kusuguana' na utamaduni [kama, katika siku za maisha ya Yesu duniani chumvi ilisuguliwa katika nyama ili kuihifadhi na kuipa ladha,] na kupenya katika kila Nyanja ya maisha na kuweka ladha katika jamii ambamo tunaishi. (Lakini maneno mawili ya tahadhari: Mara kwa mara Wakristo wanasongwa na shughuli za kujenga taasisi zinazoonekana—majengo, vituo vya kufanya maombi ya kujitenga na mahali pa ushirika—hapo tuko hatarini kuwa nguzo za chumvi. Swala la msingi si dunia kuona jinsi taasisi zetu zilivyo tukufu; lakini dunia ihisi uwepo wetu kati yao. Na pili, lazima tuwe makini tusipoteze ladha yetu kama chumvi. Ili kuweza kuhifadhi, ni muhimu kwa chumvi kutunza ubora wake na tabia yake kama ilivyo [**Marko 9:50**].)" (Colson 1992: 366)

b. *Nuru ni ya kuonekana.* Kanisa linapaswa kuishi na kuenenda kwa namna ambayo itawezesha watu kuona injili na maisha mapya ya upendo, rehema, Amani, haki, na kweli ambavyo hupatikana kwa Yesu. Nuru pia huwapa watu joto; hutoa nje giza; huleta ufasaha wa mambo; husababisha kukua; husababisha watu kuiona njia yao; husababisha watu wanaotaka kufanya mambo mabaya au ya aibu kujificha; huleta furaha. Kanisa linatakiwa kufanya mambo haya yote wazi wazi ili watu wayaone. "Jambo la msingi kuhusu nuru ni kwamba mng'ao wake unaweza kuonekana vizuri katika giza nene. Ni vigumu kuona mshumaa ndani ya chumba chenye mwanga mkali, Lakini washa hata kijiti kimoja cha kibiriti ndani ya chumba chenye giza, na kila jicho litavutwa nacho." (Colson 1992: 352-53)

3. Katika maandiko wakati wote tunaona kwamba kuna uhusiano uliowazi wa kati ya yale tusemayo, jinsi tunavyotenda, na kile tunachoamini. Uhusiano huu unaonekana wazi katika **Efeso 2:8-10**: **Efeso 2:8-9** inabainisha kwamba wokovu wetu si matokeo ya matendo yetu bali ni neema ya Mungu tu kupitia imani yetu; hata hivyo, **Efeso 2:10** inaendelea kusema kwamba, ingawaje wokovu wetu si matokeo ya matendo yetu lakini ni matokeo ya *kazi ya Mungu*, kusudi au lengo la wokovu wetu ni kwamba tunaokolewa *ili* tutende matendo mema: *"Maana tu kazi yake tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema,ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo."* Kwa maneno mengine, Mungu amefanya kazi yote, ametufanya kazi yake, na kama sehemu ya kazi ya kuokoa ametenda kazi ndani yetu, alishaandaa matendo mema kwa ajili yetu ili sisi tuyetende na ametuwezesha kuyafanya. Kwa hiyo, mtu hawezi kutenganisha imani na matendo, kuamini na kutenda. Misheni ni matokeo yanayoonekana nje kama ishara inayodhihirisha hali yetu ya ndani ya imani na kiroho.

a. *Yesu alijali hali za kimwili za watu kama alivyojali hali zao za kiroho.* Hivyo, aliwalisha wenye njaa na kuponya wagonjwa. Kwa hakika ilikuwa kupitia huduma ya Yesu katika ulimwengu wa mwili alidhihirisha mamlaka yake katika ulimwengu wa roho (ona **Math 8:5-13; 9:1-8; 11:2-6; Marko 2:1-12; Luka 5:17-26; 7:1-10, 18-23**). Kwa sababu tuna *"tanafananishwa kwa mfano wa [Kristo]"* (**Rum 8:29**), zaidi na zaidi tutaendeleza mtazamo huo na kufanya kama yeye alivyofanya.

b. *Ni lazima kanisa liuonyesha upendo wa Kristo, kuwahurumia maskini, kuwasaidia wahitaji na walio katika shida, nk., ikiwa litatekeleza wajibu wake wa kuwafikia wengine na injili na kuwahudumia wengine (ona **Math 5:38-48; Luka 10:25-37; Rum 12:9-21; 15:1-3; 2 Kor 8:21; Gal 6:9-10; Kol 4:5; Tito 2:7-8; Yak 1:27; 1 Pet 2:12**).* Kwa hakika, ikiwa tunachodai tunaamini hakiambatani na matendo mema, hapo imani yetu "imekufa" (**Yak 2:14-26**).

c. *Kuwabariki watu kimwili na kuhudumia katika mahitaji yao hufungua milango ya injili na ya huduma za mahitaji ya kiroho ya watu.* "Tendo la kuwabariki watu hupekelea wao kutaka kujua kitu kinachoendelea 'Kwa nini mnafanya haya?' Swali kama hili linapoulizwa huleta furaha kwake yule aliyejiandaa kuulizwa swali hili. 'Mimi ni mfuasi wa Yesu, na ninawabariki kwa sababu hicho ndicho alichokuja kufanya.' Jibu hili hufungua mlango wa kufanya mazungumzo ya kiroho." (McNeal 2009: 32-33) Jambo hili limethibitishwa kihistoria. Mwanahistoria Rodney Stark anaonyesha kwamba katika karne za awali za kanisa "wapagani wengi walivutwa kwenye imani ya Kikristo kwa sababu kanisa lilitenda matendo dhahiri ya kuwabariki wafuasi wake (sio tu 'kiroho'). Lililo kubwa miongoni mwa misaada hii ya mwilini ni kwamba, katika ulimwengu ambao ulikuwa hauna huduma za jamii kabisa, Wakristo ndio waliokuwa wategemeza ndugu.

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

> Mwishoni mwa karne ya pili, Tertullian aliandika kwamba, wakati mahekalu ya wapagani yalipokuwa yakitumia michango yao kwenye 'sherehe za anasa na ulevi,' Wakristo walitumia michango yao 'kusaidia na kuzika watu maskini, kuwapatia mahitaji vijana wa kiume na kike walio maskini na wazazi na wazee wasiona uwezo wa kutoka katika makazi yao.' Vivyo hivyo, katika barua kwa askofu Antioch mwaka 251, askofu wa Roma alisema 'zaidi ya mara 1,500 ya kwamba wajane na wenye shida katika kanisa lake walikuwa wakihudumiwa na kanisa lake. Madai haya kuhusiana na upendo wa Kikristo yalithibitishwa na wapagani walioona." (Stark 1998: n.p.)

4. <u>Kile tunachofanya katika maisha haya—hasa hasa jinsi tunavyowatendea watu—ndicho kitakacho kuwa kipimo ambacho kwacho tutahukumiwa katika hukumu ya mwisho.</u> Hatuwezi kutendea kazi wokovu wetu bali tumeokolewa kwa neema kwa imani ya Mungu ndani ya Kristo (**Yoh 3:16-18; 6:28-29; Rum 2:16-17; 10:8-13; Efeso 2:8-9; Gal 3:1-14**). Hata hivyo, "Matendo mema ni ishara ya hali ya kiroho ya moyo wa mtu. Hatuambiwi kama vitabu hivi [katika **Ufu 20:11-15**] vina matendo mazuri au mabaya. Hata hivyo hukumu haikuwa kupima uwiano wa uzito kati ya mema na mabaya. Badala yake, matendo yanaonekana kama ushahidi usiopingika wa uaminifu wa moyo; yenadhihirisha kuamini au kutokuamini, uaminifu au kukosa uaminifu. Hukumu itadhihirisha ikiwa uaminifu wa watu umekuwa kwa Mungu na mwana Kondoo wa Mungu au kwa maadui wa Mungu." (Ngundu 2006: 1576) Kama mtume Yakobo anavyosema, *"Lakini mtu atasema, wewe unayo imani, nami ninayo matendo. Nionyeshe imani yako pasipo matendo, nami nitakuonyesha imani yangu kwa njia ya matendo yangu. . . . Maana kama vile mwili pasipo roho umekufa, vivyo hivyo imani pasipo matendo imekufa."* (**Yak 2:18, 26**) Kwa hiyo, kama vile kile tunachofanya—hasa hasa namna tunavyowatendea watu—ni kipimo katika maisha haya kinachothibitisha jinsi sisi tunavyomfikiria Mungu, kipimo hicho hicho kinaonekana katika muktadha wa hukumu ya mwisho. Hili linaonekana mara nyingi na kwa njia nyingi katika Biblia yote.

- Kwa mwongozo na mfano Mungu huhukumu watu na mataifa na kuwalipa "kulingana na matendo yao [au "njia" au "matendo"]" (**Waamuzi 1:6-7; 9:22-24, 56-57; 2 Sam 12:9-12; 1 Waf 2:32-33; 1 Waf 20:35-42; 1 Waf 21:17-19; 2 Nyak 6:23, 30; Ayubu 34:11; Zab 18:24; 31:23; 62:12; Mith 24:12; Mhu 12:13-14; Isa 59:18; Yer 17:10; 25:14; 32:19; Ezek 7:3, 8-9, 20, 23-24, 27; 9:10; 11:21; 16:43, 59; 18:30; 22:31; 24:14; 33:20; 35:6, 11, 15; 39:24; Hos 12:2; Yoeli 3:5-7; Obad 15; Zek 1:6; Math 16:27; 25:14-30; Luka 12:47-48; Yoh 5:28-29; Rum 2:1-6; 12:19; 1 Kor 3:8, 11-15; 2 Kor 5:10; 11:15; Gal 6:7-8; Efeso 6:8; Kol 3:25; 2 Tim 4:14; Ebr 10:26-27; 1 Pet 1:17; 2 Pet 2:20-22; Yuda 14-15; Ufu 2:23; 14:13; 20:11-13; 22:12**).
- Hukumu ya mwisho ya "matendo" yetu ni pamoja na maneno yetu (**Math 5:21-22; 12:36-37; Luka 12:2-3; Yuda 14-16**), pamoja na matendo ya sirini na "matendo yaliyofichika" ya mawazo, ufahamu, moyo, makusudio na vichocheo (**1 Sam 16:7; 1 Nyak 28:10; 29:17; 2 Nyak 6:30; Mith 21:2; Isa 29:13-14; Yer 17:10; Math 5:21-22; 6:4, 6, 18; 10:26; Marko 4:21; Luka 2:34-35; 12:2; Rum 2:16; 1 Kor 4:5; Ebr 4:12; Ufu 2:23**).
- Namna tunavyowatendea watu katika maisha haya ndilo litakuwa jambo la msingi katika hukumu yetu ya mwisho, kwa ajili ya thawabu na adhabu, kwa kuwa hilo hudhihirisha hali halisi ya mioyo yetu na uhusiano wetu halisi na Yesu (**Math 6:1-4, 12, 14; 10:42; 24:45-51; 25:31-46; Marko 9:41-42; Luka 6:35; 12:33, 41-48; 14:13-14; 16:1-9; Rum 2:1-6; 1 Tim 6:18-19; 2 Tim 4:14; Ebr 6:10; 1 Pet 5:1-4**).

## IX. <u>Vipengele Bayana Vya Misheni Nzuri</u>

### A. *Ili kuwa la kimisheni zaidi, kanisa linahitaji kubadili mtazamo wake*

1. <u>Katika kiini cha misheni ya kanisa ndipo penye swali kuu la kiroho: Mungu anataka nini kwa ajili yetu?</u> Kanisa lolote lazima kwanza "liulize swali la kiroho: 'Mungu anataka nini kwa ajili ya kanisa letu? Ni nini kilichoko moyoni mwake?' Hilo linapaswa kuibua swala la kimkakati: 'Angetaka tumfanyie nini, kama mtu mmoja mmoja na kama mwili?' Ndipo hapo unapoweza kuuliza: 'Ni kwa namna gani tutapangilia huduma yetu ili iweza kutekeleza mikakati hiyo?'" (Minatrea 2004: xviii)[29]

---

[29] Hili linaweza kuchukua muda na litahitaji mchakato. Edward Setzer aliombwa kuchunga kanisa la watu 35, ambalo wastani wa umri wa watu ulikuwa miaka 68. Kanisa lilikuwa likipungua na jamii ilikuwa imebadilika kwa kiwango kikubwa tangu kanisa lile kuanzishwa miaka ya nyuma. Hata hivyo, mwenyekiti wa baraza la uongozi alisema, "Tutafanya kila tuwezacho kuifikia jamii" (Setzer and Putman 2006: 41). Setzer anaripoti, "Tuliendelea kuomba na kumtafuta Mungu

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

Kwa maneno mengine, mtazamo wa msingi ni wa kiroho; ni kumjua Mungu na mapenzi yake kwa ajili ya kanisa *hili* na kwa watu *hawa* katika eneo *hili* katika mazingira *haya* tukiwa na mahitaji *haya* na rasilimali *hizi*.[30] Hili husababisha tuyaonae mazingira halisi tuliyonayo na mahitaji ya watu katika kijiji hiki, jamii, au eneo na kutambua kwamba *mambo hayapaswi kuwa hivi*. Hilo, kwa upande mwingine, hutupeleka kwenye swali: Ni kitu gani tunachoweza kufanya pamoja kama kundi ambacho hatuwezi kufanya mmoja mmoja? Hakika, tunapaswa kuuliza: Tungeweza kufanya nini endapo kanisa letu litaungana na kanisa jingine lenye nia kama ya kwetu ambacho hatungeweza kukifanya peke yetu?

Kwa kuwa Mungu anasema na kutenda kupitia mwili wake, kanisa, njia mojawapo ya kutambua mapenzi ya Mungu kwa ajili ya kanisa lako ni viongozi wa kanisa kuwajua watu wao vizuri—matumaini yao, ndoto zao, shauku zao, mahitaji yao, vipawa vyao, na uwezo wao. Kanisa moja lilianza safari yake ya kuwa la kimisheni zaidi na kuwa na agenda ya "kuendeleza watu" kwa viongozi kufanya mazungumzo ya binafsi na washirika wake. Mazungumzo haya yalihusisha pia seti tano za maswali ya msingi (ona McNeal 2009: 124-26):

- Ni nini unachofurahia kukifanya? Kile wanachofurahia watu kinaweza kuwa ndio namna ambayo Mungu anataka kuwabariki watu wengine kupitia wao.
- Ni katika eneo gani unamuona Mungu akitenda kazi sasa? Mungu yuko kazini wakati wote na katika maeneo yote. Swali hili linawasaidia watu kumonaMungu kwa watoto wao, kwa jirani, kazini, nk.
- Ni kitu gani ungependa kumwona Mungu akifanya katika maisha yako katika miezi 6-12 ijayo? Tukusaidieje? Hili huenda kwenye eneo la maendeleo ya binafsi na huwasaidia watu kuona kwamba *wao* na sio idadi, majengo, na pesa kuwa ndicho kipimo cha kanisa na mafanikio. Swali hili huwawezesha viongozi kuwaelekeza watu kwenye vyanzo nje ya kanisa na kujua aina ipi ya fursa ya maendeleo wanatakiwa kuiwekea mipango.
- Ungependa kuwahudumia watu wengine kwa namna gani? Tukusaidiaje? Watu wengi hukua kwa njia ya kuwahudumia wengine. Zaidi ya hayo, hiki ndicho kipimo cha namna Roho anavyoliita kanisa kuendea jamii (endapo utakuwa na watu mbali mbali ambao wanataka kufundisha watoto katika shule, au kuhudumia yatima, au watu wanaoishi na VVU, hiyo ni ishara inayokuelekeza kwamba ni mkondo upi utaufuata katika kuingia ndani ya jamii). Hii pia inaonyesha ni mafunzo gani watu wapate ili wawe wahudumu bora.
- Tukuombeeje? Hii inaonyesha kwamba viongozi kwa kweli wanajali kuhusu maslahi ya watu wao. Vikundi vya maombi vinaweza kuanzia hapo pia.

Kumjua Mungu na moyo wake, kuyatafiti mazingira yetu, na kuuliza maswali hutupeleka mwenye *maono*. **Mith 29:18** (KJV) inasema, *"Pasipo maono, watu huacha kujizuia."* Maono huongoza kwenye mipango iliyo bayana, mikakati, programu, na mifumo ambayo hupelekea kwenye mabadiliko.

- Kwa mfano, William Carey, ambaye anajulikana kama "baba wa umishenari wa kizazi cha sasa," alitumia miaka 41 kule India ambako alitafsiri Biblia katika lugha kuu, alijenga mashule na kufanya kazi kwa ajili ya kuleta mabadiliko muhimu ya kijamii ("William Carey" 2007: n.p.). Kile alichofanya kilitokana na kumjua Mungu na mpango wa Mungu kwa ajili ya maisha yake, akielewa mazingira yake, na kuona jinsi vitu *vitakuwa*: "Mahali ambapo Carey aliona nyika iliyokuwa tasa, hakurudi nyuma na kuanza kuomboleza, lakini alianza kupanga misitu, Alijifunza mambo ya miti,

na kuomba atuguse kwa muda wa miezi sita. Katika kipindi hicho cha maombi, Mungu akaanza kutubadilisha sisi kama mwili. Tukafanya mabadiliko makubwa katika maisha ya kanisa, lakini kanisa lilifanya hayo maamuzi." (Ibid.) Kanisa likaamua Jumapili ya Pasaka itakuwa ni siku ya kuwafikia wengine. Washirika wakawakaribisha watoto, wajukuu, majirani, na marafiki. Zaidi ya watu 200 walifika, na miaka miwili iliyofuata kanisa lilikua kufikia idadi ya zaidi ya washirika 200 kwa wastani wa mahudhurio. Setzer anahitimisha kwamba wito wa lile kanisa ulikuwa kwa jamii ile bila shaka. Kanisa lilipogundua kwamba jamii yao imebadilika, "walianza kuwafikia tena, na injili ikaanza kuota mizizi. Kanisa lilibadilishwa na maisha yao yalibadilishwa kwa sababu hiyo." (Ibid.: 42) Tunaweza kutarajia Mungu abadilishe makanisa yetu, pia, tutakapoutafuta moyo wake kwa kumaanisha na kuwafikia majirani zetu na jamii.

[30] Ni muhimu kutambua kwamba kilichofanikiwa katika jamii moja huenda kisifanikiwe katika jamii nyingine. Kila jamii ni *ya kipekee* hivyo uwanja wake wa kuifikia una matakwa yake binafsi, mahitaji, na matatizo, maswala, mazingira, historia, utamaduni, nk. Ingawaje injili haibadiliki, namna tunavyowafikia watu na jinsi tunavyoiwasilisha injili (ikiwa ni pamoja na jinsi tunavyoabudu) yaweza kuwa tofauti kutegemeana na jamii husika tunayojaribu kuifikia. Ndio maana Setzer na Putman wanakazia kwamba ufanikiwaji wa misheni huanza na wito kutoka kwa Mungu. Hata hivyo, kuitikia wito huo, ni lazima tu "ijaribu jamii," chunguza njia ambazo Mungu anafanyakazi katika jamii kama hizo, tafuta maono ya kipekee kwa ajili ya kanisa lako na rekebisha maono hayo kwa kadiri muktadha wa mazingira unavyobadilika, kama ilivyojadiliwa katika kanisa la Setzer hapo juu katika 29 (ona Setzer na Putman 2006: 21-28).

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

akaipanda, na kisha akafundisha mambo ya misitu. Alipoona magugu aliwaza bustani, akazilima, akaandika vitabu, na kanzisha majukwaa kama vile Agri-Horticultural Society of India ili kupata msaada udumuo kwenye majukumu haya." (Mangalwadi 1999: 115)

- Vivyo hivyo, Israeli ya leo ina msitu kati kati ya mahali ambapo palikuwa jangwa. "Yalikuwepo maono ya aina mbili kwa ajili ya ardhi. . . . Waisraeli, wakimwabudu Yehova, walimwamini Mungu aliposema kwamba hii ni nchi inayotiririka maziwa na asali. Wapalestina waliamini kwamba Allah ameilaani nchi ile. Hapo una watu wawili tofauti wakiwa na maono mawili tofauti kwa ajili ya nchi moja." (Miller 1998: 116) Maono tofauti huleta matokeo tofauti.
- Kwa upande mwingine, nchi ambazo hazijafikiwa na injili ndizo ambazo ziko miongoni mwa zile zenye uhitaji mkubwa. Huu si ulinganifu wa hivi hivi. . . . Kwa hiyo kwa nini watu ni maskini wa vitu na wenye njaa? Ispokuwa kwa majanga kama ya vita, ukame, au mafuriko, umaskini wa vitu hautokei hivi hivi.' Ni matokeo ya kimantiki ya namna watu wanavyojiona na dunia inayowazunguka. . . . Umaskini wa vitu una misingi katika mtazamo wa umaskini, mfumo wa fikra ambao umefungamana na kusababisha tabia za aina fulani. . . . Wale wenye mtazamo wa umaskini huionadunia kupitia miwani ya umaskini. Wanasema, au matendo yao yanasema kwa niaba yao, 'Mimi ni maskini. Nitaendelea kuwa maskini, na hakuna ninachoweza kufanya ili kubadili hali hii' (imani kwamba kilichopangwa kimapangwa huwezi kukigeuza). Au, kama wengi wanavyosema leo, 'Mimi ni maskini kwa sababu wengine wamenifanya niwe maskini. Itabidi watatue matatizo yangu. Mimi mwenyewe siwezi.' . . . Kwa kawaida misingi ya tatizo hili ni ule mtazamo ambao hurudisha nyuma au hupinga maendeleo, ukiwafunga watu katika umaskini." (Miller 1998: 65-67)
- Huu "mtazamo wa umaskini" unaonekana katika ukweli kwamba katika maeneo mengi ya Afrika (na kwingineko) mafurushi makubwa ya uchafu, mifuko ya plastiki, na uchafu mwingine unaweza kuviona vimeachwa vikizagaa katika maeneo ambayo watu wanaishi. Hii haipendezi na inaonyesha kukosa kujiheshimu na kuiheshimu thamani ya maisha. Majaa ya mataka ndipo yalipo mazalia ya mbu ambao hueneza malaria, nzi, wadudu waharibifu na vimelea vingine vya magonjwa. Femi Adeleye anaielezea tabia isiyo ya kibiblia inayosababisha hali kama hii: "Naifahamu Nyumba ya Wageni ya Kikristo katika moja ya nchi zetu za [Afrika] ambayo imezungukwa na uchafu mwingi. Nilionajinsi watu ndani ya hiyo nyumba na wengine barabarani walivyokuwa wakiendelea kutupa uchafu zaidi katika lundo liloendelea kukua na kutoa uvundo. Harufu ilikuwa mbaya mno kiasi iliingia kupitia madirishani mpaka kwenye vyumba vya ile nyumba. Niliamua kuuliza kwamba ni wajibu wa nani kuondoa uchafu ule. Nikaambiwa 'ni kazi ya serikali lakini hawajakuja kwa muda mrefu'. Niliona maeneo yanoyonizunguka nikaona kuwa kuna malundo mengi ya uchafu katika bara bara, mengine karibu kabisa na milango. Ilionyesha kuwa wananchi wengi walikuwa wakingojea serrikali ije kuondoa ule uchafu. . . . Tabia ya jinsi hii inachochewa na hali ya watu kuwa na mitazamo yenye kutofautisha kati ya vilivyo vitakatifu na ambavyo ni vya kawaida au kati ya vile tunavyoviona kuwa ni vya kiroho na vya kimwili. Tunachukulia kuondoa uchafu, kuyatengeneza mazingira na kutunza mali za serrikali ni majukumu 'ya kidunia', kwa hiyo hatujali. Tunayatoa maisha yetu kwa vitu ambavyo tunaona ni vitakatifu au vya rohoni. . . . Tunatakiwa turudi kwenye mtazamo wa Biblia. Katika mtazamo wa Biblia vyote vinavyohusu maisha ni vitakatifu." (Adeleye 1999: 127) Kanisa lingeweza kutekeleza umisheni wenye faida kwa kuelimisha watu kuhusiana na mazingira na kwa kusafisha vijiji na kuondoa malundo ya takataka na uchafu. Wakifanya vitu hivi, makanisa yatakuwa yanawaambia watu: "Afya zenu, maisha, na ubora wa maisha yenu ni vitu vya thamani kwetu. Ninyi ni wa muhimu mno hamwezi kuishi katika jalala. Tunawajali, na thamani ya maisha ya kijiji hiki." Serikali ya Rwanda kisheria imesababisha badiliko kubwa katika swala hili. Inawataka watu kufanya usafi katika maeneo yao mara kwa mara. Matokeo yake, Rwanda ni nchi safi kwa kiwango kikubwa kuliko nchi nyinginezo za Afrika ya Mashariki. Wakristo hawapaswi kuitegemea serikali iweke sheria kuhusiana na kitu ambacho tunaweza kufanya na ambacho twapaswa kufanya wenyewe.
- Vivyo hivyo, "[Katika kijiji kimojawapo huko Tanzania] mti mmoja ulikua, mwembe wenye refu wa kawaida lakini wenye matawi mengi. Palikuwa na mduara wa kivuli chini yake. Ndani ya huo mduara walikuwepo watu thelathini, wakibanana ili kila mtu awe chini ya kivuli, wakitazamwa na mbuzi aliyefungwa Kamba na asiye na furaha akiwa juani. Kile ambacho kilionekana kama mchezo wa kundi lile ilikuwa Dhahiri kwamba hiyo ndiyo iliyokuwa kawaida ya kimbilio la kila mchana wakati wa jua. Kilichonifurahisha mimi zaidi ni kuhusiana na kundi hili la wanakijiji chini ya mti huu mmoja ni swala kwamba hakuna hata mmoja miongoni mwao ambaye alipata wazo la kupanda miti ya miembe zaidi kwa ajili ya kupata kivuli katika eneo hili lenye joto. Ilikuwa ni kitu

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

rahisi zaidi kupanda mti—mwembe huu peke yake uliweza kutoa mbegu elfu moja—hata hivyo hakuna hata mmoja aliyepanda moja, au kama kuna aliyefanya hivyo, huo mti ulishakatwa. Muonekano wa hawa Waafrika katika hapa mahali padogo katika nchi ya Tanzania wakiminyana kugombania kivuli ulibaki kwangu kama kielelezo halisi cha kupanga mipango kabla au kukosa kufanya hivyo." (Theroux 2003: 248)

2. Mtazamo wa kanisa kuhusiana na nini maana ya kanisa yabidi ubadilike. Kujua kile ambacho kipo ndani ya moyo wa Mungu kwa ajili ya kanisa lako kutasababisha mabadiliko kadha wa kadha kutoka kwenye vipaumbele na vile ambavyo makanisa mengi huvipa uzito na kwa namna ambavyo makanisa mengi huendeshwa. "Ili kuwa la kimisheni itahitajika kufanya mabadiliko katika maeneo matatu, katika kufikiri kwako, na katika tabia:

- Kutoka kwenye kufokasi ndani kuja nje kuhusiana na fokasi ya huduma
- Kutoka kwenye kuendeleza programu hadi kuendeleza watu katika shughuli zilizo kiini
- Kutoka kwenye mtazamo wa kikanisa hadi mtazamo wa kiufalme katika agenda ya uongozi

Mabadiliko haya ndiyo muhuri wa maana ya sifa za kuwa wa kimisheni." (McNeal 2009: xvi) McNeal anafafanua kile anachomaanisha katika mabadiliko haya matatu, kama ifuatavyo:

- Badiliko la 1: Kutoka kwenye fokasi ya ndani kwenda ya nje. Swala hapa si tu kanisa "kuhusika katika huduma fulani ya jamii." Badala yake, badiliko la fokasi kutoka ndani kwenda nje "huhusisha kubadilisha mtazamo wa kile ambacho hufahamika kuwa ni kanisa, si tu kile ambacho linafanya, ingawaje hilo nalo hubadilika vile vile. Kubadilika na kuwa na fokasi ya nje husukuma kanisa kutoka katika kufanya umisheni kama mradi namba mbili ambao uko umbali wa maili moja na kuwa katika misheni kama mtindo wa maisha. . . . Inaweza kulinganishwa na mabadiliko makubwa ya kifikra ambayo yalitokea ilipogundulika kwamba jua, na sio dunia, lilikuwa ndicho kiini cha mfumo wa sayari angani. . . . Katika mtazamo wa kiufalme na kidunia, lengo la upendo wa Mungu unaokomboa ni kuigusa dunia, si kanisa ('Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda *ulimwengu*,' Yesu alisema; sio 'kwa maana jinsi hii Mungu alilipenda *kanisa*'). . . . Katika mtazamo wa kimisheni, kanisa huhusisha dunia, dunia inampata Yesu, ambaye makao yake ni mitaani au popote ambapo atahitajika ili aunganishwe na watu ambao anawatafuta, ikimaanisha kila mtu. . . . Kinisa lipo kila mahali ambapo wafuasi wa Yesu wapo. Watu *hawaendi* kanisani; wao *ni* kanisa. Hawawaleti watu kanisani; wanalileta kanisa kwa watu." (McNeal 2009: 42, 44-45) Haya yote huwa wazi pale viongozi na washirika wa kanisa watakapopata kuelewa kiundani kwamba "kanisa ni miongoni mwa mashirika machache duniani ambayo yapo si kwa faida ya watu wake" (Setzer na Putman 2006: 44).
- Badiliko la 2: Kutoka katika kuendeleza programu kwenda katika kuendeleza watu. Wakati Reggie McNeal alipokuwa akitumika kama mchungaji mwanzilishi wa kanisa, Mungu alisema naye kwamba, "Je watu wanakuwa na nafuu zaidi wakiwa sehemu ya kanisa, au ndio wanachoka zaidi na kuwa maskini zaidi?" Swali hili lilimsumbua, kwa kuwa aligundua "Sikuwa na njia yoyote ya kufanya watu waendelee kibinafsi; Nilikuwa na njia za kutathmini kujihusisha kwao na utendaji wao kanisani. Nilijua ni mara ngapi walihudhuria katika shughuli za kanisa, lakini sikuwa naelewa kabisa ni mara ngapi waliwahudumia jirani wao. Nilifuatilia mahudhurio ya ibada ya kila wiki, lakini sikuwa naelewa chochote kiuhalisia kwamba ni ndoa ngapi zilikuwa na afya na zilikuwa zikikua. Zaidi ya yote: Niliweza kujua jinsi watu walivyokuwa wakijishughulisha na kanisa lakini sikuweza kujua jinsi maisha yao yalivokuwa yakienda." (McNeal 2009: 89) Tena, "mtindo wa maisha na viwango vya washirika wa kanisa kwa kiwango kikubwa ulifanana na ule wa utamaduni"; kwa hiyo "kujishughulisha na kanisa sio ishara ya uhai wa kiroho" (Ibid.: 93).

Tukio hili la kukabiliwa na Mungu la McNeal lilibadilisha fokasi ya huduma ya kanisa lake. Kanisa likabadili ratiba zake, vipindi na kuyafanya maudhui ya huduma kuwa yenye mlengo wa kuwaendeleza watu zaidi. Badiliko hili ni gumu zaidi kuliko lile la kwanza, na mafaniko kiidadi si rahisi. Ufunguo mmoja ni huu "kuwajenga watu huhitaji kujenga mahusiano, si kutoa bidhaa au huduma" (Ibid.: 90). Hili ni eneo moja ambapo, vikundi vidogo vya kufanya wanafunzi ambavyo vina misingi katika kujenga mahusiano, hukutana na umisheni.

- Badiliko la 3: Kutoka kwenye uongozi wenye mtazamo wa kikanisa kwenda kwenye uongozi wenye mtazamo wa kiufalme. "Badiliko kutoka kulionakanisa kama kiini kwenda kwenye kuuonaufalme kama kiini ndio theolojia na filosofia tegemezi ya hatua ya kutoka kwenye fokasi ya ndani kwenda kwenye fokasi ya nje. . . . [Viongozi wenye mtazamo wa kimisheni] hutafuta namna na njia za kuwaingiza katika matukio ya kimisheni. Wanahakikisha kwamba wanasherehekea juhudi hizo ili kwamba wengine katika kusanyiko nao wapate uzoefu. . . . Wakati ambapo kanisa la

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

kawaida husherehekea mafundisho, mabadiliko ya kimisheni yanatafuta waandishi ambao watatuambia kile ambacho Mungu anakusudia kufanya wakati huu. . . . Viongozi wenye mtazamo wa kimisheni huelewa kile ambacho Mungu anafanya na kisha wao kuwaambia wengine kuhusiana na hicho. Kwa njia hiyo, wao huwa kama waandishi wanaotusaidia na sisi kuelewa pia. Hii ina maana wanatumia muda na Mungu katika maombi, wakimwomba awaoonyeshe kile anachokifanya. . . . Na inamaanisha wanajizamisha wao wenyewe katika maisha. . . . Viongozi wenye mtazamo wa kimisheni, wana mawasiliano na Mungu na wana mawasiliano na dunia, husema kwa ushawishi mkubwa kuhusiana na kile ambacho watu wa Mungu wanapaswa kufanya. Huwezi kuwa katikati ya viongozi wa jinsi hii kwa muda mrefu usipate kuelewa kwamba mioyo yao inafinyagwa kutokana na makabiliano ya na Mungu." (McNeal 2009: 42, 138, 141, 143)

**B.** ***Ili kuwa la kimisheni zaidi, kanisa linahitaji kubadili mtazamo wake wa vigezo vya kile kinachofikiriwa kuwa kanisa "lililofanikiwa"***

Kwa kawaida, makanisa mengi ya mahali pamoja yanachukuliwa kama "mahali pa kwenda" na kama "mtoaji wa bidhaa na huduma za kiroho." "Watu ambao wamepoteza hali yao ya kutumwa hutarajia kanisa lao kuwatekelezea ahadi kutokana na mahitaji yao, kuwahudumia na kuwafanya wajisikie vizuri. . . . Watu ambao wamepoteza hali yao ya kutumwa hupima mafanikio ya wachungaji wao kutokana na vipimo kama vya mauzo ya bidhaa: wateja zaidi, pesa zaidi na, chumba kizuri zaidi cha kuonyeshea bidhaa." (Hammond na Cronshaw 2014: 33) Ili kubadili hali ya namna hiyo ya mtazamo wa kanisa, wachungaji, na hata washirika wenyewe, kipimio kipya kinahitajika. "Kwa kuwa watu huhamasika zaidi kwa kufanya kitu ambacho huwapa tuzo au zawadi fulani, utengenezaji wa kadi za umisheni za kunakili alama za viwango vya utendaji ni muhimu. Kadi hizi zitawaelimisha watu katika upeo mwingine wa kuelewa namna mambo yanavyowezekana, na kusababisha tabia mpya na pia ushiriki mkubwa wa kuitambulisha misheni ya Ukristo." (McNeal 2009: 37-38) McNeal anapendekeza yafuatayo katika kubadilisha vigezo au "kadi za kunakili alama" kwa kile kinachoitwa kanisa lililofanikiwa:

- "Husisha na endeleza majukumu ya huduma za kijamii kama sehemu ya wajibu wa kila jukumu la kiongozi, hasa kwa wafanyakazi. Majukumu haya yazingatie shauku na kipawa cha kiongozi. Ni mpaka washirika wa kanisa watakapoona viongozi wao wamejihusisha na majukumu haya, hawatoamini kwamba fokasi ya nje ni muhimu. . . . Weka ukomo wa idadi ya wafanyakazi wa kanisa na majukumu ya viongozi watakayoyabeba ili wawe na muda wa kufaa kuwa wamisionari. . . . Tenga muda ambao wafanyakazi wa kanisa na viongozi watakuwa pamoja na jamii (ikiwa ni pamoja na mahusiano na viognozi wa jamii) kama sehemu ya upimaji wa utendaji wao. Kwepa mtazamo uliozoeleka na wengi kwamba muda unaotumika katika jamii ni kama tu mambo ya kuongezea. Ikiwa mtazamo huu utaendelea, utahakikisha kwamba mahitaji ya jamii yatapungua ukilinganisha na mahitaji mengine yanayosumbua ya utawala wa kanisa." (McNeal 2009: 75, 78)
- "Sisitiza kwamba kila darasa la shule ya Jumapili, kikundi kidogo, kwaya, na wahuduma wana huduma ya nje. Chaguzi hizi ziinuke kutokana na shauku na mapenzi ya kikundi." (McNeal 2009: 75-76). Kwa sababu hii, Coleman anaonyesha kwamba "haitoshi peke yake kuhusisha watu tu katika kundi la ushirikiano, ambapo kanisa ni mojawapo lakini katika hali kubwa. Ni lazima wapewe namna ya kutendea kazi vitu walivyojifunza. Ni mpaka fursa itolewe ya kutoka namna hii, vinginevyo hili kundi linaweza kubaki kama lilivyo katika hali yake ya kuridhika, na mwishowe kubaki katika hali ya kutoweza kupokea mambo mapya na kuwa jamii inayojipenda yenyewe." (Coleman 1964: 120)
- "Walete viongozi wa jamii kanisani ili wawafundishe viongozi wako kuhusiana na mahitaji ya jamii. Hili linaweza kufanyika wakati wa ibada au semina, na pia kupitia mahojiano yaliyorekodiwa au makongamano ya simu." (McNeal 2009: 76)
- "Uwe na ofisi za wafanyakazi viongozi katika maeneo mengine mbali na kanisani. Hizi zinaweza kuwekwa sehemu za kimkakati kulenga watu wa aina fulani au uwezekana wa huduma fulani. . . . Uwe na wafanyakazi viongozi ambao wako tayari kwa ajili ya mashirika mengine kama sehemu ya jukumu lao. Wafanyakazi wako wana uwezo wa kutumika kama wanasihi, makocha, washauri kwa ajili ya maswala ya miradi midogo midogo ya kimaendeleo, wataalam wa mafunzo ya uongozi na wakufunzi wa aina zote za taaluma za kuendeleza mtu mmoja mmoja na familia." (McNeal 2009: 76)
- "Anza mpango wa kanisa sanjari na kalenda ya jamii" (mfano, ni lini maonesho ya kata, ni lini shule zinafunguliwa na lini zinafungwa), na hakikisha kwamba "matukio ya jamii yamewekwa katika kalenda na sio ya kanisa lako tu" (McNeal 2009: 78). Kwa mtazamo huu, "fuatilia muda unaotumika katika ibada wakati jamii iko kwenye agenda. Hii ni pamoja na muda wa mahubiri, maombi, vipindi vya shuhuda, kufanya mahojiano na viongozi wa jamii," na "wasaidie washirika wa kanisa kuona namna jamii iliyopo

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

inavyohusika, ikiwa ni pamoja na kazi wanayofanya kwa ajili ya kupata kipato, kama fursa ya msingi kwa ajili ya huduma.” (Ibid.: 79)

- “Utamaduni wa kuendeleza watu” ndani ya kanisa utaonekana katika vitu kama: mahusianoa ambayo watu huyajenga kwa makusudi; watu kuachiliwa katika kutumika; uendelezaji wa maisha ya mtu binafsi; pesa kutumika kwa ajili ya watu, jamii, na umisheni badala ya majengo na utawala; wafanyakazi kuwepo kwa ajili ya kukochi watu kwa ajili ya maendeleo ya binafsi na taaluma ambazo watu wanazihitaji ili kuitumikia jamii. Mambo kama idadi ya masaa ya watu wanaojitolea (tengeneza mfumo utakaowasaidia watu kujua masaa yao ya kujitolea na kuhudumia), simulizi kuhusu yale ambayo washirika wa kanisa wanafanya na mguso walionao, zisherehekewe mara kwa mara kwenye ibada ya Jumapili na wakati mwingine, simulizi kuhusu jinsi watu wanavyowabariki wengine ziwe sehemu ya mahubiri (kwa ruhusa ya watu, bila shaka), na kuwe na namna ya kuwapongeza kwa njia fulani, ana kwa ana na kwenye tovuti ya kanisa, kama ipo. Kutambua mbele za watu na kutoa zawadi huonyesha namna tunavyothamini na vipaumbele vya kanisa na huwatia moyo washiriki na wengine (McNeal 2009: 77, 79, 112) McNeal anahitimisha kwa tahadhari na ushauri: “Ikiwa juhudi za kanisa za pamoja kama hizi zitasherehekewa peke yake tu, kuna kitu kitakosekana tena. Ili muwe katika uhalisia zaidi, fanyeni kila muwezacho ili kusherehekea maisha na huduma ya watu katika maisha yao ya kila siku nje ya kanisa, pale pale wanapoishi, wanapofanyakazi, wanapokwenda shule, na kufurahia.” (Ibid.: 53)

**C. *Ili kuwa la kimisheni zaidi, yabidi kanisa kupanga kwa upya matumizi ya rasilimali zake na kipaumbele kiwe umisheni***

Makanisa yana vyanzo tofauti tofauti vya kutendea kazi: vya mwili (ardhi, majengo, vifaa mbalimbali); vinavyohusu fedha (pesa na mapato); watumishi (watu na muda wao, vipawa, na vyanzo vingine). Swala la msingi ni *vipaumbele*. Kile ambacho kanisa linafanya na vyanzo vyake huonyesha ni kitu gani kwao ni muhimu kweli, kama vile Yesu alivyosema, *“Kwa kuwa hazina yenu ilipo, ndipo itakapokuwepo na mioyo yenu”* (**Math 6:21; Luka 12:34**). Hapa ni mapendekezo fulani:

- <u>Vyanzo vya mwili.</u> “Katika kanisa la kimisheni, swali la kwanza kuhusu majengo linaweza kuwa , ‘Je tunahitaji kweli kutumia pesa hizi kwenye majengo, au badala yake tuwekeze kwenye miundo mbinu ya jamii na hitaji?’” (McNeal 2009: 79) Tukichukulia kwamba unajenga jengo la kanisa, kanisa linapaswa kuuliza, “Tunawezaje kujenga majengo kwa ajili ya kuibariki jamii yetu na kisha tuonae namna ambavyo kanisa linaweza kuyatumia?” (Ibid.: 80) Swali kwa makanisa ambayo tayari yana majengo ni hili, Tunawezaje kutumia kile ambacho tayari tunacho kuibariki jamii? . . . Kanisa la kimisheni hupata njia za kuihudumia jamii kwa majengo waliyo nayo.” (Ibid.) Kanisa linaweza kutumika kama mahali pa kukutana kwa huduma nyingine au NGOs; linaweza kuwa na ubia na mashule kutoa sehemu ya kukutania, sehemu ya mafunzo kwa ajili ya walimu, nafasi kwa ajili ya matamasha, nk.; kanisa linaweza kuruhusu jengo lake litumiwe na makanisa mengine kwa ajili ya ibada zao au huduma za kuifikia jamii. “Kanisa moja liligundua kwamba linaweza kutoa chakula kwa watoto ambao hawakuwa na chakula cha kutosha na kutoa semina ya ujuzi wa msingi katika maisha kwa wazazi, wakati fulani waliufungua ukumbi wa ushirika wao ili utumike kwa ajili ya kuwalisha wanachama wa klabu wa shughuli za kanisa. Kanisa jingine limegeuza kiwanja chake cha ndani cha mpira wa kikapu kuwa mahali pakuu pa jamii kukutania kwa kushirikiana na idara ya burudani ya eneo lile. Licha ya hayo, visanduku vya kuweka mahitaji ya maombi viko kila mahali katika majengo yale, na matangazo hutolewa wakati wote kwamba kuna watu wako tayari wakati wote kuomba na watu na kuwapa ushauri.” (Ibid.: 81) Kanisa moja “lilitoa majengo yao kutumiwa kwa ajili ya huduma za jamii na taratibu likafanyika makao ya Skauti, klabu ya 4-H, darasa la mazoezi ya kuongeza hewa, kundi la kuwasaidi wahanga wa kisukari, kikundi cha ulinzi shirikishi, na Shule ya Polisi ya wananchi. Ingawaje washirika wa kanisa hawakuwa viongozi katika shughuli hizo zote, kwa kutoka na kuwa wasikivu kanisa taratibu lilijulikana kama mahali ambapo unaweza kupata msaada katika jamii.” (Minatrea 2004: 179) Matokeo mengine ya kufanya majengo yake yatumiwe na vikundi vya jamii ilikuwa ni kwamba “kadiri watu wengi walivyokuja kwenye majengo kwa ajili ya matukio ya kijamii, taaratibu walianza kujenga mahusiano na baadhi ya washirika wa kanisa. Wengine walianza kuhudhuria ibada kwa ‘kualikwa’ na washirika.” (Ibid.) Pendekezo jingine ni kutafuta eneo la nje ili kukodi au kulinunua ambalo linaweza kutumika kwa ajili ya matukio ya mikutano ya injili kwenye jimii. Hapa tena, kielelezo cha Mungu sio kuwaleta watu kwenye jengo letu la kanisa (kubwa, zuri) (kwa kiwango chochote kile tunavyopenda vitu hivyo) lakini kulichukua kanisa kwa watu.

  Makanisa mengi yana ardhi ambayo haitumiki ipasavyo. Miti ya matunda au mazao mengine inaweza kupandwa na matunda yake yanaweza kuuzwa kwa ajili ya kipato au kuwapa wenye uhitaji. Matumizi mengine ya ardhi ya kanisa, katika maeneo ambayo watu wengi hawalimi ardhi yao, itakuwa ni kutumia

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

sehemu ya ardhi kama bustani ya jamii ambapo viwanja vinaweza kutolewa au kukodishwa kwa wanajamii tofauti tofauti. Jambo hili litawavuta wanajamii kuja kanisani. Mikutano ya pamoja miongoni mwa wanajamii ambao ni wanachama wa bustani inaweza kupangwa.

Makanisa mengi madogo ambayo hukutana katika majengo madogo au kupangisha vyumba katika majengo mengine hata hivyo huwa na vyombo vya mziki vikubwa vyenye vipaza sauti vikubwa ambavyo ni maalum kwa ajili ya mikutano ya hadhara, ingawaje majengo yao ni madogo na hayangehitaji vyombo hivyo. Kwa kuongezea, vyombo vile vikubwa vya kuhuburia vinaweza kusababisha kelele zinazosababishwa na sauti "kuakisiwa" na kusababisha sauti miluzi na sauti kutosikika vizuri kutoka kwenye vipaza sauti katika chumba kile kidogo cha mkutano. Katika mazingira kama haya, ingekuwa ni bora kutotumia vipaza sauti na badala yake kuzungumza kwa kawaida tu. Vivyo hivyo matumizi ya vyombo vya mziki. Vifaa vya kuongoza mfumo wa sauti vinatosha kabisa, havina gharama kubwa. Swala ni uwakili wa vyanzo vya fedha vya kanisa. Ingawaje baadhi ya wachungaji wa Afrika ya Mashariki husema kwamba watu hutarajia vyombo vinavyotoa sauti kubwa na huvutwa na sauti kubwa, hilo si kweli kabisa. Na hata kama ingekuwa kweli, haiko sawa kimaandiko. Watu huvutwa (au wanapaswa kuvutwa) na nguvu ya injili. Kama kanisa ni la kimisheni hasa katika kuwafikia watu wengine na katika kujihusisha kwake katika jamii na watu wanaendelea kufanywa wanafunzi na kukua katika Kristo, watu watavutwa kwenye kanisa hili kwa sababu hii tu.

- <u>Vyanzo vya fedha.</u> Inabidi makanisa yote yaweke kumbu kumbu za fedha na kuwa na bajeti iliyoandikwa; hilo ni swala tu la uwakili wa kibiblia na uwajibikaji katika mambo ya fedha. Makanisa ya mahali pamoja na madhehebu yanaweza kuchukua hatua nyingi ili kujitegemeza. Makanisa yanaweza kujihusisha na shughuli za kuzalisha kipato ili yasitegemee kipato chote kutoka kwenye mishango ya washirika tu. Makanisa mengi humiliki ardhi lakini hayaitumii ardhi ile kwa manufaa. Makanissa yanaweza kupanda bustani katika ardhi yao na kuuza mazao yake. Makanisa mengine hupanda miti, ambayo inaweza kuuzwa kwenye makampuni ya kuzalisha umeme, makampuni ya ujenzi, au inaweza kutengenezwa mkaa. Kwa mfano, mchungaji mmoja wa Kenya alisema kwamba miti ya mkaratusi 200-250 inaweza kupandwa kwenye ekari moja ya ardhi. Inapokomaa inaweza kuuzwa kwa kiasi cha shilingi za Kenya 10,000 kwa kila mti. Mchungaji wa Uganda alikadiria kwamba viazi mviringo vinaweza kuuzwa kwa kiasi cha sh. 120,000 za Uganda kwa gunia. Hivyo, ekari ya ardhi iliyopandwa viazi mviringo inaweza kuwa na thamani ya kati ya shilingi milioni 5-10 za Uganda. Vyanzo hivyo (na mapato) huweza kuzungushwa. Dayosisi moja ya Kenya ilianza ufugaji wa nguruwe, na askofu humtaka kila mmoja wa washirika wake kuwa na ng'ombe. Makanisa yanaweza kutoza kiwango fulani cha pesa kwa ajili ya wale wanaotaka kutumia ukumbi wa kanisa ili kufanya sherehe za arusi na vikundi vinavyotaka kukutana kanisani. Makanisa mengine yanatoa huduma za chakula au nyumba za wageni ili kujipatia kipato. Njia za kuzalisha kipato ni nyingi kupita maelezo, kutegemeana na ubunifu wa mtu na rasilimali zilizopo. Hata hivyo, ikumbukwe wakati wote kwamba shughuli ya kuzalisha kipato ni *njia* ya kusaidia misheni na kusudi la kanisa. Isije ikawa, au ikashinda makusudi na misheni ya msingi ya kanisa. Kitabu cha ECLEA kiitwacho *Uwakili wa Kibiblia* (http://www.eclea.net/courses.html#stewardship) kina sehemu inayozungumzia kuhusu kanisa na fedha, ikiwa ni pamoja na utaalamu wa kutunza kumbukumbu za fedha, kupanga bajeti, na kuwa kanisa linalojitegemea.

Kile tunachokifanya kwa pesa zetu huonyesha dhahiri kuliko kitu kingine chochote katika maisha yetu ni nini vipaumbele vyetu, kile tunachothamini, na kile tunachoona kuwa ni muhimu zaidi katika maisha yetu. Hili ni kweli pia katika makanisa kama ilivyo kwa watu binafsi. McNeal anapendekeza kwamba "asilimia kubwa zaidi ya mapato iende kwenye uwekezaji wa huduma za jamii kuliko kwenye matumizi ya ndani" (McNeal 2009: 83). Ili kuweza kufanya anachopendekeza McNeal hili lenyewe litahitaji yatokee mabadiliko makubwa kuhusiana na namna kanisa linavyoendeshwa. Milfred Minatrea anasema, "Kwa kila shughuli ni vizuri kuuliza: 'Ni kwa namna gani shughuli hii au tukio linatufikisha katika kutekeleza kusudi letu na misheni yetu?' 'Je shughuli hii imeandaliwa kwa ajili ya washirika tu au itatuunganisha na wale ambao hawajawa washirika bado?' 'Kama tungekuwa hatujaanza kufanya shughuli hii, Je tungeianzisha leo kwa misingi ya misheni yetu na kusudi letu?'" (Minatrea 2004: 104) Maswali hayo hutumika kwenye shughuli zote kiujumla na matukio ya kanisani na katika kutengeneza bajeti. Minatrea anaonyesha, "Hakuna shirika ambalo linaweza kuwekeza katika mwelekeo mpya bila kuacha vitu vingine. . . . Manisa ya kimisheni yanapopanga shughuli zao kutegemeana na kusudi lao, lazima wanaendelea kuachana na shughuli zile ambazo haziwapeleki kwenye kutekeleza kusudi lao." (Ibid.: 106-07) jambo hili linaweza kuwa gumu, na hata kuwa na maumivu, kulitenda, lakini ni muhimu sana kuwa na jicho lililo wazi kufanya maamuzi ambayo yanatakiwa kufanywa ikiwa kusudi la *Mungu* kwa ajili ya kanisa yabidi lifikiwe.

Pendekezo la McNeal linatekelezeka. Mfano ni kanisa la Antiokia Presbiteri la Chonju, Jamhuri ya

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

Korea. Kanisa lilipoanzishwa mwaka 1983, moja ya kanuni za msingingi ilikuwa kwamba watatoa angalau asilimia 60 ya mapato yake kwa ajili ya umisheni. "Kanisa likajenga jina la utani 'Kanisa la Tin Can' kwa sababu wanafunzi wa Shule ya Jumapili walitangaza kwamba lilionekana kama kikopo kitupu kilicholala upande mmoja, kikiwa kimezikwa ardhini upande mmoja. Mwanzoni watu wengine waliona kama maono ya kutoa kwa ajili ya umisheni yatazuia kukua kwa kanisa. Kinyume chake, kutokana na Mchungaji Lee, pesa iliyotumika kanisani haikusababisha kukua, lakini ongezeko la utoaji kwa ajili ya umisheni uliathiri ukuaji wa kanisa. Kusanyiko lile sasa lina watu 4,000. Mwaka 2001, kanisa lile lilitoa asilimia 75 ya mapato yao kwa ajili ya umisheni. Mwaka 2002, kiwango kilikuwa asilimia 70 na mwaka 2003 ilikuwa asilimia 72.3. Sambamba na hayo, mchungaji mmoja alithibitisha tarakimu hizi na kusema, 'Tafadhali elewa. Mwaka 2002 na 2003 tuliwekeza asilimia 70 tu na 72.3 kutoka katika mapato ya mwaka na kutoa kwa ajili ya umisheni kwa sababu tulijenga kituo cha vijana na kituo cha mikutano katika miaka hii miwili. Ili waweze kutoa fedha kwa ajili ya umisheni, Mch. Lee wa kanisa la Antiokia Presbiteri na wachungaji kutoka katika makanisa mengine walianzisha 'Misheni ya Paulo' mwaka 1986. Hadi kufikia 2004, wamisionari 248 walikuwa wametumwa nchi 70. Misheni ya Paulo pia ilihamasisha uinjilisti, kupanda makanisa, elimu ya kitheolojia, huduma ya magerezani, huduma za rehema, mafunzo ya umisheni, programu za watoto na vijana, na ushauri kwa ajili ya familia. Programu ya kiinjilisti ya redio ya Thailand ni huduma nyingine ya Misheni ya Paulo. . . . Kanisa la Tin Can limegundua kwamba kuweka malengo ya kuwapenda wengine kwa ajili ya Yesu ilisababisha ukuaji wa kanisa lao na uhai kama mazao." (Ronsvalle 2004: "A Korean Church That Gives 60% To Missions")

Zaidi ya hayo, makanisa yanaweza kutafuta mitaji kwa ajili ya miradi ya kuifikia jamii kama wanavyofanya kwa ajili ya miradi yao ya ujenzi au wana weza kutoa zaka kwenye mfuko wa kuifikia jamii kutoka katika mfuko wowote wa mradi wa "ndani." McNeal anapendekeza njia nyinginezo bunifu za kuhamasisha upatikanaji wa mapato kwa ajili ya umisheni kwa jamii: "Wakaribishe viongozi wa jamii katika mchakato wako wa bajeti. Wakupeni taarifa za mahitaji na maeneo ambayo ni vyanzo vya mapato." (McNeal 2009: 84); "Wape semina kuhusu mipango ya fedha na huduma kwa jamii, hasa kuwasaidi wasio na uwezo kwenye jamii ili wajue namna ya kupanga bajeti vizuri na kuweka mipango kwa ajili ya wakati ujao" (Ibid.); "Anzisha vyombo vya kuinua uchumi wa walio maskini ili kuwasaidia kuanzisha biashara zao wenyewe au washiriki katika uchumi" (McNeal 2009: 84); "Tafuta njia za kuwasaidi washirika waweze kufuatilia matumizi yao wenyewe na kuyapunguza. Sherehekeeni upatikanaji na uhifadhi wa pesa kwa ajili ya huduma kwa pamoja kwa kufuatilia ni kiasi gani cha pesa kimehifadhiwa na kuelekezwa kwanye huduma. Tambua kwamba hili yabidi lifanyike katika ngazi ya viongozi, au halitapata mvuto wowote kwa washirika." (Ibid.: 85); "Buni njia mbali mbali nzuri za kutoa kwa jamii. Kanisa moja linatoa kwa jamii kiwango cha pesa kinacholingana kodi endapo kama lingepaswa kutoa kodi." (Ibid.) "Unganisha nguvu na makanisa mengine. Katika kanisa la asili, makanisa kushindana kupata pesa. Katika kanisa la mtazamo wa kimisheni mahitaji ya kutatua ni makubwa kwa mtu mmoja au kundi kuyamudu, hali hii husababisha uhitaji wa ushirikiano kati ya makanisa." (Ibid.: 84) Minatrea anaendelea kusema, "Siwezi kusema hili kwa msisitizo unaotosha: hakuna mafanikio yatakayoridhisha katika Ufalme mpaka pale makanisa yatakapothamini Ufalme kuliko mafanikio yao ya kundi binafsi" (Minatrea 2004: 127).

- Vyanzo vya wafanyakazi. Sehemu **VI.A.** ***Ili kuwa la kimisheni, inabidi kanisa libadili mtazamo wake*** na sehemu **VI.B.** ***Ili kuwa la kimisheni, inabidi kanisa ibadili vigezo vyake kwa kile kinachofikiriwa kuwa kanisa "lililofanikiwa" likoje***, hapo juu, tumejadili njia mbali mbali ambazo kwazo viongozi wa kanisa na washirika wanaweza kuzitumia kimisheni. Zaidi ya hayo, kanisa linaweza kuorodhesha na kuchapisha mahitaji ya jamii na fursa za kuihudumia jamii. Watu wengi wangependa kujihusisha katika kuwasaidia wengine, lakini hawayajui mahitaji na namna wanavyoweza kusaidia. Panga kuhusu namna ya kuwahusisha wasio washirika katika kanisa lako katika huduma za kuwafikia watu walio nje ya kanisa lako. Watu hawa wana ujuzi ambao unaweza kuwa muhimu kwa ajili ya huduma, na kuhusika kwao kutawafanya wawe hawana hofu ya kujihusisha na kanisa tena. Watakuwa wamekutana na injili ana kwa ana kimatendo, jambo ambalo litawaweka tayari kumpokea Yesu watakapokutana na injili yenyewe.

**D.** ***Mifano ya kampeni za kimisheni***

Fursa za umisheni ni nyingi na hutofautiana kama vile watu, mahitaji, na vyanzo. Hapa ni baadhi ya mifano ya huduma za kimisheni ambazo makanisa yanafanya au yanaweza kufanya:

- "Kanisa linaweza kutafuta nyumba mjini kwa ajili ya kuwasaidia watu wanatoka gerezani kwa kuwafunza na kuwategemeza" (McNeal 2009: 1).
- "Weka watu katika maeneo ya makazi, vituo vya paki za malori makubwa, na sehemu zenye jamii msongamano ili watumike kama wamisionari wakazi. Kisha wategemeza kwa kuwapa wasaidizi wa

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

kujitolea, pesa na mahitaji mengine muhimu wakiwa wanaibua mahitaji na kuwahudumia watu. Asilimia ya watu ambao hujiunga na kanisa kutoka katika jamii ya watu waishio katika makazi yenye msongamano si kubwa. Haijalishi hata kama kanisa liko karibu. Hata hivyo kuwa katika makazi yao kabisa ni njia bora zaidi ya wao kujua kinachoendelea kwenye makazi ya watu wengi. Kanisa moja huwategemeza wanandoa vijana kama wamisionari wao wa mtaani, wakiwalipa mshahara na kukutana na mahitaji ambayo wale wamishenari wanayaibua katika jamii ile huku wakijenga mahusiano. Darasa moja la shule ya Jumapili huandaa chakula cha mchana kwa ajili ya wakazi; wengine hufanya ukarabati wa vyumba vya watu katika jamii." (McNeal 2009: 77)

- Kila mwaka kuna karamu kubwa katika kitalu cha Madison, Wisconsin, katika eneo la chuo kikuu cha Wisconsin. Baada ya karamu, eneo limekuwa chafu kwa karatasi, chupa, na aina nyingine za uchafu. Gazeti la mjini liliandika, "washirika wa kanisa la Blackawk, lililoko upande wa magharibi mwa Madson, walifika saa 12 asubuhi siku ya Jumapili kusafisha uchafu uliokuwa umebaki barabarani, kwenye njia za waenda kwa miguu, na kwenye nyasi za mbele. Huu ni mwaka wa pili mfululizo kanisa la Blackhawk limewasaidia huduma ya usafi makazi. . . . Ingawaje umoja wa mtaa wa Mifflin pia ulipanga kufanya usafi wa maeneo asubuhi hii . . . kwa sababu kanisa lilifanya usafi wa kutosha kabisa ule umoja haukuona ulazima wa kufanya usafi wowote wa ziada. 'Wakati wengi wetu tulipokuwa bado vitandani, hili kundi la kanisa lilikuwa likifanya usafi huku mvua inanyesha,' [afisa wa serikali Mike] Verveer alisema." (Heidmann 2006: n.p.)
- Kanisa moja dogo lilifanya kliniki ya baiskeli kwa ajili ya watu kati ujirani. Maelekezo na mbinu za utengenezaji yalitolewa, marekebisho na ripea ndogo ndogo zilitolewa, na vinywaji vilitolewa. Kliniki ilipokelewa vizuri mno na itarudiwa kwa vipindi hapo baadae.
- "Darasa moja la wakina mama watu wazima hutumia kila Jumatano asubuhi kuwaogesha na kuwalea watoto katika nyumba za wazazi ambao wamezaa watoto watano pacha, ongezeko la watoto watano kwa wawili ambao tayari walikuwepo. Wamama hawa huwaogesha na kuwavalisha nepi, hupika na kufanya kazi nyinginezo zitakazohitajika kufanywa, na wameweka nadhiri kufanya hivyo mpaka watoto wale wawe wakubwa kiasi cha kuanza kwenda shule. Vikundi vingine vitaunganisha nguvu zao wanapogundia wengine ambao wanashiriki wito wa huduma yao." (McNeal 2009: 76)
- "Jamii zote za kimisheni ambazo ninazokutana nazo hutenga na siku fulani za ibada kwa ajili ya kuihudumia jamii kama tendo la kuabudu. Kusanyiko moja hutumia Jumapili moja kwa mwezi kama siku ya kuihudumia jamii. Baada ya washirika kukutana na kuomba na kupokea maagizo, hutoka na kwenda kuubariki mji. Familia nzima zitafanya kazi pamoja mara nyingi zikihudumia familia nyingine nzima katika siku ile. Wakati mwingi changamoto maalum huhitaji juhudi za wamama tu au vijana tu. Hatimaye kusanyiko hukutana tena kwa pamoja ili kula pamoja na kushuhudiana mambo waliyokutana nayo katika utumishi ule." (McNeal 2009: 60-61)
- Maombi ya kutembea: "Maombi ya kutembea yanaweza kufanywa na kanissa lote au mtu mmoja mmoja kwa wakati wao. Shughuli hii hutuwezesha kufokasi katika eneo fulani ili kujua kile anachofanya au anachotaka kufanya Mungu katika eneo fulani mahususi. . . . Inakuwa na nguvu zaidi kama majirani wanajua kwamba wanaweza kushirikisha mahitaji yao kwa waombaji." (McNeal 2009: 71) Vizimba vya maombi: "Hii huhusisha aina fulani ya huduma ya maombi iliyo wazi ambayo huwekwa mahali maalum ambapo watu huja na kushirikisha mahitaji yao ili waombewe. . . . Baadhi ya makusanyiko ambayo nimefanya nayo kazi huweka vizimba vya maombi katika maonesho ya kitaifa au wakati wa sikukuu za kijamii mahali ambapo watu wanaweza kuweka maombi yao kwenye sanduku la maombi au mahitaji yao kuombewa papo hapo." (Ibid.)
- Kuwapata viongozi wa jamii kwa ajili ya maombi: "Wazo hapa ni kuwasiliana na viongozi wa jamii katika eneo, na kuwajulisha kwamba wana nafasi ya kushiriki katika maombi, na kuwapa namba ya mawasiliano ambayo wanaweza kutumia kutuma maombi ambayo wanaweza kuwa nayo. Wakati mwingine inasaidia kuwahamasisha hawa viongozi kwa kuwaambia kwamba wanaweza kuorodhesha changamoto ambazo wanaweza kuwa nazo na kuwahakikishia kwamba mtamwomba Mungu na yeye atashughulika na changamoto zao zote. . . . Viongozi wa kiserikali hupokea malalamiko mengi. Jaribu kuwaza jinsi watakavyotiwa moyo watakapojua kwamba kuna watu wanawainua!" (McNeal 2009: 72)
- Chukueni shule. . . . Hakuna mkakati wenye mafanikio zaidi kuliko huu kuwaita watu na vipawa vyao kwa ajili ya huduma katika jamii." (McNeal 2009: 77) Kanisa moja lililoko kaskazini mashariki ya Marekani linataarifu, "Ushirikiano mkubwa ambao Mt Paulo wanao na Norwalk International Academy ya shule ya Sekondari ya Brien McMahon ni wakutatua mahitaji ya wanafunzi wakimbizi. Wakikimbia madhara ya maisha yaliyoathiriwa na madawa ya kulevya, nchi zilizo kwenye ukanda wa vita kama Guatemala na Honduras, vijana hawa tunaokutana nao wamehatarisha maisha yao ili kufika kwenye

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

usalama. Wengi wameshuhudia au wamekuwa wahanga wa vurugu kubwa. Wanachama wa St. Paul hutumika kama wakufunzi na wenza wakati wanafunzi wakijifunza lugha ya Kiingereza na kujenga ujuzi wa Hisabati. Wanaojitolea si lazima waseme lugha ya Kihispania; wala hawahitaji kujuwa kufundisha kama walimu." ("Social Justice & Outreach" n.d.)

- Mungu ameumba mimea mingi ambayo ina uwezao wa kuponya na ina thamani ya kitabibu. Tunaweza kuwafundisha watu ndani ya kanisa na pia ndani ya jamii kuhusu mimea hii na namna ya kuiotesha katika bustani zetu. Tunapotumia tiba hizi za asili tunaweza kukinga magonjwa yasitupate na kwa njia hiyo tunaweza kuokoa pesa nyingi ambazo tungeweza kuzitumia kununulia madawa ya kisasa, ambayo yametengenezwa kwa kutumia kemikali. Tunatakiwa kutumia manufaa ya vyanzo hivi tulivyo navyo kama shule, mashirika ya serikali, NGOs, mashirika ya watu binafsi na yale ya misaada, na maktaba ili kuongeza maarifa ili tuweze kuwa watendaji wenye hekima na umakini kadiri iwezekanavyo na kuwawezesha watu wa kanisani na kwenye jamii kufanya mambo kwa uonafu na hekima kadiri iwezekanavyo.
- Mapendekezo yote ambayo yametolewa hapo juu katika sehemu **VII.C.** ***Huduma ndani ya kanisa inahusisha huduma katika eneo la "kimwili" na pia katika eneo la "kiroho"*** na inaweza kuhusisha jamii yote. Kanisa lapaswa kuwa ndipo mahali ambapo watu wanajifunza mambo ya msingi ya afya na namna ya kupangilia matumizi ya pesa. Ikiwa kanisani yuko daktari au muuguzi ambaye ni muumini, kwa vipindi fulani wanaweza kufanya kliniki za huduma za matibabu bure kwa ajili ya jamii (na yule daktari na muuguzi Mkristo wanaweza kuwaandaa baadhi ya wafanyakazi wenzao kushiriki hata kama wao si Wakristo). Seremala au mafundi wengine walio Wakristo wanaweza kuwafundisha ujuzi wa kazi zao na wafanya biashara walio Wakristo wanaweza pia kuwashirikisha uzoefu wao wa biashara. Kitabu cha ECLEA kiitwacho *Uwakili wa Kibiblia* (http://www.eclea.net/courses.html#stewardship) kina mifano mingi inayohusu afya ya msingi na maswala yahusuyo usafi ambayo kanisa linaweza kuyafanyia kazi na kufundisha na kuonyesha matumizi ya kimatendo ya uwakili wa fedha na vitu tunavyomiliki, ikiwa ni pamoja na jinsi ya kupanga bajeti, katika sehemu yake inayohusu "Uwakili wa Mwili" na "Mtazamo wa Biblia Kuhusu Pesa na Vitu tunavyomiliki."
- Umuhimu wa kutoka kwa ajili ya umisheni unakaziwa na ukweli kwamba kila Ijumaa wanawake wa Kiislamu hupeleka chakula kizuri kwa wagonjwa wote kwenye hospitali kubwa kule Kigali na Dar es Salaam. Nimetaarifiwa kwamba hakuna kanisa ambalo limefanya kitu cha namna hiyo. Wagonjwa wale watakapotoka hospitali, watakapokuwa na mahitaji, je watakimbilia kanisani au msikitini ili kupata msaada? Ingawaje baadhi ya wachungaji watasema kwamba "kanisa langu ni dogo sana kuweza kufanya kile kinachofanywa na wale Waislamu," ikiwa kanisa A litaunganika na kanisa B, C, na D, kwa pamoja wanaweza kufanya makubwa ambayo hakuna mmoja wao ambaye angeweza kufanya peke yake.

Kanisa linapaswa kuwa taasisi iliyo muhimu kuliko zote kijijini au katika jamii mahali lilipo. Ni lazima litambuliwe na serikali za mitaa na wakaazi. Jambo hili litakuwa Dhahiri tu ikiwa kanisa linachukua hatua za makusudi kujihusisha na mambo ya kijamii waziwazi. Mipaka ya fursa zinazohusu mambo yepi kanisa litajihusisha nayo katika jamii hutegemeana na maono yao na uhaliasia wa kanisa na watu wake.

## X. <u>UMOJA (UKAMILI)</u>

Misheni na kusudi la kanisa huonekana wakati tunapokuwa na umoja na ukamili. "Umoja ndani ya kanisa ni muhimu sana kiasi kwamba katika Agano Jipya umepewa uzito kuliko mbinguni au motoni. Mungu anatamiani hasa tuwe na umoja na upatanifu kati ya sisi kwa sisi. Umoja ndiyo moyo wa ushirika. Uharibu, na utautoa moyo ndani ya Mwili wa Kristo. Ni kiini, moyo, wa jinsi Mungu anavyotaka sisi tuishi kwa pamoja katika kanisa lake. Kielelezo chetu kikuu ni Utatu. Baba, Mwana na Roho Mtakatifu wako umoja kama kitu kimoja. Mungu mwenyewe ni kielelezo kikubwa cha upendo wa kujitoa, unyenyekevu, kuwafikiria wengine, na makubaliano makamilifu." (Warren 2002: 160) Kuonyesha upendo na ukamili ni ishara muhimu kwamba kanisa linamwabudu Mungu, likifanya washirika wake kuwa wanafunzi, na kweli liko katika misheni ya Mungu kwa dunia. Kristo ameliita kanisa kuonyesha upendo kama inavyoonyesha katika maombi yake ya Kikuhani Mkuu katika **Yoh 17:18-21**: ***18****Kama vile ulivyonituma mimi ulimwenguni, nami vivyo hivyo naliwatuma hao ulimwenguni.* ***19****Na kwa ajili yao najiweka wakfu mwenyewe, ili na hao watakaswe katika kweli.* ***20****Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao.* ***21****Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiye uliyenituma."*

### A. *Umoja na ukamili wa kanisa hutiririka kutoka katika asili ya kanisa*

1. <u>Kristo aliomba kwamba "wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu na mimi ndani yako; hao nao wawe ndani yetu" (**Yoh 17:21;** ona pia **Yoh 17:11**).</u> Paulo alisema kwamba kwa kuwa

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

Kristo hajagawanyika, hatupaswi kugawanyika (**1 Kor 1:11-13**). Aliwaagiza waamini *"mwenende kama inavyoustahili wito wenu mlioitiwa; kwa unyenyekevu wote na upole, kwa uvumilivu, mkichukuliana katika upendo; na kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani . . . hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani, na kumfahamu sana mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kuwa mwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo"* (**Efeso 4:1-3. 13**). Kuwa na umoja ni alama muhimu ya ukomavu katika mwendo wa kanisa na mwamini binafsi na pia ni alama muhimu ya lengo ambalo kwalo sote tunapaswa kutafuta kufikia.

2. Umoja ndani ya kanisa na makanisa ya mahali pamoja na madhehebu hutiririka kutoka katika yale mambo muhimu ambayo sote tunayo kila mmoja. Wakristo wote, makanisa yote ya mahali pamoja, na madhehebu yote yana Bwana mmoja (**Rum 10:12; Efeso 4:5**), mwili mmoja (**Rum 12:4-5; Efeso 4:4**), kusudi moja (**1 Kor 1:10; Fil 2:2**), Baba mmoja (**1 Kor 8:6; Efeso 4:6**), Roho mmoja (**1 Kor 12:13; Efeso 4:4**), tumaini moja (**Efeso 4:4**), imani moja (**Efeso 4:5**), ubatizo mmoja (**Efeso 4:5**), na upendo mmoja (**Fil 2:2**). "Tunashiriki wokovu ule ule, maisha yale yale, na wakati ujao ule ule—hizi ni kweli muhimu zaidi kuliko tofauti zozote tunazoweza kuzitaja" (Warren 2002: 161).

Haya ni mambo ya msingi. Mambo ya "Msingi" ni yale mambo ambayo ni kiini cha imani na ambayo Wakristo wote wanapaswa kukubaliana: Biblia ni Neno la Mungu; Mungu ni utatu; mwanadamu ameanguka dhambini kabisa na hawezi kujiokoa mwenyewe; Yesu ni Mungu kamili na mwanadamu kamili; Kristo ndiye njia pekee ya wokovu; tunaokolewa kwa neema ya Mungu kwa imani katika Kristo; tumeitwa kuishi maisha ya upendo. Mambo ya "kundi la pili" ni yale mambo ambayo Biblia huyazungumzia lakini si wazi kabisa. Mambo haya ya kundi la pili ni pamoja na: Je watoto wabatizwe au watu wale wanaokiri imani? Je mfumo wa uongozi wa kanisa uwe vipi? Je Kristo hujihudhurisha kwa njia fulani maalum wakati wa Meza ya Bwana au la? Ni lipi jukumu la wanawake katika huduma? Mambo "ambayo yametungwa na wanadamu" ni yale ambayo Biblia haisemi chochote kuhusu hayo, lakini watu wameyatungia sheria fulani au taratibu fulani wao wenyewe. Mambo ambayo yemetungungwa na wandamu ni pamoja na mambo kama: taratibu za mpangilio wa ibada; kuvaa mavazi fulani maalum; aina gani ya matukio (mfano, muziki, sinema, chakula na vinywaji) yanafaa kwa Wakristo. Tofauti kati ya mambo ya kundi la pili na yale yaliyotungwa na wanadamu haiathiri wokovu wetu hivyo haipaswi kuathiri ushirika wetu. Chakusikitisha, matengano mengi kati ya medhehebu na kati ya Wakristo yanatokana na mambo ya kundi la pili na yale yaliyotungwa na watu—yaani ni yale mambo ambayo *hayana* uzito kabisa. Kudumisha mahusiano ya karibu kikazi kati ya waamini, makanisa na madhehebu hakupaswi kuathiriwe na tofauti walizonazo katika mambo ya kundi la pili na yale yaliyotungwa na wanadamu. Yanayotuunganisha ni mengi kuliko yale yanayotutenganisha. Tunahitaji kudumisha umoja kwa kuona misingi ya imani na tuwe na upendo kwa waamini wengine kuhusiana na mambo ya kundi la pili na yale yaliyotungwa na wanadamu.

3. Mifano ambayo Biblia inatumia kulielezea kanisa huonyesha kwamba kanisa lazima liudhihirishe umoja na ukamili.

a. *Kanisa ni mwili wa Kristo.* Kanisa ni mwili mmoja wenye kichwa (Kristo). Kila mmoja ni mtu muhimu, kwa sababu kila mtu ni "kiungo" cha mwili. Mmoja akiumia, mwili wote huumia, Viungo vyote huhitajika na huhitajika kufanya kazi sawa sawa ili mwili uwe sawa na kamili (**1 Wakorintho 12;** ona **Rum 12:4-5; Efeso 1:22-23; 4:1-6, 11-16; Kol 1:18, 24; 2:19; 3:15**).

b. *Kanisa ni jengo au hekalu la Mungu.* Sisi ni "mawe yaliyo hai" ambayo kila mmoja ana mahali pake kamili katika jengo. Kuwa nje ya jengo ni kupoteza mwelekeo au kuvunjika vipande ni huliathiri jengo kwa sababu sivyo lilivyokusudiwa kuwa (ona **1 Kor 3:9-17; 2 Kor 6:16; Efeso 2:19-22; 1 Pet 1:4-6**).

c. *Kanisa ni familia ya Mungu.* Familia nzuri, na inayojiendesha vizuri haina sifa ya kuwa na hasira, matengano, au magomvi kati ya wao kwa wao. Familia nzuri, na inayojiendesha vizuri huwa na upendo, heshima, furaha, umoja, na sifa nyingine nyingi kwa pamoja. Kanisa linahitaji kuonyesha, ndani yake lenyewe na kwa dunia, namna vile familia nzuri na inavyotendakazi vizuri ilivyo (ona **Marko 10:29-30; Rum 8:14-17; 2 Kor 6:18; Efeso 1:5; 2:19; Gal 3:26-4:7; 1 Tim 3:15; 5:1-2**).

**B.** ***Umoja na ukamili wa kanisa hutiririka kutoka katika yale aliyofanya Kristo***

1. Kristo ametupatanisha na Baba. Kwa hiyo, tuna huduma ya kuwapatanisha wengine (**Rum 5:10; 2 Kor 5:18-20; Efeso 2:16; Kol 1:21-22; Ebr 2:17**).

2. Kristo alivunja kiambaza pekee kilichokuwa kikitutenganisha ambacho kilikuwa na maana katika AK (kiambaza kati ya Wayahudi na Wamataifa). Kwa hiyo, tusijenge viambaza vipya kati ya sisi kwa sisi

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

(**Yoh 17:11, 20-21; Rum 3:21-22; 1 Kor 12:12-13; Gal 3:26-28; Efeso 2:11-3:6; Kol 3:9-11**).
3. Kristo alifanya zaidi ya kuangusha ukuta wa matengano kati ya watu; aliumba "mtu mpya" kutoka kwa watu ambao hapo mwanzo walikuwa wamegawanyika. Kwa hiyo, tuwe na umoja na upya katika Kristo (**Efeso 2:11-22**).
4. Kristo amewanunua watu wake kutoka katika kila kabila, lugha, jamii, na taifa duniani. Kwa hiyo, tumtangulize Kristo kwanza na tusijigawe kutokana na rangi, kabila, lugha, na tofauti za kiutamaduni (**Ufu 5:9; 7:9**).

**C.** ***Umoja na ukamili wa kanisa ni muhimu kwa ajili ya ushuhuda wa kanisa kwa dunia***

1. Kristo aliomba tuwe na umoja "ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma" (**Yoh 17:21**). Umoja wetu, au kutokuwa na umoja na ukamili kwetu kama mwili, huathiri moja kwa moja vile namna watu watamwona Yesu kwamba ni nani. Kwa kweli, ishara moja ambayo Yesu alitupa ambayo kwayo *"watu wote watatambua ya kuwa mmekuwa wanfunzi wangu"* mkiwa *"na upendo ninyi kwa ninyi"* (**Yoh 13:34-35**). Ikiwa kweli tutakuwa na upendo huo kati ya sisi kwa sisi, na kuuonyesha, *tutakuwa na umoja na ukamili.*
2. Mitume walikuwa na umoja na walituagiza na sisi tuishi kwa umoja na ukamili (**Zab 133:1; Matendo 1:14; Acts 4:32; Rum 12:16; 15:5-6; 1 Kor 1:10; 12:24-25; 2 Kor 13:11; Efeso 4:11-13; Fil 1:27; 2:1-5; Kol 3:14; 1 Pet 3:8**).

**D.** ***Umoja na ukamili unapaswa kudhihirika kimatendo katika ngazi zote—ndani ya mtu mwenyewe; kimahusiano ndani ya kanisa la mahali pamoja; na kati ya makanisa na madhehebu tofauti***

1. Ukamili huanza na mtu mwenyewe. Kristo huwaokoa watu kutoka katika dhambi zao na kwa njia hiyo huleta uponyaji (**Math 1:21**; **8:16-17; 1 Pet 2:24**). Amemtuma Roho Mtakatifu kukaa ndani ya waamini (**Yoh 14:16-18**). Hutuongoza katika kweli (**Yoh 14:26; 16:13**). Hutupa Amani na "*tunda la Roho*" ili tuwe na maisha yaliyo kamili kabisa (**Yoh 14:27; Gal 5:22-23**). Tuna nia ya Kristo (**1 Kor 2:16**). Ametuasili katika familia yake (**Rum 8:14-17**). Hakika, Yesu alikuja ili watu *"wawe na uzima kisha wawe nao tele"* (**Yoh 10:10**). Kadiri Kristo anavyofanya kazi katika maisha yetu, na kadiri tunavyotii na kufuata na kuendelea kuwa kama yeye, kila mwamini mmoja mmoja anapaswa kudhihirisha ukamili zaidi na zaidi.
2. Wito wa mitume wa umoja ulilenga kwa kiwango kikubwa watu ambao wako katika kanisa la mahali pamoja. Mitume waliweka mkazo katika nia moja na umoja katika *mahusiano* ndani ya mwili wa Kristo (ona **Rum 12:16; 15:5-6; 1 Kor 1:10; 12:24-25; 2 Kor 13:11; Efeso 4:11-13; Fil 1:27; 2:1-5; 1 Pet 3:8**). Umoja wa namna hii wa kimahusiano hutiririka kwa asili na utakuwa wazi kwa wengine ikiwa kanisa linaitii "amri mpya" ya Kristo ambayo aliwapa wanafunzi wake usiku ule kabla ya kusulubiwa, *"Mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo"* (**Yoh 13:34-35**). Ikiwa kweli tunaona kwamba kanisa la mahali pamoja ni familia, na sisi wenyewe kama kaka na dada, tunapaswa kuonyesha umoja na upendo kati ya sisi kwa sisi bila tatizo lolote.
3. Eneo jingine muhimu la umoja na ukamili ndani ya kanisa ni umoja kati ya makanisa ya mahali pamoja tofauti na madhehebu tofauti. Madhehebu tofauti na itikadi zinaweza kuleta utajiri wa kanisa kwa ujumla, kama utajiri wa familia unavyothibitishwa na ukweli kwamba baadhi ya wana familia huishi mijini, na wengine vijijini, wengine wako katika biashara, wengine wakulima; hata hivyo, familia yote inapokusanyika, wote hufurahia ule ukweli kwamba wote ni wa familia moja, familia kubwa.
    a. Ingawaje madhehebu yaliudwa baada ya Biblia kuandikwa, maombi ya Yesu katika **Yohana 17** na wito wa Yesu na mitume katika AJ yote kwa ajili ya umoja ni mpana vya kutosha kuhusisha umoja kati ya makanisa ya mahali pamoja tofauti na madhehebu tofauti.
    b. Matamko mengine ya Yesu (**Math 12:25, 30; Marko 3:24-25; 9:38-40; Luka 9:49-50; 11:17, 23**) na Paulo (**1 Kor 1:10-15; Fil 1:12-18**) pia hushughulika na swala la umoja miongoni mwa vikundi ndani ya kanisa.
    c. *Umoja kati ya makanisa au madhehebu tofauti haimaanishi kwamba tuachane na mafundisho au taratibu ambazo ni muhimu kwetu.* Tunahitaji kutofautisha kati ya mambo yale ambayo ni mafundisho ya msingi kwetu na mambo ya kiimani (ina maana, Biblia ni Neno la Mungu; hali ya mwanadamu ya dhambi ya kurithi na kushidwa kujiokoa; Uwepo wa Yesu Kristo na kazi aliyoifanya; njia pekee ya wokovu, kwa neema kupitia imani ndani ya Kristo; sheria ya upendo) na yale ambayo sio. Umoja unapaswa kuwepo kwenye mambo ya msingi ya kiimani. Tunapaswa kufanya kazi, kushirikiana, na kujenga mahusiano kati ya sisi kwa sisi. Tusiruhusu imani na itikadi ambazo ziko nje na misingi ya imani ya Kikristo itenganishe ushirika wetu.

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

Ikiwa tutafanya hivyo, tutagundua kwamba kuna mengi sana yanayotuunganisha kuliko yale yanayotutenganisha. Rick Warren anahitimisha, Mungu anataka umoja, si kufanana. Lakini kwa ajili ya umoja tusiruhusu tofauti zetu kututenganisha. Lazima tubaki katika fokasi katika yale ambayo ni muhimu zaidi—tukijifunza kupendana kama Kristo alivyotupenda, na kutekeleza kusudi la Mungu . . . kwa ajili ya kila mmoja na kanisa lake." (Warren 2002: 161-62)

**E.** ***Umoja na ukamili ndani ya kanisa hutendeka kwa njia tofauti***

1. Kukusanyika pamoja kwa ibada ya pamoja (**Ebr 10:23-25**).

2. Kushiriki katika sakramenti pamoja (ona **Math 28:19; Matendo 2:38; 1 Kor 10:17**). Ingawaja ubatizo, tofauti na Meza ya Bwana, unapaswa kufanyika mara moja tu, tabia nzuri ambayo inatusaidia kuushikamanisha mwili pamoja ni kukumbuka ubatizo wetu mara kwa mara. Njia moja ya kufanya hili ni kuwataka washirika wakiri nadhiri zao za ubatizo wakati mtu mwingine anapobatizwa na kuahidi kumwombea yule anayebatizwa.

3. Milo ya pamoja na ushirika (**Matendo 2:42, 46-47**). Ushirika ndani ya kanisa unafafanuliwa kwa neno la Kiyunani *koinonia* ambalo humaanisha "kuhusiana kwa karibu kunakohusisha vile ambavyo watu wanapenda na kushirikiana; Ushirika Mtakatifu; mwenendo wa kuaminiana ambao unadhihirisha mahusino ya karibu." Ushirika wa jinsi hii unapaswa kuwa umoja halisi, upendo, na kitu cha kufurahia ambacho huonyeshwa na wana familia kati ya wao kwa wao. Makusanyiko ya kanisa lote na vikundi vidogo ndani ya kanisa na njia nzuri za kuhamasisha ushirika.

4. Kushirikiana na kusaidiana vitu (**Matendo 2:44-45**). Wana familia husaidiana. Kuwasaidia wahitaji huonyesha kwamba sisi ni familia kiukweli (ona **Gal 6:10; Yak 2:14-26**).

5. Kufanyakazi pamoja kila inapowezekana. Makanisa yote na madhehebu hukutana na matatizo kama hayo, hasa yale ambayo yapo katika mazingira au jamii moja. Watu katika jamii fulani au mahali—wawe Wakristo au wasiwe Wakristo—pia wana matatizo kama haya. Kanisa ni ndilo kundi lililowekwa wakfu na Mungu lililopo duniani na katika jamii. Makanisa tofauti na madhehebu yangeweza kuwa na mguso mkubwa katika jamii na maeneo yao endapo yangechukua hatua za kuanza kufanya kazi pamoja ili kutatua matatizo waliyonayo na ya watu wao. Njia iliyo rahisi zaidi ya kuanza kufanya hivyo ni kwa makanisa tofauti ya dhehebu moja kuanza kufahamiana, kutathimini mahitaji yao makubwa na mahitaji ya jamii ni yepi, wapate mipango na mikakati ya kutatua matatizo hayo na wafanye kazi pamoja kutatua matatizo hayo. Njia inayofuata rahisi ni kwa makanisa kutoka madhehebu tofauti ambayo yana itikadi zinazofanana (Wapentekoste; Makanisa ya Kiinjili; waliowengi) kufanya mambo yanayofanana. Kufanya hivi hufanya iwe rahisi kuvuka mipaka ya dhehebu au itikadi ili kufanya vitu vinavyofanana. Hii haimaanishi kwamba makanisa yafanye kila kitu kwa pamoja, lakini yanaweza kufanya baadhi ya vitu kwa pamoja. Wanapofanya, watagundua kwamba ni rahisi kuliko walivyofikiri, Mungu anafunua maeneo mengine ambayo wanaweza kufanya kazi pamoja, na watapata uzoefu mpya utakaoleta nguvu kubwa katika maisha ya rohoni.

**F.** ***Kanisa linapofanya yale linayopaswa kufanya matokeo ni umoja na ukamili***

1. Maombi ya Kristo "Wote wawe na umoja" (**Yoh 17:21**) ni "wakati usiofaa." Hii inaonyesha kwamba umoja (umoja; ukamili) ni *matokeo* au *zao la* kitu kingine, si kitu ambacho tunakifikia "moja kwa moja". Kile "kitu kingine" ni misheni na makusudi ya kanisa: kuabudu; kuendeleza (malezi); na huduma (kufikia wengine).

2. Kanisa litaonyesha umoja na ukamili ikiwa—na kwa kiwango—litadhihirisha mambo ya msingi matatu ya misheni na makusudi.

a. Hatuko "kamili" kama tunadharau kusudi lolote kubwa la kanisa. Katika hali hiyo tunakosa mizania.

b. Kadiri kanisa linavyomwabudu Mungu kiukweli "katika Roho na kweli" ni lazima liwe na umoja na ukamili.

c. Kadiri kanisa linavyowatendea wale walio ndani yake kama ndugu wapendwa wa familia, waamini watakuwa kamili wakipata malezi, wakiendelezwa, na kuandaliwa.

d. *Kadiri kanisa linavyotumika na kuwafikia wengine, waamini ndani ya kanisa watakuwa wakitumia vipawa vyao na uwezo wao ambao kwa huo wameandaliwa.* Watakuwa wakijenga "misuli ya kiroho" kama mazoezi ya mwili yanavyojenga misuli ya mwili (ona **1 Tim 4:7-8**).

e. *Kadiri kanisa linavyotumika na kuwafikia wengine, hao wengine watafanyika kuwa waamini ndani ya kanisa.* Kanisa litakua.

f. *Waamini wapya watakuwa waabuduo.* Kadiri waamini wapya wanavyofanywa kuwa wanafunzi, wanavyolelewa, na kuandaliwa, watakuwa kamili. Ndipo watatumia karama na

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

vipawa na uwezo wao na kuwafikia wengine. Mzunguko utaendelea kujirudia wenyewe.

## XI. Kanisa: Hitimisho

Katika hali yake ya kuonekana na kuwa mahali pamoja, kanisa ni shirika. Hata hivyo kanisa pia lina uhai: ni mwili, familia, mti, mzabibu, jingo la "mawe yaliyo hai." Kwa hiyo wanachama wa kanisa ni umoja; lazima wote watumie vipawa vyao na kufanya kazi pamoja. Kama vile Kristo hakugawanyika (**1 Kor 1:13**), hivyo haipasi kuwa na migawanyiko kanisani, *"Na kiungo kimoja kikiumia, viungo vyote huumia nacho, na kiungo kimoja kikitukuzwa viungo vyote hufurahi pamoja nacho"* (**1 Kor 12:26**).

Kwa njia hiyo hiyo, misheni zote za msingi na makusudi ya kanisa vinahusiana na ni muhimu. Hakuna hata moja inayojitosheleza kibinafsi kati ya makusudi na misingi ya misheni za kanisa. Utekelezaji wa misingi mitatu ya misheni na makusudi kwa pamoja *husababisha umoja na ukamili* na *hupelekea ongezeko la kuabudu, maendeleo (kufanya wanafunzi), na kufikia wengine (umisheni).* Sababu ni kwamba kanisa linafanya kile linachopaswa kufanya. Hiyo ndiyo tabia ya kuabudu; hiyo ndiyo asili ya upendo. Kanisa linapofanya tunaweza kuwa na uhakika kwamba *"Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema"* (**Fil 2:13**), hadi mwisho kwamba *"wala malango ya kuzimu haitalishinda [kanisa]"* (**Math 16:18**), na Kristo anatukuzwa sasa na hata milele.

## BIBLIOGRAFIA


Adeleye, Femi. *Preachers of a Different Gospel.* Kampala, Uganda: International Fellowship of Evangelical Students.

Alexander, T. Desmond. 2008. *From Eden to the New Jerusalem.* Nottingham: Inter-Varsity.

Ambassador Church. 2010a. *Transformational Discipleship-Part 1*. Online: http://ambassadorchurch.com/wp-content/uploads/2010/01/Discipleship-Workbook.pdf.

_______. 2010b. *Transformational Discipleship-Part 2*. Online: http://ambassadorchurch.com/wp-content/uploads/2010/02/Discipleship-Workbook-2.pdf.

_______. 2010c. *Transformational Discipleship-Part 3*. Online: http://ambassadorchurch.com/wp-content/uploads/2010/10/Discipleship-Workbook-part-3-Jn.-15-211.pdf.

Archer, Gleason. 1982. *Encyclopedia of Bible Difficulties.* Grand Rapids: Zondervan. Online: http://sent2all.com/Archer-Introduction%20to%20Bible%20Difficulties.pdf.

The Augsburg Confession. 1530. Online: http://bookofconcord.org/augsburgconfession.php.

"Baptism." Not dated. Online: http://www.growingchristianresources.com/search/label/Baptism.

Bearing Precious Seed Canada. Not dated. *Bible Basics for the new Believer.* Online: http://www.bpscanada.org/docs/ADULTDiscipleshipPageStyle.pdf.

The Belgic Confession. 1561. Online: http://www.creeds.net/belgic/.

Billy Graham Evangelistic Association. 1998. *Thirty Discipleship Exercises.* Online: noordwyk.sagemeente.com/Publisher/File.aspx?id=70779.

Blackaby, Henry, and Claude King. 1994. *Experiencing God.* Nashville, TN: Broadman & Holman. 2008 edition preview online: https://www.google.com/search?tbo=p&tbm=bks&q=isbn:0805447539.

Bonhoeffer, Dietrich. 1954. *Life Together.* Translated by John Doberstein. New York: Harper & Row. Online: bearsfc.tistory.com/attachment/cfile26.uf@213C214854ADB05A0CCBE3.pdf.

_______. 1963. *The Cost of Discipleship.* New York: Macmillan. Preview of another edition online: https://books.google.com/books?isbn=0684815001.

_______. 1971. *Letters and Papers from Prison,* enlarged ed. Edited by Eberhard Bethge. New York: Touchstone. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=1451650531.

Breen, Mike. 2011. *Building a Discipling Culture,* 2d ed. Pauleys Island, SC: 3 Dimension Ministries.

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

The Bridge. 2013. *Discipleship Training Manual.* Online: http://www.thebridgeonline.net/wp-content/uploads/2015/03/Discipleship-Training-Manual-All.pdf.

Calvin, John. 1960. *Institutes of the Christian Religion.* Two Volumes. Edited by John McNeill. Translated by Ford Battles. Philadelphia: Westminster. Another edition online: http://www.ccel.org/ccel/calvin/institutes.i.html.

Carson, D. A. 1991. *The Gospel According to John* (PNTC). Leicester, England: Apollos. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=0802836836.

Carter, Matt, Halim Suh, and Tyler David. 2014. *The Gospel & How the Gospel Relates to Sex, Money, & Work.* Online: http://my.vergenetwork.org/wp-content/uploads/2014/03/TheGospelAndEbook.pdf.

Cheney, Tom, J. David Putnam, and Van Sanders, eds. 2003. *Seven Steps for Planting Churches*. Alpharetta, GA: North American Mission Board. Online: https://swbts.edu/sites/default/files/images/content/docs/Seven_Steps_for_Planting_Churches.pdf.

Church Planting Movements: Best Practices from Across the Globe. 2015. Online: http://www.churchplantingmovements.com/.

Churches Alive. 1996. *Build a 21st Century Disciplemaking Church.* San Jose, CA: Churches Alive.

*1 Clement*. 1989. In *The Apostolic Fathers*, 2nd ed., edited and revised by Michael Holmes, translated by J. B. Lightfoot and J. R. Harmer, 28-64. Grand Rapids: Baker. Online (another edition): http://www.ccel.org/ccel/lightfoot/fathers.ii.i.html.

Clowney, Edmund. 1995. *The Church.* Downers Grove, IL: InterVarsity.

Cole, Neil. 2011. "Can Groups be Missional & Make Disciples?" Online: http://www.vergenetwork.org/2011/05/24/neil-cole-can-groups-be-missional-make-disciples/; http://cole-slaw.blogspot.com/2011/05/hanging-great-weight-on-thin-wires-can.html.

Coleman, Robert. 1964. *The Master Plan of Evangelism*. Old Tappan, NJ: Revell. Online: http://campusministryunited.com/wp-content/uploads/2013/11/MasterPlanOfEvangelism.pdf.

Colson, Charles. 1992. *The Body.* Dallas: Word. Preview online: https://www.google.com/search?tbo=p&tbm=bks&q=isbn:1418514586 (later edition).

Core Discipleship. 2003. *Core Discipleship Group Workbook.* Online: http://www.corediscipleship.com/Downloads/Core/coreworkbook2.pdf.

_______. Not dated. "Core 3 Strand Discipleship." Online: http://www.corediscipleship.com/core-3-strand-discipleship/.

Daniel, C. J. 2010. "Meeting the Saviour Through the Quran." In *Where There Was No Church,* ed. E. J. Martin, 31-47. Learning Together.

Danker, Frederick, ed. 2000. *A Greek-English Lexicon of the New Testament and Other Early Christian Literature.* Chicago: The University of Chicago Press.

Demarest, Bruce. 1997. *The Cross and Salvation.* Wheaton, IL: Crossway. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=1433519577.

*The Didache*. 1989. In *The Apostolic Fathers*, 2nd ed., edited and revised by Michael Holmes, translated by J. B. Lightfoot and J. R. Harmer, 145-58. Grand Rapids: Baker. Online (another edition): http://www.ccel.org/ccel/lightfoot/fathers.ii.xii.html.

Disciple Nations Alliance. 2009. *Lifework Bible Study.* Online: http://www.disciplenations.org/media/Lifework-Small-Group-Bible-Study.pdf.

Discipleship Course. 2016. "The Lessons of the Discipleship Course." Online: http://www.discipleshipcourse.org/material.html.

Discipleship Evangelism. Not dated. "Discipleship Evangelism 48-Lesson Condensed Version." Online:

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

http://delessons.org/tools/de_program_condensed/index.jsp.

Discipleship Ministries. 2017. "Church Planting Strategies." Online: https://www.umcdiscipleship.org/new-church-starts/strategies.

Dodson, Jonathan. 2012. *Gospel-Centered Discipleship.* Wheaton, IL: Crossway. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=1433530244.

e3 Partners Ministry. 2011. *First Steps: Mobilize your Church into God's Harvest Fields.* Plano, TX: e3 Partners Ministry. Online: https://www.cmaresources.org/files/FirstSteps2011-e3PartnersCSergaent.pdf.

Earle, Ralph. 1978. "1 Timothy." In *Expositor's Bible Commentary,* vol.11, ed. Frank Gaebelein, 341-90. Grand Rapids, MI: Zondervan.

*The Epistle of Barnabas*. 1989. In *The Apostolic Fathers*, 2nd ed., edited and revised by Michael Holmes, translated by J. B. Lightfoot and J. R. Harmer, 162-88. Grand Rapids: Baker. Online (another edition): http://www.ccel.org/ccel/lightfoot/fathers.ii.xiii.html.

Equip Disciples. 2007-2008. *Worldview Discipleship: Pictures.* Online: http://equipdisciples.org/Theological/Worldviewpicsv2-English.pdf.

________. 2007-2009a. *Inyigisho za Bibiliya zifasha Abantu Gukura mu Gakiza* [course]. Online: http://equipdisciples.org/Theological/TheologicalDiscipleship_Kinyarwanda.pdf.

________. 2007-2009b. *Inyigisho z'Imana zo Gufasha Abantu Gukura mu Gakiza* [pictures]. Online: http://equipdisciples.org/Theological/TheologicalDiscipleshipPictures_Kinyarwanda.pdf.

________. 2007-2009c. *Uanafunzi Unaozingatia Theologia* [course]. Online: http://equipdisciples.org/Theological/TheologicalDiscipleship_Kiswahili.pdf.

________. 2007-2009d. *Uanafunzi Unaozingatia Theologia* [pictures]. Online: http://equipdisciples.org/Theological/TheologicalDiscipleshipPictures_Kiswahili.pdf.

________. 2007-2010. *Theological Discipleship.* Online: http://equipdisciples.org/theological/TheologicalDiscipleship_English.pdf.

Erickson, Millard. 1998. *Christian Theology,* 2nd ed. Grand Rapids: Baker. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=0801021820. First edition online: http://media.sabda.org/alkitab-2/PDF%20Books/00031%20Erickson%20Christian%20Theology%20Part%201.pdf (Part 1); http://media.sabda.org/alkitab-2/PDF%20Books/00031%20Erickson%20Christian%20Theology%20Part%202.pdf (Part 2); http://media.sabda.org/alkitab-2/PDF%20Books/00031%20Erickson%20Christian%20Theology%20Part%203.pdf (Part 3).

"Eucharist in Lutheranism." 2017. *Wikipedia.* Online: https://en.wikipedia.org/wiki/Eucharist_in_Lutheranism.

Exponential.org. 2017. "Resources." Online: https://exponential.org/.

Followers. 2010. "Real-Life Discipleship: Building Churches That Make Disciples" chart. Online: http://followers.org.nz/wordpress/wp-content/uploads/2012/11/App-A-Putman-RLD.pdf.

Garrison, David. 1999. *Church Planting Movements.* Richmond, VA: International Mission Board. Online: http://www.churchplantingmovements.com/images/stories/CPM_Profiles/cpm_booklet_standard_english.pdf.

________. 2004. *Church Planting Movements: How God is Redeeming a Lost World.* Midlothian, VA: WIGTake Resources. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=0974756202.

________. 2010. "Discipleship in Church Planting Movements." Online: http://www.churchplantingmovements.com/index.php/vert5parts/vertdiscipleship/61-discipleship-in-church-planting-movements.

________. Not dated. *Summary of Church Planting Movements.* Online: http://christfellowshipslc.com/wp-content/uploads/2014/11/CF-church-planting-movement.pdf.

Copyright © 2017 by Jonathan Menn. All rights reserved.

George, Timothy. 1998. "What I'd Like to Tell the Pope About the Church. *Christianity Today* (June 15): 41-44. Online: http://www.christianitytoday.com/ct/1998/june15/8t7041.html.

Global University. 2008a. *21st Century Discipleship (Book 1): Getting Started.* Springfield, MO: Global University. Online: http://www.globalreach.org/english/images/da2101en_entire.pdf.

_______. 2008b. *21st Century Discipleship (Book 2): Facing Issues.* Springfield, MO: Global University. Online: http://www.globalreach.org/english/images/da2102en_entire.pdf.

_______. 2008c. *21st Century Discipleship (Book 3): Making a Difference.* Springfield, MO: Global University. Online: http://www.globalreach.org/english/images/DA2103EN_Entire.pdf.

Green, Joel, and Scot McKnight, eds. 1992. *Dictionary of Jesus and the Gospels.* Downers Grove: InterVarsity. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=0830817778.

Grudem, Wayne. 1994. *Systematic Theology.* Grand Rapids: Zondervan. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=0310286700.

Guthrie, Donald. 1990 (reprinted 2000). *The Pastoral Epistles,* rev. ed. (TNTC). Leicester, England: Inter-Varsity.

Hammond, Kim, and Darren Cronshaw. 2014. *Sentness.* Downers Grove, IL: IVP Books. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=0830884068.

Harrington, Bobby, and Josh Patrick. 2014. *Discipleship Handbook: The Six Elements of a Personal Discipleship Lifestyle.* Online: http://discipleship.org/wp-content/uploads/2014/06/Discipleship-Handbook-Final-REVISED-AND-REDUCED-PDF.pdf.

Heidmann, Lynn. 2006. "Mifflin volunteers aid quick cleanup." *The Badger Herald.* Online: https://badgerherald.com/news/2006/05/01/mifflin-volunteers-a/.

Henrichsen, Walter. 1988. *Disciples are Made not Born.* Wheaton, IL: Victor. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=1434704718.

Hodge, Charles. 1993 (reprint of 1886 edition). *Commentary on the Epistle to the Romans.* Grand Rapids: Eerdmans. Another edition online: https://archive.org/details/commentaryon1873hodg.

Holmes, Michael, ed. *The Apostolic Fathers,* 2nd ed. Translated by J. B. Lightfoot and J. R. Harmer. Grand Rapids: Baker. Preview of third edition online: https://books.google.com/books?isbn=0801031087.

Hunt, Dave. 1995. "Baptismal regeneration?" Online: https://www.thebereancall.org/content/baptismal-regeneration.

Ignatius. 1989. "To the Smyrnaeans." In *The Apostolic Fathers*, 2nd ed., edited and revised by Michael Holmes, translated by J. B. Lightfoot and J. R. Harmer, 110-15. Grand Rapids: Baker. Online (another edition): http://www.ccel.org/ccel/lightfoot/fathers.ii.viii.html.

Jadeed, Iskander. 1996-2015. *Did God Appear in the Flesh?* Rikon, Switzerland: The Good Way. Online: http://www.the-good-way.com/eng/books.

Johnson, Dennis. 2007. *Him We Proclaim: Preaching Christ from All the Scriptures.* Phillipsburg, NJ: P&R.

Johnson, Jeremiah. 2016. "Does Baptism Save You? (1 Peter 3:21; Acts 2:38)." Online: https://www.gty.org/library/blog/B160815.

Justin Martyr. 1885. *First Apology*. In *The Ante-Nicene Fathers,* vol. 1, edited by Alexander Roberts and James Donaldson, revised by A. Cleveland Coxe, 159-87. New York: Christian Literature Publishing Company. Reprint, Peabody, MA: Hendrickson, 1994. Online (another edition): http://www.ccel.org/ccel/schaff/anf01.viii.ii.html.

Kalinowski, Caesar, and Seth McBee. 2013. *Be the Church: Discipleship and Mission Made Simple.* Online: http://my.vergenetwork.org/wp-content/uploads/2014/03/0e916875_bethechurchpdf-1.pdf.

